Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 25 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 255

### Kibali cha Ajira Katika Ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji

**MHE. MWIGULU LAMECK MCHEMBA MADELU** aliuliza:-

Nafasi nyingi katika ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji vimeshikiliwa na watu wanao kaimu hivyo

kupunguza ufanisi katika utendaji kutokana na kuchelewa kwa vibali vya kuajiri kutoka Serikalini:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa vibali vya kuajiri watumishi katika ngazi hizo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kutoa mwongozo kuwa watumishi wa ngazi hizo wawe wenyeji/wazawa wa Wilaya husika?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kutekeleza ukomo wa muda wa Kukaimu Kisheria?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mchemba Madelu, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ajira katika utumishi wa umma, hutolewa kwa nafasi za ajira mpya zilizoidhinishwa katika Ikama na kutengewa fedha katika Bajeti ya mwaka husika na kuidhinishwa na Bunge.

Kati ya mwezi Julai, 2011 na Mei, 2012 Serikali imetoa vibali vya ajira kwa nafasi mpya 48,333 kuwawezesha waajiri kujaza nafasi katika kada

mbalimbali zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya nafasi 1,239 za kada za msingi zimeombwa na kuidhinishiwa fedha kama ifuatavyo: Afisa Tarafa nafasi 54, Mtendaji Kata nafasi 410, Mtendaji wa Kijiji nafasi 692 na Mtendaji Mitaa nafasi 83.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuajiri watumishi wake inazingatia Sheria na taratibu zinazozingatia Umoja wa Kitaifa na zinazotaka nafasi husika kujazwa kwa uwazi *(Open Recrutment System).* Hivyo si utaratibu wa Serikali kuajiri watumishi kwa misingi ya uwenyeji/uzawa waliokozaliwa kwani kufanya hivyo ni kinyume na ibara ya 22 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1997, toleo la Mwaka 2008 inayompa fursa kila Mtanzania kufanya kazi yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi.

Aidha, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma toleo la mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria na. 18 ya mwaka 2007, zimeeleza kuwa ajira ya Utumishi wa Umma zitajazwa na watu wenye sifa kutoka sehemu yoyote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa changamoto za ajira za watendaji wa ngazi za msingi, Serikali imekwishaamua kuweka utaratibu utakaoziwezesha Halmashauri za Wilaya kuajiri zenyewe kada hizo ili kukabiliana na changamoto. Hatua inayofuata sasa ni

kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na Kanuni zake ili iweze kuzingatia uamuzi huo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni D.24 (3) cha Kanuni za Kudumu, Toleo la mwaka 2009, muda wa Kukaimu nafasi ya Uongozi ni miezi sita. Katika kipindi hicho mamlaka za ajira zinatakiwa kuchukua hatua za kujaza nafasi husika.

Serikali inakubaliana na rai ya Mheshimiwa Mbunge ya kutekeleza ukomo wa muda wa kukaimu kisheria. Hivyo ninatoa wito kwa waajiri wote kuhakikisha kuwa nafasi husika zinajazwa mapema iwezekanavyo na kwa kuzingatia mwongozo wa makadirio ya ikama na mishahara wa mwaka 2009/2010 kama ulivyoidhinishwa kwa ajili hiyo.

**MHE. MWIGULU LAMECK MCHEMBA MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Mheshimiwa Rais, ndiye Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya CCM. Utakumbuka kwenye Kamati Kuu ya Mwisho ya Mwaka jana tulipitisha uamuzi kwamba ngazi hizi ziachiwe jukumu la kuajiriwa watu hawa kupitia ngazi ya Halmashauri ili kuondoa ukiritimba.

Lakini pia na kuzingatia hali halisi ya sasa kwamba watu wenye sifa za aina hii kufuatana na shule za Kata watapatikana kule kule na Wilayani.

(a) Je, ni lini uamuzi huu tena umekuja kubadilika na kuja na majibu ya aina hii?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali ili iheshimike ni kuajiri na kufukuza tumekuwa tukilia kila wakati kwamba waajiriwa wakikosea sehemu fulani katika Halmashauri wanahamishiwa sehemu nyingine kwa sababu uhamishaji unatokana na mwajiri kuwa wa ngazi ya juu.

Je, kwa nini sasa tusiipe mamlaka Baraza la Madiwani la kuajiri hawa watumishi wadogo wadogo ili wanapokosea katika ngazi husika waweze kufukuzwa bila kusubiria kibali kutoka Makao Makuu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mchemba Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba Mheshimiwa Mwigulu Mchemba Madelu, anayezungumza hapa Mbunge wa Iramba ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi, ninatambua hilo. Siwezi ku-*doubt* kabisa uelewa wake kuhusu jambo hili tunalolizungumza hapa. Kitu kinachosema hapa hizo kada zilizosemwa zote na kama anavyosemwa

Mheshimiwa Mchemba ni kweli Serikali imekubali kwamba zote zirudishwe katika Halmashauri.

Nakuomba nikutajie hawa ni pamoja na wahudumu wa Ofisi za Afya, Madereva, Maafisa Watendaji wa Mitaa, Maafisa Watendaji wa Kata, Wapishi, Madobi, Walinzi na Makatibu Muhtasi na wasaidizi mbalimbali. Anachosema ni kweli kabisa ambacho tunakisema hapa hawawezi ile Kamati ya ajira inapokutana katika Halmashauri ikimwita dereva inataka ku-*recruit* inamwuliza wewe ni mzaliwa wa hapa au siyo mzaliwa wa hapa? Ndicho hicho tu tunachosema hapa.

Hicho unachokisema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa unavyosema. Hapa nilipoulizwa ni kwamba tutoe mwongozo kuhusu uzawa ndicho kilichosemwa hapa ndicho tunachosema ndio maana nimekwenda nika- quote Katiba inayosema kwamba mtu yeyote katika Tanzania mahali popote pale anaweza akapata ajira.

Hili tunayozungumza hapa kwa vile na wewe amekutaja hapa ili kama mtauliza maswali ya nyongeza mwulize vizuri ili niwaeleze kwa sababu hapa nimejiandaa vizuri, hakuna ugomvi kuhusu kuajiri hawa watu katika ngazi ya Halmashauri, hiyo tumesharudisha. Sasa ataniuliza swali kwa nini hamfanyi?

Ile sheria iliyowachukua hawa waliotamkwa hapa ikawapeleka kule utumishi kwa maana ya kuwapeleka kule kwenye kamisheni, sheria ile ilibadilishwa. Kwa

hiyo, sheria ile sasa inafanyiwa kazi na *cabinet* imekwishakupitisha jambo hili sasa kinachofanyika hapa sasa hivi ni kuleta sasa mabadiliko haya na *AG* ataileta hapa hivi karibuni.

La pili, mtu amefanya makosa katika Halmashauri moja anahamishwa anapelekwa Halmashauri nyingine, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba yuko *right* na tumesema akifanya makosa mtu pale Magu hatumpeleki Songea tunamwacha pale pale Magu na tutashuka naye pale pale Magu tena jumla jumla. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa kama ninyi mnayo mifano na hili limepita mpaka kwenye ile Kamati kwenye Baraza ikaonekana kuna makosa yamefanyika pale na hasa hasa kwa yale yaliyoonekana na *CAG report* amesema hapa Mheshimiwa Hawa Ghasia na wale wengine wote waliohusika wameeleza hapa kwamba utaratibu ni kwamba hahamishwi tena anabaki pale pale. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nilikuwa naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri je, Serikali inajua umuhimu wa watendaji wa vijiji, umuhimu wa watendaji wa Kata na kama inajua kwa nini inachelewesha kutoa vibali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalo hili nililieleze vizuri, vibali vilivyotoka ni 1239 nataka nikuambie hapa Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu mimi najua kwamba swali hili litaulizwa hivyo vibali vilivyotolewa ndivyo vilivyoombwa vyote mpaka kule kwako kule Peramiho vyote ndivyo vilivyoombwa.

Mtu akitaka akacheki na nimecheki mpaka asubuhi na Mkurugenzi Mhusika nikamwambia una hakika hakuna wengine, sasa inawezekana kabisa kwamba kule anakozungumza Mheshimiwa Mbunge, wako wengine wamefariki, wengine wameondolewa na nini, wengine wamestaafu na nini hii inaweza ikawa ni kitu kingine kipya.

Lakini nataka nikuthibitishie katika nyumba hii nimecheki na wote wanaohusika haya maombi ya 1239 yote yameingizwa katika Bajeti hii ambayo imepitishwa hapa. Kwa hiyo, wawe na hakika kwamba watendaji wote wa kata na wale wa tarafa pamoja na vijiji wote vibali vimeshatoka tayari. (*Makofi*)

Na. 256

**Ahadi ya Kuwapatia Wananchi Umeme**

**MHE. JEROME DISMAS BWANAUSI** aliuliza:-

Katika mwaka wa Fedha 2011/2012 Serikali iliahidi kuwapatia umeme wananchi wa vijiji vya Chiwata, Nanjota, Mbuyuni, Mkangaula, Luatala, Mchauru na Mnavira:-

(a) Je, Serikali imekwishafanya matayarisho ya kupata gharama?

(b) Je, ni lini sasa kazi ya kupeleka umeme maeneo hayo itaanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* na *REA* imeandaa mpango kabambe wa awamu ya pili ya kupeleka umeme vijijini yaani (*Turnkey Rural Electrification Project Phase 2).* Tayari maandalizi yameshafanyika kwa asilimia 95 na zabuni inatarajiwa kutangazwa mwezi Agosti, 2012. Awamu hii ya pili ni mwendelezo wa awamu ya kwanza ambapo Wilaya na vijiji katika Mikoa 16 ilifaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* imeshakamilisha tathimini kujua gharama za awali za mradi huu wa kuwapatia umeme wananchi wa vijiji

vya Nanjota, Mbuyuni, Mkanaula, Luatala, Mchauru na Mnavira.

Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 33 yenye urefu wa km 45 na ujenzi wa njia ya usambazaji umeme za msongo wa kV 0.4 zenye urefu wa kilomita 15 pamoja na ufungaji wa jumla ya *transfoma 8.* Mradi huu ambao utagharimu jumla ya shilingi bilioni 2.

**MHE. JEROME DISMAS BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake ya msingi ameelezea tu kuhusu matayarisho ya *tender* ambayo inataka kutolewa mwezi Agosti, lakini hajawaeleza wananchi wa Chiwata, Nanjota, Mbuyuni, Mkangaula, Mnavira pamoja kule Mchauru juu ya kazi hii ya ujenzi itaanza lini?

(b) Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba upanuzi wa maeneo ya utoaji wa umeme unazingatia upatikanaji wa umeme na bahati nzuri katika Mkoa wa Mtwara na Lindi kumepatikana gesi ya kutosha hivyo kutegemea kuwa na umeme wa kutosha.

Je, anaweza akawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi juu ya bomba la gesi linalojengwa litanufaisha vipi wakazi wa Mkoa huo

hususan katika maendelezo ya viwanda katika maeneo ya Mtwara na Lindi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu kama wananchi wa maeneo haya niliyoyataja ya Nanjota, Mbuyuni, Mkangaula, Mnavira, Mchauru ni lini tuwaambie mradi utaanza?

Mchakato kama utaanza mwezi wa nane ni dhahiri kwamba kwenye mwezi wa 12 Januari, 2013 hivi tunaweza tukawa tumeanza ujenzi wa mradi huu.

Hivyo wakae mkao wa matayarisho na waandae nyumba kwa ajili ya kuanza kufanya *wiring* kwa sababu pengine umeme unaweza ukawahi kufika kabla hawajafanya maandalizi.

Lakini swali la pili,ni kweli kwamba upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi hakuna matatizo. Hivi tunavyozungumza kuna *MW* sita pale zimekaa tu pale Mtwara hazina matumizi.

Kwa hiyo, hatuna tatizo kabisa juu ya uwezo wa umeme wa Kusini na nitaka nichukue nafasi kwa niaba ya Serikali kuwaomba sana watu wa Mtwara na Lindi kwamba neema sasa imefunguliwa kwao kwa sababu kama gesi inatoka Mtwara na Lindi ni dhahiri kabisa ni lazima tuonyeshe manufaa ya wazi kwao na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, iko tayari kuhakikisha

inadhihirisha hayo kwa kuanza matumzii ya bomba la gezi ambao tunaamini kabisa ni lazima wao wawe wanufaikaji wa kwanza.

Lazima pale Halmashauri zinapata fedha nyingi kutoka kwenye *industry* hii ya gesi na ni lazima tutahakikisha kwamba wanapata kipaumbele na kwa kuanza tu hili, Waziri wangu, ameniruhusu tarehe 1 nikimaliza tu Bajeti yangu ambayo naamini mtaipitisha bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitahakikisha nakwenda kukaa siku kumi Lindi na Mtwara kuhakikisha kote naweka *infrastructure* ikae sawa sawa ili wawe wanufaikaji wa kwanza na umeme huu wa gesi. (*Makofi*)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa sababu matatizo ya Lindi yanafanana sana na matatizo ya kule Mbeya, ningeomba Mheshimiwa Waziri atueleze barabara ya kutoka Mbeya kuelekea Chunya kuna Kijiji kinaitwa Lwanjilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umepita juu kwa juu ningeomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini umeme utashushwa katika Kijiji hicho kwa sababu maeneo yote yamepewa umeme isipokuwa hicho Kijiji. Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanjelwa kama ifuatavyo:-

Tulionana na Mheshimiwa Mwanjelwa. Kwanza nikupongeze kwa namna unavyofuatilia na ulinieleza juu ya Kijiji hiki na leo umepata fursa ya kuuliza hapa. Ninaomba nikuhakikishie kwamba sisi Serikali kwa sasa Wizara ya nishati na Madini tunataka kuhakikisha kwamba, hatutaki kuona wananchi wa Kijiji fulani wanaziangalia tu waya za umeme zinapita.

Kwa hiyo, mimi ninachowaomba kwenye Bajeti yetu kama mtatupitishia vizuri na nina amini mtafanya hivyo, nitajitahidi kuweka programu Fulani kadogo ambako katahakikisha kwamba umeme unashushwa. Maana pale pengine inahitajika *transformer* moja na nyumba kadhaa, Vijiji viwili, vitatu vinapata umeme. Kwa nini tusiwasaidie Watanzania hao?

Kwa hivyo, umeme kuruka Kijiji itakuwa ni kweli ni kosa kubwa na sisi tutajitahidi sana tunaanzisha kaprogramu fulani ndani ya Wizara katakachoshughulikia eneo hilo. Tunajua tunayo programu ya *REA* ambayo inatusaidia kupeleka umeme Vijijini. Lakini kuna sehemu ambazo umeme umepita haujashushwa ni kushusha tu. Lazima tuje na programu maalum kwa ajili ya jambo hilo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa kwamba sina jibu la moja kwa moja nini

nitafanya baada ya hapa na wananchi wale wategemee nini lakini wategemee kwamba ndani ya mwaka huu huu wa fedha, tutajitahidi kuanzisha kakitu fulani katakachoweza ku-*implement* hiyo programu ya kuhakikisha umeme kwenye Vijiji hivyo. (*Makofi*)

Na. 257

**Mpango wa Kupeleka Umeme Kata za Bukoba Vijijini**

**MHE. JASSON SAMSON RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, mpango wa kupeleka umeme eneo la Bugado, Kata za Buhendangabo Kaagy, Kishanje na Rubafu katika Jimbo la Bukoba Vijiji unaendeleaje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Maeneo ya Bugado, Kata za Buhendagabo, Kaagya, Kishanje na Rubafu katika Jimbo la Bukoba Vijijini, yanategemea kupata umeme chini ya awamu ya pili ya mpango kabambe wa kupeleka umeme Vijijini utakaofadhiliwa na Serikali kupitia wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Mradi huu unategemea kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013.

Upembuzi yakinifu umeshafanyika ambapo mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya umeme yenye urefu wa km 54.4 ya msongo wa kV 33 njia ya umeme ya msongo wa kV 0.4 yenye urefu wa km 46 na ufungaji wa *transfoma* 23 zenye ukubwa wa kVA 50 kila moja na *transfoma* 4 zenye ukubwa wa kVA 100 kila moja. Mradi huu unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi 3.2.

**MHE. JASSON SAMSON RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyonipa, lakini napenda nimpe swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ya CCM ina lengo la kupeleka umeme Vijijini katika awamu hii, Serikali ya awamu ya nne ifikapo mwaka 2015 kwa kiwango cha asilimia 35 Vijiji vyote nchini na kwa kuwa Wakala wa Umeme Vijijini chini ya Uongozi wa Dkt. Mwakayesa inafanya kazi nzuri sana inayoonekana kupeleka umeme Vijijini.

Sasa kwa nini Serikali isilete Sheria hapa Bungeni kuongeza mapato ya *REA* kwa kuongeza makato kwenye ankara za umeme za watu wa Mjini badala ya asilimia 2 ikawa labda asilimia 4 kusudi *REA* iwe na uwezo zaidi kupeleka umeme Vijijini? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rweikiza, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali ya CCM imedhamiria na tuna uhakika kwamba tutafikia lengo la asilimia 30 ya umeme Mijini na Vijijini. Lakini ni kweli pia kwamba *REA* inafanya kazi nzuri na kweli kabisa Dkt. Mwakayesa anafanya kazi nzuri na kwamba iko haja ya kufikiria kuongeza mapato ya *REA* ili tuweze kufikia malengo mapema iwezekanavyo katika utekelezaji wetu wa sera za Chama cha Mapinduzi.

Lakini hadi sasa, ni kwamba tunapata fedha kutoka kwa wateja watumiaji wa umeme tunakata kiasi cha asilimia kidogo pale, lakini ukisema tuongeze ni jambo linalohitaji mjadala kwa sababu hata hivi sasa hivi, bado umeme ambao wateja wetu wanatumia kwa Tanzania unauzwa kwa bei rahisi ukilinganisha na nchi za wenzetu katika *East Africa Community.*

Sisi umeme wetu Tanzania uko chini sana na kwa kufanya hivyo, bado tunaangalia *logistics* za *economics* za nchi kama zinaweza kuturuhusu ili tuweze kuongeza. Lakini ili uweze kuongeza bei ya umeme, ni lazima umeme huo uwe *reliable.*

Kwa hiyo, tu *buy time,* tuone itakavyokuwa. Lakini mimi naamini kwamba baada ya muda mchache tunaweza tukafikiria vyanzo vingine vitakavyosaidia mpangu huo wa *REA* unaofanya kazi vizuri ili kuweza kuwapatia umeme wananchi wengi sana Vijijini kadiri iwezekanavyo.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, mwaka jana Wizara yake ilitoa majibu hapa Bungeni

kwamba ile ziada ya umeme ya takribani *megawatt 4* inayopatikana pale Kigoma Mjini wangeweza kufanya utaratibu wa kuisogeza iweze kuvisaidia Vijiji vya Kandaga, Kazulamimba ambapo kimsingi ni njia ya kuelekea Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Uvinza. Ningependa kujua mpaka sasa Serikali imetekeleza jambo hilo kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kafulila kama ifuatavyo:-

Ni kweli Kigoma kuna *megawatt 4* ambazo hazitumiki na ni kweli kwamba viko Vijiji na hususani Vijiji vinavyoelekea Uvinza havina umeme na vingehitaji kupata umeme. Mheshimiwa njoo ofisini kwangu nikuonyeshe mambo yalivyo mazuri. Umeme, mipango iko vizuri na tutahakikisha kwamba tunapeleka umeme Uvinza. Ahsante sana.(*Makofi*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFU***:* Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Pamoja na maelezo mazuri sana ya Naibu Waziri yako maeneo katika nchi hii ambayo yaliuona umeme wakati wa ukoloni. Kwa mfano maeneo yaliyoko karibu na mashamba ya katani, Lushoto kulikokuwa na mashamba ya chai na kahawa. Maeneo hayo mpaka leo wananchi wa jirani wanauona umeme kwa mbali. Sasa Waziri anatamka nini ili azama ya Chama cha Mapinduzi kupeleka umeme hasa kwa wananchi kama wale wa maeneo ya Tarafa ya Mlola kule Lushoto?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekifu, kama ifuatavyo:-

Ni kweli yako maeneo katika nchi yetu ambayo kutokana na mfumo na uchumi wa wakati ule wa ukoloni, yalibahatika kuuona umeme na baadaye ukatoweka kama nimempata sawa sawa.

Lakini kama nilivyosema sisi kama Wizara tumeamua kujipanga na tunataka kuhakikisha kwamba sehemu yeyote ambayo kumepita waya, umeme unashushwa. Nikuhakikishie Mheshimiwa Shekifu kwamba dhamira yetu hii ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, itafikiwa tu endapo tu kama mtaiunga mkono Serikali katika jukumu lake hili na dhamira yake ya kuhakikisha kwamba umeme Vijijini unafika. *(Makofi)*

Na. 258

**Watoto Kuwekwa Katika Mazingira Hatarishi**

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED** aliuliza:-

Umasikini na athari za Ukimwi vimechangia kuwaweka baadhi ya watoto nchini katika mazingira hatarishi kutokana na kukosa malezi, matunzo na ulinzi yanayostahili na tatizo hili linazidi kuongezeka sambamba na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kitekinolojia:-

Je, Serikali inalishughulikia vipi jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhammed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia hili, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa miaka minne (4) (2007-2010) wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Mpango huu umefanyiwa tathmini ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji ili kuwezesha kuandaliwa kwa mpango mwingine wa (2011-2015). Mpango huo unatoa dira na mwelekeo wa wadau mbalimbali katika utoaji huduma kwa watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Septemba 2011, jumla ya watoto 849,051 kati yao wa kiume 449,997 na wa kike 399,054 wametambuliwa kuishi katika mazingira hatarishi katika Halmashauri 95 kati ya Halmashauri 133. Watoto hawa wanaendelea kupatiwa huduma stahiki na jamii, Serikali na wadau mbalimbali. Huduma hizo ni pamoja na matibabu, msaada wa kisaikolojia na kijamii, ada na vifaa vya shule, mavazi, malazi na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeandaa miongozo mbalimbali ili kuboresha utoaji huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Miongozo hiyo ni pamoja na utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi, stadi za malezi kwa wazazi na walezi wa watoto walio katika mazingira hatarishi, uboreshaji viwango vya huduma, uanzishaji na usimamizi wa makao ya kulelea watoto.

Aidha Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha mafunzo kwa wazazi, walezi na watoa huduma wengine ili kuwajengea uwezo juu ya stadi za malezi, uboreshaji viwango vya ubora wa huduma, huduma za kisaikolojia na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. *(Makofi)*

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Wizara iliandaa mpango wa miaka minne kuanzia 2007 -2010 na kutokana na mpango huo wameweza kujua tathmini na kwa kuwa tathmini hiyo hatujaisikia wala kuiona bado wanaendelea kupanga mpango mwingine wa 2011- 2015.

(a) Je, Serikali iko tayari kuwasilisha mpango huo hapa Bungeni ili kila mmoja auone na ausikie? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa wimbi la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi linazidi kukuwa na kwa kuwa kuna *NGO's* na watu binafsi ambao wanawashughulikia watoto hawa na wakati mwingine baadhi yao hufanya kama ni mradi.

Je, kwa nini Serikali hamwajengei nyumba watoto hawa mkawaweka pamoja wakaweza kustirika na wakaweza kufanya kazi zao kwa vizuri zaidi na akapata maisha mazuri kama vile mnavyojenga makambi ya Jeshi, JKT na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Thuwayba, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli hakutakuwa na tatizo la kuwasilisha mpango ili wenzetu muweze kuuona kwa sababu mpango wa kwanza ulikuweko na ukaweza kutekelezeka na tathmini imefanyika na ndiyo ambayo imepelekea kuchakarisha mpango mwingine. Kwa hiyo, kwenye hili hatutakuwa na tatizo la kuwasilisha huo mpango.

(b) Mheshimwia Mwenyekiti, ni kweli kuna *NGO's* nyingi na watu binafsi ambao wameanzisha makazi kwa ajili ya kutoa matunzo kwa ajili ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kwamba ukubwa wa tatizo hili ni kubwa kwa sababu asilimia kama 12 hivi ni ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Katika hao tunafahamu kwamba zaidi ya asilimia 53 wanatunzwa na Bibi, Babu na asilimia nyingine 31 wanatunzwa na Ndugu na Jamaa.

Ni kweli kwamba unaweza ukaamua uanzishe kitengo kwa ajili ya kuweza kuwatunza sasa watoto hao wote. Lakini tatizo hili ni kubwa na linahitaji

msaada wa kila mmoja wetu katika kutimiza wajibu wetu wa kutunza watoto wetu.

Mimi naamini katika maeneo yetu ya Kiserikali, maeneo yetu ya kijamii katika Serikali zetu Vijiji na Serikali zetu za Halmashauri bado tuna nafasi ya kuweza kutoa mchango wetu katika kuhudumia hao watoto. Pale inapokuwa imeshindikana kuwa na maeneo ya malezi ya matunzo kwa ajili ya watoto kama hao basi itakuwa ni lazima kufanya hivyo, Serikali itaendelea kufanya hivyo.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge naomba niwakatishe kidogo nina tangazo hapa nadhani ni muhimu nilitoe sasa hivi. Nimepokea taarifa kwamba wenzetu wa *TBC* hawatakuwa hewani katika kipindi cha leo asubuhi kipindi hiki cha maswali na majibu kwa sababu leo kule Dar es Salaam katika Viwanja vya Mnazi mmoja kuna sherehe za Kitaifa za mashuja zinaendelea.

Kwa hiyo, wameomba msamaha sana watakuwa wanaendelea kurusha shughuli ile inayoendelea pale katika Viwanja vya mnazi mmoja. Lakini mara shughuli ile itakapokuwa imekamilika basi wataunganishwa tena na shughuli za Bunge na hivyo wataendelea kurusha matangazo kutoka hapa Bungeni. Lakini nadhani wenzetu wa *Star TV* wao watakuwa wanaendelea kurusha matangazo kama kawaida. Nimeona nisimame niwatangazie hili kusudi kama kuna lolote litatokea ama mtu anaweza akafikiri vinginevyo, sababu kubwa ni hiyo. *(Makofi)*

Na. 259

## Upungufu wa Watumishi wa Afya - Wilaya ya Nkasi

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Kutokana na upungufu mkubwa wa Watumishi wa Afya Mkoani Rukwa hususan katika Wilaya ya Nkasi, Uongozi wa Kanisa Katoliki katika Jimbo la Sumbawanga wameamua kujenga Chuo cha *St. Bakhita* - Namanyere Mjini kinachotoa Mafunzo ya Uuguzi na Wataalam wa Maabara kwa ngazi ya cheti, ambapo jumla ya wauguzi 80 huhitimu kila mwaka:-

(a) Je, kwa nini hospitali teule ya Namanyere ina upungufu mkubwa sana wa wauguzi na kuna mpango gani wa kumaliza tatizo hilo?

(b) Je, ni lini Serikali kwa kushirikiana na Chuo cha *St. Bakhita* watawezesha kutoa mafunzo ya ngazi ya Stashahada na Shahada?

(c) Je, Serikali ina mchango gani katika kazi ya upanuzi wa Chuo hicho unaendelea kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawii wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Watumishi wa Afya unaoikabili Hospitali Teule ya Namanyere ni tatizo ambalo pia lipo katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Katika kukabiliana na upungufu huu, Wizara imeongeza idadi ya wadahiliwa katika vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Afya.

Hata hivyo, tunazishauri Halmashauri za Wilaya nchini ikiwemo Nkasi, kuomba vibali vya kuajiri Watumishi wa Afya kulingana na mahitaji kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma kisha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itawapangia vituo kulingana na nafasi zilizotolewa.

Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wilaya ya Nkasi ilipata kibali cha kuajiri Watumishi wa Afya 25 ambao ni Wauguzi daraja la II- 15 na Wahudumu wa Afya 10 ambao wote wamepangiwa vituo katika Wilaya hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inasimamia na kutoa miongozo ya mafunzo kwa vyuo vinavyotoa mafunzo katika fani ya afya nchini kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE).*

Kwa wakati huu, Chuo cha *St. Bakhita* kinatoa mafunzo ya Uuguzi katika ngazi ya Stashahada. Kutokana na mtaala wa kuendesha mafunzo ya Uuguzi katika ngazi ya Stashahada, chuo kimeelekezwa kutimiza mahitaji mbalimbali ikijumuisha sifa na idadi ya

walimu, miundombinu na vifaa vya kufundishia ili kukidhi vigezo vinavyohitajika.

Hivyo, Wizara inaendelea kushirikiana na Uongozi wa chuo hicho ili kiwe na uwezo wa kuendesha mafunzo katika ngazi ya Stashahada. Vile vile, katika juhudi za Wizara za kuongeza udahili wa wanafunzi vyuoni, Chuo cha *St. Bakhita* ni mojawapo ya chuo kilichofanyiwa upembuzi mwaka 2011 ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia (*Global Funds*) inakipanua chuo hicho kwa ujenzi wa madarasa 4 yenye uwezo wa wanafunzi 400, maabara, mabweni yenye uwezo wa wanafunzi 500; nyumba za wafanyakazi 6 na ununuzi wa samani katika majengo hayo. Ujenzi huo unatarjiwa kumaliza ifikapo mwezi Oktoba 2012 na hii itakiwezesha chuo hicho kuongeza idadi ya wanafunzi zaidi ya wale wanaodahiliwa sasa na kuanzisha kozi zingine.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Wilaya ya Nkasi, iliendelea kukumbushia kuomba kibali cha kuajiri mwaka 2011 na 2012 kwa kuomba nafasi kadhaa, lakini nafasi hizo ambazo Mheshimiwa Waziri, anazisema kwenye jibu lake kwamba, tumepata 25, hatukupata. Tumepata, badala yake tumepata wauguzi watatu na wahudumu *(Medical Attendant)*

ambao hatuwahitaji, wametuletea 8, ambao hata hatukuomba hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna zahanati zaidi ya 36, tukiwa na Waganga 10 tu. Hii si udhalilishaji wa wananchi wa Namanyere na Wilaya ya Nkasi, kwa kuomba Waganga na wao wanaletewa Wahudumu. Si udhalilishaji wa makusudi wa Wizara? Wizara itachukua hatua gani kwa hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Hivi karibuni, tumeshuhudia kuna migogoro ya Madaktari nchini na Waganga Wasaidizi Mkoa wa Rukwa, waliweza kukaa katika Kikao chao cha tarehe 1 Juni, 2012, kuangalia maslahi yao pamoja na hatma ya kada zao. Wakabaini kwamba, mishahara baina ya Waganga Wasaidizi, *ADO* na *AMO*, imepishana sana na Madaktari *(MDs),* kitu ambacho hakilingani na namna majukumu yao yasivyopishana. Na kwamba... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Swali; uliza swali sasa.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, swali.

Je, Serikali, iko tayari kupokea Waraka huu, ambao Madaktari walikaa ili iufanyie kazi na kuondosha migomo inayoweza kutarajiwa baadaye katika Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya Nyongeza ya Mheshimiwa Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoa maelezo katika jibu langu la msingi ni kwamba, maeneo mengi nchini, tuna changamoto ya uwepo wa Watumishi, hasa wa Wizara hii ya Afya. Na juhudi tumezieleza karibu mara mbili, nilipokuwa nikijibu maswali katika vipindi vilivyopita, namna ambavyo Serikali, imekuwa ikijitahidi ili kuweza kupunguza na kuziba pengo hili la upungufu wa Watumishi katika maeneo yote nchini.

Mojawapo nimelielezea katika jibu hili kwamba, Chuo hicho cha *St. Bakita,* chenyewe kinapanuliwa, ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoweza kudahiliwa pale, kwa kusudio la kutokuzalisha wafanyakazi ambao wataweza kuziba mapengo ya watumishi kwenye maeneo yetu.

Lakini pia, maombi haya yanapitia Utumishi wa Umma, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na baada ya kibali kutolewa cha kuajiri ndio Wizara, inaamua sasa kupeleka kule Watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba, wenzetu kule Nkasi, watawasilisha maombi yao. Pale kibali kinapokuwa kimetolewa, basi Wizara itajaribu kushirikiana kwa kiwango cha hali ya juu, ili kuwapeleka watumishi waliopo kwa wakati huo, wanaoweza kukidhi nafasi Mheshimiwa anazozizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tofauti za mishahara kati ya, kama nimemwelewa vizuri, kati ya *ADOS (Assistant Dent Officers)* na *AMOS (Assistant Medical Officers).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sina jibu sasa la kuelezea ni kwa nini liko hivyo. Lakini nafikiri ni suala ambalo linahitaji kuliangalia kwa vizuri na baadaye kulitolea jibu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani anachozungumzia Mheshimiwa Mbunge, ni tofauti ya mishahara kati ya *AMOS* na *ADOS* na ile ya Madaktari *(MDS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwarifu tu kwamba, Waraka anaouzungumzia ninao, nimeupata na vilevile nimepata nafasi ya kuzungumza na hao *AMOS* wa pale Dar-es-Salaam, kuhusu suala hili. Nimewaahidi kwamba, tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Utumishi, ili kuweza kuangalia kwa kiwango gani tunaweza kuboresha maslahi ya *AMOS* na *ADOS,* ili yaendane na kazi wanazozifanya. Kwa sababu, ni kweli, kwamba, kazi wanazozifanya ni zile zile wanazofanya Madaktari na hususan upande wa Vijijini na Wilayani huko, walio wengi ni wao. Ninataka

nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya na kujiepusha na migomo inayoendelea nchini. *(Makofi)*

Na. 260

**Ongezeko la Vituo vya Kulelea Watoto Yatima Nchini**

**MHE. JOYCE J. MUKYA** aliuliza:-

Je, Serikali, inafanya uhakiki wowote wa kuhakikisha ubora wa Vituo vya kulelea watoto yatima nchini vinavyoongezeka, ili kubaini kama vyote vinatekeleza malengo yaliyokusudiwa, badala ya waanzilishi wake kuvitumia kujinufaisha kupitia migongo ya watoto wenye shida?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce John Mukya, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara na Idara za Serikali, Wadau wa Maendeleo na Taasisi binafasi, imakuwa ikihakikisha kuwa watoto walio katika mazingira hatarishi, wanapatiwa malezi, matunzo na ulinzi kwa kuzingatia viwango vya ubora unaotakiwa.

Katika kusimamia Vituo vya Kulelea Watoto Yatima, Wizara, inalo jukumu la kufanya usajili na kuvipatia leseni vile vinavyokidhi matakwa, kwa mujibu wa Sheria. Kupokea na kuhakiki Taarifa za utekelezaji wa Vituo, ili kuona maendeleo ya watoto na Vituo kwa ujumla. Hadi sasa, vipi Vituo vya Kulelea watoto Yatima na walio katika mazingira hatarishi 98 vilivyosajiliwa Kisheria na vinatoa huduma kwa watoto wapatao 3,958.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ubora wa huduma zinazotolewa katika Vituo vya Kulelea Watoto Yatima, Wizara, imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Vituo vya Kulelea Watoto walio katika mazingira hatarishi,  wakiwemo yatima kwa mwaka 2006. Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa Huduma za Malezi, Matunzo na Ulinzi kwa watoto walio katika Mazingira hatarishi kwa mwaka 2009.

Aidha, Wizara, imeandaa Kanuni kwa ajili, ya utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, ambazo zinatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa ongezeko la Vituo vya Kulelea Watoto Yatima hapa nchini, mwaka 2011 Wizara, kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto *(UNICEF),* imefanya tathmini ya makao ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, ili kuona hali halisi ya huduma zitolewazo kwa watoto katika makao hayo na iwapo hazikidhi masharti, kwa mujibu wa Sheria.

Matokeo ya tathmini hiyo, yamesaidia kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha huduma katika makao hayo, mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha Vituo vyote vinavyokidhi vigezo vipatiwe leseni na uendeshaji kwa mujibu wa Sheria na visivyokidhi vigezo vifungwe. Kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo kwa wamiliki na walezi wa vituo vya kulelea watoto yatima na Maafisa Ustawi, ngazi ya Halmashauri, kuhusu utoaji wa huduma zinazozingatia viwango vya ubora; mkakati huo, utaanza kutekelezwa mwaka 2012/2013.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni vigezo vipi vya msingi, vinavyowezesha kuanzisha vituo hivi Kisheria na kupata leseni?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vituo hivyo viweze kukudhi viwango vile, ni pamoja na uwepo wa watunzaji, uwepo wa nafasi za kutosha kwa ajili ya malazi na uwepo wa kuthibitika kuona kwamba, kuna chakula, kuna uwezekano wa kupata matibabu na kuna huduma za mawasiliano. Lakini vilevile, pale ambapo kunawezekana, basi kuna uhusiano kati ya hao watoto na familia zao kwa pale ambapo wanakuwepo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naomba kumwuliza swali moja dogo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, vipo Vituo vya Kulelea Watoto ambavyo ni vya binafsi na havikidhi vigezo, lakini vimekuwa vinaweka watoto maeneo yale. Na tumekuwa tunaona hata kwenye vyombo vya habari, watoto wanaishi katika mazingira magumu sana, wengine wanalala chini kwenye *floor,* wengine hawana vyakula, inakuwa ni kama ombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sasa Serikali, inaweza kuweka utaratibu maalum kuanzia kwenye ngazi za Vijiji, kabla ya mtoto kuwekwa kwenye Kituo, wahakikishe kwamba, vigezo vimekidhiwa kwenye vile vituo kwa kuepuka watoto hawa kuteseka?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kuna vituo vingi ambavyo havijakidhi vigezo na havikuweza kusajiliwa. Kwa jumla tulikuwa na vituo vilivyo, uchambuzi umevigundua vituo 282 na kati ya hivyo 99 tu, ndio ambavyo vimepata usajili na hivyo vingine vimo katika hatua ya kuweza kufuatiliwa ili vitakavyokuwa vimekidhi usajili, vinaweza kupata usajili; na vile ambavyo havitakidhi usajili hata baada ya kufuatiliwa, vyenyewe vitafungwa.

Na. 261

**Sheria ya Uanzishwaji Mamlaka ya Uhifadhi**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori kama vile, *Ngorongoro Conservation Authority,* imeonesha mafanikio makubwa katika kukuza utalii na uhifadhi wa maliasili katika eneo husika:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kuleta Bungeni Sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka za Uhifadhi katika mapori ya akiba ya wanyamapori yaliyopo hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustine Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Namba 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, kimempa Mamlaka Waziri wa Maliasili na Utalii kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. Mchakato wa uanzishaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania, umeanza na sasa uko katika hatua ya kuainisha muundo na kazi za Mamlaka hiyo.

Aidha, kikundi kazi kinachoshughulikia uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania, kimetembelea Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, ili kujifunza Muundo wa Mamlaka.

Kikundi kazi kilipata fursa ya kufahamu miundo ya kiutumishi, iliyopo katika Taasisi hizo na kukiwezesha kupendekeza muundo bora utakaotumika kwenye Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. Kazi ya kuainisha muundo na kazi za Mamlaka, unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2012.

Baada ya kukamilika kwa kazi hiyo, kwa maana ya muundo wa uongozi, itafuatiwa na kazi ya kutengeneza Sheria ya kuanzisha Mamlaka kwa kuzingatia muundo na kazi za Mamlaka kama itakavyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya Sheria ya Kuanzisha Mamlaka yataanza mwezi Oktoba, 2012 na kukamilika mwezi Disemba 2012. Rasimu ya Sheria, itawasilishwa Bungeni kwa kufuata taratibu na kanuni.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini pamoja na hayo, ninaomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Pori la Akiba la Kigosi, linakabiliwa na uhaba mkubwa wa watumishi, ambapo Pori hili lina ukubwa wa kilometa za mraba 9,000 na watumishi waliopo ni watumishi 30 tu. Je, Serikali, ina mpango gani kuongeza idadi ya Askari Wanyamapori ili Pori hilo liweze kulindwa dhidi ya majangili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, katika Pori hili la Akiba la Kigosi, hakuna mioundombinu ya barabara ambayo ingeweza kusaidia katika shughuli za utalii; naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa barabara na mahoteli ya kitalii katika eneo hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Augustino Masele, kama ifuatavyo:-

Moja, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Augustino Masele, kwamba, Pori la Kigosi pamoja na mapori mengine mengi nchini ambayo, yalianzishwa Kisheria, yana upungufu mkubwa sana wa watumishi. Yana uhaba mkubwa sana wa ubora wa miundombinu. Mapori mengine hayana kabisa barabara, mapori mengine makubwa yana watumishi 5, yana watumishi 10 na hii imesababisha Serikali, iamue kuanzisha mara moja Mamlaka ya Wanyamapori, ambayo pamoja na mambo mengine, itatatua hili tatizo sugu sana la mapato, vyanzo vya mapato vya kuendesha mapori haya yote ya akiba. Pori hili, amegusia suala la barabara na miundombinu mingine pamoja na uwekezaji. Mamlaka hii pamoja na mambo mengine, itakuwa na Mamlaka sahihi ya kuweza kuajiri, kujipangia viwango vya mapato na kuweza kuendeleza utalii ukiwepo uwekezaji katika maeneo haya. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009, iliitaka Serikali, kuwa imekamilisha mchakato wa uanzishwaji wa Mamlaka ya wanyamapori Tanzania. Je, ni sababu zipi za msingi zilisababisha Wizara, kutokutekeleza agizo la Sheria hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lembeli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Sheria ya Mwaka 2009 ya Wanyamapori, ilimpa Mamlaka Waziri wa Maliasili na Utalii, kuweza kuanzisha Mamlaka hii ya Wanyamapori. Serikali, ilichokifanya, jambo la kwanza, ni kuangalia muundo bora ambao utatumika kuanzisha Mamlaka hii. Mamlaka hii, tofauti na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* tofauti na Mamlaka kama ya Ngorongoro, Mamlaka hii, itakuwa imegusa maeneo mengi sana, ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo yana wanyama pori, itagusa maeneo ambayo, tunayaita Mapori ya Akiba na tunaendelea kuyatunza yaweze kukua. Ina maeneo mengi sana na Sheria hii, lazima iweze kuangaliwa vizuri kimuundo jinsi gani wataweza kuajiri wafanyakazi, lakini jinsi gani ile Kada ya Uhifadhi Wanyamapori, inaweza ikafanya kazi vizuri kwa kutumia utaratibu na uzoefu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Lembeli na Bunge lako Tukufu kwamba, Mamlaka hii, itaanzishwa.

Na. 262

**Kuboresha Elimu katika Shule za Kata Wilayani Geita**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Ziwa Rukwa, lina mamba wengi sana, lakini wananchi hawafaidiki na mamba hao zaidi ya mamba kuwajeruhi na kuwaua watu:-

(a) Je, Serikali, ina mpango gani wa kuwapunguza mamba hao kwa kuwavuna?

(b) Je, mamba hao wamewahi kuvunwa huko nyuma, na je, wananchi wa maeneo hayo walifaidikaje?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas malocha, Mbunge wa Jimbo la Kwela, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupata idadi itakayotuwezesha kupanga kiwango cha uvunaji, ili kukabiliana na tatizo la kuongezeka mamba kupita kiwango kinachotakiwa *(Carrying Capacity)* katika

Ziwa Rukwa, Wizara yangu imetenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili, ya kuhesabu namba nchi nzima, ikiwa ni pamoja na Ziwa Rukwa.

Katika kufanya hili, Wizara itapata takwimu sahihi zitakazotumika kupanga viwango vya uvunaji na hivyo kupunguza tatizo la mamba kujeruhi au kuua watu katika Wilaya ya Sumbawanga.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 hadi 2010, jumla ya mamba 220 walivunwa na kampuni ya *"Cossam Crocodile Farm"* katika Ziwa Rukwa. Uvunaji huo ulitoa ajira na fursa za biashara kwa wakazi wa maeneo yanayozunguka ziwa hilo.

Aidha, wananchi wa Wilaya ya Sumbawanga, walinufaika na mgao wa fedha za uwindaji wa wanyamapori zinazotolewa na Serikali, kwa Halmashauri za Wilaya ambazo hujumuisha pia ada za uwindaji wa mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi 8,800,000/= zilipatikana kutokana na uwindaji wa mamba 220 katika Ziwa Rukwa. Kati ya fedha hizo 25% kwa ajili, ya Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania *(TWPF),* 75% ilipelekwa Hazina na 25% ya fedha iliyokwenda Hazina, ilirudishwa tena Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali langu vizuri lakini ninalo swali. Kwa kuwa wapo wananchi ambao walishapata hasara kwa kujiruhiwa na mamba na kupata vilema

kama vile kukatwa mikono, miguu, vidole na wengine kupoteza maisha.

Je, Serikali inatoa fidia gani kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru tu kwa kuendelea kuzungumza na sisi Wizarani juu ya umuhimu wa kuweza kuanzisha huu utaratibu wa kuvuna hawa mamba na mwaka huu kuna sensa ya Taifa ya watu na kuna sensa ya nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ina utaratibu wa kutoa fidia mahali ambapo wananchi wamedhuriwa iwe na Mamba, iwe na Tembo lakini tumepokea malalamiko ya muda mrefu kwamba fidia hizi ni ndogo sana na tunaendelea na utaratibu wa kuangalia ni jinsi gani zitahuishwa au zitarekebishwa kwa kadiri Bajeti itakavyoturuhusu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata, Waheshimiwa Wabunge muda umetutupa mkono ingawa nitamwomba sana Waziri mwenye dhamana ya lugha ya Kiswahili atusaidie sana kuelewa matumizi ya hili neno tembo ndani ya ukumbi huu wa Bunge, ili tuwe tunalitumia kwa kadiri inavyotakiwa. *(Makofi)*

Na. 263

**Ubovu wa Barabara – Ileje**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (MHE. ALIKO N. KIBONA)** aliuliza:-

Wilaya ya Ileje, inaongoza kwa kiwango cha mvua nyingi na jiografia ya milima mingi, hivyo barabara zake huharibika mara kwa mara kwa kusombwa na maji ya mvua  na huwa na utelezi, hivyo kuhatarisha usalama wa abiria na mali  zao:-

Je, Serikali, haioni umuhimu wa kujenga barabara ya kutoka Kyimo *(KKT)* Rungwe, kupitia Vijiji vya Ikuti, Lusisi, Lubanda, Sange, Katengele, Kalembo hadi Ibungu na barabara ya kutoka Kasumulo Kyela hadi Isongolea, ili kuwaondolea mateso makubwa na  ya muda mrefu, wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Kyimo *(KKT)* Rungwe, kupitia Vijiji vya Ikuti, Lusisi, Lubanda, Sange, Katengele, Kalembo hadi Ibungu na barabara ya kutoka Kasumulo Kyela hadi Isongole, ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara yangu, kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mbeya.

Barabara zote ni za kiwango cha changarawe na zimekuwa zikifanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka, ili ziendelee kupitika wakati wote.

Aidha, toka mwaka 2007/2008 hadi 2011/2012, jumla ya shilingi milioni 2,336.164 kwa barabara ya Kyimo – Ibungu na shilingi milioni 264.250 kwa barabara ya kasumulo – Isongole, zimetumika kwa kuzifanyia matengenezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya, itaendelea kukarabati barabara hizi kwa kiwango cha chngarawe, ili kuhakikisha zinapitika majira yote ya mwaka. *(Makofi)*

Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 94.8 zimetengwa, kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara husika.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga hela kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizi. Je, kwanini usifikirie kujenga kwa lami kuliko kila wakati kujenga hela hili.

La pili, barabara ya kutoka Mbalizi mpaka Ileje Mjini ni barabara ambayo ni fupi kuliko barabara zote ambazo zinaelekea mjini Mbeya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa ili kuwaondolea shida au kero wananchi wa Ileje wanaokuja Mbeya? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anauliza kwanini barabara hizi zisijengwe kwa kiwango cha lami badala ya changarawe hii

tumefanya kulingana na uwezo wa Serikali tumeamua kwamba tuanze kujenga barabara kuu zile ambazo zinaunganisha miji mikuu ya mikoa halafu baadaye tutakuja kuongeza miji ya mikoa halafu baadaye tutakuja kuingia kwenye barabara za mikoa. Kwa hiyo, tunapanga kwa utaratibu huo.

Suala la barabara ya Mbalizi Ileje, kwamba ninachofahamu kama ni barabara ya mkoa basi itakuwa imepata fedha ya mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba sana mnisamehe, Mheshimiwa James Mbatia kwa heshima labda uliza swali la mwisho.

**MHE. JAMES MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwa kuwa barabara hizi za jimbo la Ileje zimetengenezwa kwa kiwango cha changarawe na Mheshimiwa Mbunge wa Ileje anaulizia mvua ambapo maji ndiyo adui mkubwa wa barabara.

Barabara nyingi za Ileje ziko kwenye miinuko ambapo mvua ikinyesha inasafisha changarawe na tatizo ni *routine maintenance* kwenye barabara hizi.

Je, Serikali haioni kwamba ni vyema barabara za Ileje kama ile inayotoka Bundani kwenda mpaka mlima Sheyo na Ibaba wakaweza kuzitengeneza hasa maeneo miinuko wakazitengeneza kwa material nyingine hata kama lami ni ya ghali wakatafuta *material* nyingine kama *Puzo lanner* na majimbo mengine kama ya Nkasi hapa Peramiho ili kuweza

kuhakikisha kwamba maeneo yote yenye utelezi yanakomaa vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hili la Peramiho amelisikia Mheshimiwa Waziri mwenyewe atalijibu baadaye, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna maeneo mengine katika wilaya ya Ileje ambayo ina miinuko mikali na pengine tungetafuta namna ya kuweza kutengeneza ili kusudi maeneo yale yaweze kupitika muda wote wa mwaka.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Sasa kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba tuna utaratibu ambao tumeshaupanga tayari wa kujenga barabara za lami, lakini maeneo ambayo ni korofi na *specific* na kama barabara ni barabara inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi tutaingilia namna gani tutaweza kuifanya. *(Makofi)*

Na. 264

**Ujenzi kwa Kiwango cha Lami Barabara ya Njombe**

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya lami kutoka Njombe (Itoni) hadi Ludewa (Manda)?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe Ludewa Manda yenye urefu wa kilomita 212 ni barabara kuu inayohudumiwa na wakala wa barabara mkoa wa Njombe. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kuna ujenzi kupitia wakala wa barabara ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami kilomita moja nukta tano, Ludewa Mjini na kazi za ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha barabara hii inatengenezwa na kupitika kwa urahisi jumla ya shilingi milioni 1,600 zimetengwa na Serikali ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 800 zimetengwa na Serikali kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hii kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Jumla ya shilingi milioni 800 zingine zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kuna matengenezo maalum ya barabara kuu changarawe kwa ajili ya kufanyia matengenezo maalum barabara hiyo ili iweze kupitika kwa urahisi katika majira yote ya mwaka.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sana mimi niseme kwa niaba ya wananchi wa Ludewa namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kututazama kwa namna ya pekee wananchi wa Ludewa na nimezungumza na wananchi wa Ludewa kwanza wanamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ujenzi na wanamtakia afya njema kwa hayo anayofanya kwa kuhakikisha kwamba Wilaya ya Ludewa inapata

barabara ya lami. Ombi lao ni moja tu sasa wanaomba ukipata nafasi uwatembelee wananchi wa Ludewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wanaomba uwatembelee hakuna swali lakini ombi hilo unalipokea Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipokea na nitakwenda Ludewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, sasa kabla hatujaingia agenda inayofuata naomba kwanza niwatambulishe wageni ambao wako ndani ya ukumbi huu wa Bunge kwa siku hii ya leo, ni hawa wanaofuata.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Profesa Makame Mbawala, ambao ni Dkt. Florence Turuka, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Patrick Makungu, yeye ni Naibu Katibu Mkuu, halafu wako wakuu wa idara vitengo vyuo na taasisi zake zilizoko chini ya Wizara hiyo. Ningeomba wasimame wote kwa ujumla wao. *(Makofi)*

Halafu tuna Dkt. Diwani Mruthu, Mwenyekiti wa Tughe Taifa, na tuna Bwana Ali Kiwenge, Katibu Mkuu Tughe Taifa. Tuna Bwana John Mchenya, Katibu wa Tughe Mkoa wa Dodoma, hawa ndiyo wageni wa Wizara nadhani leo tunaendelea na shughuli ya Wizara yenu nafikiri tutashirikiana vizuri na Waheshimiwa Wabunge.

Sasa wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine wageni hao kwanza kuna wageni wa Mheshimiwa Nassir Abdallah, hawa wageni wanatoka taasisi ya teknolojia ambao ni Ndugu Salim na Ndugu Mussa. Mheshimiwa Juma Nkamia anao wageni wake ambao ni wanafunzi wanne kutoka Chuo cha *Saint Augustine,* Mwanza wakiongozwa na Beatrice Thobias. Nadhani bado hawajaingia hapa ndani lakini tunawatambua kuwepo kwao. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Suzan Kiwanga, ambaye ni Miss Mkuha Kiwanga, ni binti wa Mheshimiwa Suzan, karibu tunashukuru.

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. Mgeni huyu ni kutoka TELESIS Dar es Salaam ambaye ni Mihayo Wilmo, halafu Baraka Mtunga na bwana Rajabu Katunda hawa ni wageni wa Mheshimiwa wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Henry Shekifu, Mbunge wa Lushoto, huyu ni Ndugu Gaston Katindila, ambaye ni mwanafunzi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, hao ni Moses Mollel, Mwenyekiti wa Kijiji cha Lekelimuni - Siha. Kuna mgeni mwingine anaitwa Paul Zacharia huyu ni Mshili wa vijana kutoka Siha, sasa maana ya Washili Mheshimiwa Mwanri utatuambia baadaye. Kuna pia Raphael Sitilu Mwenyekiti wa tawi Siha na Joseph Oleso Lengei, Mwenyekiti Mstaafu Siha. (Makofi)

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 81 pamoja na walimu wao kutoka shule ya msingi

Chinangali Dodoma, tunao walimu nane, kutoka *St. Peter Claver High School Dodoma* wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Msaidizi Ndugu Joseph Badokufa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hii ni shule ambayo iko hapa hapa Dodoma na mimi naomba ku-*declare interest* hata mwanangu anasoma katika shule hiyo kwa kweli ni shule nzuri sana. Halafu tuna wanafunzi 85 pamoja na walimu wao kutoka shule ya Ihumwa Dodoma nadhani bado hawajaingia. Tuna wanafunzi 55 pamoja na walimu wao kutoka shule msingi Kiwanja cha Ndege Dodoma. Tuna wanafunzi 24 kutoka *St. Ignash Isleth London College United Kingdom* wanafunzi 24, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ni Wabunge wako hapa Bungeni lakini nina matangazo yafuatayo. Tangazo la kwanza, Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga anawaomba Wabunge wote waliofunga Swaumu ndani ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani kukutana katika kikao kifupi kitakachofanyika leo katika ukumbi wa Msekwa saa saba mchana baada ya kipindi cha Bunge.

Kikao hicho kitahusu utaratibu wa futari maalum ndani ya mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Kwa hiyo ninaomba Waheshimiwa Tangazo hilo ni muhimu mhudhurie.

Nina tangazo lingine la kazi, Mheshimiwa Mgimwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, anaomba tafadhali niwaomba wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ya kwambe

leo tarehe 25 Julai, 2012 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo na kikao hicho kitafanyika ukumbi Namba 231 jengo la Utawala gorofa ya pili. Kwa hiyo wajumbe wa Kamati naomba mhudhurie kikao hicho bila kukosa.

Halafu nina tangazo jingine toka kwa Mheshimiwa Seleman Jumanne Zedi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Nishati na Madini, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo Jumatano, tarehe 25 Julai, 2012 kuanzia saa saba mchana, Ukumbi Namba 227 gorofa ya pili jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge tangazo jingine nimeombwa hapa niwatangazie Wabunge wote wanaotokea majimbo yenye hazina ya madini, mafuta na gesi pamoja na wengine wenye *interest* kwamba kuwa leo saa saba mchana baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge wakutane Uku mbi wa Pius Msekwa C, ili kuzungumzia masuala yanayohusiana na maliasili hizo. Kwa hiyo, Wabunge wanatoka maeneo haya wameombwa pia wakutane huko.

Nimeombwa nitangaze kwamba Waheshimiwa Wabunge wanahamasishwa kutumia bidhaa za Azam kwa wingi kadri inavyowezekana, wanasema kwa sababu bidhaa hizo zinasaidia sana katika kuweka miili sawasawa, kujenga afya na imeshauriwa kwamba washabiki wa Simba watumie zaidi bidhaa hizo za Azam. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa matangazo hayo, naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Zungu ili aendelee na shughuli zilizobakia kwa siku ya leo, mimi ninashughuli nyingine za vikao. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Zungu aje aendelee!

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba mwongozo wa kiti chako kuhusu jambo lililotokea mapema kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) ya Kanuni za Kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 3/7/2012 baada ya kukamilisha hoja ya Wizara ya Sheria na Katiba, Mwenyekiti aliagiza kwamba Kamati ya Maadili, Haki na Kinga za Bunge ikae kwa haraka na nina *Hansard* inayosema Kamati ikae kwa haraka ili kujadili kauli iliyokuwa imetolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utaratibu wa uteuzi wa Majaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe utakuwa shahidi maneno mengi sana yalizungumzwa hapa kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani imedhalilisha Majaji, imetukana na kadhalika na Mwenyekiti aliagiza kwamba Kamati ikae haraka iwezekanavyo ili hii kauli ichunguzwe na taarifa iletwe Bungeni. Sasa leo ni tarehe 25/7/2012, siku 12 zimepita lakini Kamati haijakutana na mtuhumiwa hajapewa taarifa yoyote

kwamba anahitajika kwenda kujieleza na wananchi wanaosikiliza Bunge hili wanabaki na sitofahamu kwamba pengine kweli Mheshimiwa Lissu alitukana Majaji na kuwadhalilisha na maneno mengine yote yaliyozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, tufanyaje?

**MWENYEKITI:** Kuna mwingine yeyote mwenye mwongozo, taarifa au kanuni? *(Kicheko)*
Mheshimiwa Tundu Lissu nimepokea mwongozo wako na nitautolea maamuzi kipindi muafaka. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 - Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya kuhusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2011/2012 na Malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Aidha, naliomba Bunge lako

Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili Bajeti ya Serikali. Naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu kuwa azipokee na kuzilaza pema roho za Waheshimiwa Wabunge waliotangulia mbele ya haki tokea mkutano wa Bajeti wa mwaka 2011/2012 ulipofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika Baraza la Mawaziri kufuatia mabadiliko aliyofanya mwezi Mei, 2012: Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa (Mb), kuwa Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijaribu Muhongo (Mb), kuwa Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza (Mb), kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb), kuwa Waziri wa Uchukuzi; Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara (Mb), kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki (Mb), kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda (Mb), kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. *(Makofi)*

Pia, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali: Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene (Mb), Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Seif Suleiman Rashid (Mb), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb), Wizara ya Nishati na Madini; Mheshimiwa January Yusuf Makamba (Mb), Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Charles John Tizeba (Mb), Wizara ya Uchukuzi; Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla (Mb), Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo; Mheshimiwa Stephen Julius Maselle (Mb), Wizara ya Nishati na Madini; na Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb), Wizara ya Maji. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na walioteuliwa katika kipindi cha mwaka uliopita kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki na Bunge la Afrika. Ni matumaini yangu kuwa watatuwakilisha vyema kwa maslahi na manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba za bajeti kwa mwaka 2012/13. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) na Waziri wa Fedha zimetoa dira, mwelekeo na malengo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013. Aidha, hotuba hizo zimeelezea mafanikio, changamoto, matukio mbalimbali na hali ya uchumi wa Taifa letu kwa mwaka 2011/2012 na mipango na matarajio kwa

mwaka 2012/2013. Aidha, nawashukuru Mawaziri wote walionitangulia kwa kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zinahusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba uniruhusu kutumia fursa hii kukumbuka tukio zito na la majonzi lililolipata Taifa tarehe 18 Julai 2012 wakati Bunge hili likiendelea, pale ambapo Taifa liliwapoteza watu wengi na wengine wengi kujeruhiwa kupitia ajali ya Meli ya Mv Skagit karibu na Unguja. Ninapenda kuungana na Watanzania wenzangu kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao katika ajali hiyo. Pia ninawaomba waendelee kuwa na moyo wa ustahimilivu wakati wote wa msiba huu mkubwa kwa nchi yetu. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Kwa wale waliopata majeraha na kuumia kwa namna yoyote, ninawatakia kupona haraka ili waweze kuungana na Watanzania wengine katika kuijenga nchi yetu na kuhudumia familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za pekee kwa wale wote walioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi kilichopita na ambao wamewezesha kuandaa mpango wa mwaka wa fedha 2012/2013 na kuboresha hoja ambayo naiwasilisha katika hotuba hii. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa January Yusuph Makamba (Mb.), Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Dkt. Florence Martin Turuka, Katibu Mkuu; Dkt. Patrick James Makungu, Naibu Katibu Mkuu;

watendaji wote katika Wizara, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika kufanikisha uwasilishaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa namna ya pekee Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), kwa ushauri wao unaotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa tija na ufanisi zaidi. Aidha, napenda kumshukuru kipekee sana Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) ambaye ni Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii ninayoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inayo dhamana ya kusimamia, kuimarisha na kuendeleza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kwa pamoja viweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi. Vilevile, Wizara inayo dhamana ya kusimamia na kutoa miongozo kwa Taasisi, Mashirika, Tume na Kampuni ambazo zinafanya kazi chini yake. Taasisi hizo ni:

(i) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;
(ii) Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya;
(iii) Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;
(iv) Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania;

(v) Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia;
(vi) Shirika la Posta Tanzania;
(vii) Kampuni ya Simu Tanzania;
(viii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na
(ix) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imezingatia miongozo ifuatayo; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2011/2012 – 2015/2016 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010–2015. Vilevile, Wizara inazingatia Sera, Mikakati, Sheria na Kanuni na Miongozo mbalimbali inayoongoza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu na Sera ya Taifa ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mipango na bajeti ya mwaka 2011/2012. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya Sh. 64,017,516,000. Kati ya fedha hizo, Sh. 23,799,259,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo za matumizi ya kawaida Sh. 14,765,658,000 zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na Sh.9,033,601,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za

maendeleo zilizoidhinishwa zilikuwa Sh. 40,218,257,000 ambapo fedha za ndani zilikuwa Sh.38,195,679,000 na fedha kutoka nje zilikuwa Sh.2,022,578,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yaliyotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake katika kipindi cha mwaka 2011/12 ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawasiliano. Uwekezaji, Ajira na Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano. Mawasiliano ni sekta inayokua kwa kasi hapa nchini na duniani kote na imekuwa ikichangia kikamilifu katika maendeleo ya mataifa mbalimbali na pia imekuwa ikiwezesha sekta nyingine kukua na kuboresha maisha ya wananchi wake. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi nchini, sekta ya mawasiliano ilikua kwa asilimia asilimia 20.1 (mwaka 2007), asilimia 20.5 (mwaka 2008), asilimia 22 (mwaka 2009), asilimia 21.5 (mwaka 2010) na asilimia 19.0 (mwaka 2011). Hata hivyo, takwimu hizi zilitegemea zaidi takwimu na hesabu zilizowasilishwa na watoa huduma za simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mchango wa sekta kwenye pato ghafi la taifa (*GDP*) umekuwa ukiongezeka kwa kasi ndogo isiyowiana na kukua kwa sekta yenyewe. Kwa mfano kuanzia mwaka 2007 mchango wa sekta katika pato ghafi la Taifa ulikuwa ni asilimia 2.1 (mwaka 2007), asilimia 2.3 (mwaka 2008), asilimia 2.7 (mwaka 2009) asilimia 3.1, (mwaka 2010) na asilimia 3.4 (mwaka 2011), ikilinganishwa na uchangiaji wa asilimia 9 na 5.2 katika nchi za Kenya na Uganda sawia kwa mwaka 2010. Hata hivyo, takwimu hizi

zinategemea zaidi takwimu na mahesabu yanayowasilishwa na watoa huduma wenyewe. Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na wadau wengine iko katika mchakato wa kuboresha upatikanaji wa takwimu hizi ikiwemo uwekaji wa mtambo wa kuhakiki mawasiliano *(Traffic Monitoring System - TMS)* ambao hutumika pia kupata takwimu zenye uhakika zaidi za mapato yanayotokana na huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa uwekaji wa mtambo huu ambao unatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 umekwishaanza ambapo tathmini ya makampuni yaliyoonyesha nia ya kujenga mtambo huu ilifanyika mwezi Juni 2012, na Kampuni zilizoonyesha uwezo wa kufanya kazi hiyo zimeombwa kuwasilisha taarifa zao za kitaalamu na kifedha (*technical* na *financial proposals)* kwa ajili ya hatua za kupata Kampuni itakayofanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta hii ya mawasiliano umeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa katika miaka ya hivi karibuni. Uwekezaji huo uko katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa minara ya mawasiliano, uwekaji wa vifaa vya mawasiliano na ubunifu wa bidhaa mpya za huduma za mawasiliano ikiwemo huduma ya kibenki. Kwa kutumia mfano wa uwekezaji katika miundombinu kwa makampuni matatu (3) ya simu za mkononi yanayotumia teknolojia ya *GSM* kati ya mwaka 2001 na Juni, 2012, viwango vya uwekezaji vimetofautiana baina ya makampuni kutoka TSh Bilioni 405 na Trilioni 1.13 kwa makampuni mawili na Dola Milioni 117 kwa

kampuni moja jingine. Aidha, ujenzi wa minara umefanyika katika vituo vipatavyo 3,304 kote nchini. Vituo hivi ni pamoja na minara inayotumiwa na mtoa huduma mmojammoja na ile inayochangiwa kwa ushirikiano na watoa huduma kadhaa na ile iliyojengwa juu ya mapaa ya nyumba. Katika nyanja za ajira, makampuni manne (4) kati ya mwaka 2001 na 2012 yametoa jumla ya ajira 597,856.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mchakato wa kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni endelevu na unatekelezwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi. Mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa umebuniwa kuwa na awamu tano (V). Utekelezaji wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa awamu ya I na II umekamilika. Awamu ya I ilianza Februari, 2009 na kukamilika Juni, 2010 wakati awamu ya II ilianza Agosti, 2010 na kukamilika mwezi Juni, 2012. Kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa awamu ya I na II kunaufanya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuwa na jumla ya kilomita 7,560 na umeunganisha Makao Makuu ya Mikoa ya Tanzania Bara. Aidha, ujenzi wa Mkongo huu umeweza kuunganisha baadhi ya Wilaya hususan zile zilizo ndani ya Makao Makuu ya Mikoa. Andiko kwa ajili ya awamu ya III itakayohusu kukamilisha kwa uunganishwaji wa Makao Makuu ya Wilaya zote, ujenzi wa viunganisho muhimu *(Missing links, IP-MPLS Service layer)* na Vituo Vikubwa vya Kuhifadhi Kumbukumbu *(Data Centres)* limekamilika. Juhudi za kutafuta fedha za utekelezaji wa awamu ya III zinaendelea. Aidha, awamu ya IV inahusu ujenzi wa mikongo ya mijini *(Metro Networks).* Ujenzi wa mikongo

ya mijini unaendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano na imekamilika katika jiji la Dar es Salaam. Awamu ya V inahusu uunganishaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo mengine ya matumizi ukiacha yale ambayo tayari yameunganishwa ikiwa ni pamoja na kumfikia mtumiaji wa mwisho *(Last Mile Broadband Connectivity)* na maandalizi yake yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa awamu hizi mbili, kunaufanya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuwa na mizunguko *(rings)* mitatu; ya Kaskazini *(Northern Ring),* Kusini *(Southern Ring)* na Magharibi *(Western Ring)*. Mfumo huo wa ujenzi, unaufanya Mkongo kuwa na huduma ya uhakika na isiyotetereka kirahisi kwani hata pale inapotokea upande mmoja wa Mkongo kutoweza kutoa huduma kutokana na hitilafu, huduma zitaendelea kupatikana bila ya matatizo yoyote kupitia pande nyingine ambazo hazina hitilafu hadi hapo hitilafu itakapopatiwa ufumbuzi. Aidha, kimataifa, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeunganishwa na mikongo ya baharini ya *SEACOM, EASSy* na *SEAS* unaoendelea kujengwa na ambao utatuunganisha na Sychelles. Mkongo huu pamoja na ile ya mikongo mingine ya baharini inatoa huduma za maunganisho ya mawasiliano kwa nchi zote za jirani ambazo hazipakani na bahari na kuzipa huduma mbadala zile zilizo na ufukwe wa bahari. Nchi hizi ni pamoja na Rwanda (kupitia Rusumo), Burundi (kupitia Kabanga na Manyovu), Zambia (kupitia Tunduma), Malawi (kupitia Kasumulo), Uganda (kupitia Mutukula). Vilevile, huipa

huduma mbadala nchi ya Kenya ambayo ina ufukwe wa bahari (kupitia Namanga, Sirari na Horohoro).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Juni, 2012, Kampuni 18 za mawasiliano zimeunganishwa na mkongo wa Taifa. Kati ya hizo 6 ni kampuni za ndani *(TTCL, Airtel, Tigo, ZANTEL, Iffinity na Simbanet).* Aidha, Kampuni za Simu za Malawi (MTL), Burundi (UCOM), Rwanda (MTN), na Zambia (MTN na Airtel) zinatumia huduma ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umesaidia kupunguza gharama za mawasiliano nchini na tunatarajia gharama hizo kuendelea kupungua zaidi kadiri muda unavyoenda. Nitatoa mfano wa jinsi gharama zilivyoshuka za huduma za mawasiliano zitolewazo na Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) ambayo tayari imeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mwaka 2009, kabla ya Mkongo, gharama ya huduma za *Broadband 2 Giga Byte* kwa ajili ya wateja wadogo ilikuwa ni TSh 100,000. Hivi sasa gharama ya huduma hiyo ni Tsh.30,000, ikiwa ni unafuu wa asilimia 70. Hali kadhalika, gharama za huduma za *Broadband 4 Giga Byte* ilikuwa ni Tsh.200,000 wakati hivi sasa ni Tsh.60,000 ikiwa ni nafuu kwa asilimia 70. Aidha, gharama za huduma za *Broadband 40 Giga Byte* kwa makampuni katika mwaka 2009 ilikuwa Tsh.1,000,000 wakati hivi sasa ni Tsh. 360,000 kwa huduma hiyo ambayo ni nafuu kwa asilimia 64. Gharama kwa huduma ya *Dedicated 2 Mega Bits per second* (*2Mbps*) ilikuwa Tsh.12,400,000

mwaka 2009 wakati hivi sasa ni Tsh.3,620,000 ikiwa ni nafuu kwa asilimia 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kusafirisha mawasiliano kwa masafa marefu (Mkoa moja hadi mwingine) gharama zimeshuka kwa zaidi ya asilimia 98. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kabla ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuanza kutumika, gharama za kusafirisha mawasiliano zilikuwa zinategemea umbali (Kilomita). Baada ya kuanza kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, umbali si kigezo cha gharama za kusafirisha mawasiliano. Kwa mfano, kabla ya kuanza kutumia Mkongo, gharama ya kusafirisha mawasiliano ya ukubwa wa *2 Mega bits per second* (*2Mbps*) kwa umbali wa Kilomita 451 hadi 500 ilikuwa Dola za Kimarekani 9,410 kwa mwezi wakati hivi sasa ni Dola za Kimarekani 158.7 kwa mwezi ikiwa ni nafuu kwa asilimia 98. Kwa upande wa simu za mkononi, gharama zimepungua kutoka TSh.147 kwa dakika mwaka 2009 hadi kufikia TSh.93 kwa dakika mwaka 2010 na TSh.51 kwa dakika mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa kampuni za mawasiliano kuunganisha huduma zao za mawasiliano kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kunufaika na huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuboresha huduma mbalimbali za mawasiliano na hivyo kupanua wigo wa kutoa huduma mbalimbali kwa wateja wao na pia kuchangia zaidi katika kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii wananchi kwa kupitia huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF).* Katika jitihada za Serikali kupeleka huduma za mawasiliano hadi vijijini, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*). Utafiti umefanyika wa awali ambao umebaini maeneo 239 yenye uhitaji mkubwa wa mawasiliano ambayo Mfuko utaanza kuyapatia ufumbuzi. Aidha, mwezi Julai 2011 Mfuko ulipokea taarifa za maeneo ya vijiji 2,175 yasiyo na mawasiliano kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Taarifa hizi zimetoa tathmini ya maeneo yasiyo na mawasiliano. Katika hatua ya awali, Mfuko umepeleka taarifa hizi kwa watoa huduma za mawasiliano ili waweze kuboresha mawasiliano katika maeneo yaliyoainishwa. Mshauri Mwelekezi anazifanyia kazi taarifa hizi ili kupata njia bora ya kuwashirikisha watoa huduma za mawasiliano kushiriki kwa ufanisi katika kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kushirikisha Mshauri Mwelekezi katika juhudi hizi inafuatia kutopatikana watoa huduma ambao wangeweza kuanza kupeleka huduma katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara baada ya zabuni ya kufanya kazi hiyo kutangazwa mwezi Novemba 2011 na kukosekana kwa mshindi kutokana na ruzuku iliyopendekezwa katika kupeleka mawasiliano katika sehemu hizo kuwa ndogo ikilinganishwa na gharama zilizopendekezwa na Wazabuni za upelekaji mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali. Umoja wa Mawasiliano Duniani (*ITU*) umeazimia kusitisha matumizi ya teknolojia ya utangazaji ya analojia ifikapo

tarehe 7 Juni, 2015 ili kuhakikisha kuwa teknolojia pekee itakayotumika kwa utangazaji ulimwenguni kote ni ile ya dijitali. Aidha kufuatia uamuzi huo, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) zimeazimia kusitisha matumizi ya teknolojia ya analojia ifikapo Desemba mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, maandalizi yote muhimu kuwezesha mabadiliko haya ya teknolojia yanaendelea kufanyika. Baadhi ya mambo yaliyokwishafanyika na yanayoendelea kufanyika ni pamoja na: kufanya mapitio na kuboresha sheria ambapo uandaaji wa kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (*EPOCA*) ya mwaka 2010 inayotambua mabadiliko hayo ulikamilika mwezi Desemba, 2011. Kanuni hizi zitawezesha utekelezaji wa majukumu mbalimbali katika kufanikisha mabadiliko haya ya teknolojia ya utangazaji. Hadi sasa, kampuni tatu (3) za *Agape Associates Limited, Basic Transmissions Limited* na *Star Media (T) Limited* zimepewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuwezesha urushaji wa matangazo ya televisheni katika mfumo wa dijitali kupitia vifaa maalumu vya kielekitroniki vinavyojulikana kama ving'amuzi. Aidha, ili kuwezesha wananchi wote wanaotumia televisheni kumudu mabadiliko haya, Serikali katika mwaka wa fedha 2012/13 imeondoa kodi kwenye ving'amuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za maendeleo ya sekta ya utangazaji nchini zinaonyesha kuwa eneo la nchi linalopokea matangazo kupitia televisheni kwa kutumia teknolojia iliyopo ya analojia ni asilimia ishirini

na nne (24%). Wakati huohuo, hadi kufikia hivi sasa eneo la nchi linalopokea matangazo ya televisheni kupitia teknolojia ya dijitali ni asilimia ishirini (20%). Hii inalifanya eneo linalopata matangazo ya televisheni hivi sasa lililo kwenye teknolojia ya dijitali kuwa ni asilimia themanini (80%). Ni matarajio ya Serikali kuwa, ifikapo Desemba 2012 eneo lote linalofikiwa matangazo ya televisheni kuwa litakuwa linapata matangazo ya dijitali. Jitihada zaidi zitaendelea pia kufanywa kufikisha matangazo ya televisheni ya dijitali katika maeneo mengine ambayo hayajafikiwa kabisa na matangazo ya televisheni hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ambayo tayari imefikiwa na matangazo ya dijitali ni pamoja na Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Dodoma. Katika awamu inayoendelea hivi sasa, makampuni husika yanaendelea kufunga mitambo ya dijitali katika Mikoa ya Shinyanga, Morogoro, Mara, Iringa na Kagera ambapo awamu inayofuata itamalizia ufungaji katika Mikoa iliyobaki. Zoezi hili linaratibiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambapo moja ya kigezo ni kuhakikisha kuwa mitambo inayowekwa inakidhi viwango vya ubora. Katika kipindi cha mpito hadi Desemba 2012, matangazo ya televisheni yataendelea kutolewa kwa mifumo yote ya analojia na dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kuratibu Mabadiliko ya Teknolojia imeandaa mpango wa kuelimisha Umma ambapo utekelezaji wake tayari umeanza mapema mwaka huu. Elimu kwa Umma inaendelea kutolewa kwa wananchi katika maeneo

mbalimbali nchini juu ya maana halisi ya mabadiliko haya, kuwaondolea hofu iliyotanda kuhusu mabadiliko haya na kuwaelimisha mambo wanayotakiwa kufanya ili kuendelea kupata matangazo ya televisheni. Aidha, elimu hii imekwishatolewa katika Taasisi mbalimbali ikiwemo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Elimu hii inaendelea kutolewa katika maeneo na kwa vikundi mbalimbali nchini kujenga uelewa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anuani za makazi za simbo za posta. Tanzania imeanza kutekeleza mfumo mpya wa anuani za makazi na simbo za posta. Utekelezaji huo ulianza katika Kata nane (8) za Manispaa ya Arusha ambapo uzinduzi rasmi ulifanyika mwezi Januari 2010. Aidha, utekelezaji pia umefanywa katika Kata nane (8) za Manispaa ya Dodoma. Uzinduzi wa utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi kwa jiji la Dar es Salaam ulifanywa mwezi Novemba 2011 na juhudi zinafanywa kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo huu kwa jiji la Dar es Salaam. Kutokana na umuhimu wa jiji la Dar es Salaam, maandalizi mahsusi yanakamilishwa katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi na simbo za posta katika jiji la Dar es Salaam unafanywa kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kuhakikisha kuwa kila mwananchi ulimwenguni anakuwa na anuani kamili, Umoja wa Posta Duniani (*Universal Postal Union*) katika Mkutano wake Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2012 huko Doha, Qatar agenda mojawapo itakayozungumzwa ni uhamasishaji

wa Mfumo wa Anuani za Makazi kutumika katika nchi zote wanachama wa umoja huo. Napenda kulijulisha rasmi Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imepewa heshima kubwa katika suala hili na Umoja wa Posta Duniani ambapo Mheshimiwa Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka (Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ameteuliwa kuwa Balozi Maalum wa Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta. Hii inatokana na juhudi kubwa ambazo amekuwa akizifanya katika kuhakikisha kuwa kila mtu ulimwenguni anakuwa na anuani kamili. Kutokana na uzoefu wake katika jambo hili, Mheshimiwa Prof. Tibaijuka ameombwa kuwa mzungumzaji na mhamasishaji wa mfumo huo kwa nchi wanachama ambazo bado hazijaanza kutekeleza mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe wito kwa wadau wote kuendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Wizara yangu ili Tanzania iweze kuutekeleza kwa ufanisi mfumo huu ambao una manufaa makubwa. Miongoni mwa manufaa hayo ni pamoja na: kutoa utambulisho wa kila mwananchi na mkazi wa Tanzania kupitia anuani ya makazi; kutoa utambulisho kwa urahisi kwa mali zisizohamishika; kupanua wigo wa shughuli za kibishara unaozingatia maendeleo ya kiteknolojia na utandawazi; kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii kiuchumi na utoaji wa huduma za dharura na maafa (uokoaji, zimamoto, na kadhalika). Mfumo huu vilevile, utasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa, kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kurahisisha ulipaji wa gharama za huduma mbalimbali za kiserikali, kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi na simbo za posta unafanywa kwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na utoaji wa elimu kwa wadau wa Mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta. Utoaji wa Elimu umefanyika katika ngazi mbili; kwanza ni kwa viongozi wa Wizara na Taasisi zinazoshiriki katika Mradi na Pili kwa wadau nje ya Mradi. Katika sehemu hii ya pili, Mamlaka imeendesha warsha, mikutano ya hadhara, vipindi vya luninga na redio, uchapishaji wa vijarida na vipeperushi na pia imetumia wasanii kufikisha ujumbe wa Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya TEHAMA. Mwezi Juni, 2012, Serikali ya Tanzania kwa kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imeridhia kuundwa kwa Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT Commission*). Uanzishaji wa Tume hii ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 inayoelekeza kuundwa kwa chombo mahsusi kitakachoratibu masuala ya TEHAMA. Pamoja na masuala mengine, Tume hii itakuwa na majukumu yafuatayo: (i) Kutambua fursa za uwekezaji, kutoa ushauri, kuvutia, kuendeleza na kushiriki kwenye uwekezaji katika TEHAMA, hususan kwenye miundombinu na matumizi *(applications- software and hardware development)* ya TEHAMA; (ii) Kuibua, kutekeleza, kusimamia, kuratibu na kuendeleza program za kitaifa za TEHAMA kwenye maeneo ya Rasilimaliwatu, miundombinu na matumizi ya TEHAMA; (iii) Kusimamia Usalama wa Matumizi ya TEHAMA

(*Cyber Security*) na Viwango; (iv) Kuendeleza uzalishaji wa bidhaa za TEHAMA (*soft and hardware*) na kupanua huduma za kibiashara katika TEHAMA (*Business Processes Outsourcing - BPOs*); na (v) Kushiriki katika kuandaa mipango na programu za kitaifa za kuendeleza TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa "*Video Conferencing*". Huduma hii ni muhimu katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu Serikalini kwa kupunguza gharama na muda unaotumika katika mawasiliano na vyombo vya usafiri. Kwa kutumia teknolojia ya *Video Conferencing*, viongozi/watendaji na wataalam wanaweza kufanya kazi zao kwa kushirikiana na kuwasiliana na wadau wengine wakiwa katika sehemu zao za kazi bila ya kulazimika kusafiri kutoka sehemu zao za kazi na kwenda sehemu zingine na hivyo kupunguza gharama za usafiri na pia muda ambao ungetumika kusafiri kwenda katika sehemu za mikutano. Pande mbili au zaidi zitaweza kukutana na kufanya mazungumzo kwa kuonana kwa kutumia teknolojia ya *video conference* kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Tayari majaribio yamefanyika na yameonyesha mafanikio makubwa na hivi sasa hatua zinakamilishwa za kufunga vifaa vya mawasiliano ya aina hiyo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na ofisi zote za Maafisa Tawala wa Mikoa hapa nchini ili huduma hiyo izinduliwe na kuanza kutumika rasmi kabla ya mwisho wa mwaka 2012. Aidha, vifaa vyote vinavyohitajika vimepelekwa katika ofisi hizo na kazi ya kuvifunga inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) inasimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za Mawasiliano ili kuhakikisha kuwa watumiaji wa huduma za Mawasiliano wanapata huduma bora. Ili kufanikisha hili, Mamlaka pia inahakikisha kuwa wananchi wanafahamu utaratibu wa kuwasilisha malalamiko yao. Elimu hii hutolewa kupitia semina mbalimbali, vyombo vya habari na machapisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, *TCRA* imeanzisha na inasimamia miradi na programu mbalimbali zinazolenga kuboresha mawasiliano nchini. Baadhi ya mambo yanayosimamiwa na *TCRA* ni pamoja na mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta na Kituo cha Uandikishaji wa Majina Miliki (Tanzania *Network Information Center- tzNIC*). (*Country Code Top Level Domain-ccTLD*) kwa ajili ya matumizi ya tovuti na anuani pepe Tanzania. Vilevile, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inasimamia uanzishwaji wa Kikosi Maalumu cha Ulinzi wa Kieletroniki (*Computer Emergency Response Team - CERT*) kitakachohusika na uhakiki wa usalama katika matumizi ya TEHAMA hapa nchini. Kikosi hiki kitakuwa na wataalam wenye weledi wa juu kuhusu usalama wa mitandao ya mawasiliano (*Cyber Security*) na kimekwishaanza kutekeleza majukumu chini ya uratibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta.

Mheshimuwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu Tanzania. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imelipa Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) kiasi cha TSh. 1,774,800,000 na hivyo kumaliza deni la Serikali kwa *TTCL* kufuatia huduma zilizotolewa na Kampuni hiyo kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Malipo hayo yameiwezesha *TTCL* kulipa deni la *SEACOM* na kulipia mtambo mpya wa ankara za mawasiliano (*Billing System*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya *TTCL* kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2011 yamefikia shilingi bilioni 89, ikilinganishwa na shilingi bilioni 80 katika kipindi kama hicho mwaka 2010/2011. Ongezeko hili kwa kiasi kikubwa limetokana na *TTCL* kupanua utoaji wa huduma za mtandao wa mawasiliano *(Backbone Network Services)* wenye ubora wa hali ya juu unaotumia teknolojia ya kisasa ya *Next Generation Network (NGN).* Huduma muhimu zinazotolewa na *TTCL* ni pamoja na mawasiliano ya simu, *data* na *video*. Huduma hizi kwa ujumla wake hivi sasa zimefikishwa kwenye Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania na juhudi zinaendelea kuzisambaza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba *TTCL* haipati tena tatizo la kutoa huduma kwa taasisi za Serikali pasipo kupata malipo yake kwa wakati, utaratibu maalum umewekwa wa kukusanya mapato kutokana na huduma zinazotolewa. Hivi sasa *TTCL* hukusanya ankara za simu kwa kiasi kinachofikia asilimia 96 ya gharama ya huduma wanayotoa. Lengo ni kufikia asilimia 100 ya makusanyo kwa huduma wanazozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL* kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, imeweza kupanua mtandao wake wa intaneti na simu kwa kuwaunganisha wateja wake wakubwa. Wateja hao ni pamoja na: *National Microfinance Bank,* Benki Kuu, TAKUKURU, Wizara ya Fedha, Ofisi za Bunge – Dar es Salaam na Dodoma, TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Wizara ya Mambo ya Ndani, *Nelson Mandela African Institute of Science and Technology*, *Dar es Salaam Institute of Science and Technology (DIT), Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC), Saint Augustine University of Tanzania (SAUT)* na Chuo cha Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, *TTCL* imeanza kufanya majadiliano na Kampuni ya *NEC Corporation* ya Japan ili kuingia ushirikiano wa kibiashara na *TTCL* kwa lengo la kufikisha mawasiliano kwa watumiaji wa mwisho (*last mile connectivity*). Hatua hii ni matokeo ya mkutano wa uwekezaji kwa nchi za *SADC* uliofanyika Japan ambapo Wizara ilihudhuria na kuwasilisha maeneo ya uwekezaji katika sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania (*TPC*) limeendelea kuimarika kiutendaji na kiufanisi katika kutoa huduma za kiposta nchini na kimataifa. Tathmini iliyofanywa na Umoja wa Posta Duniani (*UPU*) mwaka jana kuhusiana na ubora wa huduma umeipa Shirika la Posta cheti cha “*Bronze*”. Shirika la Posta Tanzania ni moja ya Mashirika sita (6) Afrika yaliyotunukiwa vyeti hivyo ambavyo vitatolewa kwenye Mkutano wa Umoja huo Doha Qatar mwezi Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta katika jitihada zake za kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA pamoja na kuunganisha ofisi za Posta zote za Wilaya katika Mtandao wa Kielektroniki wa Posta, Ofisi 47 ngazi ya Wilaya zimeunganishwa kwenye mtandao wa kompyuta. Aidha, vituo vya intaneti 10 vimezinduliwa na kufanya idadi ya vituo vya intaneti katika Shirika kuwa 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta linaendelea na jitihada za kupanua huduma zake, lengo ni kufikisha huhuma zake kwa wananchi wa vijijini. Katika kipindi cha mwaka mmoja Shirika limeongeza ofisi tano (5) na hivyo kufikisha jumla ya ofisi 377 ikilinganishwa na ofisi 372 zilizokuwepo mwaka 2011. Vilevile, vibali vya kuuza stempu na shajala za Posta vimeongezeka katika kipindi cha mwaka mmoja kutoka 3,064 hadi 3,098; ikiwa na maana kwamba vibali 34 vilitolewa katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta limeendelea kuboresha mazingira ya kazi na utoaji wa huduma kwa kuyafanyia matengenezo majengo ya Posta mpya Dar-es-Salaam, Mwanza na Wete. Hadi kufikia mwezi Mei 2012, kazi katika maeneo haya zilikuwa katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Dar es Salaam Posta Kuu – matengenezo na marekebisho kwa ofisi upande wa uchambuzi wa barua yanaendelea; Mwanza – matengenezo ya paa ili kuzuia kuvuja - kazi inaendelea; na kwa upande wa Wete – kazi ya kupaka rangi na marekebisho ya paa inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ni moja ya eneo muhimu katika kujenga uchumi imara uliojikita kwenye misingi ya maarifa ambalo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imepewa dhamana ya kuliendeleza. Kwa kuzingatia dhamana hii, Wizara imejikita katika kutekeleza masuala kadhaa ya ujumla yanayolenga kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kuendeleza matumizi ya sayansi na teknolojia na kuchochea ubunifu ikizingatiwa kuwa eneo hili ni mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii, masuala yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na: kuweka mifumo ya utekelezaji na udhibiti, kuandaa sera, mikakati, sheria na kanuni; kujenga miundombinu na kuendeleza utafiti; na kujenga na kusimamia taasisi za udhibiti na taasisi za kuendeleza sayansi na teknolojia, hususan rasilimali watu. Baadhi ya masuala haya nitayatolea maelezo hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga asilimia 1.0 ya pato ghafi la Taifa *(GDP)* kwa ajili ya utafiti na maendeleo (R & D). Serikali imedhamiria kutenga asilimia 1.0 ya pato ghafi la Taifa *(GDP)* kwa ajili ya utafiti na maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 25,768,769,000 kwa ajili ya kuendeleza shughuli za utafiti na maendeleo. Maeneo yatakayofaidika na fedha hizi ni haya yafuatayo: (i) Kujenga uwezo wa watafiti; (ii) kukarabati miundombinu ya utafiti; (iii) kugharimia utafiti; (iv) kuhawilisha teknolojia; na (v) kufanya usimamizi na utawala, hususan ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zilizofadhiliwa na fedha za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Desemba 2011, mfuko ulikuwa unagharimia mafunzo ya wataalamu 195 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili *(MSc)* na 100 katika Uzamivu *(PhD)* kwenye vyuo vikuu vitano (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kiwe chombo kinachowaunganisha watafiti na wagunduzi wote nchini. Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ambayo inatoa mwongozo katika masuala mbalimbali ya utafiti. Aidha, kwa sasa Wizara inakamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Sera hiyo ili kuhakikisha Sera hiyo inawezesha Tume ya Sayansi na Teknolojia kuratibu shughuli za watafiti na wagunduzi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaandaa Sheria ya Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia nchini (*Science and Technology Promotion Act*). Kukamilika kwa Sheria hii kutatoa fursa ya kurejea Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyounda Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kuhakikisha majukumu ya Tume yanakidhi mahitaji ya sasa, hususan kuwa na nguvu katika kusimamia na kuratibu shughuli za utafiti nchini. Maboresho ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini *(Science, Technology and Innovation Reform)* yatabainisha njia bora zaidi za kuendeleza na kuratibu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuishirikisha sekta binafsi katika kuchangia maendeleo na matumizi ya

teknolojia kwenye uzalishaji mali na utoaji huduma. Serikali inatekeleza Sheria ya *Public Private Partnership* ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake za mwaka 2011, kwa kuzihuisha kwenye masuala ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Kwa mfano, kupitia ushirikiano baina ya sekta binafsi na Serikali, muungano wa kampuni tatu za watoa huduma za mawasiliano *(Airtel, Tigo na Zantel)* wameweza kujenga na kukamilisha njia za mkongo wa mawasiliano katika Jiji la Dar es Salaam (*metro networks*) na hivyo kuongeza fursa za kutoa huduma bora zaidi za mawasiliano. Serikali imehakikisha kuwa ujenzi huu unafanyika vyema kwa kutoa vibali vya njia za kupitishia mkongo *(right of way)*. Serikali imepewa nguvu za kuratibu matumizi ya njia zilizowazi katika mkongo huo ili kupunguza haja ya watoa huduma wengine kujenga njia nyingine kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali imepewa fursa ya kutumia njia zilizobakia endapo itahitaji kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi hizi zitaendelea katika miji mingine mikubwa katika siku za usoni. *Tanzania Private Sector Foundation* imechangia maendeleo ya teknolojia kwenye Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kwa kutoa vifaa vya maabara. Pia, majadiliano yanaendelea kati ya HUAWEI na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeainisha maeneo ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu ambayo yanaweza kuwekezwa na sekta binafsi. Maeneo hayo ni pamoja na uanzishaji wa *Smart Village* katika eneo la Kigamboni, usindikaji mazao ya kilimo na kuendelea na kukuza matumizi ya bayoteknolojia, Nishati ya Jua,

kilimo, afya na mazingira. Pia, katika kupitia upya mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inategemewa kuwa, mwongozo utaandaliwa ili kuongoza juhudi za uanzishwaji wa taasisi za utafiti zisizo za Serikali katika sekta mbalimbali kama ilivyo kwenye mazao ya chai, tumbaku na kahawa. Sekta ya TEHAMA na Mawasiliano inahusika katika kuishirikisha sekta binafsi katika kuchangia maendeleo na matumizi ya teknolojia kwenye uzalishaji mali na utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuandaa Programu Mahsusi ya wataalamu wa kada mbalimbali za sayansi na teknolojia katika kuyafikia malengo ya dira. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imeendelea kupanua Taasisi zinazotoa mafunzo katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia. Uendelezaji huo umefanywa katika kubuni mitaala mipya ambayo inaendana na mahitaji ya hivi sasa na ya baadaye au kuzipandisha hadhi baadhi ya taasisi hizi kuwa Vyuo Vikuu au Taasisi Mahiri. Mitaala mipya ambayo inaendana na mahitaji ya sasa na Taasisi zinazohusika ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini. Aidha, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya imepandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kama ilivyokuwa imeazimiwa hapo awali. Mpango wa kuipandisha hadhi Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Tekolojia Mbeya umezingatia zaidi kozi ambazo zinahitajika kwenye soko na kutatua matatizo ya kiuchumi na kijamii. Vilevile, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia – Nelson Mandela ni taasisi mahiri katika nyanja za sayansi na teknolojia katika ukanda wa

Afrika Mashariki na ni moja ya Taasisi nne za aina hiyo zilizoanzishwa barani Afrika.

(1) DIT

(a) Stashahada

- *Biomedical Equipment Engineering;*
- *ommunication Systems Technology;*
- *Multimedia Technology* na *Information, Technology;* na
- *Mining.*

(b) Shahada

- *Laboratory Technology.*

(c) Shahada Uzamili
- *Maintenance Management.*

(2) *MIST*

Stashahada na Shahada

- Usanifu majengo; Uhandisi- Ujenzi, Umeme, *Mechatronic* na Madini, *Telecommunication*, Teknolojia ya Maabara na Sayansi na Teknolojia ya Chakula.

(3) Nelson Mandela

Shahada, Uzamili na Uzamivu

- *Material and Life Sciences*.

(4) Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania

Mafunzo maalum ya Mionzi kwa Wataalam

- Kozi fupi za usalama wa mionzi, Kozi ndefu kwa ushirikiano na taasisi nyingine, maandalizi ya kuanzisha kituo cha kuendeleza matumizi ya teknolojia ya nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatekeleza mkakati wa kuhamasisha wanafunzi katika ngazi zote za elimu kusoma masomo ya sayansi kwa bidii na kuyapenda ili kuhakikisha taasisi mbalimbali za mafunzo ya sayansi na teknolojia zinapata wanafunzi wenye viwango vizuri vya ufaulu. Uhamasishaji unaofanywa ni pamoja na kutambua wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi katika shule za sekondari katika kidato cha nne na cha sita. Aidha, Walimu na shule zilizofanya vizuri katika masomo hayo pia zimekuwa zikitambuliwa kwa kupewa vyeti na zawadi mbalimbali. Programu maalum za awali za mafunzo (*pre-entry programmes*) kwa wanafunzi zinazolenga katika kuwaongezea wanafunzi wenye ufaulu mdogo kujiunga na taasisi za sayansi na teknolojia zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara inashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika mradi wa *Technical and Vocational Education and Training (TVET)* ambao unalenga kuendeleza elimu ya ufundi ambayo itamkomboa mwananchi kiuchumi na kijamii. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeanza kufadhili wanafunzi katika nyanja za mawasiliano na

kwa kuanzia katika mwaka 2011/2012, Mamlaka imefadhili wanafunzi nane (8). Aidha, kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, jumla ya wanafunzi 295 wamefadhiliwa kusoma katika vyuo vikuu mbalimbali katika Shahada za Uzamili na Shahada za Uzamivu katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania pamoja na Wizara ya Nishati na Madini zimeshiriki kwenye mpango maalumu wa mafunzo chini ya Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani kwenye mafunzo yaliyofanyika nchini Korea kuhusu uanzishaji, uendelezaji na matumizi salama ya nguvu za nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia vyombo vya habari kutoa taarifa muhimu za sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake na wadau wengine imeendelea na jukumu la kuelimisha umma mara kwa mara kwa kutumia vyombo vya habari kama vile redio, luninga na magazeti na njia mbalimbali za mawasiliano, ikiwemo tovuti, majarida, machapisho, vipeperushi, maonesho katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Wizara imetoa taarifa zifuatazo katika nyanja ya sayansi na teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini:-

(i) Maboresho ya Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini;

(ii) Usimikaji wa taa za kisasa za kuongozea magari katika jiji la Dar es Salaam na Mbeya; na

(iii) Uchimbaji wa madini ya *uranium* na madhara yake kwa matumizi yasiyo sahihi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, vipindi maalum viliandaliwa ili kuelezea mafanikio katika Sayansi na Teknolojia wakati wa kuadhimisha Miaka 50 ya Uhuru. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara zimeendelea kuratibu vipindi maalum katika masuala ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mishahara, marupurupu na mafao ya Watafiti na Wagunduzi wetu. Serikali kwa kutambua umuhimu na kazi wanazofanya Watafiti na Wagunduzi nchini, ambao wako katika taasisi za utafiti zinazosimamiwa na Serikali moja kwa moja kama zile zilizopo katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, mishahara yao imeboreshwa kwa kuanzisha skeli mpya za mishahara ambayo inaendana na Watafiti na Wahadhiri walioko vyuo vikuu au hata katika taasisi za utafiti za mashirika ya umma kama vile *TAFIRI*, *TAFORI, TAWIRI, TPRI, NIMR* na kadhalika ambao wanatumia skeli za *PRSS* kutegemea kiwango cha elimu na machapisho Mtafiti aliyotoa. Uboreshaji huu umefanywa kupitia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 5 wa Mwaka 2010 ambao ulianza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2010. Marekebisho haya

yamesaidia sana kuwabakiza Watafiti kuendelea kufanya kazi za utafiti katika taasisi za utafiti za Serikali na pia kuvutia Wahadhiri wa vyuo vikuu kwenda kufanya kazi za utafiti katika taasisi za utafiti bila kuogopa kuwa mishahara yao itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ujumla katika Wizara. Uendelezaji wa Rasilimali Watu. Kwa upande wa kusimamia sheria, kanuni na taratibu na kuendeleza rasilimali watu, watumishi 20 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo baada ya kukidhi vigezo vya Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi wa Umma za mwaka 2002 pamoja na tathmini ya utendaji kazi kwa uwazi (*Open Performance Review and Appraisal System*). Pia, Wizara imeendelea kutekeleza kanuni za maadili ya kiutendaji katika Utumishi wa Umma kwa kuwaelimisha watumishi kuhusu sheria zinazotawala utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kujikinga na kuepuka maambukizi mapya ya UKIMWI, upimaji wa UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na virusi vya UKIMWI na kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, Wizara imeendelea kuelimisha watumishi ili wale waliopata maambukizi waweze kujitokeza na kupatiwa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Ukaguzi wa matumizi ya fedha za Wizara na Taasisi zilizo chini yake umeendelea kufanywa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika

matumizi ya fedha za umma, utendaji kazi na kuwa na matokeo mazuri na yenye tija kwa Taifa. Taarifa za ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) na pia Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi katika Sekta ya Umma (*PPRA*) umethibitisha hilo. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohitaji ushauri wa kisheria ikijumuisha masuala ya mikataba, miswada, sheria ndogondogo, kuridhia itifaki za kikanda na kimataifa na pale inapojitokeza kurejea sheria zilizopo ili kuleta ufanisi katika sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Miongozo mbalimbali katika sekta. Wizara imeendelea na jukumu lake la uandaaji wa Sera mbalimbali na utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipindi cha 2010-2015. Aidha, Wizara imehuisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia *(Communication, Science and Technology Strategic Plan)* na pia kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara na taasisi zake ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia mchakato wa kuwapata wazabuni wa kutoa huduma mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi Namba 21 ya mwaka 2004, kifungu namba 35. Shughuli zote za ununuzi na ugavi zimesimamiwa kwa kushirikiana na Wakala wa Ununuzi na Ugavi wa Serikali *(GPSA).* Aidha, ununuzi wa bidhaa na huduma umezingatia taratibu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi katika Sekta ya Mawasiliano ni jambo

lililo dhahiri lisilohitaji ufafanuzi wa ziada. Hii ni kutokana na ukweli kwamba huwezi kupanga kwa usahihi jinsi ya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano bila kujua idadi ya watu na mtawanyiko wao. Kutokana na ukweli huo, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inatoa wito wa pekee kwa Watanzania wote kujitokeza kuhesabiwa na kutoa taarifa sahihi zitakazotuwezesha kupanga mipango sahihi katika kutoa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Mafunzo. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya. Wizara imeendelea kusimamia upandishwaji wa hadhi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya (*MIST*) kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (*MUST*). Taasisi imeshapata ithibati ya muda kwa ajili ya kuendesha programu zake kama Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya. Aidha, Taasisi imekamilisha ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 800 pamoja na ukarabati wa miundombinu ya umeme na maji. Pia, taasisi inaendelea kukarabati na kuboresha vyumba vitakavyotumika kama maabara za kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Teknolojia Mbeya imeendelea na upanuzi wa udahili na uanzishaji wa Programu mpya kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika mwaka wa masomo 2011/2012, Taasisi imefikisha jumla ya wanafunzi 2,591, ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 1,757 kwa mwaka wa masomo 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*) imeendelea kufanya upanuzi wa udahili na uanzishaji wa Programu mpya kwa ajili ya kukidhi mahitaji maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika mwaka wa masomo wa 2011/2012, Taasisi imefikisha jumla ya wanafunzi 2,583 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 1,578 katika mwaka wa masomo 2010/2011. Aidha, imeendelea na ujenzi wa *DIT Teaching Tower* na usimamizi wa kituo Mahiri cha TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, inaendelea kuimarisha Kampasi mpya ya Mwanza ijulikanayo kama *Tanzania Institute of Leather Technology (TILT).* Kampasi hii inatoa programme za muda mfupi kwa wajasiriamali wa kusindika na kutengeneza bidhaa za ngozi. Lengo ni kuendesha programu za muda mrefu. Ukizingatia kuwa hii ndiyo taasisi pekee inayojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za ngozi kutokana na mifugo yetu, ni imani ya Serikali kuwa, Taasisi hii itapokuwa imeimarika kikamilifu itatoa ufumbuzi wa changamoto iliyoikumba nchi yetu ya kuuza ngozi isiyosindikwa, jambo ambalo huinyima nchi fedha nyingi za kigeni na ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (*NM-AIST*) ilikamilisha udahili na kuanza masomo tarehe 26 Oktoba, 2011 ikiwa imedahili wanafunzi 83 ambapo kati yao 53 ni wa Shahada ya Uzamili na 30 ni wa Shahada ya Uzamivu. Aidha, wanafunzi kutoka nchi za nje walishindwa

kujiunga na Taasisi kwa sababu hawakupata nafasi ya kutosha kutafuta wafadhili wa kuwalipia ada ya masomo. Hivyo, ni matazamio ya Serikali kuwa katika mwaka wa masomo 2012/2013 wanafunzi wa kigeni watapata fursa ya kujiunga kutokana na kuwepo muda wa kutosha wa maandalizi. Masomo yalianza katika fani zifuatazo:

*(i) Life Sciences and Bio-engineering (LSBE);*

*(ii) Mathematics Computational Science and Engineering (MCSE);*

*(iii) Information and Communication Science and Engineering (ICSE);*

*(iv) Hydrology and Water Resources Engineering (HWRE);*

*(v) Environmental Science and Engineering (EnSE);*

*(vi) Materials Science and Engineering (MaSE);*

*(vii) Sustainable Energy Science and Engineering (SESE);*

*(viii) Humanities and Business Studies (HuBS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kuonea fahari na lenye kutia matumaini kuwa mafanikio yote katika taasisi yetu ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, yametokana na fedha zetu wenyewe kupitia

mkopo toka Taasisi za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Katika kuhakikisha kuwa Taasisi hii inatoa elimu ya sayansi na teknolojia kwa kiwango cha kimataifa, Taasisi imeendelea kuanzisha ushirikiano na taasisi na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi katika kupata wataalam mahiri wa kutoa mafunzo. Aidha, Taasisi imevitembelea baadhi ya vyuo maarufu vya sayansi na teknolojia katika nchi za Marekani, China, Korea, India na Saudi Arabia, ambavyo vimeonyesha nia ya kushirikiana na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela katika kufundisha na kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kufuatia kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu muhimu mwezi Agosti 2011, jumla ya wanafunzi 83 walidahiliwa na kuanza masomo mwezi Oktoba 2011. Kati ya wanafunzi hao 83, wanawake ni 15 na wanaume ni 78. Aidha, kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 53 wamedahiliwa katika masomo ya Shahada ya Uzamili na wanafunzi 30 wamedahiliwa katika masomo ya Shahada ya Uzamivu. Matangazo ya maombi kwa ajili ya wanafunzi wa mwaka 2012/2013 yameshatolewa katika vyombo mbalimbali vya habari na mwitikio umekuwa mkubwa sana. Aidha, taratibu za kuzindua rasmi Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela zinaendelea kufanywa na inatarajiwa kuwa Taasisi hii itazinduliwa rasmi mwezi Oktoba 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ni chombo cha kusimamia na kuratibu tafiti za Sayansi na Teknolojia katika Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Katika kuhakikisha shughuli za Tume ya Sayansi na Teknolojia zinatekelezwa vyema Tanzania Bara na Zanzibar, Tume hiyo imefungua ofisi zake mjini Zanzibar. Baadhi ya majukumu ya Tume katika uendelezaji wa sayansi na teknolojia ni katika maeneo ya uboreshaji wa miundombinu ya utafiti na vitendea kazi katika taasisi za utafiti na maendeleo. Aidha, Tume imejielekeza katika uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa wajasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa miundombinu ya utafiti na vitendea kazi katika taasisi za utafiti na maendeleo. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupitia *COSTECH* ilikusanya taarifa kutoka vituo vyote nchini. Taarifa hiyo ilibainisha hali ya uchakavu wa miundombinu, vifaa duni vya maabara na upungufu wa vifaa vya kufanyia kazi. Jumla ya shilingi bilioni 5.2 zimetumika kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kuongeza vifaa vya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa wajasiriamali. Wizara, kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, ilitoa kiasi cha Sh. 80,000,000 kwa ajili ya shughuli za Atamizi ya TEHAMA ya Dar es Salaam (*DTB*), ambapo wabia wengine ni *INFODEV* (*World Bank*) na Vodacom Tanzania. Atamizi hiyo imeweza kuhudumia wajasiriamali ambao wameweza kuendeleza juhudi zao za ujasiriamali katika nyanja za TEHAMA ikiwa ni pamoja na kupatia ufumbuzi wa masuala ya ununuzi wa bidhaa kwa mtandao na kadhalika. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa shughuli

za ugunduzi na ubunifu, jumla ya Sh.134,894,950 zimetumika kwa ajili ya kuwahudumia wagunduzi na wabunifu kwa kuwapatia tuzo na vitendea kazi ili kuboresha shughuli zao. Jitihada zingine ni pamoja na Wizara kupokea maombi kutoka taasisi za *TEMDO* na Mzinga, Morogoro ambazo zimeomba jumla ya shilingi milioni 500 kutoka Mfuko wa Ubunifu kwa ajili ya kubiasharisha teknolojia zilizopo kwenye kongano (*clusters*) zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*) imepewa dhamana ya kusimamia na kuendeleza matumizi salama ya nguvu za atomiki. Eneo hili ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa na Tume hii ni pamoja na kuendeleza na kudhibiti matumizi salama ya nguvu za atomiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania imekuwa ikishiriki katika kuandaa mipango na taratibu za kuendeleza na kusimamia matumizi ya nguvu za atomiki hapa Tanzania. Kwa upande wa udhibiti, Tume imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia matumizi salama ya mionzi katika hospitali zetu, vituo vya huduma za afya, viwandani, kwenye migodi na shughuli za tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kuendeleza matumizi salama ya nguvu za atomiki ni pamoja na kuhakikisha kuwa, matumizi ya nguvu za atomiki yanaboresha maisha ya wananchi wa Tanzania ikiwa ni pamoja na: (i) utoaji wa huduma za tiba ya saratani,

(ii) uboreshaji wa mazao ya kilimo na mifugo, (iii) kutokomeza mbung'o katika kisiwa cha Zanzibar, (iv) kusimamia na kukagua uwepo wa mionzi kwenye vyakula na pembejeo za kilimo na kadhalika. Katika kuhakikisha kuwa shughuli za usimamizi wa matumizi ya nguvu za atomiki zinafanywa vyema zaidi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TAEC* imefungua ofisi zake mjini Zanzibar hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* uchimbaji wa madini ya urani. Kiwango kikubwa cha madini ya urani kimegundulika hapa Tanzania na hasa katika maeneo ya Namtumbo, Bahi na Manyoni. Mipango inaendelea ili kuwezesha uchimbaji wa madini haya kuanza baada ya shughuli za utafiti kukamilika. Juhudi kubwa zimeelekezwa katika kuhakikisha kuwa uchimbaji utakapoanza, masuala ya usalama wa wananchi na madini hayo unapewa kipaumbele kikubwa kabla, wakati na baada ya kumalizika kwa shughuli za uchimbaji wa madini hayo. Ili kuwezesha uchimbaji salama, Serikali kwa kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeandaa kanuni na taratibu zitakazowezesha uchimbaji, usindikaji na usafirishaji salama wa madini haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika mwaka 2011/2012, Tume kwa kushirikiana na wadau muhimu ambao ni; Wizara ya Nishati na Madini, *NEMC, OSHA*, Wizara ya Maji, pamoja na wengine waliendelea na maandalizi ya usimamizi wa migodi ya urani ili kulinda wafanyakazi, mazingira na jamii kwa ujumla. Ili kutekeleza hili, *TAEC* inatarajia kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa taratibu za usimamizi na udhibiti ;
(ii) Kuandaa taratibu za utoaji wa leseni mbalimbali;
(iii) Kuweka mkakati wa pamoja wa wadau wote wa uchimbaji wa Urani ; na
(iv) Kuboresha uhifadhi wa mabaki ya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha uhifadhi wa mabaki ya mionzi. Kuendelea kupanuka kwa matumizi ya nguvu za atomiki kunafanya kiwango cha mabaki ya vyanzo vya mionzi kiongezeke nchini. Kwa sababu hii, *TAEC* inakusudia kuboresha uhifadhi na usalama wa mabaki ya mionzi kwa:-

(i) Kuboresha uhifadhi wa mabaki haya kwa kuongeza ulinzi na usalama wa jengo la uhifadhi wa mionzi lililoko Arusha;
(ii) Kukusanya mabaki haya kutoka kwenye mazingira ili kuepusha hatari zozote ambazo zingeweza kutokea; na
(iii) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu hatari na athari za mabaki ya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka viwango vya mionzi. Kwa kuzingatia kuwa matumizi ya vyanzo vya mionzi yanaongezeka siku hadi siku, shughuli za udhibiti nazo zinaongezeka. Kwa sababu hii, Tume ya Nguvu za Atomiki inaona kuna haja ya kuweka viwango (*standards*) za vyanzo vya mionzi ili kurahisisha shughuli za udhibiti. Kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania, Tume itaendelea kuratibu na kushiriki katika kuandaa viwango hivi muhimu na hatimaye kuweza kuvitumia na kuvitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza matumizi ya teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo ya kiuchumi. Teknolojia ya nyuklia ina mchango mkubwa katika maendeleo ya Tanzania. Teknolojia hii inahitaji kuendelezwa na kutumiwa kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu. Baadhi ya sekta ambazo teknolojia hii inaweza kuleta michango muhimu ni pamoja na afya, kilimo, mifugo, maji, elimu na utafiti na viwanda. Katika mwaka wa Fedha 2012/2013, Wizara kupitia *TAEC* inatarajia kufanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza upatikanaji wa huduma za kutambua na kutibu ugonjwa wa saratani katika vituo vya Mbeya (Hospitali ya Rufaa Mbeya), Kilimanjaro (Hospitali ya *KCMC*) na Zanzibar (Hospitali ya Mnazi Mmoja);

(ii) Kuboresha huduma za tiba ya saratani katika vituo vya *Ocean Road* na Bugando kwa kupata vifaa na nafasi za mafunzo kwa ajili ya wataalam kwa kushirikiana na taasisi husika;

(iii) Kuongeza maeneo ya Tume kwa ajili ya kupanua wigo wa shughuli za Tume kwa lengo la kuongeza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia nchini;

(iv) Kuandaa mpango mkakati wa kujenga kinu cha utafiti wa nyuklia nchini (*nuclear research reactor*) katika mpango wake wa muda wa kati ili kuboresha utoaji wa huduma mbalimbali zinazohusu nguvu za atomiki;

(v) Kuandaa mipango ya kujenga mfumo wa uhifadhi wa mazao ya kilimo kwa kutumia teknolojia ya nyuklia *(Food Irradiation Facility);* na

(vi) Kuandaa mipango ya kuanzisha Kituo cha Kuendeleza Matumizi ya Nguvu za Atomiki (*Center of Excellence in Nuclear Science and Technology*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mipango ya Wizara kwa mwaka 2011/12. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara imekabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zilichangia katika kutofikiwa malengo kulingana na mpango. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Uhaba wa Wataalamu wa kutosha katika nyanja mbalimbali za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu jambo ambalo limeathiri mafanikio ya sekta. Aidha, changamoto kubwa katika eneo hili ni pamoja na kuwa na idadi ndogo ya wataalam hususan wenye weledi katika TEHAMA ikilinganishwa na mahitaji; wataalam wengi kuwa wa umri mkubwa, wataalam kutokuwa na uelewa wa teknolojia mpya na uwiano baina ya wataalam mbalimbali (kama vile uwiano wa Wahandisi na Mafundi wa ngazi ya Cheti na Diploma) kutokuwa mzuri. Wizara, kupitia Sera ya Utafiti na Maendeleo inaandaa mikakati ya muda mfupi na mrefu ili kupata ufumbuzi wa kudumu kukabiliana na changamoto hii;

(ii) Kuongeza uelewa wa umuhimu wa sayansi na teknolojia ili kuendana na dhana ya kuwa na jamii inayoongozwa na maarifa (*knowledge-led society*). Utekelezaji wa Sera na mikakati mbalimbali iliyotajwa ikiwemo Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu unalenga kubadilisha uelewa,

mtazamo wa wananchi na kiwango cha matumizi ya sayansi na teknolojia katika nyanja zote za maisha ya wananchi;

(iii) Uhaba wa miundombinu ya kuendeleza sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambao unahitaji uwekezaji mkubwa: Miundombinu ya Teknolojia ya Mawasiliano inahitaji uwekezaji mkubwa na wa haraka. Moja ya sababu ni mabadiliko ya haraka ya teknolojia inayotumika katika nyanja hii. Mabadiliko haya yanahitaji uwekezaji mkubwa ili kuendana na wakati. Hii inajitokeza pia katika fani ya sayansi na teknolojia hususan katika vifaa vya utafiti na uchunguzi (maabara za kisasa);

(iv) Uharibifu na kukata nyaya za Mkongo unaotokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu na manufaa ya Mkongo kwa jamii unachangia katika uharibifu wa nyaya za Mkongo unaofanywa na wananchi katika baadhi ya maeneo. Mkakati wa namna ya kutatua changamoto hiyo ni kwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuweka Sera shirikishi na kutenga fedha za kutosha kuendesha elimu kwa Umma;

(v) Licha ya Bajeti ya Wizara kuwa ndogo, mtiririko wa fedha kwa kila mwezi ulikuwa hauendani na utekelezaji wa majukumu. Wizara imekuwa ikipokea fedha kidogo kila mwezi ukilinganisha na mahitaji halisi ya Wizara na Taasisi zake. Aidha, kwa baadhi ya miezi Wizara imekosa kabisa fedha za uendeshaji, jambo ambalo liliathiri sana utendaji wa Wizara na taasisi zake pia; na

(vi) Shughuli za Utafiti na Maendeleo (*Research and Development – R&D*) kutotengewa fedha za kutosha: Serikali kwa kutambua tatizo hili, imeendelea kutenga fedha kulingana na uwezo wake. Serikali katika Bajeti yake ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 ilitenga Sh.25,768,769,000/= kwa ajili ya shughuli za utafiti. Vile vile, Serikali na asasi za utafiti zimeendelea kutumia njia nyingine kufadhili utafiti ikiwa ni pamoja na kushirikiana na mashirika ya nje na sekta binafsi katika kuchangia shughuli za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nilizozieleza hapo juu, Wizara itajitahidi kutekeleza majukumu yake ili kuwezesha upatikanaji wa miundombinu bora itakayowezesha uendelezaji wa sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Mawasiliano. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Itakamilisha mchakato wa kuanzisha Tume ya TEHAMA nchini ambayo itasimamia na kuratibu maendeleo ya Tehama nchini;

(ii) Itaratibu utekelezaji wa Mradi wa Kitaifa wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta;

(iii) Itaratibu utekelezaji wa mabadiliko ya Teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali hadi ifikapo Desemba 2012;

(iv) Itaratibu na kusimamia utendaji kazi wa Kampuni ya Simu (*TTCL),* Shirika la Posta Tanzania *(TPC),* Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)* na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF);*

(v) Itaimarisha ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuchochea ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano nchini;

(vi) Itaratibu mpango wa kuanzisha na kuendeleza vituo vya mawasiliano ya kijamii nchini;

(vii) Itaanzisha mpango mkakati wa kitaifa wa kukuza ubunifu katika sekta ya mawasiliano kwa wajasirimali wadogo;

(viii)Itaratibu utekelezaji wa Mradi wa Habari Jamii;

(ix) Itaratibu Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya pamoja na kuunganisha Taasisi za Umma kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(x) Itaratibu mradi wa kuunganisha katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, shule za msingi, sekondari, vyuo vya afya pamoja na taasisi zilizoainishwa kwenye mradi wa *Tanzania Beyond Tomorrow;*

(xi) Itaratibu uwekaji wa viwango vya mifumo, vifaa, mitambo na huduma za TEHAMA nchini na kuandaa mwongozo kuhusu usalama wa mitandao ya TEHAMA (*Cyber Security*) kuhakikisha matumizi mazuri na salama ya TEHAMA nchini; na

(xii) Itaratibu kuunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Hospitali za Rufaa, Mikoa, Wilaya na Teule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Kwa upande wa Sayansi na Teknolojia, Wizara itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuratibu mahusiano ya kikanda na kimataifa katika masuala ya sayansi na teknolojia na ubunifu;

(ii) Itakamilisha Andiko la Programu ya Matumizi ya Teknolojia za Nyuklia;

(iii) Itaratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Sayansi, Tekonolojia na Ubunifu;

(iv) Itaendelea kutekeleza programu ya kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi, teknolojia na uhandisi; na

(v) Itaendelea na programu ya kuhamasisha wananchi kutumia sayansi na teknolojia katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ujumla. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Itawapandisha vyeo watumishi 11 wenye sifa na wanaokidhi vigezo vya Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi wa Umma za mwaka 2002 pamoja na tathmini ya Utendaji Kazi kwa Uwazi *(OPRAS);*

(ii) Itasimamia utekelezaji wa mkakati wa uadilifu kwa kutekeleza kanuni za maadili ya kiutendaji katika utumishi wa umma, kwa kuwaelimisha watumishi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002, kanuni, taratibu za uendeshaji katika utumishi wa Umma na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 ili Utumishi wa Umma uwe wenye ufanisi na wa kuheshimika;

(iii) Itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao ili kuwa na watumishi wenye afya bora na wenye kutekeleza majukumu yao kwa Taifa na familia zao;

(iv) Itaendelea kusimamia utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007, kuhusu mfumo wa kupima tathmini ya utendaji kazi kwa uwazi *(OPRAS)* kwa kuwawezesha watumishi 138 kujaza mikataba ya kazi;

(v) Itawapeleka kwenye mafunzo watumishi kumi na sita (16) katika maeneo ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji wao wa kazi;

(vi) Itaendelea kusimamia na kuimarisha Sekta ya TEHAMA, Sayansi na Teknolojia kwa kuweka mifumo ya kimenejimenti kama Miundo ya TEHAMA, mgawanyo wa majukumu na Mpango wa Kurithishana Madaraka;

(vii) Itaendelea na Usimamizi wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 *(PFA)* na marekebisho yake;

(viii) Itaendelea kutayarisha na kusimamia Hesabu na Taarifa za Fedha za Wizara;

(ix) Itaendelea kusimamia miongozo ya Serikali inayohusu matumizi sahihi ya Fedha na Mali zote za Serikali. Aidha, itasimamia Sheria ya Ununuzi wa Umma *(PPRA)* ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005;

(x) Itaendelea kuandaa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya malipo ya pensheni;

(xi) Itaratibu uandaaji na uhuishaji wa sera na sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara;

(xii) Itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2012/2013-2016/2017);

(xiii) Itaratibu uandaaji wa taarifa ya kusimamia, kudhibiti na kuratibu mapato na matumizi ya Serikali;

(xiv)Itaratibu uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015;

(xv) Itaratibu utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake;

(xvi)Itafanya tathmini ya matumizi ya fedha katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (*Public Expenditure Tracking);*

(xvii)Itashirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala ya madai, usuluhishi au jinai yanayohusu Wizara; na

(xviii)Kushirikiana na vyombo vya habari kuelimisha umma kupitia redio, luninga, magazeti, machapisho na tovuti ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya TEHAMA, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Wizara itatekeleza yafuatayo kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam:-

(i) Itadahili wanafunzi 1,505 katika programu mbalimbali za Ufundi Mchundo, Sanifu na Uhandisi (*IT Basic Certificate* 95, Diploma 780 na *Bachelor of Engineering* 630);

(ii) Itaanza kufundisha kozi mpya ya Shahada ya Uzamili ya Uhandisi (*Master of Engineering in Maintenance Management*);

(iii) Itaendeleza wafanyakazi 15 katika masomo ya juu, Wakufunzi nane (8) na Waendeshaji saba (7). Pia, Taasisi itaendelea kuhudumia wafanyakazi 27 walioko masomoni, wakufunzi 20 na Waendeshaji saba (7);

(iv) Itaendesha Mafunzo ya Awali (*Pre-entry Training*) ili kuwawezesha wanafunzi wengi wa kike kujiunga na kozi za Ufundi Sanifu. Katika mafunzo haya, tunategemea kuwa na wanafunzi wa kike 60;

(v) Itaweka mikakati ya kuendeleza ardhi yake iliyopo Mbezi Kilongawima, Dar es Salaam;

(vi) Itaanzisha mradi wa majaribio wa Matibabu Mtandao (*Telemedicine*) utakaounganisha *DIT*, Hospitali za Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Tumbi na Bagamoyo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya

Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine;

(vii) Itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi lijulikanalo kama *DIT Teaching Tower*;

(viii) Itakamilisha ujenzi wa Maktaba na kuipatia vifaa vya TEHAMA ili iweze kuendana na teknolojia ya sasa na hasa kutoa huduma bora kwa wanafunzi, wafanyakazi na wanajumuiya kwa ujumla;

(ix) Itaendelea kujitangaza ili kupata zabuni za kufanya miradi mbalimbali kama vile kutengeneza na kuweka taa za kuongoza magari barabarani, upimaji udongo na nyinginezo; na

(x) Itaendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya Kampasi ya Mwanza (kilichokuwa Chuo cha Ngozi Mwanza) ili kiweze kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na hatimaye mafunzo ya Stashahada ya Teknolojia ya Ngozi na bidhaa za Ngozi yanayotegemewa kuanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 2,591 hadi kufikia wanafunzi 3,000, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16;

(ii) Itaendelea kutoa Mafunzo ya Awali (*Pre-entry programme*) kwa wanafunzi wa kike kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike 100;

(iii) Itakamilisha uandaaji wa mitaala ya fani za mekatroniki, sayansi na teknolojia ya vyakula, uhandisi usalama, uhandisi mawasiliano na uhandisi madini;

(iv) Itaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja;

(v) Itaendelea na ujenzi wa jengo la maabara ili kukabiliana na uhaba wa vyumba vya maabara katika Taasisi;

(vi) Itashirikiana na Wizara kuhakikisha kwamba, mchakato wa kuifanya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia unakamilika mapema na udahili wa wanafunzi unaanza kabla ya mwaka 2015;

(vii) Itaanzisha na kuendeleza uhusiano na taasisi mbalimbali za sayansi na teknolojia Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; na

(viii) Itaajiri watumishi wapya 104, ili kuendana na uhitaji wa rasilimali watu unaotokana na kupanuka kwa Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ya Nelson Mandela itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Itadahili wanafunzi wapatao 100 katika ngazi za Uzamili za Uzamivu;

(ii) Itajenga nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo na kuweka samani na vifaa mbalimbali;

(iii) Itajenga Kituo cha Afya;

(iv) Itaimarisha uhusiano na ushirikiano na vyuo pamoja na asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujijenga, kikanda na kimataifa;

(v) Itaajiri wafanyakazi wapya 54,

(vi) Itajenga Kituo cha TEHAMA na kuweka vifaa mbalimbali kwa ajili ya kituo hiki;

(vii) Itanunua vifaa vya kujifunzia na kufundishia; na

(viii) Itakamilisha uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi *(Land Use Plan)* wa eneo la Taasisi lililopo Karangai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Tume ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Itaendelea kuratibu shughuli za utafiti nchini, ikiwa ni pamoja na zile zinazofadhiliwa kupitia MTUSATE na TASENE *(Tanzania, Sweden and Netherlands);*

(ii) Itaendelea na kuratibu shughuli za uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali nchini;

(iii) Itaendeleza programu mbalimbali za kuimarisha Sayansi na Teknolojia ikiwa ni pamoja na: (1) Uendelezaji wa rasilimali watu (2) Kuboresha mazingira ya utafiti-miundombinu na vitendea kazi na (3) miradi mipya ya utafiti kulingana na vipaumbele vya taifa;

(iv) Itaanzisha atamizi ya biashara na kilimo (*Agri-business Incubator)* ili kukuza ujasiriamali katika sekta ya kilimo, hususan usindikaji wa mazao;

(v) Itaendeleza uratibu na uboreshaji wa kongano *(Clusters*) 45 ili ziweze kufanya vizuri zaidi katika soko la ushindani kwa kutengeneza bidhaa zenye ubunifu na ubora wa hali ya juu;

(vi) Itahamasisha mfumo wa kuendeleza teknolojia (*Promoting Technology*

*Development)* mbalimbali katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti;

(vii) Itaendelea kubaini vipaji mbalimbali kupitia wagunduzi na wabunifu;

(viii) Itaboresha shughuli za kuratibu tafiti katika ofisi ya Zanzibar kwa kushirikiana na SMZ; na

(ix) Itasimamia ujenzi wa kijiji cha kisasa cha TEHAMA "*ICT Technology Park*" ambacho kitachangia sana katika kuleta makampuni makubwa ya kimataifa na hatimaye kuweza kukuza uchumi wa maarifa (*knowledge economy).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Itapokea na kutathmini maombi mbalimbali ya leseni ili kukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004;

(ii) Itaendeleza zoezi la upimaji wa viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,300 wanaotumia vifaa vya mionzi katika vituo mbalimbali (*Personnel Dosimetry Service*);

(iii) Itatoa elimu na kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi katika maabara maalumu *Central Radioactive*

*Waste Management Facility- CRWMF* iliyoko *TAEC* – Arusha;

(iv) Itatoa elimu kwa wananchi waishio maeneo yenye madini ya urani kwa nia ya kuongeza uelewa na kuweka tahadhari pale panapostahili;

(v) Itapima vyanzo vya mionzi katika sampuli za vyakula 5,000;

(vi) Itaendeleza ukaguzi wa migodi 40 ili kubaini hali ya usalama;

(vii) Itaendeleza kituo cha kupima mionzi katika mazingira *(Radionuclide Monitoring Station, (TZP-RN64, Dar es Salaam)* chini ya mkataba wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty of Nuclear Weapons – CTBT*; na

(viii) Itaanzisha Ofisi ya Kanda katika Mkoa wa Ruvuma (Namtumbo) ili kusogeza huduma ya kupima mionzi karibu na migodi ya urani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Shirika la Posta Tanzania litatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Litaendeleza, kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika huduma zitolewazo na Shirika ikiwa ni pamoja na kuunganisha ofisi za Posta za Mikoa na Wilaya

katika Mtandao wa Ki-Elektroniki wa Posta kutoka ofisi 65 za sasa hadi 95;

(ii) Litaendesha mafunzo katika maeneo ya uendeshaji pamoja na TEHAMA kama ifuatavyo:-

(a) Kozi ya uendeshaji 225;
(b) Huduma kwa wateja 116;
(c) Mafunzo ya awali ya huduma za Posta 20;
(d) Uendeshaji wa *Bureau de Change* 20; na
(e) Mafunzo katika nyanja ya TEHAMA 100.

(iii) Litaanzisha miradi ya ujenzi mpya wa Posta za Kibondo na Katesh na kuendeleza upanuzi katika Posta za Dodoma, Singida, Mbeya, Mahonda (Zanzibar) na Sengerema; na

(iv) Litafanyia matengenezo majengo yafuatayo: Posta Mpya Dar es Salaam, Mwanza, Moshi, Musoma, Manyoni, Dodoma Hpo, Tanga, Lindi, Kigoma, Posta House, Sokoine Drive, Dar es Salaam GPO, Songea, Mwanza, Bukoba, Arusha, Karatu, USA River, Iringa, Shinyanga, Chuo Kikuu Mzumbe, ikiwa ni pamoja na Kijangwani, Shangani, Chake Chake, Mkoani, Posta Kongwe na Wete kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kampuni ya Simu litatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuongeza tija na ufanisi wa Kampuni kwa kuboresha mapato kutoka Sh. bilioni 89 mwaka 2011 hadi Sh. bilioni 110 mwaka 2012;

(ii) Itaongeza idadi ya wateja wake wa huduma mbalimbali za simu (*voice* na *data*);

(iii) Itaboresha huduma kwa wateja kwa kuweka mitambo *(switches)* ya Kisasa inayotumia teknolojia ya *Next Generation Network* kwa kuondoa mitambo ya simu ya zamani aina ya *NEAX, AXE10, DTS* na *GX 5000*; pia kurekebisha njia za simu zilizoharibika pamoja na kuboresha huduma kwa wateja ili kukidhi mahitaji halisi ya kibiashara ya simu na data;

(iv) Itapanua Mtandao wa intaneti (*Fixed and Wireless Broadband Services)* kwenye miji mikubwa nane (8) Tanzania Bara na Visiwani kwa kuongeza vituo vya mtambo (*BTS*). Miji mikubwa itakayohusika na mpango huu ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Morogoro, Moshi na Zanzibar; na

(v) Kuendelea kushiriki kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, pamoja na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Itaendelea na kuratibu utekelezaji wa mfumo mpya wa utangazaji wa digitali (*Digital Broadcasting*) kwa kutoa elimu kwa umma na watoa huduma za mawasiliano kulingana na kanuni na Sheria husika;

(ii) Itaboresha mifumo itokanayo na utangazaji katika mfumo wa teknolojia ya digitali kama ifuatavyo:-

(a) Kuweka viwango vya gharama za kurusha vipindi *(transmission fees)* wanavyotozwa watengeneza vipindi (*Content Services Providers*) na wasimika miundombinu ya utangazaji (*Multiplex Operators*);

(b) Kusimamia utekelezaji wa muingiliano wa ving'amuzi (*Inter-operability of Set-Top-Boxes);*

(c) Kusimamia ubora wa ving'amuzi na kuweka mpango wa kusitisha uagizaji wa luninga za analojia;

(d) Kuwezesha uboreshaji wa mifumo ya utengenezaji wa maudhui ili kukidhi ongezeko la wigo wa masafa unaotokana na teknolojia ya digitali; na

(e) Kuweka mifumo na kanuni za utoaji wa huduma mbadala za digitali kama vile

matangazo ya televisheni kwenye simu, huduma za kibenki, afya na nyinginezo.

(iii) Itaendelea kupokea na kutathmini maombi ya leseni;

(iv) Itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa huduma za mawasiliano kwa kufanyia kazi ukaguzi kampuni zilizosajiliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vilivyowekwa kwenye leseni zao; na

(v) Itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika utelekezaji na utoaji wa elimu kwa wadau wa mradi wa kitaifa wa Mfumo mpya wa anuani za makazi na Simbo za Posta (*Post Code Project*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)* utatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Utasimamia utekelezaji wa makubaliano na watoa huduma za mawasiliano ya kupeleka huduma katika maeneo yaliyoainishwa kulingana na mikataba baina ya pande hizi mbili;

(ii) Utaendelea kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara na kuanzisha miradi itakayohakikisha mawasiliano yanafika kwenye maeneo hayo kwa kushirikiana na

wadau wa sekta kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwenye zabuni ya miradi ya awali ya Mfuko;

(iii) Utaanzisha vituo vya mawasiliano vya jamii na kupeleka huduma za intaneti kwenye shule kwa ushirikiano na jamii na miundombinu iliyopo; na

(iv) Utaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya Posta kuhakiki mahitaji ya huduma za posta na namna ya kuziboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Malengo katika mpango wa muda wa kati na mrefu. Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau wengine kutoka sekta ya umma na sekta binafsi inaazimia kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeazimia kutekeleza yafuatayo katika sekta ya mawasiliano:-

(i) Kukamilisha mabadiliko ya mfumo wa utangazaji, kutoka analojia kwenda dijitali;

(ii) Kutekeleza Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta *(Physical Addressing and Post Code System)*;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mawasiliano na haki za watumiaji wa huduma;

(iv) Kuboresha utoaji wa huduma za simu katika sehemu zisizo na mvuto kibiashara;

(v) Kuendeleza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*The National ICT broadband Backbone Infrastructure*) katika awamu ya III;

(vi) Kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa Vituo Vikuu vya Kumbukumbu (*Mega Data Center*); na

(vii) Kuandaa Sera ya Usalama wa TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Wizara imeazimia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(ii) Kuratibu uboreshaji na upanuaji wa taasisi za sayansi na teknolojia nchini;

(iii) Kuweka na kusimamia utaratibu wa usajili na kulinda haki miliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti na wagunduzi;

(iv) Kuendelea kuratibu mahusiano ya kikanda na kimataifa katika nyanja za sayansi na teknolojia;

(v) Kuendelea kuandaa na kuhuisha sera na sheria za sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa sera hizo; na

(vi) Kukamilisha Andiko la Programu ya Matumizi Salama ya Teknolojia za Nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na taasisi za fedha kwa misaada yao ambayo imeiwezesha Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza baadhi ya malengo yake muhimu. Wahisani hao ni pamoja na Serikali za Marekani, Sweden, Norway, Finland, Uholanzi, Japan, Italia, Afrika Kusini, Jamhuri ya Korea, China na India. Mashirika wahisani ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, KOICA, UNESCO, UNCTAD, UPU na ITU. Mashirika ya fedha ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Benki ya Exim ya China. Aidha, naishukuru sana sekta binafsi kwa mchango wao katika kuendeleza sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika

mwaka wa fedha 2012/2013 yamekadiriwa kuwa Sh. 70,107,712,000. Kiasi hicho cha fedha kimepangwa kutumika kama ifuatavyo:-

Mchanganuo wa Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013

1. Mishahara Makao Makuu 1,628,205,000
   Taasisi 21,640,905,000

2. Matumizi Mengineyo (OC) 7,006,176,914

**Jumla ya Matumizi ya Kawaida 30,275,286,914**

3. Fedha za Maendeleo za ndani 38,706,547,000
4. Fedha za Maendeleo za nje 1,125,878,000
   Jumla ya fedha za Maendeleo 39,832,425,000

**JUMLA KUU 70,107,712,000**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza mipango yake iliyojiwekea katika mwaka wa wa fedha 2012/2013, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha matumizi ya jumla ya Sh 70,107,712,000 kwa mchanganuo ulioelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu hii. Hotuba hii itapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni www.mst.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JUMA A. KAPUYA - (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii, kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba niungane na wenzangu kutoa pole na kuwaombea ndugu wa marehemu ambao waliathirika katika ajali ya M.V. Skagit. Mungu awape subira *inna lillahi walahillah rajuuni.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Januari Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Ni imani ya Kamati hii kuwa atatekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Naipongeza pia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa ujumla kwa maandalizi na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2012/2013. Aidha, Wizara iliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati na utekelezaji wa Bajeti ya mwaka uliopita wa 2011/2012 na kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha wa 2012/2013; ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa majadiliano ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/2012. Mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamati ilitoa mapendekezo kadhaa kwa ajili ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha. Kamati inashauri Serikali ipunguze urasimu katika utekelezaji wa majukumu yake kwani, kwa mwaka mzima, utekelezaji wa maagizo mengi ulikuwa bado uko kwenye mchakato au juhudi zilikuwa zikiendelea hata kwa masuala yaliyo ndani ya uwezo wa Wizara. Kwa mfano, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)* ni mwaka wa saba tangu uanzishwe na mwaka mzima wa 2011/2012, Wizara imekuwa katika mchakato wa zabuni ambayo hata hivyo haikukamilika. Kamati inaendelea kuishauri Wizara kwamba maagizo yote

ambayo hayajatekelezwa yakamilishwe na taarifa ya utekelezaji wake utolewe kabla ya bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2011/2012. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Sh.2,012,000/= kama mapato ya Serikali. Hadi kufikia Mei, 2012, Wizara ilikusanya jumla ya Sh.5,208,900/= ambazo sehemu kubwa ya fedha hizo zilitokana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali, mishahara isiyolipwa na marejesho ya masurufu ikiwa ni ongezeko la asilimia 258.9% ya makisio kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 ziliidhinishwa jumla ya Sh.64,017,516,000/=, kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa Sh.23,799,259,000/= na shughuli za maendeleo zilikuwa ni Sh.40,218, 257,000/= ambapo kati ya fedha za maendeleo Sh.38,195,679,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na Sh.2,022,578,000/= zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 4 Juni, 2012 jumla ya Sh.29,766,634,534.85/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo zilikuwa zimetolewa ambayo ni sawa na asilimia 46.49 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii. Huu ni mwendelezo wa Serikali kutoa fedha pungufu kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo na mpango wa bajeti kwa mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inakadiriwa kuwa na matumizi ya jumla

shilingi bilioni 70,107,712,000/= ambapo shilingi bilioni 30,275,286,914/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.39,832,425,000/= ni kwa ajili ya maendeleo ambazo kati ya hizo Sh.38,706,547,000/= ni fedha za ndani na Sh.1,125,878,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati baada ya kuujadili mpango na bajeti hiyo kwa kina, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kupanga kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha nyingi kutoka vyanzo vya ndani. Pesa zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni jumla ya Sh.39,832,425,000/= ambapo fedha za ndani ni Sh.38,706,547,000/= na Sh.1,125,878,000/= ni pesa kutoka vyanzo vya nje ambayo ni 2.8% ya fedha ya maendeleo iliyokadiriwa. Uzoefu umeonyesha kuwa fedha nyingi zinazoahidiwa na wafadhili huwa hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitimii au kutototolewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa kutekelezwa kutokana na kutokutolewa kwa ukamilifu fedha kwa ajili ya miradi hiyo. Jumla ya fedha kutoka vyanzo vya ndani iliyokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ilikuwa ni Sh.38,195,679,000/=, iliyokuwa imetolewa hadi Mei, 2012 ni Sh. 8,744,060,000/= sawa na 22.9% tu. Kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 hata kama 77.1% ya fedha yote iliyobaki ilitolewa baada ya mwezi Mei, 2012 miradi iliyopangwa haingeweza kutekelezwa ipasavyo ndani ya mwezi

mmoja. Ni matumaini ya Kamati kuwa mwenendo huu wa utekelezaji wa miradi hautajirudia tena katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta na Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta. Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta ni utekelezaji wa Sera ya Posta ya mwaka 2003 ambayo ilibainisha umuhimu wake kwa maendeleo ya ya Taifa letu. Kwa makadirio ya mwaka 2009 mradi ulitarajiwa kugharimiu shilingi bilioni 158 ambazo zingechangiwa baina ya Wizara hii na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo, kwa kupitia Halmashauri, pia ingetenga fedha pamoja na kupima maeneo yatakayohusika na mradi huu. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa ukisuasua kwani mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitenga Sh.150,000,000/= na mwaka huu wa fedha imetenga Sh.709,518,000/=. Kutokana na ufinyu wa bajeti Halmashauri zote hazijawahi kuchangia kiasi chochote kwenye maendeleo ya mradi huu. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mapema mradi huu muhimu. Wizara hizi zishirikiane kwa karibu kwa vile mradi huu ukikamilika utasaidia kufanikisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara, kijamii pamoja na utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kushauri kuwa Serikali iendelee kuimarisha Shirika la Posta nchini, pamoja na mambo mengine ilipatie mtaji utakaowezesha kuweka mitandao ya kompyuta (*internet)* katika utoaji wa huduma zake ili kuhimili ushindani unaotokana na mabadiliko ya teknolojia.

Shirika pia lifanye juhudi ya kutangaza huduma zake ili wananchi wazielewe na kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano ya Simu. Kwa namna ya pekee Kamati yangu inayapongeza Makampuni ya Simu za Mikononi kwa jitihada zao za kupanua huduma za mawasiliano ya simu hadi vijijini. Makampuni ya simu yamechangia kuboresha maisha ya Watanzania kwa kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania kwa ajira ya moja kwa moja au kwa kupitia biashara zinazotokana na huduma za simu pia kwa kudhamini shughuli mbalimbali za maendeleo. Kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya nchi yetu katika taarifa yake ya mwaka 2011/2012, Kamati iliishauri Serikali kuoanisha tozo zote zinazopaswa kulipwa na makampuni ya simu kwa Halmashauri badala ya hali ya sasa ambapo kila Halmashauri inajipangia yenyewe na hivyo kuleta mkanganyiko kwa wawekezaji. Hata hivyo, tarehe 7 Juni, 2012, Kamati ilielezwa kuwa majadiliano yalikuwa yanaendelea baina ya wadau ambao ni ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano Tanzania na Tume ya Taifa ya Mazingira *(NEMC).* Kamati inaitaka Serikali kuharakisha mchakato huo wa majadiliano kwa kuhakikisha kuwa unakamilika ndani ya mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2006 Sheria ilitungwa ili kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(Universal Communication Access Fund)* kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma za mawasiliano maeneo

mbalimbali vijijini. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa na ucheleweshaji wa utekelezaji wa Mfuko huo kwani tangu mwaka 2006 mpaka mwezi Februari, 2011 watendaji bado walikuwa wanajipanga na sasa bado wanafanya tathmini ya kitaalamu ya mahitaji ya fedha na mbinu bora za kufikisha mawasiliano katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* imeonyesha uwezo wa kujiendesha kwa mafanikio na ufanisi mkubwa endapo itawezeshwa kimtaji na menejimenti hii ni pamoja na kutoa huduma za maunganisho ndani na nje ya nchi. Hadi hivi sasa, *TTCL* ndio kampuni pekee ya simu nchini iliyofanikiwa kuunganisha nchi za jirani kama vile Zambia, Rwanda na Malawi ili kutoa huduma za mawasiliano za nchi nyingine duniani hasa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia ipo katika hatua za kukamilisha mkataba kati yake na *TTCL* ili iweze kutoa huduma za *Internet* za Kimataifa kupitia Mkongo wa baharini wa *SEACOM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa *TTCL* inafanya majadiliano ya kibiashara na kampuni mbalimbali ikiwemo *NEC Corporation* ya Japani ili kuanzisha ushirikiano wa kibiashara na kuendeleza mtandao wa *TTCL* pamoja na nia hiyo nzuri, Kamati inashauri menejimenti kuwa makini ili makubaliano yatakayofikiwa baada ya majadiliano hayo yawe na manufaa kwa *TTCL* na Taifa kwa ujumla. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kusimamia Wizara na Taasisi zake ambazo zilikuwa zinadaiwa na *TTCL* kulipa madeni

haya kwa mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ambazo zilifikia kiasi cha shilingi bilioni 6.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu inaamini kwa dhati kabisa kwamba sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ndiyo mhimili wa maendeleo na uchumi wa kisasa tunaotaka kuujenga. Hapa nchini kwa sasa simu ya mkononi sio tu ni kwa ajili ya kuzungumza, bali ni benki ya kuhifadhia na kutuma fedha ni kiungo cha kuingia kwenye mtandao wa *internet* na kiungo cha kupata taarifa mbalimbali, ikiwemo bei za mazao, milipuko ya magonjwa na mambo mengineyo muhimu kwa ustawi wa maisha ya Mtanzania. Mawasiliano ni uwezeshaji muhimu kama ilivyo mitaji mingine na pia ni kivutio cha uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, kama nchi yetu inataka kupiga hatua ya maendeleo kwa haraka, ni lazima mawasiliano yapatikane kwa watu wote, kwa wakati wote na kwa gharama wanayoweza kuimudu. Kwa sasa, hali haiko hivyo kwani maeneo mengi nchini hakuna mitandao ya simu za mikononi. Kwa mfano Kata zifuatazo hazina kabisa minara ya simu au mitandao ya simu. Kata ya Igwisi kule Wilaya mpya ya Kaliua, Saswi, Ichemba, Kanoge, Mwongozo, Silambo na kijiji cha Ilindonne hawana kabisa mtandao hii. Pia bei ya kupiga simu ni kubwa hasa kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine. Kamati inaendelea kuishauri Serikali iyashawishi makampuni ya simu kuondoa gharama za kupiga simu kati ya mtandao mmoja na mwingine *(interconnection charges*). Kuondoa gharama hizi kutawapunguzia Watanzania gharama za kutumia simu na kutembea

na simu zaidi ya moja, kuwa na *simcards* zaidi ya moja. Kamati inashauri makampuni ya simu yashindane kwa bei zao, kwa mawanda *(scope)* ya mitandao yao mpaka vijijini, ubora wa mitandao, huduma bora kwa mteja (*customer care)* na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Sayansi, Taasisi na Vyuo vya Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa kuna Watanzania wenye vipaji vya ugunduzi, kwa mara nyingine Kamati inaishauri Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuhamasisha ugunduzi huo kwa kutunga sera maalum na sheria ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazogunduliwa *(prototypes)* zinatengenezwa kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Hii itaokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa elimu ya Sayansi iimarishwe katika shule za msingi pamoja na sekondari; ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa Walimu wa masomo ya sayansi na kujengwa kwa maabara ili kuwaandaa vijana kwa ajili ya masomo ya sayansi. Hata hivyo elimu ya sayansi haitakuwa na maana iwapo Wagunduzi wetu hawatiwi moyo na kupewa fursa ya kuonyesha ugunduzi wao na vipaji vyao kwani sayansi tunayoisisitiza leo zao la gunduzi mbalimbali zilizofanywa miaka iliyopita. Kamati inapongeza Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa kutambua vipaji vya Wagunduzi ikiwemo Taasisi na watu binafsi na kutoa Tuzo mbalimbali. Hata hivyo Tunzo na fedha hizo hazitakuwa na maana iwapo gunduzi zao haziendelezwa na kunufaisha jamii. Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa 2011/2012 ilitoa Tuzo

kwa wabunifu binafsi sita na Taasisi tatu, naomba kuwatambua Wagunduzi hao kwa kuwataja majina pamoja na kazi zao kama ifuatavyo:-

(i) Ndugu Elias M. Msengi - Mgunduzi wa lami ya kutengeneza barabara itokanayo na mmea wa mnyaa;

(ii) Ndugu Natalia Mwenda - Mgunduzi wa *search engine* iitwayo *Rasello.com* inayoweza kuainisha na kutambua maneno mbalimbali ya Afrika Mashariki;

(iii) Ndugu Castor Felix Turuka - Mvumbuzi wa gari litumialo injini ya pikipiki yenye ukubwa wa 125 cc na yenye kuweza kuvuta mzigo wa zaidi ya kilogram 750;

(iv) Ndugu Said Omary Said - Mvumbuzi wa gari "SUGU II-Car" litumialo jenereta ya 5.5 HP na *clutch system* inayotumia *pulleys* zilizounganishwa na *gear box*;

(v) Ndugu George Buchafwe - Mgunduzi wa mashine ya kutengenezea sabuni;

(vi) Ramadhani Omary - Mgunduzi wa *Spark Plug* ya gari yenye kiwango kidogo cha hewa-ukaa (hewa zinazoongeza joto);

(vii) Tanzania *Coffee Research Institute* iliyoko Moshi.

(a) Utafiti na uendelezaji wa aina ya kahawa yenye mazao mengi, yenye kuvumilia magonjwa na yenye ubora wa hali ya juu.

(b) Utafiti na uendeshaji wa aina ya kahawa isiyoshambuliwa na minyoo fundo (*Nematodes).*

(c) Utafiti wa teknolojia mbalimbali za kusindika kahawa.

(d) Utafiti wa teknolojia za kulinda utunzaji na uwepo wa mbolea kwenye udongo.

(Viii) *Kisangani Smith Group* - Mgunduzi wa jiko la kutumia mabaki ya mimea lisilo na moshi, kwa matumizi ya ndani ya nyumba. Teknolojia hii inapunguza uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miti. Mgunduzi ameweza kufundisha na kusambaza teknolojia hii kwa watu zaidi ya 300 Wilayani Njombe; na

(ix) AMREF Tanzania – Mgunduzi wa teknolojia ya *Solar Pump* kwa matumizi ya usambazaji wa maj ya visima katika jumuiya za Mtwara Vijijini. Teknolojia hii hupunguza matumizi ya genereta za kusukuma maji na hivyo kupunguza hewa-joto na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha nyingi zinatumika kuagiza bidhaa nje ya nchi wakati tuna wabunifu, Kamati inashauri Serikali itoe maelezo ya mikakati inayopimika ya namna inavyotumia Wagunduzi hawa na wengine watakaojitokeza hapo

baadaye na kazi zao katika kukuza vipaji vyao na kuwezesha uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na gunduzi zao kwa manufaa na maendeleo ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kukamilisha sheria ya kulinda gunduzi hizi.

Aidha, kwa kuwa Bunge lako limekuwa na utamaduni mzuri wa kuwatambua watu mbalimbali wanaoliletea Taifa letu mafanikio kuja hapa Bungeni na kuwapongeza, Kamati inashauri Wizara ifanye utaratibu wa kuwaleta hapa Bungeni Wagunduzi hao wakiwa na kazi zao. Hatua hii itawatia moyo na kuhamasisha wengine kufanya mambo mazuri kama Wagunduzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vyuo vya Serikali vilivyojikita katika kutoa Shahada za Sayansi na Uhandisi hapa nchini ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela cha Arusha, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya. Vyuo hivi vina wataalam wengi wenye sifa za kihandisi na wanaweza kubuni vitu mbalimbali na kufanya tafiti zinazoweza kuwa na manufaa kwa jamii. Ili kuepuka kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi, Kamati inashauri kuwepo kwa kiunganishi baina ya watalaam na wabunifu kutoka vyuo na taasisi hizi na watumiaji wa utaalam huo katika jamii. Aidha, kwa kuwa taasisi hizi zinafanya kazi zinazofanana ziunganishwe kwenye mtandao ili kubadilishana uzoefu na kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela cha Arusha, ni cha Kimataifa na bado ni kipya. Kwa sasa miundombinu na majengo yake mengi ni mapya. Aidha, chuo kimeshaanza kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Kamati inashauri Serikali ijipange kuhakikisha kuwa majengo na miundombinu ya chuo hiki yanakarabatiwa mara kwa mara ili yasichakae na kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi zilizoendelea tafiti nyingi za kisayansi zinafanywa na Majeshi, Vyuo Vikuu na Taasisi za Sayansi na Teknolojia na unapewa kipaumbele. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka mazingira mazuri na kuzijengea uwezo wa kifedha Taasisi zetu, kujenga maabara za kisasa zenye vifaa na mashine za kutosha kuwawezesha Wahandisi na Wataalam wetu kufanyia kazi zao za kiutafiti; kujenga karakana zenye sifa na viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inashauri kuwa vyuo vinavyotoa elimu ya ufundi kama vile ngazi ya Fundi Mchundo viendelee kuwepo ili kukidhi mahitaji ya kuwa na mafundi wa kufanya kazi chini ya Wahandisi kwa uwiano unaohitajika kitaalamu badala ya hali ya sasa kuwa vyuo vyote vilivyokuwa vinatoa Mafundi Mchundo vinataka kugeuzwa kuwa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vyetu vinazalisha wataalam wazuri sana. Kwa mfano, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam *(DIT)* wataalamu wake wana uwezo wa kupima udongo kwa njia ya kitaalamu

zaidi kabla ya kuanza kutumiwa katika shughuli mbalimbali kama ujenzi wa majengo ya Serikali pamoja na nyumba za watu binafsi. Kamati inashauri Serikali na wananchi kuitumia kikamilifu Taasisi hii ili kupata nyumba na majengo yenye viwango bora kwa kuzingatia kuwa Taasisi hii ina uwezo huo badala ya kujenga bila kujua hali ya udongo na hivyo kuhatarisha usalama na uimara wa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuongeza fedha katika bajeti ya Taasisi hii ili kuongeza utendaji wa chuo katika utoaji wa elimu kwa vitendo, utafiti, utoaji wa ushauri wa kitaalamu kwa jamii na ukarabati wa miundombinu ya Taasisi kwa ujumla ikiwemo karakana na mabweni ya wanafunzi ambayo yanahiji fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo, hii itasaidia kuvutia usajili wa wanafunzi wa katika chuo hiki na kuongeza wataalam wa Sayansi, Uhandisi na Ufundi. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kutangaza shughuli zinazofanywa na chuo hiki ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa mfumo wa magari unaotumia gesi badala ya petroli, utengenezaji wa hadithi za watoto na matangazo mbalimbali ya biashara kwa njia ya katuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa madini ya urani. Kuna taarifa za kwamba uchimbaji wa madini hayo unaanza hivi karibuni. Kwa kuwa madini haya yanahitaji uangalifu mkubwa na usalama wake usipozingatiwa athari zake ni kubwa sana kwa afya ya watu na viumbe wengine. Kamati inaendelea kushauri itungwe sheria na kanuni za uchimbaji na matumizi ya madini haya ili shughuli hiyo iweze kuleta manufaa

katika maendeleo ya nchini yetu. Ifahamike kuwa mionzi ya madini haya na nishati ya nyuklia ni hatari sana na ni suala linalotatiza dunia kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na hatari hii Dr. Gordon Edwards katika mada yake ya Uranium*. Known Facts and Hidden Dangers* iliyotolewa katika Mkutano wa *World Uranium Hearings* alisema, nanukuu:-

"*And so this one material, uranium, is responsible for introducing into the human environment a tremendously large range of radioactive materials which are all very inimical to biological organisms. These are not invisible rays, they are materials. They get into our water, our food, and the air we breathe. They're exactly like other materials except for the fact that they're radioactive".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi alisema:-

*"Hii ndiyo urani, ndiyo inayohusika kuingiza katika mazingira ya wanadamu miozi ya aina mbalimbali ambayo yote ni hatari sana kwa viumbe hai. Hii ni mionzi isiyoonekana, lakini ipo. Inaingia kwenye maji yetu, vyakula vyetu na kwenye hewa tunayovuta. Yako kama vitu vingine isipokuwa ukweli ni kwamba ni mionzi"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali pengine Dr. Gordon Edwards anasema, nanukuu:-

*"All uranium ends up as either nuclear weapons or highly radioactive waste from nuclear reactors. That's the destiny of all the uranium that's mined. And in the process of mining the uranium we liberate these naturally occurring radioactive substances, which are among the most harmful materials known to science."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri isiyo rasmi inasema:-

*"Urani yote inaishia kuwa ama silaha za nyuklia au mabaki ya mionzi kutoka katika vinu vya nyuklia ambayo ni hatari sana. Hiyo ndiyo hatma ya urani tunayoichimba na katika mchakato wa kuchimba urani tunaruhusu hii mionzi iliyokuwa kwenye uasili wake kutoka, ambayo ndiyo hatari kuliko vitu vyote vinavyotambuliwa na sayansi."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia taasisi ya *Green Peace* ya Uingereza ikielezea namna Uingereza inavyotatizwa na mabaki ya madini ya urani inasema, nanukuu:-

*"The UK now has enough radioactive waste to fill the Royal Albert Hall five times over. There's still no safe way to deal with it. The government plans to bury it deep underground - out of sight, out of mind, for now at least. But no one can guarantee that this highly radioactive waste won't leak back into the environment, contaminating water supplies and the food chain."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake isiyo rasmi ni:-

*"Kwa sasa Uingereza ina mabaki ya kutosha kujaza ukumbi wa Royal Albert zaidi ya mara tano. Hakuna namna ya salama ya kuyashughulikia. Serikali inapanga kuifukia chini kabisa ardhini angalau kwa sasa isionekane na hata isifikiriwe lakini hakuna anayeweza kuwa na uhakika kwamba mabaki haya mionzi yake haitavuja na kuharibu maji na mnyororo wa chakula".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo nia ya Kamati kupinga uchimbaji wa madini haya. Hata hivyo ni wajibu wa kizazi hiki kuamua kufanya mambo ambayo hayana athari kwa kizazi chetu na kijacho na inapoamua kufanya ichukue kila tahadhari katika kushughulikia uchimbaji wa madini haya, kuyatunza na kuyatayarisha na kuyatumia. Aidha, kuwe na uhusiano wa karibu baina ya Wizara ya Nishati na Madini na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ili kuratibu shughuli za uchimbaji na uhifadhi salama wa madini ya urani. Pia ni muhimu kuwepo na maandalizi ya kutosha ya wataalamu wa nguvu za Atomiki ili kuhakikisha usalama wa madini hayo na uandaaji wa mikataba mizuri yenye maslahi kwa taifa na tusiwaachie wageni peke yao kushughulikia madini haya kwani wao hawana uchungu na nchi yetu wana uchungu na maslahi yao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TEHAMA. Ili kwenda na wakati katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia hasa katika masuala ya TEKNOHAMA, Kamati inashauri Ofisi ya Bunge na Wabunge waanze kutumia mfumo wa kompyuta katika kufanya mawasiliano na kupeana nyaraka mbalimbali. Mfumo huu utapunguza

Wabunge kubeba nyaraka nyingi badala yake nyaraka zitatumwa kwenye mtandao na kuwawezesha kusoma humo au kuzichapisha zile anazozihitaji tu. Kwa sasa Ofisi ya Bunge inaingia gharama kubwa kwa ajili ya uchapishaji wa nyaraka hizi. Kwa mfano, ukiondoa gharama wino, nguvu kazi, kuhudumia mashine na mengineyo karibu Sh.33,000,000 kwa mwaka zinatumika kwa ajili ya kununulia karatasi tu kwa ajili ya kuandaa Orodha ya shughuli za Bunge, Taarifa za Kamati na wasemaji wa Upinzani na *Hansard,* lakini Kamati inaamini kuwa kuingiza nyaraka hizi kwenye mtandao hakugharimu fedha zaidi ya nguvu kazi kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inajiandaa kuingia kwenye Serikali mtandao (e-*Government*) na imeunda wakala wa kuratibu Serikali mtandao. Kwa hatua hiyo inamaanisha kwamba Serikali itakuwa inafanya kazi kupitia mtandao na maamuzi na maelekezo katika ngazi mbalimbali za uongozi Serikalini yatatolewa kupitia mtandao. Kutokana na azma hii ya kutumia Serikali mtandao, Kamati inashauri sheria na kanuni zote zinazokinzana na azma hii zirekebishwe ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia ya mawasiliano inabadilika kwa kasi na hivyo kuwa na athari chanya na hasi pia. Siku hizi kuna uhalifu *(cyber crime)* mwingi unaofanywa kwa kutumia teknolojia hii ikiwemo wizi wa fedha, kamari zisizo halali kuharibu kompyuta za watu kwa kutengeneza *virus*, kutuma, kutunza, kusambaza na kuiba taarifa isivyo halali. Kutokana na masuala haya na mengine yanayoweza kujitokeza, ni vema

Serikali iandae sheria na kanuni ili kudhibiti uhalifu wa aina hii kutumika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya mtandao katika shughuli mbalimbali za kijamii na uchumi yamepanuka sana ikiwemo kufanya biashara, kupata elimu na kuhitimu, kulipia ankara mbalimbali na mengineyo kufanyika kwa njia ya mtandao. Kutokana na matumizi haya, Kamati inashauri Serikali itoe elimu kwa wananchi ili wajue haki na wajibu wao wakati wanatumia mitandao hiyo. Aidha, Kamati inawashauri Watanzania wanaotaka kufanya biashara kwa njia ya mtandao na makampuni nje ya nchi wajiridhishe kuhusu uwepo na uhalali wa makampuni hayo kabla ya kufanya malipo ili kuepuka kutapeliwa kwani kuna baadhi ya makampuni ni batili na yanaendeshwa na watu wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kupanuka kwa matumizi ya mtandao katika nyanja mbalimbali za maisha, Kamati inashauri kuwe na kitengo maalum kitakachoratibu na kufuatilia matumizi ya mitandao hapa nchini. Kamati inafahamu kuwa masuala ya mwasiliano yanaratibiwa na Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano Tanzania, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, masuala ya Utumishi na uendeshaji wa Serikali mtandao yanasimamiwa na Tume ya Utumishi wa Umma na mengineyo. Kamati inaishauri kuwa taasisi moja ipewe majukumu ya kusimamia matumizi ya mtandao kwa ujumla wake na taasisi zingine zisimamie mtandao unaohusika na majukumu ya taasisi husika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa kwa sasa Serikali imeanzisha Wakala wa Serikali Mtandao *(e-government Agency*) na Tume ya TEHAMA *(ICT Commission).* Kamati inataka kujua majukumu ya kila Taasisi hizi na kama hakutakuwa na migongano katika utekelezaji wa majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Ili Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia iweze kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka 2012/2013, inaomba iidhinishiwe jumla ya Sh.70,107,712,000/=. Kati ya hizo fedha za Matumizi ya Kawaida ni Sh.30,275,286,000/=. Aidha, fedha za Bajeti ya Maendeleo zinazoombwa ni Sh. 39,832,425,000/=, kati ya hizo Sh.38,706,547,000/= ni fedha za ndani na Sh.1,125,878,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na kupitia kifungu kwa kifungu na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya Sh. 70,107,712,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mb, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mb, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Dkt.

Florens M. Turuka, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano wao ambao umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka wakati wa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba, kwa heshima kubwa, niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Inocent Edward Kalogeresi, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikira, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mheshimiwa Mbarouk Rajab Mohamed, Mheshimiwa Faith

Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya na Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashililllah, Katibu wa Kamati, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Msaidizi wake wa karibu Ndugu Happy Ndalu kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niwashukuru sana wananchi wa Urambo Magharibi ambao sasa ndiyo Wilaya mpya ya Kaliua, kwa ushirikiano na mshikamano wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kufanya kazi hizi kwa makini na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu Tatu, watoto na wajukuu zangu wote kwa utulivu wanaonipa ili kuweza kutekeleza majukumu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwapa pongezi viongozi wapya wa Wilaya ya Kaliua ambao wameteuliwa wakiongozwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Zavel Maketa, *OCD* wetu Bwana Shana, Katibu wa Wilaya wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Yawoo, Katibu wa UWT Wilaya, Teresia Martin na Afisa Usalama wa Wilaya, ndugu Rebecca. Nataka niwahakikishie kwamba mimi na wananchi wa Kaliua tuna imani na nyie, tutashirikiana na nyie bila kumsahau Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Fatuma Maswa kwa jinsi ambavyo amejitoa kuisadia Wilaya ya Kaliua na sasa inaanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa pongezi sana kwa timu ya Simba kwa kuonyesha kwamba wanaweza kujitolea kuilea timu changa kama Azam pamoja na matokeo ya jana. Simba hawafanani kabisa na wale jamaa wengine ambao baada ya kufungwa 3-1 na salamu imebadilika sasa hivi imekuwa "*Ghwi! Ghwa!*" kwa kusalimiana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele yenu maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyenzi Mungu, ambaye kwa neema zake imempendeza ya kuwa leo nisimame kwenye mimbari hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuendelea kunipigania siku zote na sasa nimesimama hapa ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa chama changu –CHADEMA kwa kiniteua na mwishowe kunipigania na hadi kuwa Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki. Sambamba na hilo nimshukuru sana Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, kwa kutupa dhamana ya kuisimamia Wizara hii yenye changamoto nyingi mimi pamoja na Waziri Kivuli Mheshimiwa Suzan Anselm Lyimo. Tunapenda kumhakikishia kuwa tutatekeleza wajibu wetu kwa uwezo na nguvu zetu zote kama yalivyo matarajio ya Watanzania kwa chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niwashukuru sana wazazi na familia nzima ya Mchungaji Samwel Meiyackyi Nassari ambayo imenilea, kuniombea, kunitia moyo na kunisomesha kwa shida, mpaka kufika hapa nilipofika leo. Ninawashukuru sana wazazi wangu

hawa kwa kunilea kwenye njia ipasayo na ninawaomba wazidi kuniombea na kunitia moyo, ipo siku tutafika nchi ya ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashuru sana Makamanda wote wa CHADEMA, wapenda haki, Wabunge na wasiokuwa Wabunge, ambao waliacha familia zao na wakapiga kambi Arumeru Mashariki kuhakikisha kuwa haki inatendeka na hatimaye kupata chaguo sahihi la wananchi kupitia sanduku la kura siku ile ya tarehe mosi, Aprili 2012. Niwahahidi kwamba kama tulivyosema “tulianza na Mungu, ndivyo Tutakavyomaliza na Mungu”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru sana Mameneja wangu wa Kampeni Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Israel Natse na *Operation Commander*, Ndugu John Mrema kwa kazi kubwa isiyoelezeka waliyoifanya kule Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimshukuru sana Kaka na Rafiki yangu wa siku nyingi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, Ndugu Godbless Lema. Najua yupo likizo fupi lakini atarejea mapema, ili kwa pamoja tuendelee na harakati za kuifikia nchi ya ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya sayansi na teknolojia katika maendeleo ya nchi. Kambi Upinzani inaendelea kusisitiza kuwa tofauti kubwa kuliko zote ya kimaendeleo baina ya nchi zilizoendelea na nchi ambazo zinaendelea hukutwa katika mambo mawili:-

(i) Ubora na Uenevu wa Elimu ya Sayansi na Teknolojia na Uimara wa Vyuo na Taasisi za kisayansi; na

(ii) Kiwango cha usambaaji na utumiaji wa sayansi na teknolojia katika maeneo mbalimbali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi huanza kupiga hatua za kimaendeleo inapokamilisha zoezi la kuhawilisha sayansi na teknolojia katika maeneo mbalimbali ya uchumi na maisha, mijini na vijijini na kuanza kufanya ugunduzi katika maeneo mbalimbali ambayo yanalenga utatuzi wa matatizo yanayowakabili wananchi wake. Bila kufanya hivyo, maendeleo hayawezi kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ina shughuli kuu mbili; kukuza Teknolojia ya Mawasiliano katika vipengele vyake vyote na kukuza Sayansi na Teknolojia. Kambi ya Upinzani inahoji hivi inawezekana vipi kwa Wizara hii kuweza kutekeleza majukumu haya kwa kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 39.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Wizara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011, 2011/2012 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 71,071,600,000 kati ya fedha hizo shilingi 26,590,690,000 zilikuwa ni kwa ajili matumizi ya kawaida

na shilingi 44,426,910,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2011, fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa shilingi 21,927,092,337.84 sawa na asilimia 82.46 ya bajeti iliyotengwa na shilingi 21,672,706,747 zilipokelewa kwa ajili ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 49 ya bajeti nzima iliyotengwa. Utaratibu huu wa kupeleka fedha kidogo ambazo hazifikii hata nusu ya bajeti iliyotengwa hasa kwa miradi ya maendeleo ni kuifanya nchi yetu kuendelea kutegemea na kutumia teknolojia kutoka nje kwa kushindwa kuwa na teknolojia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 64,017,516,000 kati ya hizo shilingi 14,765,658,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 9,033,601,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 40,218,257,000 ni fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani na shilingi 2,022,578,000 fedha za maendeleo kutoka nchi wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mei, 2012, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi 29,673,390,411 sawa na asilimia 46.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 9,318,942,064 (shilingi 8,744,060,000 sawa na asilimia 21.7 ya fedha za ndani zilizotengwa na shilingi 574,882,064 sawa na asilimia 28.4 ya fedha kutoka nje) sawa na asilimia 31.4 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kwa utoaji huu wa fedha hususani katika mwaka wa fedha wa 2010/2011

na 2011/2012, inaonyesha wazi kuwa Serikali haina nia ya dhati kwa ajili ya kuendeleza sayansi na teknolojia kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 70,107,712,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, kati ya fedha hizo sh. 30,275,287,000 sawa na asilimia 43.2 ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo na shilingi 39,832,425,000 sawa na asilimia 56.8 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inashangaza na hasa kitendo cha Serikali kupunguza fedha kwa ajili ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 ambapo Serikali imetenga shilingi 39,832,425,000 ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2011/2012 ambapo Serikali ilitenga shilingi 40,218,257,000 kuna tofauti ya shilingi 385,832,000. Hii inaashiria wazi kuwa Serikali haioni umuhimu wa kuwekeza, kuendeleza na kukuza teknolojia katika nchi yetu. Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu sahihi ni kwa nini Serikali inapuuza kiasi hiki uwekezaji katika kukuza teknolojia nchini mwetu na hivyo kuendelea kudidimiza uchumi wa taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi, teknolojia na ubunifu, eneo la sayansi na teknolojia linazo taasisi na vituo vya utafiti vya umma takriban 90, ambavyo vinashirikishwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia. Taasisi na vituo hivi hushirikisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda na nishati, maliasili, afya na vyuo vikuu.

Kuna Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali ambazo zinaelekeza utendaji kazi katika taasisi na vyuo hivi. Kwa hakika bado kuna changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Sayansi na teknolojia ni nyenzo muhimu katika kumwezesha binadamu kuweza kumudu, kuhimili na kuyatumia mazingira yake kikamilifu katika kuweza kujiletea maendeleo. Hakuna popote duniani tunapoweza kutenganisha maendeleo yaliyofikiwa bila kuhusisha moja kwa moja maendeleo yake na kiwango cha ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumzia nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea, kinachotutenganisha ni ubora wa sayansi na teknolojia tunayotumia katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Nchi zote duniani zilizoendelea zimefikia hatua hiyo baada ya kufanya ugunduzi na mageuzi makubwa katika maendeleo ya sayansi na teknolojia hivyo nasi hatuna budi kufanya mapinduzi katika eneo hili kama tuna nia ya dhati katika kuwaletea maendeleo watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ina jukumu la kusimamia vituo vya utafiti vilivyopo nchini. Hivi sasa Tanzania ina jumla ya taasisi na vituo vya utafiti vya umma 79 vilivyoshirikishwa na Tume katika sekta zifuatazo: kilimo (18), mifugo na uvuvi (10), viwanda na nishati (8), maliasili (10), afya (8), vyuo vikuu (32). Sekta binafsi nazo zimeanza kuingia kwenye shughuli za utafiti na kwa hivi sasa kuna taasisi 11 za sekta binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali hapa nchini, (Chanzo:

Taarifa ya Wizara katika Maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na idadi kubwa ya vituo vya utafiti, Serikali imeshindwa kabisa kuviwezesha vituo hivi ili viweze kufanya tafiti zitakazoweza kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa matokeo ya tafiti hizo. Serikali imekuwa ikitoa ahadi nyingi na matumaini hewa katika utekelezaji na uendelezaji wa sekta hii muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekiri wazi kuwa tatizo la upungufu wa fedha umekuwa ukiathiri ufanisi wa shughuli za utafiti na maendeleo na katika kutatua tatizo hilo, Serikali ilitoa tamko la kutenga fedha kufikia asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti. Hata kwenye bajeti mbalimbali ambazo tumekuwa tukizitenga mfano ni kwa mwaka wa fedha 2010/2011 zilitengwa shilingi 30 bilioni kwa ajili ya tafiti, lakini tumeona ilikuwa ni ahadi hewa kwani Serikali ilishindwa kufikia lengo hilo na hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, Serikali iliweza kutoa Sh.19,494,651,700 sawa na asilimia 63.4 ya fedha zilizotengwa Sh. 30,746,000,000 kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuongeza kiwango hicho kwa bajeti zinazofuata hadi kufikia au kuzidi asilimia moja (1%) ya pato ghafi la Taifa, ahadi ambayo imekuwa haitekelezeki. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Serikali imetenga shilingi 22,455,914,000 zikiwa shilingi 21,474,961,000 fedha za ndani na shilingi 975,953,000 kwa ajili ya Tume ya

Sayansi na Teknolojia kugharamia miradi yote ya utafiti na kutoa mwanga kwa tafiti mbalimbali. Kiwango kilichotengwa ni kidogo ikilinganishwa na tamko la Serikali la kufikia asilimia moja ya pato ghafi la Taifa. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ni kwa nini Serikali imekuwa inatoa matamko bila ya kuyatekeleza? Mbona tumeweza kwenye bajeti za Vyama vya Siasa na Bunge, tunashindwa nini kutenga fedha kwa ajili ya eneo hili muhimu kwa uchumi wa Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinafika sehemu za vijijini, Serikali ilianzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ukiwa na madhumuni ya kusaidia juhudi za upelekaji wa mawasiliano ikiwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa wawekezaji watakaokuwa tayari kupeleka mawasiliano maeneo ya vijijini na mijini pasipokuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malengo haya mazuri, hakuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini wanapata mawasiliano kama ilivyo sehemu nyingi za mijini. Mfano katika bajeti ya mwaka 2011/2012, Serikali ilitenga shilingi 419,068,000 katika Mfuko wa Mawasiliano kwa wote na fedha zilizotolewa na Serikali ni shilingi 150,000,000 sawa na asilimia 36 tu ya fedha zilizotengwa. Kwa mwaka huu wa fedha Wizara imeomba shilingi 200,068,000 kwa ajili ya mfuko huo ikiwa na tofauti ya shilingi 219,000,000 kulinganisha na mwaka wa fedha uliopita ambayo ni sawa na asilimia 52.3, huu ni ushahidi tosha wa dhamira butu ya

Serikali katika kuhakikisha wananchi wa vijijini nao wanapata habari na kufikiwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya kutotekelezwa kwa azimio hili la kusambaza habari vijijini, husababisha taarifa za tafiti nyingi zinazofanyika kutowafikia walengwa hususani waishio vijijini. Hali hii inathibitishwa na kauli ya Mkurugenzi wa Nyaraka na Mawasiliano kutoka *COSTECH*, Raphael Mmasi, akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa sayansi na teknolojia kutoka nchi 40 uliofanyika jijini Dar es Salaam alisema, nanukuu:-

*"Tanzania inakabiliwa na tatizo la tafiti za sayansi na teknolojia kutowafikia walengwa. Pia Tume hiyo imefanya tafiti 70 za kilimo na 340 za ufugaji lakini zimebaki kwenye makaratasi badala ya kuwafikia walengwa ili wazitumie katika kuinua uchumi."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mkakati wa kuibua na kuendeleza wabunifu katika kuibua na kuendeleza teknolojia hapa nchini. Pamoja na nchi yetu kuonekana kuwa na vijana wenye uwezo wa hali ya juu katika kubuni na kuendeleza teknolojia itakayoweza kuinua uchumi wa nchi, Serikali imeshindwa kutambua fursa hiyo na kuwaendeleza wabunifu hao. Mfano ni kijana Frank Waya kupitia kipindi cha *Jenerali on Monday* kinachorushwa na Televisheni ya *Channel Ten* ameonyesha uwezo mkubwa katika kubuni teknolojia ambayo ikiendelezwa itasaidia sana taifa katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kipaji alichonacho, ameweza kuonyesha jinsi teknolojia ya simu inavyoweza kutumika katika kutengeneza mfumo wa kuzuia vyombo vya moto kutoungua kutokana na shoti ya umeme na hata kutumia simu kwa ajili ya umwagiliaji wa bustani na shamba kwa kutumia pampu ya maji hata mtu akiwa mbali na shamba au bustani. Pia ameonyesha uwezo wa kutengeneza *inventor* inayoweza kukaa na umeme kwa siku saba (7) baada ya umeme wa *TANESCO* kukatika. Hiki ni kipaji cha hali ya juu ambacho kikitumiwa vizuri na kuendelezwa, kitasaidia Taifa hili kupiga hatua ya kimaendeleo. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kuna mkakati gani wa Serikali wa kuhakikisha kuwa vipaji kama hivi vinaendelezwa katika nchi yetu na je, wenye vipaji kama hivi ni nani mwenye wajibu na jukumu la kuviendeleza na kuvikuza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano na kilimo. Kwa kuwa idadi kubwa ya Watanzania wakiwemo wakulima wa vijijini wanatumia simu za mikononi, Kambi ya Upinzani inaona umuhimu mkubwa uliopo wa kutumia sekta ya mawasiliano katika kuinua uchumi wa wakulima na wafugaji. Tunaitaka Serikali ibuni mkakati wa kuhakikisha kuwa wakulima na wafugaji wanapata taarifa sahihi na muhimu zenye kukuza sekta ya kilimo kupitia simu za mikononi. Taarifa hizi ni kama vile Hali ya Hewa, masoko na bei za bidhaa, magonjwa ya mazao na mifugo na jinsi ya kukabiliana nayo kitaalam, taarifa za tafiti mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sayansi na teknolojia shuleni/vyuoni. Moja ya mambo yanayotarajiwa kutekelezwa na Wizara hii kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013, ni kuandaa program ya kuwahamasisha wanafunzi kuchukua masomo ya Sayansi, Teknolojia na uhandisi. Tatizo lililopo si wanafunzi kutopenda kusoma masomo ya Sayansi, bali ni mazingira mabovu yasiyoweza kuwavutia wanafunzi hao kupenda kuchukua masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mazingira hayo ni ukosefu wa Walimu wa kutosha kwa masomo ya sayansi, maabara na vifaa vya maabara na kadhalika. Pia wataalam waliopo wengi wao wana uwelewa mdogo wa teknolojia mpya. Mfano kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Chama cha Waandishi wa Habari wanawake Tanzania (TAMWA) inaonyesha katika Wilaya ya Mpanda ina Walimu wawili (2) tu wa masomo hayo (imeripotiwa katika gazeti la Mwananchi la tarehe 22/05/2012).

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingine zimeonekana kuwa na Mwalimu mmoja ama wawili huku shule nyingi zikikosa kabisa Walimu wa kada hiyo. Kwa mfano Mkoa mzima wa Singida una Walimu 294 wanaofundisha masomo ya Hisabati, Fizikia na Kemia, katika shule 154. Hii ni sawa na kusema kuwa kila shule kwa wastani ina Mwalimu mmoja, hii ni kwa mujibu wa Mratibu wa Masomo ya Sayansi wa Idara ya Elimu ya Sekondari katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ndugu Dorothy Mwaluko alipofanya mahojiano na gazeti la Mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na msingi mbovu wa masomo ya sayansi katika shule za msingi na sekondari, pamoja na kuwa na shule nyingi za sekondari za kata, shule hizi hazina maabara ambazo ndizo kitovu cha sayansi. Hali hii imepelekea wanafunzi wengi sana kushindwa kupata maarifa stahiki kutokana na ukosefu wa vifaa na walimu kwa ajili ya masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa kushirikiana na "*International Telecommunication Union*" (ITU) imekuwa ikiratibu maendeleo ya TEHAMA lengo likiwa ni kuunganisha shule za msingi, sekondari na vyuo katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Hofu inayojitokeza hapa ni juu ya utekelezaji wa teknolojia hiyo shuleni ikiwa Serikali imeshindwa kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu ya kawaida kama vile kusambaza madawati na vitabu vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi. Sasa tunatakiwa tujiulize ni kwa namna gani tunaweza kuitekeleza teknolojia ya kufundisha kwa mtandao wakati kutoa elimu kwa njia hii ya kawaida bado ni shida ukizingatia shule nyingi hazina umeme na hata Walimu walioandaliwa kwa ajili ya masomo kama hayo.

Mheshimkiwa Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali ilitenga shilingi 2,000,000,000 kutoka fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo katika sekta hii ya TEHAMA na kwa mwaka huu wa 2012/2013, Serikali imetenga kiasi hichohicho cha fedha. Hii ina maana hakuna maboresho katika kuendeleza sekta hii muhimu na kuhakikisha inafika hadi vijijini. Kambi ya Upinzani

inataka kupata majibu, Serikali imeandaa mikakati gani katika kuhakikisha kuwa shule zetu zinaandaliwa kwa ajili ya kuweza kutumia teknolojia hii mpya ya kufundishia hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa mtandao wa elimu na utafiti. Katika hotuba ya Waziri wakati akiwasilisha mapato na makadirio kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ukurasa wa 10, Waziri alisema Serikali imekamilisha tathmini ya uanzishwaji wa Mtandao wa Elimu na Utafiti *(National Education and Research Network – NREN)* utakaounganisha vyuo vikuu na vyuo vya Utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa uwanzishwaji wa mtandao huu ambao utawezesha kuunganisha vyuo vikuu na vituo vya utafiti, pia kuwezesha vituo vya tafiti kupata tafiti nyingi na kuzitumia tafiti zinazofanywa na wasomi ambazo zinatoa suluhisho kwa masuala ya kiuchumi na kijamii, Serikali imeshindwa kuhakikisha mtandao huu unaanza kwani katika bajeti yake ya 2012/2013, Serikali imeshindwa kutenga fedha kwa ajili ya kuanzisha mtandao huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kuanzishwa kwa mtandao huu unachangia kwa kiasi kikubwa kuchelewesha kuwaletea wananchi maendeleo kutokana na kukosa taarifa mbalimbali za tafiti zilizofanyika nchini hususani katika sekta ya elimu. Kwa maneno yake mwenyewe Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa anasema, naomba kununukuu:-

“*Nchi bila tafiti haiwezi kupata maendeleo, Singapore imefanikiwa kwa sababu ya tafiti na elimu.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza hapa ni kuwa Serikali yenyewe inakiri hakuna maendeleo bila tafiti lakini Serikali hiyohiyo inashindwa kutekeleza na kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uhakika wa fedha kwa ajili ya tafiti. Kambi ya Upinzani inahoji hivi mtandao huu ndio umekufa au Serikali ina mpango gani katika kutekeleza ahadi yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Kambi ya Upinzani katika hotuba zake mbalimbali, toka 2009/2010 - 2010/2011 - 2011/2012, imekuwa ikiitaka Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kuwa matumizi ya *ICT* yanatiliwa mkazo na kuhakikisha mitaala inaandaliwa na kutekelezwa hatua kwa hatua, pamoja na kuhakikisha umeme vijijini unapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Mwaka 2011 kulikuwa na jumla ya makampuni saba (7) yaliyokuwa yanatoa huduma ya mawasiliano kwa njia ya sauti. Watumiaji wa simu za viganjani walikuwa 23,979,870 hii ni sawa na kusema kuwa nusu ya Watanzania wanamiliki simu ama wanamiliki laini za simu. Pamoja na kuongezeka kwa watumiaji wa simu za mikononi nchini lakini ukiangalia taarifa ya hali ya uchumi inaonyesha kuwa sekta ya mawasiliano kwa ujumla wake ilichangia kiasi cha asilimia 2.2 tu kwenye pato la Taifa. Kwa mfano Ghana,

asilimia 10 ya mapato ya Serikali yanatoka kwenye kampuni za simu. Ghana ina watu milioni 25 na wateja wa simu milioni 17 tu wakati Tanzania ina watu zaidi ya milioni 45 sasa na watumiaji wa simu zaidi ya nusu ya idadi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka *TCRA* kuisaidia Serikali ili kuhakikisha kuwa Makampuni ya simu yanalipa kodi stahiki, ikizingatiwa kwamba hili ni jukumu mojawapo kati ya majukumu kadhaa yanayotakiwa kufanywa na *TCRA* katika usimamiaji sekta ya mawasiliano hapa nchini na iwapo *TCRA* itasimamia vema zoezi hili, Makampuni yote yataweza kulipa kodi na sekta hii ya mawasiliano itakuwa ni sehemu yenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupata majibu ya kina ni kiasi gani cha kodi kiliweza kukusanywa na Serikali kutoka kwenye makampuni haya ya simu kutokana na watumiaji kuongezeka kwa mwaka jana na ni kampuni ipi inaongoza kwa kulipa kodi na ni kodi gani. Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza umuhimu wa kufuta misamaha yote ya kodi ambayo kampuni za simu na hasa kampuni ya *Vodacom* walipewa na hivyo kusababisha kutokulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za mawasilino ya simu na matumizi ya simu zimeongezeka kutoka watumiaji 90,198 mwaka 1995 hadi kufikia watumiaji 23,979,870 mwaka, 2011. Pamoja na ongezeko hili, Serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi ukiachilia mapato yanayotokana na *VAT* ambayo kimsingi

yanalipwa na watumiaji kutokana na kutokuwa na *Monitoring system* ya upigaji huu wa simu na kodi inayotokana na *Cooperate Tax*. Ukosefu wa *monitoring system* ya simu zote zinazopigwa inakadiriwa kuwa Serikali inapoteza wastani wa 12% ya mapato yote ya kampuni za simu ambazo ni sawa na/au zaidi ya Sh.1.7 trilioni fedha ambazo zinaweza kuokolewa kwa kuwa na *monitoring system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi walitarajia kuwa baada ya kuundwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano (*TCRA*) itasimamia na kuhakikisha gharama za huduma za mawasiliano ya simu zinapungua na kuwa na uwiano sawa kwa tozo la makampuni yote hapa nchini. Mamlaka imeshindwa kuwaeleza Wantazania kwa uwazi na huku ikitambua kuwa moja ya jukumu lake ni kupanga bei elekezi (*harmonize price)* kwa makampuni ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa Watanzania wamechoka kutembea na simu zaidi ya moja za mitandao tofauti, kwa sababu ya kutafuta punguzo kwa mtandao husika, hii hali tutaendelea nayo hadi lini? Hivi kweli hakuna Sheria ambazo zitawalazimisha wamiliki wa mitandao kuwa na bei zenye uwiano wa karibu. Mbona *TCRA* imelala na kuona Watanzania wananyonywa hadi Senti yao ya mwisho bila kuchukua hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ni kuwa wamiliki wa mitandao ya simu walikuwa na hoja ya msingi ya kwamba gharama za uedeshaji wa shughuli za mawasiliano zilikuwa juu sana kwa sababu mawasiliano

yaliwezeshwa kwa kupitia kwenye *Satellite*, lakini hivi sasa tuanao Mtandao wa Mkongo wa mawasiliano (*FIBRE OPTIC*) ambao gharama zake za uendeshaji ni ndogo sana na unafanya kazi vizuri kwa haraka zaidi na hivyo basi uwezekano ni mkubwa wa kupunguza gharama za mawasiliano hapa nchini. *TCRA* katika kuhakikisha kwamba gharama za mawasiliano zinapungua kwa sasa ni lazima ikubali kupunguza gharama zake kama vile kusitisha malipo ya tozo ya maunganisho (*Interconnection rate*) yanayolipwa kwa fedha za kigeni (DOLA) kwa Makampuni ya Simu, pia kiwango kinachotozwa bado ni kikubwa na kinapaswa kuondolewa au kupunguzwa kwani hakina faida kwa mtumiaji. *TCRA* inapaswa kupunguza gharama za malipo (TOZO) ya umiliki wa njia za Mawasiliano (*Frequency*) inayolipwa kwa fedha za kigeni na kiwango kilichopo ni kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* inapaswa kupunguza Malipo (TOZO) inayoyatoza Makampuni ya Simu kama gharama za malipo ghafi kwa mwaka (*Loyalty fee*). Ni ukweli kiwango hiki cha asilimia 0.8 ni kikubwa na kinasababisha watumiaji kuumia, vilevile inapaswa kupunguza gharama za malipo ya Mawasiliano Vijijini (*Rural areas*) ya asilimia 0.4 yanayotozwa Makampuni ya Simu. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kama gharama hizo zitapungua mzigo wa gharama za simu utapungua kwa kiwango kikubwa na kama *TCRA* haitachukua hatua, tutapendekeza siku zijazo mamlaka hii ivunjwe kwani imeshindwa kumwondolea mwananchi gharama za simu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtambo maalum wa kufuatilia watumiaji wa simu. Kambi Rasmi ya Upinzani tuna taarifa kuwa mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ipo kwenye juhudi za kupata mtambo wenye uwezo maalum wa kisasa kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa simu hapa nchini na ambao Serikali imeiagiza mamlaka hiyo kuweza kuhakikisha kuwa unapatikana na kufungwa nchini ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu na ambao utatumika katika Makampuni yote ya simu nchini. Taarifa zilizopo ni kuwa mtambo huo utakuwa na jukumu la kutambua uhalali wa mapato ya Serikali, kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa, ulinzi wa kimataifa, uzuiaji  wa fedha haramu kuingizwa nchini na kufuatilia mienendo ya watumiaji wa simu mbalimbali waliopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati taarifa hizo zikionyesha hivyo kuna taarifa nyingine zinaonyesha kuwa kwa kutumia mfumo wa teknolojia upo mtambo ambao umenunuliwa kutoka nchini Israel kwenye kampuni ya *NICE* ambao unajulikana kama *Gi2* ambao ni maalum kwa ajili ya kufanya kitu kinachoitwa "*sms spoofing*" na uliweza kuuzwa kwa Jeshi la Polisi mnamo mwezi April 2012. Wataalam mbalimbali tuliowasiliana nao pamoja na mitandao mbalimbali kama vile *www.textfromwho.com* waliweza kuonyesha kuwa mtambo huu wa *"sms spoofing"* unao uwezo wa kutumika na kutuma meseji za simu kwa kutumia simu ya mtu ambaye hajui na kuweza kutumia namba yake na kutuma *sms* kwa mtu mwingine kana kwamba ni mtu husika mwenye namba ya simu ndio ametuma ujumbe huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo kimojawapo kilichopo India cha “*The Asian Schools of Cyber Laws” (Pune)* walifanya utafiti juu ya jambo hili na majibu ya utafiti huo ni kuwa waliweza kutuma ujumbe mfupi wa simu kwa kutumia njia hii na waliweza kutumia simu za watu waliokuwa mtandao wa “*GSM*” kwenye mabara ya Afrika na Asia na utafiti ulionyesha kufanikiwa kutumia namba za simu za watu wengine na kutuma ujumbe mfupi wa simu. Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya taarifa ni kuwa mtambo kama huu unatumika sana kwenye nchi za Israel na Ujerumani ila kwa nchi nyingine kama Australia kufanya tendo hilo ni kosa kisheria kwani wao wamepiga marufuku matumizi ya mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2008 nchini Uingereza Mthibiti wa Mawasiliano wa Viwango vya Juu *(Premium Rate Regulator)* inayojulikana kama “*phone pay plus”* ambayo kabla ilijulikana kama *ICSTIS* walianzisha kanuni kwa ajili ya wateja kuweza kutoa malalamiko kama simu zao zimefanyiwa uharamia huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupata majibu juu ya mambo yafuatayo:-

(i) Je, Taarifa za mtambo huo wa *Gi2* kununuliwa na kuletwa nchini na kutumiwa na Jeshi la Polisi mwaka huu ni za kweli?

(ii) Je, umeletwa kwa madhumuni gani hasa na utakuwa unatumika kwenye masuala gani?

(iii) Mtambo utakaonunuliwa na *TCRA* ni wa aina gani na utakuwa na uwezo wa kufanya *sms spoofing*? Kama jibu ni ndio zitatumika kufanyia shughuli gani hasa?

(iv) Ni lini Serikali itaweka sheria ya kuthibiti matumizi ya taarifa za "*sms spoofing*" hapa nchini ama kukubaliana na matumizi yake au kupiga marufuku kama walivyofanya nchi ya Australia na Uingereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalifu wa Kimtandao (*Cyber Crime*). Kumekuwa na kuongezeka kwa kasi ya wizi kwa njia ya mtandao, kwa sasa kiasi kilichoripotiwa Polisi kuhusiana na wizi kwa njia ya mtandao hapa nchini ni shilingi 1.3 bilioni, Euro 8,897 na dola za kimarekani 551,777, hizi ni fedha nyingi sana kwa nchi yenye uchumi mdogo kama wa kwetu na pia inatishia uwekezaji na wawekezaji nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalifu wa kimtandao ambao unakuja juu zaidi ni uhalifu au uharamia wa mtandao kwa ajili ya kutafuta taarifa kuhusu Taifa fulani, vikundi fulani vya watu wanaotumia mitandao kuwasiliana zaidi mitandao jamii na wavuti za Serikali za nchi wanazopingana nazo au za wanaharakati au vyama vya siasa labda upinzani au vinavyotawala. Uhalifu huu wa kimtandao unaongezeka kwa kasi kubwa sana hapa nchini mwetu na unatishia uhai wa uchumi wetu kama taifa kama hatua hazitachukuliwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi mbalimbali zimefanikiwa zaidi katika kukabiliana na uhalifu huu kwa kutumia njia ya kubadilisha program na mfano ni Umoja wa Ulaya ambao umeingia mkataba maalumu na kampuni zinazotengeneza programu hizo kama *Microsoft, Oracle, Adobe, Symantec* na kadhalika. Kambi ya Upinzani inataka kujua Serikali imejiandaa vipi ili kuweza kukabiliana na uhalifu huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya simu na huduma za fedha. Taarifa ya Hali ya Uchumi iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha hapa Bungeni ilionyesha kuwa idadi ya Watanzania wanaotumia simu za mkononi imeongezeka mwaka hadi mwaka na sasa ni zaidi ya milioni 23. Pamoja na ongezeko hilo, Kambi ya Upinzani ina mambo kadhaa ambayo inabidi Serikali iyatolee maelezo kama ifuatavyo:-

(i) Gharama kubwa zinazotozwa na makampuni hayo kwa watumiaji;
(ii) Makampuni huendesha kamari kwa watumiaji na kuwatoza fedha nyingi. Je, Serikali inaratibu vipi gharama hizi na kamari ambazo zinatozwa na makampuni hayo ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya huduma za fedha kwa kutumia mitandao ya simu yameongezeka sana katika siku za karibuni. Hivi sasa kuna huduma za M-PESA, ZAP, Z-PESA na TIGO PESA. Pamoja na kuwepo kwa sheria zinazoratibu masuala ya kifedha nchini, mathalani Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na pia Sheria inayounda Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,

bado hakuna uratibu wa moja kwa moja unaolenga kuyasimamia na kuyaongoza makampuni haya ya simu katika kutoa huduma kwa wateja wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa uchumi wa kati unajengwa kwa watu wengi kushiriki katika taasisi za kawaida za benki, lakini kwa Tanzania ni asilimia chache sana ya watu ambao wanapata huduma hizi. Hili limepelekea kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za kielektroniki za kutuma na kupokea fedha zinazotolewa na makampuni ya simu. Tumeshuhudia hata huduma za jamii na taasisi zingine za Kiserikali kama *TANESCO* na *DAWASCO* kuanza kutumia makampuni ya simu badala ya benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali ama kutunga sheria au kufanya marekebisho ya sheria zilizopo ili ziweze kuratibu matumizi haya ya huduma hii ya fedha kwa kuwa inawezekana kabisa Serikali inashindwa kupata mapato kwa sababu tu hakuna sheria iliyopo inayoelekeza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tunaitaka Serikali kutoa maelezo kama Mamlaka ya Mawasiliano imeshaanza kuchukua hatua ya kuratibu huduma hizi za fedha kwa njia ya mitandao ya simu kwa kuwa pamoja na kuwa katika sheria inayounda Mamlaka haya hakuna kipengele kinachoyaruhusu moja kwa moja makampuni haya kutoa huduma hizi bado Mamlaka ina uwezo wa kutunga kanuni zinazoratibu huduma hizi na kumlinda mteja kwa kuwa hata Sheria

ya Ushahidi, Sura ya 6, pamoja na kufanyiwa marekebisho ili kukidhi haja ya ushahidi wa kielektroniki, bado ina upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji. Serikali imekuwa ikisisitiza juu ya mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda *digitali* na katika utekelezaji huo, Serikali imetoa leseni kwa makampuni matatu ambayo ni *Agape Associeties Ltd, Basic Transimission Ltd na StarMedia (T) Ltd.* Pamoja na hatua hiyo, kuna ulazima sasa wa kuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha *chanel* zote za ndani zinaingizwa katika ving'amuzi tofauti na sasa mtu akinunua king'amuzi cha *StarMedia* hawezi kupata *chanel* kama vile *Star Tv* na ITV, mwananchi akitaka kupata chaneli hizo itamlazimu kununua king'amuzi kingine na hii ni gharama kubwa kwa mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ni kwamba ving'amuzi vyote *channel* zinazoonyeshwa ni zaidi ya asilimia 85 na za ndani ni *chanel* chini ya tano. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kigezo cha ulazima kuwa ving'amuzi vyote ni lazima viweke *channel* zote za ndani na za nje kwa kadri watakavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Florence Turuka, alisema, naomba kunukuu:-

*"Suala la king'amuzi kimoja kuonesha vituo vyote vya ndani ni la kitaalamu ambalo limejadiliwa katika*

*Mikutano ya Nchi za Afrika Mashariki na ule wa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC)...wataalamu wanalishughulikia suala hilo litakalokamilika kabla ya teknolojia ya analojia haijafungwa rasmi nchini jambo litakalowasaidia watangazaji kupata wateja kutokana na kupata watazamaji wengi. Serikali kupitia Wizara yake pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA), watahakikisha kuwa mabadiliko hayo yanafikiwa bila kuathiri teknolojia na mifumo mbalimbali ya mawasiliano iliyopo nchini."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna mkanganyiko wa habari kwa sababu mfanyabiashara yeyote analenga kupata faida kubwa, mahitaji ya ving'amuzi kuanzia sasa yatakuwa makubwa na mahitaji yake yataongezeka siku hadi siku. Maana yake ni kwamba mahitaji ya bidhaa yoyote yanapoongezeka yatalazimisha bei ya ile bidhaa kupanda kwa sababu inawezekana kwa wakati uliopo bidhaa ile inaweza kuwa haba kutokana na mahitaji kuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ving'amuzi hivyo vinauzwa kati ya Sh. 70,000/=, Sh. 100,000/= na Sh. 200,000/= hadi Sh. 300,000/=. Kulingana na wingi wa *channel* ambazo mtumiaji ataweza kupata na bado gharama za kulipia huduma hiyo kila mwezi kwa mtumiaji ambayo hailipwi kulingana na utumiaji, bali ni kulipia kiwango maalum *(fixed rate)* bila kujali ameangalia mara ngapi *television* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwa hakika kuwa gharama hizi ni kubwa sana, na swali la kujiuliza ni: Je, ni Watanzania wangapi wenye uwezo wa kununua na kulipia kila mwezi huduma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia - Mheshimiwa Charles Kitwanga aliwahi kutoa taarifa katika Semina ya Wabunge ambayo pamoja na masuala mengine, ililenga kuwaelimisha juu ya mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali kuwa, "yapo mazungumzo yanayoendelea juu ya upunguzaji wa bei kwa vifaa hivyo." Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji: Je, mazungumzo hayo yamefikia wapi na maamuzi yaliyofikiwa ni yapi mpaka sasa?

Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni muhimu Serikali ikapunguza kodi kwenye vifaa vya digitali ili kuepusha bei kuwa kubwa kama ilivyo sasa na kuhakikisha kuwa runinga za dijitali zinashushwa bei ili kuwezesha wananchi wengi kuzitumia kuliko kutumia zinazohitaji ving'amuzi. *(Makofi)*

Pia kitendo cha *TCRA* kuharakisha uzimaji wa mitambo ya analojia ifikapo Desemba 31, mwaka huu 2012, wakati Umoja wa Mataifa ulitoa muda wa ukomo kuwa ni mwaka 2015, siyo sahihi, kwani teknolojia hii bado haijasambaa hasa vijijini na hata kwenye baadhi ya Miji yetu. Yafaa muda ukaongezwa ili kuweza kuwaandaa wananchi na wadau wa habari kuweza kujipanga na kujiandaa kimkakati zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya simu hususan katika matumizi ya ujumbe mfupi na maneno, matumizi ya barua pepe, matumizi ya simu katika kutuma na kupokea fedha, matumizi ya Posta katika nchi zilizoendelea pamoja na nchi hizo kupiga hatua kubwa katika Sayansi na Teknolojia, bado ni makubwa ikilinganishwa na nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Afrika mtu mmoja anapokea wastani wa barua tatu kwa njia ya Posta kwa mwaka, Ulaya mtu mmoja anapokea wastani wa barua 400, Marekani 300 na Asia 200. Hivyo, Serikali haipaswi kupuuza uboreshaji wa Shirika hili, kwani hata katika nchi ambazo Sayansi na Teknolojia ilipoanzia wanatoa kipaumbele katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania *(TPC)* ni kati ya mashirika yaliyobaki mikononi mwa Serikali huku yakiwa yanajikongoja katika utendaji wake.

Mwishoni mwa mwaka 2011, Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia, alikwenda kutembelea shirika hilo ambapo alishuhudia changamoto mbalimbali zikiwa zinalikabili. Moja ya changamoto alizokutana nazo ni teknolojia duni, ushindani na mtaji duni. Kutokana na changamoto hizo, Postamasta Mkuu, Ndugu Deos Mndeme, alisema ili shirika liweze kusimama lenyewe na kuendesha shughuli zake, linahitaji mtaji wa kiasi cha Shilingi bilioni 30.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kuwa, Serikali imeshindwa kutenga fedha kwa ajili ya kuliendeleza na kulinusuru Shirika hili ambalo lipo mahututi, badala yake Serikali imetenga Sh. 709,518,000/= kwa ajili ya mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta ambao utahusisha kuhuisha mpango na muundo wa utekelezaji wa mradi, kuelimisha umma kuhusu mfumo mpya wa Anuani za makazi na Simbo za Posta, kuhamasisha Taasisi, makampuni mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, kuchangia utekelezaji wa mradi, kuwezesha utekelezaji wa mradi katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam, kujenga uwezo wa watendaji wa mradi na kutangaza Postikadi katika ngazi za Kimataifa kupitia Mkutano Mkuu wa Umoja wa Posta duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna fedha kwa ajili ya mkakati mahususi wa kuwezesha Shirika hili kuweza kujiendesha na kukabiliana na ushindani uliopo sasa pamoja na Shirika hili kuwa na mkakati wa miaka mitatu ambao ni kuliendesha Shirika hilo kwa mtazamo wa kibiashara. Wanachosubiri ni fedha, na kwa mwaka huu Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya kuliboresha Shirika hili ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa viwango vya kimataifa. Kwa mujibu wa viwango vya Umoja wa Posta Duniani (UPU), Ofisi moja ya Posta inapaswa kuhudumia watu 7,000 lakini Tanzania, Posta moja inahudumia wastani wa watu 80,000. Hii inatokana na Serikali kutotenga fedha kwa ajili ya kuboresha na kuliimarisha Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali ya ushindani inayokabiliana nayo sokoni, Shirika hili kwa zaidi ya miaka 15 sasa, limekuwa halipati ruzuku kutoka Serikalini. Shirika la Posta lilipoanza mwaka 1994 lilikuwa likifanya kazi bila kupewa mtaji, huku likiwa limeahidiwa kupewa mtaji wa Shilingi bilioni 19.3 kiwango ambacho hakikupatikana. Kutopatikana kwa mtaji kwa kipindi hicho kumesababisha kuongezeka kwa gharama, hatua ambayo imesababisha Sera za Shirika kupoteza dira mpaka kufikia hatua ya kuanzisha maduka yanayouza pipi na soda kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Shirika hili ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2015, inakuwa na Ofisi hadi vijijini, dhamira ambayo kamwe haiwezi kufikiwa kutokana na Serikali kushindwa kutenga bajeti katika kufanikisha mpango huo. Kambi ya Upinzani, inahoji hivi mradi wa anuani za makazi utaweza vipi kutekelezwa kama Shirika hili litaachwa bila kutengewa fedha na kufa kabisa? Au Serikali inataka kutekeleza mradi huo kwa kutegemea Makampuni binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi ya Nelson Mandela; Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013, Serikali iliazimia kujenga Kituo cha *TEHAMA* na kuweka vifaa mbalimbali katika Kituo hiko. Katika kutenga bajeti, Serikali imeonyesha itanunua vyombo vya mtandao wa *TEHAMA (Communication Network Services)* na hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo hicho kama ilivyoeleza katika hotuba ya Bajeti ya Waziri kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ukurasa wa 71, alipoeleza nia ya Serikali ya kujenga

Kituo hicho (*ICT Resource Centre)* na katika malengo ya Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2012/2013. Kambi ya Upinzani inauliza, ni kwanini Serikali inaendelea kutoa ahadi ambazo inashindwa kuzitekeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya sasa haikidhi haja ya wanafunzi wanaosoma Ph.D, mtazamo wa awali ulikuwa ni idadi ndogo ya wanaosoma Ph.D kwa kudhani idadi yao kuwa robo ya wanaosoma M.A, lakini kwa sasa wanafunzi wa Ph.D wamefikia nusu ya wanafunzi wa M.A. Kutokana na kutokuwa na msingi wa masomo ya Sayansi kwa shule zetu, ni wazi kuwa kwa siku zijazo, Chuo hiki kitakuwa kimebeba wanafunzi wengi kutoka nje ya Tanzania na kutowanufaisha Watanzania, pamoja na Chuo hicho kujengwa hapa nchini.Kambi ya Upinzani inahoji, kuna mkakati gani wa makusudi uliowekwa na Wizara wa kuhakikisha kuwa Chuo hiki kinawanufaisha vijana wa Kitanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, kwa mwaka wa Fedha 2011/2012, Serikali ilikusudia kukarabati na kufunga mitambo katika Vituo vitatu vya Habari Jamii vya mradi wa *Super Computer* vilivyopo Morogoro, Dodoma na Mtwara (Hotuba ya Waziri kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ukurasa wa 68) kitu ambacho kimerudiwa tena katika mwaka huu wa fedha 2012/2013, lakini ikiwa tu Serikali ikipata ruzuku, na haijaonyesha ni kiasi gani inachohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Serikali imeeleza kuwa Taasisi hii itaanzisha mradi wa majaribio

wa matibabu mtandao *(Tele-medicine)* utakaounganisha *DIT*, Hospitali za Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Tumbi na Bagamoyo. Ila la kushangaza ni kuwa hakuna bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu. Kambi ya Upinzani inahoji mradi huu utaendeshwa bila gharama au ni kuendeleza utamaduni ule ule wa Serikali wa kuahidi wakati ikijua kuwa haiwezi kutekeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetenga Sh. 75,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, na imetenga Sh. 98,000,000/= kwa ajili ya posho ya kujikimu kwa safari za ndani katika kitengo cha utawala na utumishi pekee. Kambi ya Upinzani, tunahoji kipaumbele chetu kama Taifa na hususan Wizara hii, kiko wapi? Au ni posho kwanza, maarifa baadaye?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani iliridhia kwa dhati kabisa Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ili kukuza ushirikiano, maendeleo, uhawilishaji na umahiri wa sayansi, teknolojia na bidaa/ubunifu/ugunduzi katika Mkutano wa tatu wa Bunge. Tunapenda kusisitiza kuwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ina jukumu kubwa la kutekeleza itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hili, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaishauri Serikali iendelee kuipa fedha ya kutosha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili iweze kuratibu masuala mbalimbali ya sayansi nchini kwa ufanisi. Hata hivyo tunaitaka Serikali kupitia upya

sera ya sayansi na teknolojia ili kuhimili changamoto mbalimbali za sayansi zilizopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa za kuwepo kwa wawekezaji wakubwa wanaofanya utafiti na uchimbaji wa *urani* (*uranium*) katika Hifadhi ya *Selous* (Mkuju, Namtumbo - Songea). Taarifa hizo zinasema kwamba wananchi wanaokaa maeneo hayo hawakushirikishwa, na baadhi ya wananchi wameshaanza kuathirika kutokana na madini hayo ya urani. Tunashauri Serikali iiagize Tume ya Nguvu za Atomiki iende ifanye utafiti kuhusu hatari iliyopo katika machimbo ya urani ili kupata ukweli na kutoa ushauri juu ya hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Tume ya Nguvu za Atomiki imeshafanya kazi nzuri. Kambi ya Upinzani inakumbushia ushauri uliotolewa mwaka wa fedha uliopita kuwa wafanyakazi wa Tume hii wapewe posho ya mazingira hatarishi *(risk allowance)* na bima ya mazingira hatarishi. Tunaomba maelezo ya Serikali kama tayari imeshazingatia ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha na naomba hotuba yote kama ilivyo kwenye kitabu, iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Joshua Nassari. Sasa mkiendelea kupiga makofi, utabakia muda kidogo wa kuchangia hapa.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache katika Wizara hii. Naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake kwa kujiandaa kikamilifu katika kuwapunguzia matatizo ya mawasiliano Watanzania.

Pili, naomba nitoe pole kwa ujumla kwa wafiwa wa Marehemu ambao wamepatwa na mauti katika ajali ya meli ya hivi karibuni. Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali pema Peponi na awape subira wale ambao wamepatwa na msiba huu mkubwa ambao ni msiba wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na masuala ya Makampuni ya Simu. Makampuni haya ya simu yanajitahidi sana kuweka minara katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Lakini lazima tunapofanya jambo, tuangalie pande zote, faida na hasara. Kuna faida kubwa katika suala la mawasiliano. Lakini pia kuna athari zake katika kuweka minara. Kwa mfano, wanapotaka kuweka mnara, watu wa kampuni wanakata miti, wanachonga milima, kwa ufupi wanachafua mazingira. Naomba niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri: Je, hao watu wa makampuni wanachangia kiasi gani katika mfuko mkuu wa mazingira? Hilo ni swali langu katika hili. Namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu wakati wa kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba kuchangia kuhusu *DIT*. Nimesoma humu katika hotuba

yake Mheshimiwa Waziri kajitahidi sana kuweka mikakati ya kuboresha na kujenga. Hivi sasa ukienda katika Chuo kile cha Sayansi na Teknolojia, utakuta bweni limeoza *(dometry);* nakusudia, halitamaniki. Ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maabara zina vifaa tangu mimi sijazaliwa. Hakuna vifaa vya kisasa. Vifaa vya kupimia udongo hakuna, ni vifaa vya kale vya zamani na sasa hivi tuko katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia na hii ndio Wizara yenyewe na hiki ndiyo Chuo tunahitaji mabadiliko ya haraka ili kupata tija inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, Posta zimetupwa. Baadhi ya Posta hazifanyi kazi, hazikidhi haja. Kwa mfano, Posta za kule Pemba hasa ile ya Wete, Mheshimiwa Waziri imekufa. Ukienda pale kutaka huduma zaidi ya kwenda kuweka na kuchukua barua, hakuna huduma nyingine ya msingi ambayo inapatikana. Ukituma fedha hapa Dodoma kupeleka kule Wete, basi itachukua wiki mbili hujapata hizo hela. Ina maana ile Posta haina fedha, imekauka. Ina maana haipewi huduma, haiwezeshwi, imechoka, imekauka. Namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe hizi Posta anaziangalia kwa jicho la huruma. Waswahili wanasema asiye na kwao ni mtumwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri akuangalie sana kule kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za mawasiliano ni jambo ambalo linawanyanyasa Watanzania. Gharama za mawasiliano ni kubwa. Asilimia kubwa ya

Watanzania ni wanyonge, mawasiliano ndiyo jambo pekee ambalo linawasaidia. Akitaka kuomba hela kwa mwenzake anatumia mawasiliano, akitaka kutuma taarifa za msiba au za ugonjwa anatumia mawasiliano.

Tunaomba sana gharama za mawasiliano mziangalie na badala yake basi haya mawasiliano yanayotumiwa na Makampuni ya Simu, kwa mfano *Zantel* wanakupigia simu, Mheshimiwa Waziri utakimbia mbio wewe, utadhani labda kuna simu muhimu, unafukuzia ukienda unakwenda kupokea simu unasikiliza wimbo. Inasaidia nini? Wanatupotezea muda! Unaweza ukajikwaa kwa kufukuzia simu, ukifika unasikia wimbo. Usikilize wimbo, kwani mimi nina shida ya wimbo? Hatuna shida ya wimbo. *(Makofi)*

Hizi simu ni kwa ajili ya mawasiliano kwa mambo muhimu, siyo kusikiliza wimbo, halafu zile *message* wanazotuma za ajabu ajabu, hazina mahitaji yoyote kwa Watanzania. Watanzania ni watu ambao wana shughuli muhimu sana za kufanya za kujitafutia maendeleo katika maisha yao. Kwa hiyo, tunaomba sana, hizi huduma za ajabu ajabu ambazo hazikidhi mahitaji ya Watanzania ziondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, sitaki nipoteze muda. Mimi leo nimekusudia kusema yale ambayo yananikereketa sana. Ujenzi wa Ofisi ya *TTCL* kule Pemba ni ajabu na ni aibu. Mtaendelea kukodi mpaka lini? Hatuna uwezo wa kujenga Ofisi hata ndogo basi! Au ndiyo Pemba? Maana yake kule kumewekwa mkiani, kwa hiyo, kila jambo linawekwa nyuma. Mambo mengi ya msingi na ya muhimu hayapelekwi

kule. Mheshimiwa Waziri huduma za simu/huduma za mawasiliano ni muhimu. Basi angalau wale wafanyakazi wenu wahurumieni, wajengeeni Ofisi, msikodi kila siku, ni gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo dogo ambalo linanikereketa sana, huwa nasikia malalamiko sana ya wafanyakazi wa Kampuni ya Zantel. Nakusudia wafanyakazi walinzi wa minara. Wale wana malalamiko makubwa sana na sijui kama hawakusudii kwenda Mahakamani. Lakini kama hawajakwenda, sina hakika. Lakini wanalalamika kweli wale walinzi kwa sababu wanasema wenzao waliotangulia wamepewa mikataba, malipo yao yalikuwa yanaridhisha, wao hawakupewa mikataba na malipo hayaridhishi, ni duni sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hili suala ulifuatilie kwa umakini mkubwa ili kila mtu ambaye anastahili kupata haki yake, basi apate haki yake. Tunasema sisi haki sawa kwa wote. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mchango wangu kwanza ningependa kujikita katika masuala mazima ya mawasiliano, hususan kutokana na mitandao ya simu ama simu za mikononi, na Makampuni yote ya Simu katika pato la Taifa. Yaani ni kiasi gani Kampuni za Simu zinachangia katika Taifa letu ama zina mchango gani ambao unachangiwa? Kama ambavyo tunaona katika takwimu za mwaka 2011 zinaonyesha Tanzania pato ambalo tunalipata

kutoka katika Makampuni ya Simu ni asilimia 2.2 tu kutoka katika Makampuni mbalimbali ya Simu.

Kwa Tanzania, tukiangalia watu ambao wanatumia simu za mikononi hawapungui milioni 23, yaani ni zaidi ya nusu ama ni nusu ya Watanzania ambao wanamiliki simu za mikononi na wanatumia simu na hata ambao wanamiliki laini. Kwa hiyo, takwimu hiyo na kipato ambacho tunakipata kama Taifa kutokana na mawasiliano, kwa kweli tunaona halitoshi kutokana na idadi kubwa ya watu wanaotumia mitandao ya simu.

Mfano mzuri, ni wenzetu Ghana. Ghana wana watu ambao wanaotumia simu za mikononi pamoja na laini, hawazidi milioni 17 ya Waghana wote. Lakini tuangalie, sisi tuna watu zaidi ya milioni 23 ambao tunapata asilimia 2.2 kama pato la Taifa ambazo ni kodi zinatozwa kutoka katika Makampuni, wakati wenzetu Ghana wanapata asilimia 10 ya pato wanaingiza katika Taifa lao kama michango na kodi ambayo Serikali inapata. Hivyo basi, naitaka Serikali/Wizara kupitia *TCRA* ambao wanahusiana na hawa kuiga mfano wa wenzetu na kuona ni njia gani wanafanya, mambo gani wanafanya ili na sisi tuwe tunapata pato kubwa au tunapata pato stahiki kupitia mitandao ya simu za mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kuiga ni kusoma. Ukitaka usome ujue, basi uangalie mazuri anayofanya mwenzio nawe yakufae. Hivyo basi, naendelea tu kuishauri Serikali, Wizara ya Mawasiliano kupitia *TCRA* walione hili na waone umuhimu wake

katika kuongeza pato letu la Taifa kupitia mitandao ya simu na kudhibiti Makampuni ama ubabaishaji unaofanywa na Makampuni katika kulipa kodi. *(Makofi)*

Vile vile katika mambo hayo hayo ya simu, ningependa kutoa malalamiko ya Watanzania wengi na hili nadhani Mheshimiwa Waziri tumeshawahi kulifikisha kwako, na kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na bado tunaona linazidi kuwa *issue* kwa Watanzania.

Aidha, tuseme ni makubaliano ama mkataba, ama ni kitu gani ambacho wanafanya watu wa *TANESCO* ambao wanalipa kabla, wanafanya malipo kupitia simu za mkononi, wanaolipa kwa kweli mambo mengine sielewi. Lakini mfano mzuri, wanaonunua umeme kupitia *TANESCO, TANESCO* wanaoungwa kutokana na mitandao ya simu, tunaomba kwamba Watanzania wengi sasa wamerahisishiwa huduma ya kununua umeme ama kupata malipo ya vitu mbalimbali kupitia kwenye simu zao za mkononi. Lakini tunasema Mheshimiwa Waziri mnatuletea janga, kwa sababu hii ni njia nzuri na tunai-*support* lakini ina matatizo ambayo hatujui nani anatutatulia.

Mfano mzuri, mtu ananunua umeme kupitia simu yake, fedha inakatwa, umeme hapati, akienda kwa Wakala wa *TIGO*, ama Wakala wa *VODA*, ama mtu yeyote ambaye anamkata ile pesa kupitia kwenye simu, anakwambia nenda *TANESCO*. Unatoka, unaacha kazi zako unakwenda *TANESCO*, unafika nako unaambiwa kweli hii namba ipo, umenunua, lakini kuna hili na hili, rudi nenda kwa Wakala wako,

tutaliangalia. Hivi huyu mtu ambaye anakuwa anazungushwa, hana kazi za kufanya? Hana mambo mengine? Tunataka kuuliza: Je, huku ni kurahisisha ama kutuletea usumbufu kwa wateja wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa lugha nyepesi tunaweza kusema ni wizi kupitia mitandao ya simu na vile vile tunaweza kusema wizi huu unafanywa na *TANESCO* na Makampuni ya simu ambayo yanakusudia kurahisishia watu. Lakini tunaona imekuwa kero kwa Watanzania wengi, wateja wao wengi ambao wanatumia huduma hizi katika mitandao yao. Hivyo basi, namtaka Mheshimiwa Waziri atuambie jibu sahihi, ama atupe jibu ni kitu gani? Ama atuambie mwelekeo mzuri, ni kitu gani cha kufanya, ama ni hatua gani wanachukuliwa ambao wanakata Watanzania pesa katika kupata huduma na hatimaye hakuna huduma ambayo wanaipata kutoka katika chombo husika ambacho wametarajia kiwasaidie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nipo katika masuala ya mitandao. Katika mawasiliano kuna kitu kinaitwa *Central Equipment Identification Registrar.* Hii watu wa *TICRA* wanataka kuianzisha kwa ajili ya kuzuia utumiaji mbaya wa simu za mkononi, ama kuzuia wahalifu wa simu za mkononi. Lakini ningependa kuwasisitizia, kwamba walifanyie haraka, kwani hii *system* ambayo inatumika sasa, matumizi mabaya ya simu za mkononi bado yana vitisho, yanaendelea kuwaathiri Watanzania walio wengi hasa watumiaji wa simu za mkononi. Hivyo basi, tunataka suala hili lifanyiwe haraka kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kugusia katika *COSTECH*. *COSTECH* hawa tunaona kwamba wanasimamia masuala mazima ya tafiti mbalimbali, yanaonyesha mambo mbalimbali ambayo yanatokea. Lakini tunataka tuwaambie, kuiga kitu kizuri ni njia mojawapo ya kusoma ama ya kutaka maendeleo.

Serikali pamoja na Wizara, kubwa ni kuiambia kwamba, kuna vijana wengi wenye vipaji vingi ambao wamefanya tafiti mbalimbali, wamegundua vitu mbalimbali, lakini tunaona bado haijawaona. Bado pesa katika tafiti zetu zinakuwa ndogo, watafiti wanavumbua mambo mengi, yanashindwa kufanyiwa kazi.

Mfano mzuri, kuna vijana ambao wamegundua mfumo rahisi wa kuhesabu kura kwa urahisi zaidi kwa kutumia teknolojia, lakini sisi bado hatujaliona hilo. Mpaka sasa ninavyoongea, vijana hawa wana maongezi na Serikali ya Kenya na kutokana na uzito na umuhimu wa tafiti yao, Serikali ya Kenya imewaona kwamba wanawafaa na sasa wana maongezi, aidha wakubaliane nao kama waingie nao mkataba katika kuwasaidia, ama *whatever* ambavyo watafanya. Lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango katika Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Lakini mchango wangu utakuwa zaidi kwenye maeneo

mawili tu. Moja, biashara ya *ring tones;* pili, Shirika la Posta. Mawili tu. Leo hii, kwa wale Wabunge ambao wamewahi kumpigia simu Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna kipindi wakimpigia simu, watasikia mziki wa *gospel* wa Rose Muhando, ukimpigia simu Mheshimiwa Adam Malima utasikia wimbo wa "Dar mpaka Moro" ya *Wanaume Family*. Ukinipigia simu mimi kama hautasikia *Quran*, utasikia mziki ama wa CHADEMA au wa Kidumu Kibido.

Waheshimiwa Wabunge, Makampuni ya Simu kwa mwaka yanapata Shilingi bilioni 43 kutokana na biashara ya *ring tones*. *Ring tones* ambazo mnatumia ni fedha, lakini tulitarajia na watu wengi tunapokuwa tuna-*subscribe*, kwamba fedha zile, wasanii wetu pia wapate.

Kwa hiyo, leo ukinunua wimbo wako Sh. 400/= na kila siku unakatwa Sh. 37/=, iwe ni *AIRTEL, VODA, ZANTEL* au ni *TIGO*, asilimia 80 ya fedha hizo inakwenda kwenye Kampuni ya Simu, asilimia saba ya fedha hizo ndiyo inayokwenda kwa msanii; asilimia 13 inakwenda kwa *middle companies* na hivi sasa Tanzania ina *middles companies* kadhaa. Lakini kuna kampuni moja ambayo yenyewe ndiyo imehodhi kazi yote, ndiyo imeingia mikataba na makampuni makubwa ya simu, ambayo ni Kampuni ya *AIRTEL* na kampuni ya *VODA.* Kampuni hiyo inaitwa *Onmobile*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepeleka suala hili kwa Mheshimiwa Makamba, nimemweleza suala hili Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA*, nimemweleza suala hili Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia nilimemweleza

Mheshimiwa Waziri wa Habari. Kampuni ya *Onmobile* inafanya kazi hapa nchini bila leseni. Haina *Application License* ya *TCRA.* Waliomba, hawajapewa, lakini kampuni hii inafanya kazi ikiwa kwenye Makampuni mawili ya simu makubwa *AIRTEL* na *VODA*. Leo hii, ukienda Ofisi za *VODA* na *AIRTEL* utakuta Maafisa wa Kampuni hii hawajaajiri watu wengi kwa sababu biashara yao ni ya teknolojia. Wameajiriwa watu wawili tu, lakini wao ndiyo wenye mikataba, ndiyo wanaohodhi mikataba yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu, nimekaa, nadhani mlisikia kwamba tulikuwa tunaanda tamasha la vijana wasanii wa Mkoa wa Kigoma, nimekaa nao wakati wanatunga wimbo ule pale *Studio* za *THT* wiki nzima unaona namna ambavyo vijana wetu wanahangaika kutunga nyimbo zao, kulipa Studio, zinachezwa hawalipwi *royalty* hata televisheni na redio ya Serikali ambayo ingepeswa kuwa ya kwanza kulipa *royalty*, hawalipi *royalty*. Lakini inauma zaidi kwamba kijana huyu ambaye amehangaika, Kampuni ya Simu yake ni ku-*provide network* peke yake, *network* tu inakula asilimia 80 ya mapato yote ya wimbo.

Jambo hili nilimwomba kijana mwenzangu Mheshimiwa January kwamba, sisi ndiyo tunaopaswa kusimama kidete kutetea masilahi ya vijana hawa. Nilimwomba Mheshimiwa January, na ninamwomba tena. Nilimwomba tukiwa wawili, na sasa namwomba ndani ya hadhara kwamba tuwasaidie vijana wasanii wapate haki yao, walipwe kutokana na jasho lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaomba watu wa *TCRA,* kwanza nawashukuru, walifuata agizo la Kamati yetu kwa ajili ya kufunga mtambo wa ku-*monitor* mapato ya Makampuni ya Simu. Kwa hiyo, nawashukuru watu wa *TCRA* na ninawapongeza kwa kazi hiyo na najua wanajitahidi sana ku-*protect the industry*, lakini kazi ya dola kokote duniani ni kumlinda mnyonge. Kampuni za simu ni *giants,* wana nguvu, wanasema kwamba wao hawaingii mikataba moja kwa moja na wasanii, sawa. Lakini wanaingia mikataba na ma- *middle men,* ni jukumu lao na ni *ethical. Actually* ni *ethical* wao kuhakikisha ule wimbo ambao unawapa mapato, msanii anapata haki yake.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tukubaliane sote, msanii yeyote kazi yake inapotumika asipate chini ya asilimia 50 ya mapato yale yanayopatikana. Kama Kampuni itaamua kuwapa zaidi, iwape zaidi. *(Makofi)*

Pili, najua kuna majibu ya ki-*bureaucracy* ya kwamba taratibu za leseni zinafuatwa, na nini. Kama kuna kampuni imejaribu na imethubutu kuingia nchini kwetu na kufanya kazi bila *Application Licence*, kampuni hiyo inapoteza sifa ya kupewa leseni nchini. Tusione kwamba wamepewa sijui *exemption,* wameambiwa wafuate leseni, hapana. Wapewe, waondolewe ili wasanii wetu waweze kupata haki yao inayostahili. Kwa hiyo, hili nilikuwa naomba nilisisitize sana. Haiwezekani Kampuni ya Simu ichukue asilimia 80 ya mapato, msanii, kijana wa Kitanzania anayehangaika apate asilimia saba tu ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni pendekezo la kwamba, tumefanikiwa, na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tulilizungumza hili kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, walikuwa wamelisahau, akaliweka kwenye hotuba yake kwamba tumefanikiwa. Sasa kazi za wasanii zote zitakuwa na stika. Lakini kuna tatizo kubwa sana la *distribution.* Bado makampuni ya *distribution* yataendelea tu kuwanyonya wasanii. Sasa naliomba Shirika la Posta kwamba lijiandae kufanya kazi ya kusambaza kazi za wasanii kama wanavyouza stempu, kama wanavyouza kitu chochote kile. Shirika la Posta lipewe maelekezo maalum kwa sababu Posta imezagaa nchi nzima. Kwa hiyo, Shirika la Posta litaingia makubaliano na wasanii na kazi zao zitaweza kuuzwa maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mambo mawili nilitaka niyazungumze na nashukuru kwamba nayamaliza na muda wako kidogo unabaki. Najua suala la tamasha la Kigoma limeleta maneno kidogo ya kisiasa, lakini hayo ni maneno tu yatapita, kwa sababu kama Urais upo, utakuja tu, kama haupo hautakuja hata mtu afanye nini. Muhimu ni kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ya ziada kuitetea nchi yetu. Jambo moja tu sina mashaka nalo hata kidogo, ni uwezo, uadilifu, na uzalendo kwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu. Hili sina mashaka nalo hata kidogo. Naweza kuwa na mashaka na mengine, lakini kwenye hili, sina mashaka nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie katika hoja hii muhimu. Leo naomba nichangie kuhusu matumizi ya *internet* au mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, matumizi ya *computer* na *internet* yanatusaidia sana, yana faida nyingi sana ikiwemo kurahisisha utunzaji wa kumbukumbu, kusaidia watu kusoma, kusaidia hata walimu kufundisha kwa njia ya mtandao na mimi nikiwa mmoja wao, ikiwemo kurahisisha kufanya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya watu nchini, wamekuwa waki-*abuse* matumizi ya *internet* ama kwa makusudi ama kwa kutokujua, yaani kwa ajili ya *ignorance*. Lakini nadhani wengi ambao wanatumia vibaya *internet* na mitandao ya jamii kwa ujumla ni wale ambao hawana uelewa kwamba makosa ya *cyber* ambayo yanaitwa cyber *crimes* huwa yanachunguzwa kwa wenzetu ambao wameendelea kama Marekani. Makosa hayo huchunguzwa na watu ambao hubainika kutenda makosa hayo, huadhibiwa kama wahalifu wengine wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nchi yetu hii, haijawekwa sheria ya kuthibiti makosa ya kwenye mitandao. Hatuna *cyber laws*. Kwa hiyo, ndiyo maana watu unawakuta wamejikita kwenye mitandao, wanatukana Viongozi wakifikiri kwamba hawawezi wakabainika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwadhihirishie Watanzania, utafiti au uchunguzi wa makosa ya *cyber* upo na endapo Serikali yetu itaweka bayana Sheria ya kuwawezesha wataalamu kufanya uchunguzi wa makosa haya, nina uhakika tutakuwa na watuhumiwa wengi sana watakaotuhumiwa kwa matumizi mabaya ya *computer* na *internet*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wangu kwa Wizara hii husika, ishirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria kuleta Muswada hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuupitisha huo Muswada utakaoleta sheria ya kuthibiti matumizi mabaya ya mitandao na *computer* kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mashaka kwamba Waheshimiwa Wabunge wataunga mkono Muswada huo.

Ukizingatia asilimia ya Viongozi hapa mmeshatukanwa kwenye mitandao, ukizingatia Taifa letu sasa hivi linakosa heshima hata nje ya nchi yetu, kwa sababu ya watu wachache ambao wanatumia vibaya mitandao. Wakati wa Utawala wa Baba wa Taifa, pamoja na kwamba tulikuwa wadogo, hatujawahi kusikia hata siku moja eti Kiongozi wa nchi anatukanwa kwenye mitandao. Ni jambo la kushangaza, endapo tutaendelea kufumbia macho jambo hili, hakika hatutaheshimika popote pale duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, ninawaomba sasa tuweke

msukumo kwenye Wizara husika hii ya *Science and Technology,* walete Muswada haraka iwezekanavyo. Tumechoka kudhalilika, kuulizwa maswali ambayo hayaleti hadhi kwa Taifa letu tunapotoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote, ni kweli kwa sababu ya kutokujua, kuna watuhumiwa wengi ambao wamekuwa watuhumiwa bila kujua, wanatumia mitandao na wengine wanafikiri kwamba, nani atajua mimi nimeweka hayo maneno? Kuna *investigations* za *cyber crime.* Someni, nendeni kwenye *websites*, mtajua kwamba ukibainika kwa kosa la matumizi mabaya ya *computer* au *internet,* kwa mfano, Marekani unaweza ukala kifungo cha miaka mpaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Watanzania, wanafahamu kwamba hata tunapotumia *e-mail,* mawasiliano ya *e-mail,* nchi yetu haina Sheria inayoruhusu matumizi ya *e-mail?* Kwa hiyo, tunapotumia *e-mail, internet,* ni kama tunafanya *illegal?* Siyo kitu ambacho kimehalalishwa nchini, kwa hiyo, naomba Serikali ifanye haraka kuleta Muswada ambao utatuwezesha kuwa na Sheria ya kuturuhusu kuendelea kutumia hata *internet* na kudhibiti makosa ambayo yanafanywa na watu wengine kwa sababu ya *ignorance,* wengine bila kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo tu. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa utangulizi, kwanza niwape pole wafiwa wote katika ajali ile na Mwenyezi Mungu, awape moyo wa subira.

La pili, nampongeza aliyekuwa Waziri wa Miundombinu wa Zanzibar, Mheshimiwa Hamad Masoud, kwa kitendo chake cha ushujaa cha kubeba dhamana na akaweza kujiuzulu. Kwa mfano huo huo, kwa sababu, suala hili ni suala mtambuka, meli hizi zote zinaanzia safari aidha, Dar es Salaam au Zanzibar. Kwa hiyo, na mwenzake wa uchukuzi hapa akichukua hatua kama ile, atajijengea heshima na itakuwa ni funzo kwamba amewajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litupe funzo kama utangulizi kwamba, leo yametokea kwenye meli, lakini tujiangalie: Je, na ndege zetu zinaandikishwa kihalali? Zinakwenda zile *service* kubwa za kawaida? Kwa hiyo, tusingoje likatokea janga. Serikali, ni lazima ishituke! Hapa tunazungumzia Wizara ya Sayansi, na haya pia ndiyo mambo ya Sayansi. Kwa hiyo, jambo hili liangaliwe, tusije tukasema tumesoma, tumesoma, tumesoma; kama hatujasoma, hatuwezi kusoma tena milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika bajeti hii. Bajeti ya Wizara hii kwa ufupi ni yale maneno tunasema *business as usual.* Mwaka 2011 ilipangiwa Shilingi bilioni 64, lakini bajeti ya maendeleo, katika Shilingi bilioni 40, zilipatikana 23% tu. Wizara ambayo ina tafiti nyingi na mambo mengi, ndiyo kweli pana mpangilio wa kwenda mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Wizara hii imepangiwa Shilingi bilioni 70, lakini katika hizo Shilingi bilioni 70, za maendeleo ni pesa za nje. Mwaka 2011 ilikuwa Shilingi bilioni 500 tu za nje na ikapatikana asilimia ndogo ile. Mwaka huu imepangiwa Shilingi bilioni 1,125 za nje. Sidhani kama tutafanya kitu. Ikiwa Shilingi milioni 500 hazikutolewa, je, hiyo Shilingi bilioni 1,125? Ni tatizo! Kwa hiyo, siku ya mwisho itakuwa *business as usual,* hatuwezi kusonga mbele katika bajeti finyu ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri, atajitahidi na vijana wake, lakini kwa mfumo huu, hatufiki mbele. Tukumbuke ahadi namba moja. Agizo namba moja la Kamati, lile la 1% kama ilivyotoka katika *SADC,* ya *GDP;* mwaka 2010/2011 Shilingi bilioni 30 zilizotengwa, zikatolewa 19. Mwaka 2011/2012 Shilingi bilioni 25 zilizotengwa, zikatolewa Shilingi bilioni tatu; ahadi ya Mheshimiwa Rais, Shilingi bilioni 100. Je, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hoja za kuziangalia; namna gani tutafika? Katika mpangilio kama huu, atalaumiwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kufuata itifaki za nje, ambapo baadaye tutashindwa kutekeleza, ndio hiyo hiyo Mheshimiwa Waziri, leo anatuambia tutakwenda *digital* mwisho wa mwaka huu wakati *ITU* inasema Juni, 2015. Sisi tunaharakisha, halafu mwisho mambo yatushinde. Hili Mheshimiwa Waziri, hapa atueleze, hivi ni sababu gani ya

kuharakisha wakati *ITU* inasema Juni, 2015, sisi Watanzania eti kwa sababu ni Afrika Mashariki, tunasema mwishoni mwa mwaka huu? Sababu gani ya kuharakisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukumbuke hapa hapa Bungeni tulipitisha ile Sheria na ikabidi simu zisajiliwe. Sasa tujiulize leo, Mheshimiwa Waziri atuletee tathmini, simu kiasi gani zimesajiliwa? Je, hawawezi kununua simu watu Mitaani sasa hivi? Mbona bado kadi Mitaani tele zimejaa na watu wanazitumia? Sasa haya mambo ya kujifunga, aidha kwa kisingizio cha Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya *SADC,* hayo yanatushinda. Sasa tunakuja Jumuiya ya Afrika Mashariki, wenzetu watatekeleza, sisi tutashindwa. Hakuna haja ya kuwa na haraka hii ya kwamba lazima iwe ni mwisho wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la ving'amuzi. Suala hili la ving'amuzi hivi sasa, mtu mmoja inabidi anunue ving'amizi vitatu, vinne, wengine vitano. Leo ukitaka *TVZ* Dar es Salaam ununue king'amuzi chake, sijui *TV 2* hizi utapata king'amuzi kingine, *TV* nyingine hizi upate king'amuzi kingine. Mtu mmoja atakuwa na ving'amuzi kiasi gani? Halafu kila mwezi ulipie Sh. 9,000/=. Mnyonge ataweza wapi? Tunaitaka *TICRA,* walete king'amuzi siyo kwa malengo ya kufanikisha watu kibiashara, walete king'amuzi kimoja kitakachobeba *TV* zote za ndani. *TV* za nchini zote, ziwe zinapatikana kwenye king'amuzi kimoja na bei iangaliwe. Kodi ya Sh. 9,000/= kwa kila mwezi ni kubwa, wanyonge hawawezi, watashindwa kuangalia hata habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni jambo lingine. Tusifanye kwamba kila mtu anayetaka kuleta biashara yake ni *dampo* Tanzania, aje hapa, hapana. *TICRA* wasimamie hili, tuwe na king'amuzi kimoja, *TV* zote za ndani zipatikane kwenye king'amuzi kimoja. Haiwezekani leo mtu awe na ving'amuzi vinne, vitano, sita, ndani ya nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Agizo Na. 7 la Kamati hii, lilitaka kwamba, Wizara hii ionekane ina sura ya Muungano. Iwe ya Muungano! Mimi nafikiri agizo hili halijatekelezeka. Kuna Mashirika, Idara na Makampuni tisa yanayosimamiwa na Wizara hii, lakini kuna Posta na Simu, ndiyo vinavyojionesha. Halafu mpaka leo, ndio inatafutwa nyumba kwa ajili ya *COSTECH.* Mpaka leo, sijui kaajiriwa mtumishi mmoja, sijui wa *atomic* kule Zanzibar, halafu unasema Wizara hii ina sura ya Muungano. Hamna! *Infact,* Mheshimiwa Rais, hakukosea kukuweka wewe kwamba, kama wengine wameshindwa, wewe uifanye iwe na sura ya Muungano hasa! Usione haya kwa hili, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaambiwa ina Sura ya Muungano, tukiangalia wale katika ile Bodi ya Sayansi, wanaotajwa mle wote, kuna Mzanzibari mmoja tu. Sasa kwa nini nyingine ziwe na *Directorate* kule Zanzibar, kama *TTCL* na hizi nyingine ziwe na uwakilishi wa mtu mmoja mmoja? Kwa nini Bodi isiwakilishwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili namwomba Mheshimiwa Waziri alisimamie kwa nguvu. Vinginevyo ndiyo mnawapa moyo, mnawapa nguvu, wale wenzetu wengine wakasema hapana; na ndiyo maana tunasema Muungano wa namna hii, itafika labda suluhu, haya mabadiliko ya Katiba ndiyo yatatupatia *solution* sasa. Kwa sababu mnashindwa, mnaonesha ule upendeleo wazi wazi. Wewe umewekwa kwa upande mwingine ulisimamie suala hili liwe na sura ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende harakaharaka, kengele imeshagongwa. Tuje kwenye hili suala la nguvu ya atomiki; hivi sasa ndiyo tafiti za uchimbaji wa mwanzo wa *uranium* ndio unaanza. Lakini ni Mheshimiwa Waziri aliyetuambia kwamba, kuna Kitengo ambacho ni kwa mujibu wa Mikataba ya Kimataifa, wanaita *Radio Nuclaid Monitoring Station.* Je, kina uwezo wa namna gani? Hivi sasa tumekiwezesha namna gani kabla ya kuchimba hizi *uranium?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo. Ikiwa kwanza hatujakiwezesha na kikaweza kufanya kazi ipasavyo, halafu huku tunaingia katika mambo hayo makubwa, ni matatizo. Madini haya, yanahatarisha maisha ya mwanadamu, madini haya si ya kufanyia mchezo, yanaua kidogo kidogo, pengine kupitia maji tu, pengine kupitia hewa nyingine na tunajua athari zilizotokea miaka hiyo ya zamani huko Hiroshima. Kwa hiyo, hiki Kituo kifanyiwe uwezekano wa kuwezeshwa na kiendelee kufanya kazi. Vinginevyo, haitakuwa na

haja ya kuharakisha kuchimba *uranium,* ikiwa maisha ya Watanzania yako taabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika hizi tafiti nyingi zinazofanywa zote zimeelekezwa upande mmoja wa Jamhuri. Bara; mifugo, sijui kitu gani, Tanzania ina kilometa 800 na upuuzi, Ukanda wa Bahari na Visiwa hivyo vya kwetu na vingine. Kwa nini, kusiwe na tafiti za baharini za kuwawezesha Wavuvi?

*(Hapa, kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii…

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mnyaa…

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha, eeh?

**MWENYEKITI:** Eeh, habari ndiyo hiyo! *(Kicheko)*

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwanza, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara ya Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia, kwa kuanzisha Mpango wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF).* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu kama utaweza kutekelezwa vizuri, naamini kabisa kwamba utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa Watanzania wengi ambao wako kule Vijijini na hasa katika maeneo ambayo hayajapata mawasiliano mpaka sasa. Mpango wa Mawasiliano kwa Wote ni mpango mzuri sana, lakini nasikitika mpango huu umechelewa, umechukua muda mrefu mno. Mpango uko kwenye *logistics* tu. Mwaka 2011 nilisimama pia nikaongelea suala hili. Mwaka huu sasa nasimama kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Ujenzi, nisingependa tena kusimama katika bajeti ya mwakani 2013, bado tunazungumzia Mpango wa Mawasiliano kwa wote na bado utekelezaji wake ukiwa haujatimia kusema ukweli, haitakuwa sawasawa. Nategemea kabisa mwak 2013, tutakapokuja katika bajeti mwezi wa Saba kama huu, Mheshimiwa Waziri atuambie kwamba mpango huo umeshaanza kutekelezwa na vijiji kadhaa vimeshaanza kupata minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 Juni, 2012 wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali langu nililouliza, linalohusiana na matatizo ya mawasiliano Wilaya ya Liwale, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba, Serikali inakuja na mkakati wa kuhakikisha kwamba inapeleka mawasiliano ya uhakika kwenye vijiji 2,175, na kwamba Serikali tayari ilikuwa imeshapata Shilingi bilioni 45 kutoka Mfuko wa Benki ya Dunia, na kwamba mwaka 2011 walitangaza tenda na bahati

mbaya tenda haikupata Mzabuni kutokana na gharama kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Wizara kitu kimoja kwamba, vijiji 2,175 ni vingi sana na ninafikiri kwamba mradi huu unapaswa kuwa endelevu. Sasa badala ya kutaka kufanya vijiji vyote 2,175 kwa wakati mmoja, nafikiri wangekubali tu kwamba, tuanze na mradi huu kwa awamu. Wizara iwe na kazi ya kuangalia maeneo ambayo hayana mawasiliano au yana mawasiliano ya shida sana, kama Wilayani Liwale na kuanza na maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Shilingi bilioni 45 kama watazingatia taratibu hiyo, nina uhakika mpaka mwakani 2013 watakuwa wamefikia hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huu.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Sayansi na Naibu wake, lifanyieni kazi hili. Kwa kiasi hiki cha pesa ambacho tumekipata, basi zianze kufanya kazi. Tunahitaji sana mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ujenzi wa minara ambao unafanywa na ndugu zangu wa *Airtel, Zantel, TIGO* na *Vodacom.*

Nilikuwa nafikiri kwa mawazo yangu kwamba, ujenzi wa minara hii ni vyema ungefanyika kwenye maeneo kama kule vijijini, maeneo ya Serikali ya Vijiji, ili mapato yanayopatikana kutokana na minara hii yaingie kwenye Mifuko ya Serikali za Vijiji, ili ziweze kusaidia shughuli za maendeleo za Vijiji hivyo badala

ya utaratibu wa sasa ambao unakuta mnara umewekwa tu. Hata sijui ni kwa jinsi gani, inatokea mnara kila mahali, unakuta minara hii imejengwa kwenye maeneo ya watu binafsi, lakini maeneo ya Serikali za Vijiji yapo. Kwa nini tusiyatumie haya na Vijiji vikapata mapato yakaingia kwenye Vijiji vyao, badala ya kumpelekea mtu mmoja? Kwa kweli, siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana mnapokwenda kujenga ile minara, tafuteni maeneo ya Serikali za Vijiji ili pesa zile ziwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye Sekta ya Sayansi na Teknolojia, na hasa kwenye masuala ya utafikiti. Tafiti nyingi hapa Tanzania zinafanywa na *institutions* mbalimbali, zinafanywa na Vyuo Vyetu Vikuu, zinafanywa na *institutions* nyingine kama *TIRDO, Tanzania Food and Nutrition Centre* na Mkemia Mkuu, na kadhalika. Lakini sina uhakika kama kweli kuna chombo ambacho kinafanya *recording* ya *researches* zote zinazofanyika Tanzania hii, kwamba mtu akitaka kuona kwamba, ni nani, mtu gani na *institution* gani ilifanya *research* gani na mwaka gani? Anaweza kwenda wapi? Ni kitu gani ambacho kina-*coordinate* suala la namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawaza au nilikuwa natoa ombi kwa Waziri wa Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Naibu Waziri kwamba, ni vyema kuwe na kitu ambacho kina-*coordinate,* kinafahamu kabisa kwamba mwaka fulani kulikuwa na Mtafiti huyu, alitafiti kitu fulani na *results* zilikuwa hivi, na kitu hiki kiko hapa,

na tunaweza kumpata wapi. Hii itarahisisha sana, na pia itapunguza *repetition* ya *researches.*

Leo nafanya tafiti, *records* zangu zinabaki kwenye *institution* ambayo nimefanya na mwingine anafanya tena *research* ile ile, kwenye *institution* yake, *coordination* ya kwamba, huyu alifanya kule na huyu alifanya kule, ni nani anafanya kazi hiyo? Naomba suala hili lizingatiwe, kuwe na *centre* ambayo tunaweza kukusanya takwimu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusu matangazo ya mitandao ya watu binafsi. Sina uhakika kama hayo matangazo na hizi *promotions* sisi haitu-*cost,* hatukatwi hela yoyote kutoka kwenye hela zetu ambazo tunazitumia? Sasa, hilo ningependa kufahamu, matangazo yanayokuja na *promotions* zinazokuja, sisi kama watumiaji wa simu hizi, tunaathirika ama hatuathiriki?

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini pia matangazo yamezidi mno. Kila ukikaa dakika tano unakuta tangazo la *TIGO,* sijui nini; dakika mbili tangazo la *TIGO,* sijui nini; wakati mwingine unategemea kupata labda *message* ya pesa, una ahadi ya pesa, unaona *message* inaingia na mtu alishakwambia nitakutumia pesa au nitafanya kitu fulani kuhusiana na pesa muda fulani, ukitegemea *message* ile dakika inakuja *TIGO Promotion.* Kwa kweli inakatisha tamaa sana. Sisemi kwamba matangazo yasiwepo, lakini kwa kweli, *now it is too much.* Naomba yapunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naipongeza Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao. Lakini naomba nianze kuchangia katika eneo la kodi inayolipwa na Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zinazolipwa na Kampuni za Simu, haziendani na uhalisia, kwani, nchi yetu ya Tanzania ina watumiaji wakubwa sana wa simu na ukiangalia katika nchi za Kiafrika, ni nchi ya tatu kwa matumizi ya simu. Lakini kipato kinachoingia kwa nchi hii ni kidogo sana. Nilikuwa naiomba Wizara, iangalie kwa makini, iweze kurekebisha mipango mizuri ya kukusanya kodi ambayo itawasaidia Watanzania. Vinginevyo, tutakuwa tunawapa faida kubwa sana Makampuni, kwa kutengeneza faida kubwa ambazo zinakwenda kunufaisha nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Wizara inatakiwa ilifanyie kazi ni kuangalia umuhimu wa kudhibiti wizi katika mitandao. Watanzania walio wengi sasa hivi wanatumia mitandao kuhamisha fedha zao, lakini kumejitokeza sasa hivi aina fulani ya wizi katika Makampuni yanayoendeshwa na simu hizi; wanaiba fedha. Sasa sijui kama wanashirikiana na mabenki. Ni lazima waangalie katika umuhimu wa aina yake, vinginevyo Watanzania walio wengi wataanza kupoteza fedha kupitia kwenye mitandao. Hili ninalisisitiza kwa sababu, kumeanza kuwa na matatizo makubwa sana. Wapo wajanja wanaokuja nchini,

wanafanya shughuli za kucheza na mitandao na kuiba fedha kwenye mabenki mbalimbali. Ni vizuri wakajielekeza sana huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mawasiliano kwa wote. Eneo hili ni muhimu sana katika maeneo yetu hasa ya Vijijini. Mkoa wa Katavi ni Mkoa mpya ambao hauna mawasiliano mazuri. Nilikuwa naiomba Wizara iangalie hasa katika Jimbo langu. Kuna Kata tatu ambazo hazina mawasiliano. Kuna Kata ya Sibwesam ambayo ina Vijiji vya Nkungwi, Kabage, Katuma, Mpembe, Kaseganyama, vijiji hivi vyote vina idadi ya watu walio wengi ambao hawana mawasiliano. Mawasiliano yao wanakwenda wanapanda kwenye mti ndiyo wapate huduma ya mawasiliano. Naiomba sana Wizara iangalie maeneo ambayo yako nyuma sana kama hayo, waweke kipaumbele, wapeleke huduma inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna Kata nyingine, Kata ya Kabungu yenye Vijiji vya Kabungu, Kasinde, Mnyagala na Kamsanga havina mawasiliano ya simu kabisa na viko mbali sana na eneo la Makao Makuu ya Wilaya. Ni vizuri tukapeleka huduma hiyo iwasaidie ili wananchi nao wawe katika eneo ambalo lina mawasiliano na nchi kwa ujumla. Lakini bado kuna eneo lingine la Kata ya Ilunde katika Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kata hii iko mbali sana na maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya kiasi kwamba, huduma hiyo haipo na wananchi wanaishi kama vile wako Kisiwani. Takribani zaidi ya Kilometa 100 kama na 30 hivi kutoka Mpanda Mjini ndiyo unaikuta hiyo Kata. Wananchi hawa, wanafunga safari kutoka Kijijini kwao,

wanatembea karibu kilometa 20 kutafuta mahali ambapo pana mtandao. Tena wanapanda kwenye mti, wanapata shida sana.

Naiomba Serikali, iangalie kwa umuhimu wa aina yake, iwasaidie wananchi hao ili waweze kupata huduma ambayo itawasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya na maeneo ambako wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ikae na Makampuni ya simu, waangalie ni jinsi gani wanaweza wakasaidia kupunguza gharama za simu. Wananchi wanatumia gharama nyingi sana kwa ajili ya simu. Lakini ukiangalia fedha tunazotoa ni nyingi. Ni vizuri sasa wangeangalia wabadilishe mfumo ambao upo ili tuweze kuwasaidia wananchi hawa ambao asilimia kubwa wanatumia matumizi hayo ya simu kwa ajili ya shughuli za masoko, mawasiliano ya kawaida, na kuhamisha fedha. Kwa hiyo, ni vizuri sana tusije tukaangalia tu upande mmoja wa Makampuni kwamba yanapata fedha. Ni vyema tukaisaidia jamii ili iweze kuneemeka na mfumo mzima wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iongeze jitihada kuhakikisha katika maeneo ambayo bado hayana huduma, wapeleke huduma hiyo ili waweze kuwasaidia. Mwisho, naishauri Serikali iangalie maeneo hata yale ambayo yana mitandao, ukweli, bado mawasiliano yao siyo mazuri.

Nina baadhi ya Kata ambazo zipo katika Jimbo langu, mawasiliano yao siyo mazuri. Wanatumia fedha nyingi na wanapopiga simu, matokeo yake

wanaangalia kwenye salio, limetumika wakati bado hawajafanya mawasiliano. Ipo Kata ya Mpanda Ndogo, ambayo ina Vijiji vya Majalila, Vikonge, Ifukutwa, Mchakamchaka na Igalula, pamoja na kuwa kuna mtandao, bado mawasiliano siyo mazuri. Ni vizuri wakaenda kufanya utafiti, waangalie maeneo haya ambayo kuna minara, lakini mawasiliano ni ya shida na bado zinakata kwa wateja ambao wanatumia simu hizo bila kuwa na mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Wizara hii, iweze kuangalia umuhimu wa kufuatilia kwa karibu sana ili iweze kutoa huduma ambayo itakuwa nzuri kwa wananchi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango mizuri. Muda wetu uliobakia ni mchache. Wachangiaji wetu waliopangwa leo wamebaki watatu, na mchangiaji wetu wa kwanza jioni ya saa 10.00 atakuwa Mheshimiwa Masauni, Mheshimiwa Dkt. Nkya na Mheshimiwa Rajab, ambaye nimemtaja toka mwanzo.

Ningependa tu kukumbusha Tangazo lile la Zimamoto. Zoezi hili litaanza saa 07.30. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote wakipata nafasi, basi wapite watazame namna zoezi hili linavyofanywa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.10 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu waliobakia sasa hivi ni watatu ambao watakamilisha orodha ya wote waliomba kuchangia leo hii. Nachukua nafasi hii sasa kumwita Mheshimiwa Masauni akiwa mchangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Dkt. Nkya ujiandae na Mheshimiwa Rajab ujiandae kuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza, naomba nitoe salaam za pole kwetu sote kutokana na ajali iliyotokea ya meli ambayo imepoteza maisha ya Watanzania wenzetu. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi waliotangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufunguzi huo, mimi mchango wangu nataka nianze kujikita kwenye eneo la sera. Lakini kabla ya kuchangia, naomba ku-*declare interest.* Mimi niliwahi kuwa mjumbe wa Kamati ambayo iliandaa rasimu ya sera ya teknolojia ya *nuclear*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa nimesimama mbele ya Bunge hili Tukufu nikiwa na masikitiko makubwa sana kwamba, toka tumeandaa sera ile, rasimu imekamilika, Kamati ambayo iliundwa na Wizara ya Mawasiliano Sayansi na teknolojia imemaliza muda

wake, lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikumwona kugusia ni hatua gani ambazo zimefikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzania Atomic Energy Commission* tayari ina sheria ya mwaka 2003 ambayo inafanya kazi. Leo hii kuna michakato ya uchimbaji wa madini ya *Uranium* inaendelea, lakini sera mpaka sasa hivi ipo kwenye ma-*draw*.

Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuelezee nini hatima ya kazi ile ambayo tumetumia fedha nyingi za walipa kodi wa nchi hii na muda mwingi, imefikia wapi? Vinginevyo, tutakuwa tunarudia makosa hayo hayo. Leo nchi yetu ina tatizo kubwa la umeme kutokana na gharama kubwa ya kununua mafuta. Tumechimba gesi, bomba limejengwa, hatukuona mipango, hatukuwa na sera mpaka leo, matokeo yake bomba lile hatukujua kama mwaka 2012 litakuwa halikidhi mahitaji ya Watanzania wa sasa hivi. Lakini changamoto ziko nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule ambapo tulikuwa tunaandaa ile sera ilikuwa ni kipindi cha tatizo kubwa sana. Tukapoteza muda mwingi kufanya utafiti wa kina, kwa hiyo, ni jinsi gani katika miaka mingi ijayo miaka 20, 30 inayokuja kwamba pengine matumizi ya teknolojia ya *nuclear* yanaweza yakachangia kiasi fulani katika kushiriki kama sehemu moja ya vyanzo vya umeme nchini. Lakini tulibaini kwamba kuna mambo mengi ambayo yanahitaji kufanyika na tulifanya hivyo. Masuala ya kujenga uwezo wa Watanzania, baadaye masuala ya *regulations*, masuala ya *infrastructures* mambo mengine mengi, lakini tukaambiwa kwamba kikwazo ni sera. Ni jambo ambalo linaweza likafanyika

kwa haraka na sera hii ilikuwa na wigo mpana, siyo katika eneo moja tu, lakini matumizi ya teknolojia ya *nuclear* kwa ujumla wake. Kwa hiyo, nilitaka nisisitize kwamba Mheshimiwa Waziri ni muhimu atakapotoa maelezo atufafanulie hili.

La pili, ambalo nilikuwa nataka kuchangia ni suala hili la utafiti. Utafiti na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano *ICT* katika kutengeneza ajira na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Nataka nichukue fursa hii ya kipekee sana kuwapongeza sana Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* chini ya Mkurugenzi wake Mkuu Dkt. Hassan Mshinda kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayofanya katika eneo hili hapa.

Kwanza, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kipindi kifupi ambacho amekaa, sasa *COSTECH* ina ofisi Zanzibar. Niseme kwamba changamoto ilikuwepo na nilihudhuria wakati wa ku-*launch* ile ofisi kule Zanzibar. Kulikuwa na watafiti wengi sana ambao pengine wengine hatukutegemea kama Zanzibar kuna watu wanaweza wakavumbua magari. Sasa changamoto kwa Serikali kwamba tafiti hizi zitumike vyema kuandaa sera madhubuti ambazo zitasiaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza zaidi *COSTECH* kwa kuwa na *vision.* Nchi zote zilizoendelea ulimwenguni zimeendelea kwa sababu walikuwa na dira sahihi. *COSTECH* wana dira na wana mipango mizuri ya kutekeleza dira ile. Labda nitoe mfano mmoja. Malaysia ni nchi ambayo ilikuwa masikini sana. Haikuwa masikini, lakini ilikuwa katika

nchi masikini kama ilivyo nchi yetu, wakati huo miaka ya nyuma na nchi nyingi za Afrika zikiwemo Ghana, Egypt zilikuwa zina uchumi mkubwa kuliko hata Malaysia. Wakatoka kwenye kilimo cha kulima mpira wakaelekea kwenye viwanda. Katika mwaka 1990 Malaysia ikabadilika na kuwa ni Taifa ambalo linategemea *knowledge economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unakwenda sana lakini naomba nizungumze kwa haraka kwamba hii *Cyber Jaya* ambayo imeanzishwa Malaysia ambayo walifuata *vision* ile ya *Silicon Valley* ya Marekani, ndiyo jambo ambalo naona. Japokuwa hatuwezi kujilinganisha, Malaysia na Marekani kwa sasa hivi *COSTECH* kupitia Dar es Salaam *TEKNOHAMA Business Incubator* inafanya. Nami nimesema hivyo kwa sababu nimeshiriki katika program mbalimbali ambazo zimesaidia sana kufanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana *COSTECH* kwa niaba ya Taasisi ya *Tanzania ICON* ambayo *COSTECH* siyo tu kwamba wamefanya kazi nzuri, lakini nzuri pia ya kutanua wigo wa matumizi ya teknolojia hizi maeneo yote ya nchi yetu. Taasisi hii kwa mara ya kwanza ita-*host,* itakuwa wenyeji wa *program* ya matumizi ya *mobile,* teknolojia, kwa kutengeneza *program* mbalimbali. Lakini pia tutashirikiana vizuri kuanzisha kituo cha ambayo itakuwa ni *Centre of Excellence,* kitasaidia sana vijana wa Zanzibar. Kwa hiyo, nichukue fursa ya kipekee kuwashukuru na kuwaambia kwamba tutaendelea kuwaunga mkono katika juhudi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, nichangie suala la mawasiliano ya simu. Inasikitisha sana kwamba bado mchakato wa kuweka *traffic monitoring system,* hatujabainisha *exactly* ni lini hili litaanza. Upotevu wa mapato kwenye simu kupitia *Cooperative Tax* ni mkubwa, sina haja ya kurudia takwimu muda umekwisha lakini tunashindwa na nchi ambayo imetoka katika vita juzi tu. Kwa hiyo nilikuwa najaribu kusisitiza jambo moja la msingi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Masauni, mchango wako mzuri, lakini sasa ndiyo tunabanwa na muda. Mheshimiwa Dkt. Nkya.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki nitoe salamu za pole sana kwa wale walioguswa na janga la kuzama kwa meli ya MV. Skagit. Naomba Mwenyezi Mungu, wale wote waliopoteza maisha yao awalaze mahali pama Peponi, na aendelee kuwafariji wale ambao wamepoteza ndugu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzito na nzuri wanayoifanya, pamoja na Watendaji wao kwa hotuba hii nzuri. Pamoja na pongezi hizo, naomba nizungumze kidogo machache kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwa yale yafuatayo, kwamba Mheshimiwa Waziri anaweza akatueleza ni nani ambaye anawajibisha hawa ambao wameanzisha mitandao ya *blog* ambayo inatumika kuwatukana raia wengine wa nchi hii? Wanatukana na inawapa fursa vijana wetu kutokuwa na maadili mazuri kwa sababu wamepata ulingo wa kutukana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taifa hili lifikirie, tena liangalie na najua kwamba Mheshimiwa Waziri akikaa na wataalam wake wanaweza wakajua namna ya kuweka maadili kwa hawa ambao wana-*operate* hizi *blog*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Tanzania tunasema hii ni karne ya Sayansi na Teknolojia, lakini naomba niseme kwamba huu msemo unakuwa *applicable* katika maeneo ya Miji tu, Vijijini bado wananchi wetu hawajaonja hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nitoe ushauri kwa Serikali, kuna sehemu ambazo ni *Shopping Centres* vijijini, kuna umeme, na vijana wangependa kupata huduma za *internet*. Katika Jimbo langu Kata ya Kilole, *Center* ya Tandahe pamoja na Kiloka, vijana wako tayari kulipia au kuchangia kama watapata itawawezesha kuwa na *center* ya *internet café* na wakawa wametoa wazo kwamba, kama Serikali itapenda kuwaanzishia, basi ianzishe kwenye Shule za Sekondari ambazo ziko kwenye maeneo hayo, uwe kama ni mradi wa Shule utakaoweza kusaidia kuingiza

hela kidogo hata angalau ya kununua karatasi na wino wa kuweza kurudufua mitahani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuwa anapita kwenye Jimbo langu na kwenye maeneo mengi ya Morogoro vijiji wakati wa kampeni, aliahidi kwamba na sisi ingawa tuko kilomita 200 tu kutoka Dar es Salaam, kuna wananchi ambao wakitaka kupiga simu, ni sharti wapande kwenye miti au kwenye vichuguu au kwenye mapaa ya majumba. Hii inawafanya akina mama wanashindwa kuwasiliana na simu, wananchi wengine inabidi wasafiri waende kwenye maeneo ambayo ni ya mtandao. Kwa hiyo, inabidi alipe nauli kwenda kupiga simu, azungumze na mume wake na mtoto wake au kutoa taarifa ya kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ameahidi mara mbili katika Jimbo langu na Jimbo la Morogoro Kusini. Pia naomba Serikali leo inijibu na waniambie kabisa kwamba, ni lini basi Kata ya Kilole, Kata ya Kiloka, Kata ya Matuli, Kata ya Mkulazi, Kata ya Kitudagalo na maeneo ya Ngerengere tutapata huduma za mtandao wa simu? Ingawa wananchi kila nyumba kuna simu, ila ni mpaka wasafiri kwenda Ngerengere kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwapunguzie wale wananchi nao wajisikie kwamba wako kwenye Tanzania ambayo sasa imetimizia miaka 50 ya Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya kubadilika kutoka

kwenye huo mfumo wa analojia kwenda kwenye dijitali. Nikienda ziara, wananchi wananiuliza huyu mnyama anaitwa analojia na dijitali, ni nani? Tunasikiasikia tu wala hatuelewi. Siyo jambo la kuchekesha, hawa wananchi wana haki ya kupewa muda wa kuelewa kwamba huu mchakato unakwenda wapi? *What does it mean? Implication* yake kwa gharama ni nini? *Implication* yake kwa uelewa na mambo mengine ni nini?

Naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu iongeze muda na Wizara, sasa itengeneze mtandao wa kutoa elimu sahihi kwa wananchi kuwaondolea hofu, waelewe ni nini maana yake? *What does it mean?* Hivi vile vitelevisheni vyao vidogo vidogo vyenye mgongo vitatupwa ama vitatumika? Kama atanunua king'amuzi, maana yake ni nini? Atahitaji kulipia kwa mwezi? Huyu ni mkulima ambaye ananunua mara moja tu, anatumia betri kuweza kui-*operate* ile siku ambayo anaangalia mpira na siku ambayo anasikia Mheshimiwa Rais anahutubia au kuna tamasha kubwa Dar es Salaam. Sasa kweli *how do they operate* zile *costs?* Zitakuwa *involved* kwenye kubadilika kwenye analojia kwenda dijitali.

Naomba Serikali yetu, wananchi ambao ni wakulima walio wengi, wengi wao ni masikini, Wizara iangalie hilo na itueleze na izungumze leo ili wananchi waelewe, wasifikiri kwamba huu ni mradi wa vigogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, niwe mkweli. Wananchi walio wengi hawaelewi kwamba ni

mabadiliko ya ulimwengu, wanaona kwamba ni mradi wa vigogo kama inavyotokea wakati mwingine mnakamatwa, mnanunua *fire extinguishers* mnakuja kugundua kwamba ni za mtu.

Kwa hiyo, hili wananchi wawe na amani na imani na Serikali yao, waone kwamba Serikali yao inawajali. Tunaomba waongeze muda, elimu itolewe. Tunaweza tukatumia Walimu wa Sekondari za Kata, tunaweza tukatumia Walimu wa Shule za Msingi, na mtu mwingine yeyote ili mradi wananchi waelewe kwanini tunakwenda na mfumo wa dunia? Hakuna anayeelewa utandawazi ni nini. Kule vijijini naomba hilo liangaliwe vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni matumizi ya vijana kwenye kutangaza hii mitandao ya simu. Sawa ni ajira ya siku moja, siku mbili, lakini isiwe ndiyo sababu ya kuwafanya wasichana na wavulana kwenda kulundika kwenye Makao Makuu ya Kampuni za Simu wakisubiri kupewa karatasi za kwenda kusimama barabarani na kunengua kwenye magari bila kuwa na mfumo unaoeleweka.

Kuna ugumu gani kwa kampuni hizi kuajiri vijana ambao wanatumika kama *promoters?* Kwa sababu hawa wana-*promote* hasa wale wa kike, ana-*promote,* analipwa siku hiyo hiyo, anaondoka. Hivi kesho akikosa kuingia kwenye ule mfumo, naomba niseme kwamba wengine wananung'unika kwamba inatoa wasaa kwa wale *supervisors* kuanza kutafuta rushwa ya ngono kwa wale vijana wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mitandao ya simu sasa iangalie namna ya kuweza kuajiri hawa vijana ambao watatumika kwenye *promotion* ili nao wao basi wawe na uhakika kwamba watapata chakula na watapata ajira ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hizi kampuni zimekuwa zinatoa misaada mbalimbali lakini hii misaada inakwenda Mijini, haiendi Vijijini na watu wa Vijijini wanatumia simu.

Tunaomba sasa na wao watengenezewe mfumo ambao utaeleweka wa kutimiza *cooperate responsibility* yao isiwe ni kwamba kwa sababu wanamfahamu Mama Nkya, tupeleke kwa mama Nkya, *no*! Wananchi wote wa nchi hii wanatumia simu, hebu mwangalie namna ambavyo mtatengeneza mfumo ambao utatoa usawa kwa ile misaada mnayotoa ya kijamii na siyo vibaya wakiitengeneza ya mwaka mzima na Bunge hili likaelewa kusudi kila mmoja ajue kwamba *VODACOM* watakuja kwangu kusaidia madawati, wengine wajue aah, *Airtel* itakuja kwangu kusaidia kujenga labda *theatre* kwenye Kituo cha Afya au kuleta vitanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba Mheshimiwa anijibu lile la kwangu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Nasema, sasa naunga mkono hoja kwa sababu najua watafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru wameshakusikia.

**MHE. DKT.LUCY S. NKYA:** Naomba uje Morogoro vijijini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nataka nikupongeze wewe binafsi kwa sababu tangu ulipochaguliwa hapo, sijawahi kukupongeza kwa kuwepo hapo. Lakini la pili, nami nataka nitoe salaam zangu za pole kwa niaba ya wananchi wa Ole, kwa msiba ambao umetokea kutokana na kuzama kwa meli ya MV. Kalama. *(Makofi)*

Vilevile nataka nichukue nafasi hii na mimi kumpongeza mwakilishi wangu ambaye anatoka katika Jimbo langu, Mheshimiwa Hamad Masoud Hamad - Waziri wa Miundombinu wa Zanzibar ambaye alifanya maamuzi magumu, maamuzi ya kisiasa, maamuzi ambayo tunasema ule ndiyo utawala bora wa kukubali kuwajibika pale panapopaswa kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka nitoe mshangao wangu mkubwa kwa Mawaziri hususan Mheshimiwa Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Uchukuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba

hadi mpaka sasa hivi bado yeye anakalia Kiti cha Uwaziri! Kwa kweli ni suala la kushangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala tu kwamba ile meli imesajiliwa Zanzibar, sawa. Lakini waliokufa mle wamo wanatoka Bara, meli imeondokea bara, chini ya mikono ya *SUMATRA.* Kwa kweli nitashangaa kwamba itafika kesho kutwa Mheshimiwa Waziri atakuja hapa kusoma bajeti ya Wizara yake. Hilo nitalishangaa kwamba bado atakuwa hajajiuzulu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika mada yangu na nianzie na suala la ving'amuzi, analojia na dijitali. Lakini nataka nitoe tahadhari kwa wenzetu wa *TCRA* kwamba matumaini ya Watanzania ni kwamba gharama zipungue, siyo kuja kujikuta tunaingia katika matatizo. Suala hili la kuondoka katika analojia kwenda katika dijitali, hapa kuna miradi na hapa kuna Mapapa na Mafisadi wataingia kwa kuwa halifanywi na mkono wa raia wa kawaida, halifanywi na mwananchi wa kawaida, lakini watakaofanya hapa wenyewe wana majina yao, wanajiita *maltparts operator,* yaani wale ambao watamiliki miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna wenzetu wanaoitwa *service provider.* Hawa ni akina *ITV, TBC* na wengine. Hawa ndiyo *providers*. Lakini kuna hawa ambao watakuwa wanashikilia ile mihimili au miundombinu yenyewe ya mawasiliano. Tunawaomba *TCRA* wajaribu kukaa na hawa watu wapange bei ambazo hazitamwathiri mwananchi wa kawaida,

wasije wakaachwa peke yao, na badala ya kuona hii ni faraja, ikawa ni balaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka niingie katika suala la *Uranium*. Kwa kweli nimepata wasiwasi kwamba Mjumbe mmoja wa Kamati ambaye alisaidia kuunda sera ya mambo ya *Uranium* leo analalamika kwamba jamani, ile sera imewekwa mkobani wakati huku tunasikia kwamba *Selous* mmeshaitoa au mna lengo la kuitoa kwa ajili ya kuchimba *Uranium*. Jamani afya za Watanzania mmeziweka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema na ninachotoa tadhadhali ni kwamba Tanzania mko katika mkataba wa Kimataifa. Kuna mkataba unaitwa *Comprehensive Nuclear Test Burn Treaty* au *CTBT* ambao unahusiana na *Nuclear Weapons.* Mtakuja kuwekewa vikwazo vya kimataifa hapa, naomba mchukue tahadhari kubwa. Wale wenzetu ambao wanashughulika na Tume ya *Atomic* wajaribu kile Kituo chetu kilichopo Dar es Salaam cha *Radio Nuclear Monitoring Station,* hebu kile Kituo tukipe nguvu. Tushirikiane au mshirikiane baina ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Muungano ya Mazingira, ili hiki Kituo kabla hatujaingia katika hii mikataba, ni vyema kwamba Kituo tusikishirikishe *almost hundred percent.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo suala la Taasisi ya Teknolojia *Dar es Salaam (DIT)*. Hali ilivyo, *DIT* siyo nzuri na siyo ya kuridhisha na hadi leo hii bado Wizara inaendelea kupachika

majengo katika maeneo yale. Sasa hivi kuna jengo la ghorofa 10 wamelipachikiza tu pale. Kuna jengo lingine la utawala wamelipachika. Jamani, lile eneo limeshakuwa dogo! Hivi tutakaa kijisehemu kidogo kila siku, tunapachika majumba pale pale? Hivi hatuna akili ya kufikiri?

Naomba kitu kimoja kwamba badala ya kuendelea na utitiri wa kuchomeka majengo, hii Taasisi ina kiwanja chake ambacho inamiliki, kwanini hiki kiwanja hakiendelezwi? Ina ardhi yake iliyopo Mbezi Kilikungawima, ipo ardhi yake. Kwa nini hii ardhi haiendelezwi? Tunaendelea tu kupachika majengo palepale! Naomba Mheshimiwa Waziri kama hii ardhi mmeshaiuza, basi mtuambie maana siyo tunasimama hapa tunatetea kumbe ardhi yenyewe haipo tena, imeshauzwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hili atuweke sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kuzungumzia la mwisho kama muda utaniruhusu, nizungumzie suala la Makampuni ya Simu na kulipa kodi.

Nataka niiombe kwanza Mamlaka ya Mawasiliano, jamani kile kipengele cha kuongezwa thamani katika *air time* ambacho kilizungumzwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunaomba wenzetu wa *TCRA* kaeni na Wizara ya Fedha muwaambie kwamba, chonde chonde, msituongezee thamani katika *air time*. Zipo fedha hebu zitafuteni, Makampuni ya Simu bado yanaendelea kukwepa kodi katika nchi hii, ushahidi ni kwamba, kwa nini Makamapuni ya Simu hadi leo hayataki kuingia katika *Dar es Salaam Stock*

*Exchange?* Hetu tujiulize, ni kwa nini? Hawataki kuingia pale kwa sababu dhambi zao zitakuwa zinaonekana. *(Makofi)*

Nakuomba Mheshimiwa Waziri na Taasisi zinazohusika, hebu mtuambie, haya Makampuni ya simu ili yakubali kuingia katika *Dar es Salaam Stock Exchange,* kwa sababu pale tutaweza kuwa-*monitor,* lakini hivi wanavyokwenda, kwa kweli watazidi kutuumiza, halafu sisi leo tena tuanze kuweka mambo mengine ya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, naamini muda utaniruhusu, nataka nizungumzie suala la *GMO.* Naomba nishauri kwamba Waziri anayehusika na suala hili, hususan wa Mazingira akae pamoja na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, waziangalie zile kanuni na wazirekebishe ili *GMO* iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nataka nizungumzie suala la utiaji viatilifu katika mafuta yetu. Katika sekta ambayo tunapoteza pesa nyingi ni suala la utiaji viatilifu katika mafuta. Hili limeachiwa makampuni binafsi. *A lot of millions, almost one million dollar* tunapoteza *per month*. Ninachoomba, baada ya kutumia Makampuni binafsi, watumike *COSTECH,* tunao na *TIRDO.* Kwa nini hawa tusiwatumie? Hizi ni *agents* zetu. Hapa tutaokoa *more than one million dollars* kwa mwezi. Naomba haya yatiliwe maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, kwa sababu wenzangu walishalizungumza ni ugomvi wetu wa kawaida baina yangu mimi na wewe Mheshimiwa

Waziri kuhusiana na ujenzi wa Ofisi ya *TTCL* Pemba. Ulinidanganya na nikakubali kudanganywa, na wewe naamini kwamba ni muungwana, kwa vile wenzangu walishaliongea hili, inshaalah utalitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rajab.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa - Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii na ambayo imetoa matumaini ya hali ya juu katika nyanja ya mawasiliano. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Mheshimiwa January Makamba - Naibu Waziri wa Wizara hii muhimu kwa jitihada zake za hali ya juu ambazo zimeleta ufanisi mkubwa. Pongezi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumkumbushia Mheshimiwa Waziri, orodha ya Kata na vijiji ambavyo hivi karibuni niliikabidhi Wizara ambazo mawasiliano yake ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Viongozi Wakuu wa Wizara kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kukabidhiwa jukumu la kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, ni vyema kukawepo mfumo unaokaribia kuwa rasmi *(quasi-official)* wa kuratibu misaada inayotolewa na Makampuni ya Mawasiliano, hususan ya Simu ili misaada hiyo iegemee zaidi kuboresha huduma za jamii zinazoyagusa maisha ya masikini wa nchi yetu. Huduma muhimu ambazo zinawagusa watu wa kawaida ni elimu na afya. Eneo lingine ni watoto yatima/wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo wajibu wa Makampuni haya kwa jamii *(corporate social responsibility)* utaratibiwa vyema, hali ya sasa ya makampuni haya kuchangia michezo zaidi huku huduma hizi zikisahauliwa itarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili ni kwamba elimu jamii itolewe kwa mapana juu ya tofauti ya *analojia* na *dijitali* na faida ya *dijitali*.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pili, naipongeza Wizara kwa kuanzisha Mradi wa *Video Conference,* mradi ambao utaweza kurahisisha kufanya mawasiliano kwa haraka na ufasaha zaidi na vile vile mradi huo utaweza kuipunguzia gharama

Serikali kwa kazi zake za kila siku. Hivyo, naishauri Serikali ichukue haraka na madhubuti ili kwenda na wakati, kwani tukichelewa naona dunia inatuacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya, kama ilivyo nia ya Serikali ya kuipandisha hadhi Taasisi hiyo kuwa Chuo kikuu, napongeza kwa azma hiyo na nashauri hatua za haraka zichukuliwe. Aidha taasisi hiyo *MIST* ni muhimu katika nchi yetu. Hivyo kuna baadhi ya mambo yanaishusha hadhi ikiwemo barabara mbovu iendayo katika Taasisi hiyo ambayo pia iko vichochoroni. Ni suala la aibu ukienda huko. Pia Chuo kinahitaji kupanuliwa na maeneo yapo, lakini kimekwamishwa na malipo ya fidia katika eneo la ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni matumizi ya simu za mikononi. Kwanza niipongeze Wizara kwa kuimarisha mawasiliano ya simu za mikononi kwa wananchi wa nchi yetu. Lakini hata hivyo kuna baadhi ya Makampuni hayawatendei haki wateja wake, kwani mara nyingi ukimpigia mtu simu unasikia mlio wa simu na baadaye unaelekezwa kwa Kampuni, inakata hela yako bila kupata huduma. Naishauri Wizara ifuatilie suala hili pamoja na lile la kutumiwa *message* za Kampuni za Simu bila ridhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni Mfuko wa *(UCAF).* Naiomba Serikali kupitia Wizara itekeleze azma ya mfuko ambao umelenga kuimarisha Mawasiliano kwa wote. Siku zimekuwa nyingi na kila bajeti ikija tunaambiwa mchakato unaendelea. Nasema

tumechoka na dili hizo, tunataka huduma hiyo kwa haraka hasa kwa upande wa Zanzibar.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imepewa bajeti ndogo ambayo haiwezi ikapambana na changamoto ambazo zinakabiliana nao. Kama inapata fedha za kutosha itawezesha kupatikana kwa mawasiliano ya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu kuna Kata ambazo hazina mawasiliano kabisa katika maeneo yao. Naiomba Wizara inihakikishie katika Kata ya Sibwesa yenye vijiji vya Sibwesa, Kungwi, Gabage, Kasekese, Kaseganyama na Matena. Katika Kata ya Katuma vipo vijiji vya Mpembe, Katuma, Kapanga na Kayenze. Maeneo haya yako mbali na Makao Makuu ya Wilaya. Naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wizi wa fedha kupitia mtandao. Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inadhibiti wizi huo ambao unaanza kushamiri? Naomba Serikali ije na majibu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za simu zinazotumika ni kubwa sana, ni vizuri Serikali ikakaa na wamiliki wa Makampuni ya simu waangalie umuhimu wa kupunguza gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi wanazotozwa Makampuni ni ndogo sana kuliko mapato wanayopata. Ni vizuri Serikali ikapanga viwango vipya vya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kama nitapata majibu.

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia kwa kazi yao nzuri wanayoifanya, na pia nayapongeza Makampuni ya Simu za Mkononi kwa jitihada zao za kuchangia kuyaboresha maisha ya Watanzania kwa kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania na pia kupitia biashara zinazotokana na huduma za simu za mkononi. Kuwepo kwa simu za mkononi kunatufaidisha sana kwa kuzifanya kama benki ya kuhifadhia na kutuma fedha, tunazitumia kama ni kiungo cha kuingia kwenye mtandao wa *Internet* na kupata taarifa mbalimbali, kwa mfano taarifa za milipuko ya maradhi, bei za bidhaa mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania wengi ambao wana vipaji vya ugunduzi, lakini watu hawa baada ya kugundua, hatuoni ule ugunduzi kutumika na kunufaisha Watanzania. Kwa mfano, Chuo cha *Dar es salaam Institute Technology (DIT),* kuna wanafunzi wamefanya utafiti wa kutumia gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani. Lakini matokeo yake hatuoni namna ambavyo Watanzania wanafaidika. Badala yake Watanzania wengi wananunua gesi ya kutoka nje "*ORYX*" ambayo ni ghali. Kuna vijana *COSTECH* ambao wamegundua namna ya kudhibiti wizi wa kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika nchi yetu kuna kesi nyingi Mahakamani ambazo baadhi ya Wagombea wameyakataa matokeo ya uchaguzi na

kudai kuwa kulikuwa na uchakachuaji wa kura na matokeo siyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wagunduzi hapo hapo *COSTECH* ambao wamegundua namna ya kudhibiti upotevu wa fedha kwenye Halmashauri za Wilaya, lakini hawatumiwi kudhibiti upotevu huu na Halmashauri zetu nyingi kuna upotevu wa fedha. Naishauri Serikali iwatumie wagunduzi hawa ambao wana vipaji kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni ya Simu yanakwepa kodi kutokana na huduma za fedha kwa mfano *(Zpesa-Zantel) Tigo pesa*, *M-pesa* ya *Vodacom* na *Airtel-Money*. Waheshimiwa Wabunge tuna mashaka kuwa kodi hazilipwi ipasavyo. Serikali ifanye utafiti ili kukusanya mapato ya kodi kiusahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za simu bado ni kubwa hasa kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake ya bajeti. Wizara hii ndiyo yenye dhamana kubwa ya kuleta mabadiliko ya teknolojia na hivyo kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa heshima kubwa kuishauri Serikali juu ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, usajili wa simu za mkononi uliopo hivi sasa ni ule wa *lines.* Usajili huu hautoshi hata kidogo, kwani hauna usalama kwa mtumiaji wa simu. Nasema hivyo kwa sababu kama simu itapotea au itaibiwa ni rahisi *line* kutumiwa na mhalifu na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa watumiaji simu. Nashauri usajili ufanyike kwa simu *plus line.* Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti matumizi ya simu pale panapotokea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, gharama za upigaji simu ni kubwa sana. Wananchi wengi wa Tanzania wanatumia simu za mikononi, lakini gharama za upigaji ni kubwa jambo ambalo linawanufaisha zaidi Kampuni za Simu. Watanzania wanahitaji maendeleo katika shughuli zao kupitia mawasiliano ya aina yote. Ni vyema Wizara kuwa makini kupunguza gharama za matumizi ya mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uchimbaji wa *Uranium*, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri hususan usalama wa uchimbaji wa madini ya *Uranium*, napendekeza Wizara iwe makini sana, na iwe na usimamizi wa hali ya juu ili kuepusha madhara dhidi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, utafiti ni jambo zito na muhimu sana. Hofu yangu ni kwamba Vyuo vya Utafiti havitapewa uzito unaostahili. Napenda kuishauri Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri kuwa makini sana ili kuhakikisha Vyuo hivi vinafanya kazi na kuona matokeo. Ni vyema Vyuo hivyo vya Utafiti na kule Zanzibar vianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, utekelezaji wa mipango ya maendeleo ni jambo muhimu sana. Mara nyingi Wizara zinakuwa zinapanga mipango mizuri, lakini zinashindwa kutekeleza. Ni muhimu kuweka vipaumbele na kutekeleza ili kuweza kupiga hatua za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba majibu kutokana na ushauri wangu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongeza muda (isiwe Desemba, 2012) ili wananchi waweze kulielewa zoezi la mabadiliko ya teknolojia kwa makini na hasa watu toka vijijini. Napendekeza iwe Desemba, 2013. Tangu sasa Wizara iendelee kutoa elimu kuhusu mabadiliko haya, tena kwa mifano na siyo kinadharia. Elimu hii ipelekwe hasa vijijini na kuelezwa gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta nchini linakwisha kabisa. Sababu hasa ni nini? Sijui hata watumishi wa Shirika hili wanalipwaje mishahara. Shirika hili pamoja na kuwa mahututi, ushauri wangu ni ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Waziri aongee na Postamasta Mkuu nchini

washauriane pa kuanzia. Kama gharama za kulifufua Shirika hili, zitaeleweka, naomba zipangwe kwa awamu mfano, kama zitakuwa Shilingi billioni 20 zigawanywe kati ya miaka 2 - 3 katika bajeti ya Taifa kuanzia mwaka 2013/2014 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa ufafanuzi wa yafuatayo:-

Moja, matumizi ya vifaa vya mawasiliano na hasa simu za mikononi zina madhara kiasi gani katika maendeleo endelevu kwenye Taifa letu hasa kukosekana kwa umakini *(concentration)* zinapotumika wakati wa kazi, kwa mfano:-

(a) Daktari anatibu na hapo hapo anapokea simu;

(b) Kiongozi anaongoza kikao na hapo hapo anapokea simu;

(c) Dereva anaendesha gari na hapo hapo anapokea simu;

(d) Jaji/Hakimu anasikiliza kesi na hapo hapo
anapokea simu;

(e) Mwalimu anafundisha na hapo hapo anapokea
simu; na

(f) Mwalimu anafundisha na hapo hapo mwanafunzi
anapokea simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kujua ulinganifu wa gharama za mawasiliano na hasa simu za mikononi kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa nchi za ulimwengu wa tatu zimekuwa jalala la vifaa vingi vya *electronic* visivyokuwa na ubora stahili (unaokubalika) kimataifa: Je, Wizara inakabiliana kwa kiasi gani na udhibiti wa vifaa hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa kuwa kasi ya kukua kwa Sayansi na Teknolojia ni kubwa sana duniani: Je, tunao uwezo kiasi gani kama Taifa kudhibiti taarifa ambazo zinakiuka maadili yenye kuzingatia mila na utamaduni na desturi ya Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kwa kuwa nchi zinazojiita zimeendelea kwa vigezo wanavyovijua wenyewe, wameanza kuhamasisha wananchi wao kutumia zaidi simu za mezani ili kuokoa muda na pia angalizo la kiafya kwa mionzi ya simu za mikononi. Naomba kujua kama Wizara wana mkakati gani wa

kuhamasisha matumizi ya simu za mezani hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, nashauri wawekezaji kwenye sekta zote za mawasiliano wasiwe na haki ya miliki kwa asilimia 100. Ni vyema Serikali nao wakawa na hisa katika makampuni haya kwa nia ya udhibiti. Mfano Serikali wanaweza wakawa na hisa asilimia 51 na mwekezaji asilimia 49.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, na nampongeza Mheshimiwa Waziri Mbawala na Naibu Waziri Makamba kwa kazi nzuri sana. Naomba mawasiliano ya simu kupitia minara yawekwe Tarafa ya Mgori Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri - Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa; Naibu Waziri - Mheshimiwa January Makamba, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitishwa sana na bajeti finyu inayotengewa Wizara hii kutoka Serikalini. Ninaamini bado Serikali haijajua umuhimu wa Wizara hii katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nasikitishwa sana na ufinyu wa bajeti katika Wizara. Bado upo ucheleweshwaji mkubwa unaofanywa na Serikali wa

kuipelekea fedha Wizara tunapopitisha bajeti. Hii ilithibitika tulipofanya ziara katika Idara za Wizara hii na kukutana na changamoto zao ikiwemo na ucheleweshwaji wa pesa kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta linakabiliwa na changamoto nyingi sana ikiwemo miundombinu ya majengo ya Ofisi zao kuwa hoi sana, maslahi ya wafanyakazi na vitendea kazi ili Shirika liweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi, lakini bado Shirika hili limetengewa fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la anuani za makazi za *symbol* za Posta, pamoja na umuhimu wa mradi huu bado Serikali haijatoa mkakati utakaotumika kuhakikisha kuwa zoezi hili linafanyika kwa haraka na bado hatujajulishwa kuwa zoezi hili litakuwa limemalizika kwa nchi nzima kuwa na anuani za Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ushauri kuhusu mradi huo, kuwa kwa mradi huu ili ufanikiwe ni lazima Shirika la Posta lishirikiane na Halmashauri zetu, na kwa kuwa anuani hizi zitakapokamilika pia zitasaidia Halmashauri zetu kukusanya kodi zao kwa uhakika, basi Halmashauri au Wizara ya TAMISEMI nao watenge pesa ili mradi huu uweze kwenda kwa kasi, kwa sababu pesa iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa jitihada za kupeleka huduma za mwasiliano hadi vijijini. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kutokana na Mfuko wa

Mawasiliano kwa wote *(UCAF)* ni vizuri tukajulishwa kuwa ni mpaka lini maeneo yote yaliyopo vijijini yatakuwa yamefikiwa, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambayo mpaka sasa wananchi bado wanapata mawasiliano ya simu kwa shida sana, wanapanda katika miti na sehemu zenye miinuko ili kupata mawasiliano mazuri hasa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Iringa hasa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko makubwa sana kwa watumiaji wa simu za viganjani kutokana na kuwa na mwingiliano wa kuingiziwa vitu mbalimbali kama matangazo, nyimbo, pia kuibiwa kwa kutumia *promotion,* mfano unaambiwa umeshinda mchezo fulani, unatakiwa utume pesa, kumbe ni matapeli. Je, hakuna chombo kinachodhibiti mambo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayofanwa na Taasisi zake. Tulipofanya ziara katika Taasisi na Vyuo tuliona jinsi jitihada kubwa za tafiti zilizofanywa. Lakini: Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuunganisha jitihada hizo na shughuli mbalimbali za Wizara zetu ikiwa ni pamoja na kurahisisha utendaji wa shughuli za kila siku za Serikali? Mfano, kutumia TEHAMA katika Halmashauri zetu zote kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa kodi zote na kwa kuwa baadhi ya Halmashauri zinatumia pesa nyingi sana kutumia teknolojia hii, ni kwa nini Wizara hii isipewe jukumu hilo ili pesa hizo zirudi katika Serikali badala ya kupewa mashirika ya nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Sayansi na Teknolojia ni muhimu sana na hasa kwa ulimwengu huu ambao tunakwenda nao, lakini imekuwa kama *fashion* sasa ya vyuo vingi/Taasisi nyingi za Sayansi na Teknolojia, yaani kada ya kati (*technicians*) inaweza kupotea na kupungua, kwani vyuo vingi vya kada ya kati vinapandishwa hadhi na kuwa Vyuo Vikuu mfano *MIST* iliyopo Mbeya, *DIT* na Arusha kuna hatari kubwa ya kuwa na *gap*/mwanya mkubwa kwa wanafunzi hawa kwani kada ya kati nayo ina umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe angalizo kuwa, pamoja na kuwa na umuhimu wa kuwa na Vyuo Vikuu pamoja na kupandisha hadhi Taasisi mbalimbali pia ni muhimu Vyuo vya kada ya kati navyo kuangaliwa kwa umakini ili kuondoa *link* ya wanafunzi hawa kutoka ngazi ya chini na kwenda juu. Hivyo basi kada ya kati *(technicians)* nayo ina umuhimu wake. Naiomba Wizara iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kuwa minara ipo katika sehemu mbalimbali hususan vijijini ambapo hakuna umeme na kupelekea kutumia majenereta kwa ajili ya kuendesha/kuwezesha shughuli zake kuendelea vizuri na pia kama inavyotakiwa. Kwani matumizi ya jenereta hupelekea uchafuzi wa mazingira katika maeneo husika na chanzo chake ni moshi wa jenereta. Je, kupitia minara hiyo, Taasisi husika inatoa mchango gani katika mfuko wa Taifa wa kudhibiti mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili minara ya redio pia ina athari kubwa kwa afya za binadamu ambao wapo jirani kabisa na eneo lenye minara hiyo, Je, ni umbali gani unaotakiwa kuwepo kwa minara ya redio kutoka katika makazi ya watu ili kuzuia athari za kiafya kwa waliopo karibu/jirani na minara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahakikisha vipi/kusimamia vipi kuwa minara inakuwa mbali/haiwi jirani na makazi ya watu? Vile vile kuna kodi zinazolingana katika maeneo yenye minara, kwani kumekuwa na utaratibu wa kutoza kodi za minara kulingana na maeneo. Mfano Mkoa fulani eneo fulani hutozwa kiwango kikubwa ukilinganisha na maeneo mengine, wakati minara yote inafanana kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba ni vyema minara yote itozwe kiwango sawa bila kuzingatia maeneo, na kama kuna hoja au sababu za kutotoza *flat rate* katika minara hii, ni zipi? Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matangazo mengi kupitia simu za viganjani ambayo mengi yao hayaelimishi na wala hayana ujumbe wa maana zaidi ya kuburudisha tu. Kutokana na watumiaji wa simu za kiganjani kuwa wengi Mijini na Vijijini na hivyo watu kuwa wengi waliopo vijijini, wanashindwa kupata taarifa za muhimu kupitia simu zao wakati wale wa Mijini hupata taarifa nyingine kupitia kwenye redio na *TV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Wizara kwa makubaliano na watu wa mawasiliano (wa mitandao) waone umuhimu wa kutoa matangazo ya maana na yanayoelimisha.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi yake kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa – Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka. Pili, nampongeza kwa utendaji makini wa majukumu yake na uvumilivu wa hali ya juu alionao. Nampongeza pia Mheshimiwa January Y. Makamba - Naibu Waziri kwa utendaji mzuri na ameonyesha ni jinsi gani yupo makini, maana ni kipindi kifupi tangu uteuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ni kiungo muhimu sana katika maisha, uchumi na maendeleo ya jamii kwa karne hii na zijazo. Pamoja na ahadi zilizotolewa na Wizara hii, naomba kwa kusisitiza sana maeneo tuliyoomba kupatiwa mawasiliano kwa kutumia Mfuko wa *UCAF* yafanyiwe umuhimu wa kipekee kutokana na uhalisia wa kuwa hawana njia mbadala wa kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ni mbovu, lakini pia hakuna matangazo ya redio wala televisheni. Maeneo haya ni Chumo, Kandawale, Mingumbi, Miteja, Nandete, Mitole na Likawage. Wizara itoe ratiba rasmi ya utekelezaji wa ahadi hii ikizingatiwa kwamba ni muda mrefu tumewasilisha maombi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba nzuri ya Waziri imeainisha kuwa sekta ya mawasiliano imesaidia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi, lakini pia kutoa ajira. Naipongeza sana *TCRA* kwa kukubaliana na maombi ya kufunga mtambo maalum ili kubainisha matumizi halisi ya simu na gharama ili kulinda watumiaji na kudhibiti mapato ya Serikali ambapo kwa kipindi kirefu sana kumekuwa na malalamiko kuwa Makampuni ya Simu hayalipi kiwango sahihi cha kodi pamoja na kufanya hila katika mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufuatiliaji mzuri wa viongozi wa Wizara hizi, naishauri Serikali ihimize na kuhakikisha kuwa mkongo wa Taifa unatumika ipasavyo na kulindwa dhidi ya hujuma ambazo zinafanywa kwa makusudi na wachache. Huu ni uwekezaji mkubwa sana. Hivyo naiomba sana Serikali ishirikishe vijiji katika maeneo ambayo mkonga umepita ikiwa ni kuwaelimisha umuhimu, gharama pamoja na ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi wa anuani za *symbol* za makazi, naishauri Serikali kuchukua hatua stahiki na umakini maana ina athari zake kiusalama. Tupate funzo kwa wenzetu ambao

wameanza kutumia mifumo hii, lakini pia kwa kuangalia teknolojia nyingine zilizoingia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu Makampuni ya *TTCL* na Posta yamekuwa hayana mitaji ya kutosha ili kuweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Naishauri Serikali iharakishe mchakato huu wa kuwatafutia mitaji ili kuongeza tija na ufanisi kwa Makampuni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Tume ya Sayansi na Teknolojia itoe elimu ya kutosha kuhusu *GMO (genetical modified organism)* kutokana na hali iliyojitokeza kwa wananchi na hata Waheshimiwa Wabunge kutokuwa na ufahamu wa kutosha kwa teknolojia. Pia Serikali iwaongezee Tume fungu la kutosha ili waongezee ufanisi katika utendaji wao ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za tafiti kwa wepesi na uharaka. Nashukuru kwa kupokelewa maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na watumishi wote kwa jitihada wanazofanya katika Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba inayofanana na Wizara ya *Science* na *Technology*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *uranium* ni chanzo cha uwezo wa Taifa *(nuclear nation*) na ni madini ya kimkakati katika ulinzi wa Taifa letu. Wakati Tume ya nguvu za *Atomic* na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia zinaundwa, madini ya Urani yalikuwa hayajagunduliwa kwa uhakika kama sasa. Kwa umuhimu wa madini haya uchimbaji na uuzaji wa madini, haiwezi kuachiwa Wizara ya Madini peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nashauri Serikali itakapoleta sheria maalum juu ya madini haya, basi Tume hizi mbili zihusishwe na sheria hizi za humu zirejewe ili ziwe na mamlaka ya kudhibiti mauzo na uchimbaji kwa matumizi ya nchi nyingine. Tuweke nguvu katika kujiunga na utafiti na matumizi yatakayofanya nchi hii kuwa *nuclear power*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni ukokotoaji wa mapato ya kikundi kutoka kwa mitandao ya simu. Naomba utafiti ufanyike kuondoa ujanja unaofanywa na Makampuni haya kwa mauzo ya hisa za Kampuni hizi na matumizi. Kampuni zilizo na uhusiano wa kufanya kazi za Kampuni ambazo zingefanywa na Watanzania, aidha kama Kampuni au watu binafsi (*outstanding of services eg. procurement, customer services etc.*), hii ni njia moja ya kupunguza mapato yanayoweza kutozwa kodi. Ikumbukwe kwamba fedha za Makampuni haya zinapatikana kutoka kwa wanyonge milioni takriban 24 na ni vizuri ziada irudi kwao kama kodi badala ya kupelekwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, malipo ya kutumia simu. Jambo hili ni jema sana na mipango ya kuwafikia

wakulima ili mazao yao yalipwe kupitia simu. Ni mkakati mzuri kwa kuwa pia itawaleta wakulima na wafugaji katika mfumo rasmi na uwezekano wa kutumia *banks* kuweka fedha zao kwa usalama zaidi kwa umuhimu wa huduma hii. Sheria inahitajika kudhibiti wizi na utaratibu wa biashara hii pamoja na Bima inayohusiana na *(transactions)* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuitakia kila la kheri Wizara hii muhimu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na ongezeko kubwa la uanzishwaji wa matumizi ya mitambo ya kijamii. Kumeanzishwa mitandao mingi inayolenga malengo ya watu au makundi ya watu wenye malengo yanayofanana katika kubadilishana uzoefu, kutoa ushauri na kutoa taarifa. Ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mitandao ya kijamii imetumika vibaya kwa kutukana na kudhalilisha watu na hasa Viongozi wa nchi. Matukano na udhalilishaji huo mara nyingi unahamasishwa na siasa za kuchafuana zilizoota mizizi sana kwa sasa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itafakari na ianzishe sera na sheria ya kudhibiti hali hii. Uhalifu wa aina hii katika mitandao, katika nchi nyingine

unadhibitiwa. Nasi tunahitaji kudhibiti hali hii, vinginevyo Taifa litapata matatizo makubwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Taasisi ya Sayansi Tanzania *(COSTECH)*ni kusimamia na kutambua tafiti zote zinazofanyika hapa nchini. Lakini kwa hali ilivyo, *COSTECH* haina taarifa stahiki zilizofanyika katika Taifa letu. Wapo watu nchini na nje ya nchi kupitia wao binafsi na wengine kupitia Taasisi zao huweza kufanya utafiti bila *COSTECH* kufahamu. Hii siyo hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kila matokeo ya tafiti za kisayansi, kijamii na hata kiuchumi ni lazima yatambulike kijamii na hata kiuchumi. Ni lazima Taifa liweze kuitumia inapohitajika. Ni vizuri *COSTECH* ikaimarisha udhibiti wa utafiti nchini na kila andiko la Kitaifa na hata kitabu vitambulike na vihifadhiwe *COSTECH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuimarisha mawasiliano ya simu za mikononi vijijini ni suala la muhimu sana. Simu inawasaidia sana wananchi wetu kuwasiliana wakati wa shida na dharura, lakini pia katika biashara zao. Naishauri sana Wizara itekeleze mpango wake wa kuweka minara ya simu kwenye Wilaya zote Tanzania ili kuhakikisha kuwa mawasiliano yanakuwepo nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aelekeze Kampuni ya Simu ya *Airtel* iweke minara kwenye Kata za Itumba, Mwanshika, Igoweko, Mwamashimba, na Bukoko ili kuiunganisha Wilaya ya

Igunga kwenye mawasiliano ya simu za mikononi. Wananchi wanahitaji sana mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa matayarisho na uwasilishaji mzuri wa bajeti ambayo imezingatia hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ulanga Magharibi lenye Tarafa nne na idadi ya wakazi takribani 200,000, lakini ina tatizo kubwa sana la mawasiliano ya simu za mkononi. Jimbo lina minara katika tarafa mbili tu ambazo zinatoa huduma katika Kata karibu nane tu na kuwaacha wakazi wengi kukosa huduma hii muhimu ya mawasiliano pamoja na huduma za kusafirisha fedha kupitia M-pesa,Tigo-pesa na *Airtel money.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya jitihada za ufuatiliaji kwa kupatiwa milingoti hiyo ya Kata zilizobaki hasa Kata za Itete, Fragua na Ngoheranga ambazo kabisa hazina mawasiliano hata ule wa kubahatisha japo kwa kupanda katika miti au milimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati akikamilisha hoja yake, awahakikishie wananchi wa Kata hizo za Itete Fragua na Ngoheranga ni lini watapata huduma za mawasiliano ya simu hususan usafirishaji wa fedha ili nao wanufaike

na huduma za matibabu ya Fistula kupitia *Vodacom* (M-pesa) na hospitali ya *CCBRT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kuwasilisha bajeti iliyotoa ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupitia Wizara hii kwa kazi ya ukamilishaji wa awamu mbili za mkongo wa Taifa. Mafanikio haya yameonyesha namna huduma za mawasiliano zilivyopungua kutokana na mradi huu muhimu kwa mawasiliano ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, naiomba Wizara kukamilisha maombi yangu ya wananchi wa Sikonge kuhusu uwekaji wa mawasiliano ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Kiwere maeneo ya Kilumbi na Kiyombo Kata ya Kipipi eneo la Kata ya Kiloli na Makao Makuu ya Tarafa yaliyopo Kitunda; aidha, kwenye Tarafa ya Sikonge Kijiji cha Ibumba, nimekuwa nikiwaombea kwa muda mrefu kupata huduma hii muhimu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nawasilisha maombi yangu kupitia mchango huu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni mengi ya simu yamekuwa yakitumia mwanya ya kutokaguliwa na Bunge na kuwa na matumizi mabaya ikiwepo na ukiukwaji wa sheria mbalimbali bila sababu ya msingi. Kuna malalamiko makubwa ya ukwepaji kodi kwa Makampuni ya Simu, kutuma *message* ambazo wateja hawazihitaji na baadaye kuwatoza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni ya Simu yamekuwa yakitumia milio ya nyimbo za wasanii pamoja na matangazo mbalimbali, lakini wanakuwa wakiwalipa kidogo. Je, Serikail imejipanga vipi kutetea wasanii hao kuhakikisha wanalipwa vizuri ukizingatia wengi ni vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo mengi kumekuwa na tatizo la mitandao kwa baadhi ya Makampuni ya Simu. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wananchi wengi wa vjijini wanapata mawasiliano?

**MHE. ISMAIL A. RAGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa maana hiyo sichelewi kutamka wazi kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Tabora ina Kata 25, kati ya hizo, 11 ziko Mjini na Kata 14 ziko Vijijini. Kwa maana hiyo tunaomba msaada wa Mheshimiwa Waziri na Ofisi yake ikielewa hivyo, naomba Kata za vijijini nao wasaidiwe kupata mawasiliano. Nina imani

na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, suala hili litashughulikiwa.

Mheshimiwa mwenyekit, napenda Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba na mimi nina *radio* inayoitwa *V.O.T. FM (Voice of Tabora)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa na Serikali tutapata misaada midogo kutokana na mchango wetu katika kudumisha mawasiliano ya *radio.* Ningependa kuelewa ni lini redio hizi za Mikoani zitapatiwa hiyo misaada? Mkoa wa Tabora umesahaulika katika kutoa elimu ya kuelimisha wananchi juu ya mabadiliko ya teknolojia ya matangazo ya televisheni kutoka analojia kwenda dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni muhimu Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri wakaweka utaratibu wa kutembelea Mkoa wa Tabora ili nasi tupate kuwaeleza matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha. Pia nampongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri bila kuwasahau Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia zaidi mawasiliano vijijini. Kwanza kabisa, nachukua fursa hii

kuyapongeza Makampuni yote ya Simu *(vodacom, airtel* na *tigo).* Makampuni haya yamefanya kazi nzuri sana kuleta mawasiliano mpaka vijijini ambapo siku za nyuma ilikuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna baadhi ya vijiji bado vina tatizo la mawasiliano. Katika Wilaya ya Geita na Jimbo la Busanda zipo Kata ambazo mawasiliano ni taabu sana. Hata katika mpango wa bajeti mwaka 2011 niliorodhesha ili viweze kuhudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizi zimekuwa na changamoto kubwa sana za mawasiliano kwa muda mrefu. Kata hizo ni Nyamalimbe, Bujula, Kamena, Nyamigota, Kaseme na Nyachiluluma. Nilipokuwa napitia kitabu cha hotuba ya leo inaonyesha kuwa fedha tulizopitisha Bungeni kwa ajili ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCAF)* 2011/2012 ilikuwa Sh. 419,068,000/= na zilizotolewa ni Sh. 150,000,000/= tu. Kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwamba, kiasi tunachopitisha mwaka huu kwa ajili ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCAF)* Serikali iweke kipaumbele katika kuhakikisha fedha hizi zinapatikana kwa wakati na fedha hizi zipelekwe katika mfuko wa *UCAF* ili kuboresha mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni wizi wa kimtandao. Kumekuwa na matukio ya wananchi kuibiwa fedha zao kwa njia ya kimtandao, hasa

wananchi walio na akaunti *NMB.* Suala hili limewakumba hasa Walimu wastaafu kuibiwa fedha zao kwa njia ya mtandao. Kesi ni nyingi sana katika Vituo vya Polisi katika Wilaya ya Geita. Kilio hiki kipo, lengo la teknolojia ni kurahisisha huduma, lakini katika hili imekuwa ni kinyume na ni changamoto kubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kupitia vyombo vyake ifanye utafiti katika jambo hili ili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina la ziada, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. ABDULLA J. A. SAADALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkongo wa *Cyber crimes* kutokana na ukuaji wa taalum ya kikompyuta, kuna uwezekano mkubwa wa watu wasio wema kutumia nafasi hizi kwa ku-*sabotage*, kutumia vibaya taaluma hiyo katika wizi na ku-*penetrate* siri zetu hasa katika *e-Governance, Cyber crimes* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitengo maalum cha kiintelejensia kwa kushirikiana na vitengo vingine ya kisekta, ili kuifanya nchi yetu iwe salama. Lakini pia utumiaji wa taaluma hiyo hiyo kwa madhumuni ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumiaji wa mionzi nchini unaongezeka pamoja na kuwa sera ya matumizi ya mionzi bado haijaletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, matayarisho ya wataalamu wa uchimbaji, usafirishaji, taaluma ya sheria za kimionzi wawekezwe haraka sana, tuwe na tahadhari ya matumizi mabaya kama *smuggling* ya urani, lakini pia tukae mbali sana na hata kukemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wadogo hujihusisha na uchimbaji wa Urani kama sera ya madini inavyoruhusu (kinyume) na taaluma za *safety procedures.* Vile vile naomba uwezo wa vitengo vyetu vya uokozi viwe *equiped* kitaalum na kiuwezo wa vifaa pamoja na kuwaelewesha wananchi. Kwa mfano, tetemeko la ardhi kwa wananchi wa Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natahadharisha uwepo wa *Brief case bombs* na kuingia kwa magaidi Tanzania na ukanda wa *EAC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu simu mtambo wa ufuatiliaji mienendo ya simu nchini, mtambo huu usaidie ukusanyaji wa kodi na usalama wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri uwiano wa ongezeko la kodi za simu mpaka 12% kulingana na *harmonization* za *EAC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la kodi hii walipe wenye Makampuni ya Simu, kwa njia yoyote ile ya kitaaluma za kikodi. Lengo ni kupunguza mzigo kwa wananchi. Inajulikana *tarrifs* zao, hutoa misaada na kutengeneza wigo wao kwa kazi kubwa. Hivyo, nahisi mzigo huo uchukuliwe na Mashirika ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kuanzishwa kwa Ofisi ya *TAEC* Zanzibar. Naomba iwezeshwe kiufundi. Napongeza kufunguliwa kwa Ofisi ya Tume ya Mawasiliano Zanzibar. Naomba kuwepo kwa *Telemedicine* tuunganishwe Zanzibar na ulimwenguni kuhusiana na elimu ya *X-rays + Diagnosis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha katika Bunge lako Tukufu katika hali ya uzima. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Prof. Mbarawa kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika Wizara hii upande wa teknolojia. Bado nchi yetu hatujajipanga vizuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na usumbufu mkubwa katika matumizi ya vyombo ambavyo vinatumia dijitali, kwani ni Watanzania wachache wanaopenda kusoma masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali ifanye juhudi kuwasomesha vijana masomo ya sayansi ili Taifa letu liweze kupata wataalam wa mitandao ya dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi haiwezi kuendelea kama itakosa wataalamu, na nchi yetu imekosa wataalam hali inayopelekea rasilimali yetu hatuipati

vizuri, kwani katika sekta zote za madini, gesi na kadhalika mara nyingi tunatumia wataalam wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara ijikite katika kuwapa elimu Watanzania ili waweze kutumia (teknolojia) vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na sintofahamu nyingi kwa kiasi cha pesa zinazolipwa na wamiliki wa mitandao ya simu kuhusu nguzo zinazowekwa kwenye maeneo ya watu na maeneo ya wazi yanayomilikiwa na Halmashauri, hata Baraza la Madiwani wengi hawaambiwi. Kimsingi Halmashauri inalipwa na Wizara au Kampuni ya Simu moja kwa moja, na ni Shilingi ngapi kwa mnara kwa Halmashauri, pia kwa mtu binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ujumbe *(SMS)* nyingi zinazoingia kwenye simu za mikononi toka kwenye mitandao ya simu za mikononi bila ridhaa ya mwenye simu. Hizi *sms* za kibiashara zimekuwa kero sana kwa watumiaji wa simu. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie kama hizi simu zimedhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* juzi walirusha kipindi maalum cha ugunduzi wa *technology* ya kugundua wizi wa simu, ambayo itabaini pale ambapo mtu kaiba simu au *computer* yako, itaonesha kuwa hiyo simu inatumika na nani na wapi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu utuambie hii *technology*

itatumika lini kwenye simu za wananchi na *computer* zao ili kumaliza kabisa wizi wa simu?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizarani kwa utendaji mzuri. Katika mchango wangu ningependa kuzungumzia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu matumizi mabaya ya *blogs* mitandao ya kijamii. Natumaini Wizara na wataalam wanafahamu jinsi viongozi na baadhi ya wananchi wanavyodhalilishwa katika mitandao hii, hakuna njia ya kudhibiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajilii wa simu haujasaidia kupunguza matumizi mabaya hasa kwa kutumia ujumbe mfupi. *Line* za simu zinauzwa kiholela na bila udhibiti. Kwanini hatua hazichukuliwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usikivu mdogo wa *Radio, Television* na udhaifu katika upatikanaji wa *e-mail* na simu za mkononi katika Jimbo la Rombo. Hali hii inawafanya wananchi wa Rombo kupata habari za nchi jirani zaidi kuliko za hapa nyumbani. Je, Mkonga wa mawasiliano wa Taifa unawanufaisha vipi wananchi wa Rombo ili kuwezesha kutatua matatizo haya?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa inayofanya ya kuwahudumia Watanzania.

Ningependa kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iweke utaratibu mzuri wa kusimamia ukusanyaji wa kodi kutoka Makampuni ya Simu. Kama kuna mtambo maalum wa kurekodi *transactions* zote zinazopita katika mitandao ya simu, naomba ufungwe haraka ili kuweza kukusanya kodi sahihi kutoka katika Makampuni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iharakishe uwekaji wa minara ya mawasiliano ndani ya Wilaya ya Kisarawe katika Vijiji vya Gwata, Ving'andi, Nyani, Vikumburu, Kihere, Titu, Kimale Misale na Kibwemwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isimamie vyema uingizaji wa ving'amuzi ili kupata ving'amuzi vilivyo na ubora unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isimamie vyema uingizaji wa vifaa chakavu vya *kielectroniki* ili kuzuia madhara kwa wananchi yanayotokana na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula lina Kata 10, ukubwa wa Jimbo ni sawa na Mkoa wa Kilimanjaro.

Kata zifuatazo hazina mawasiliano Loya, Miyenze, Lutende, Kigwana na Nsololo. Nashukuru *Airtel* na *Vodacom* wametoa huduma ya mawasiliano Goweko, Igalula, Tura na Kizengi kwa baadhi ya Vijiji. Naomba Wizara itusaidie tupate mawasiliano kwa kujenga mnara kwenye Kata hizo tano zisizo na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganifu wa mapato ya Serikali kama kodi kutoka Makampuni ya Simu za Mikononi mwaka wa fedha 2010/2011 katika nchi za Afrika Mashariki walionesha tofauti kubwa kati ya Tanzania na nchi za jirani pamoja na wateja wengi kuwa Tanzania. Kenya bilioni 107, Uganda bilioni 78, Rwanda bilioni 44, Burundi bilioni 11 na Tanzania bilioni 2.7. Je, Wizara inaweka lini mtambo, *traffic monitoring system* wa kufuatilia mapato ya Makampuni haya na kuongeza pato la kodi Serikalini? Jitihada zifanyike kupata mapato ya nyuma *(restrospective corporate tax)* kwa Makampuni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni mbalimbali za kibiashara Kimataifa huwa zinatumia *(outsource)* wafanyakazi kwa ajili ya kuchambua takwimu mbalimmbali za kibiashara kwa kutumia kompyuta. Makampuni haya ya *IT* yapo *Silicon Valley, San Jose California* Marekani na kwingineko. Je, kwa kuwa na mkongo wa Taifa, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaweza kushirikiana na Wizara ya kazi na ajira ili vijana wenye taaluma ya *IT* waweze kuajiriwa na kufanya kazi wakiwa Tanzania kwenye Wilaya zao? Hili linafanyika Jamaica ikiwa *outsourced* na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukajifunze huko, haya ni maendeleo makubwa kwenye *TEHAMA*.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Wizara kwa kujenga mnara katika Kata ya Luale na kuweka katika mpango ujengaji minara Kata ya Kanga, Kijiji cha Matale na Maskati ili kupeleka mawasiliano Kata ya Kinda na Kijii cha Ndole na Semwali. Ombi langu ni kwamba mpango huo upewe kipaumbele katika awamu ya kwanza. Aidha, utekelezaji wa ujenzi wa mnara Kijiji cha Digalama ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali kufikisha mawasiliano Jimbo la Mvomero, naomba chonde chonde Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hotuba, anisaidie Pemba wapate mawasiliano ya simu. Wananchi wa Kata ya Pemba wako Kisiwani, hawana mawasiliano kabisa, wanapata taabu sana. Naomba sana wapatiwe mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani mazungumzo yangu na Waziri na Naibu wake yatapata kipaumbele kwa kutusaidia Wana-Mvomero kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie jinsi ya kusaidia wananchi kudhibiti gharama za muda wa maongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kupokea na kutuma fedha katika Jiji la Dar es Salaam na hasa

katika Jimbo la Temeke ni nyingi mno. Lakini inapotokea tatizo au makosa ya kibinaadamu, mteja anatakiwa kwenda Makao Makuu ya Makampuni hayo ambayo ni *Mlimani City* kwa *Vodacom* na katikati ya Mji kwa *Tigo* na *Osterbay* kwa *Airtel.* Huu ni usumbufu kwa wakazi wa Temeke. Ushauri wangu ni kwamba wafungue Ofisi kila Wilaya kuwasaidia wananchi kutokupoteza muda mwingi kufuata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara na wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii bila kusahau sekta binafsi ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe malalamiko kutoka Kata za Gisambalang, Sirop, Simbay, Masagaroda na Gehendu kwa kukosa mtandao. Kampuni ya *Airtel* ambayo ndiyo yenye mtandao katika eneo kubwa katika Wilaya imetoa ahadi, lakini sasa ni muda mrefu umepita. Naomba watekeleze ahadi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Kampuni za Simu nyingine ziweke mtandao wao ili wananchi wa Hanang waweze kunufaika na maendeleo ya mawasiliano. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko ni lini Kata zangu zitaboreshewa mawasiliano kwa kuwekewa minara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza Taasisi za utafiti. Ningependa ziongeze bidii ili utekelezaji usiwe wa kukisia, bali wa uhakika. Ahsante.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufaidika kikamilifu na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, ni lazima tuwaheshimu na kuwathamini wataalam wetu wa ndani. Kama ambavyo siku zote nimekuwa nikisisitiza, hii kasumba ya kujidharau sisi wenyewe haitatusaidia kamwe. Ni lazima kama Taifa tufungue macho na kuwatumia hawa wataalam wetu wa ndani, mfano wahandisi wanaomaliza katika Vyuo mbalimbali nchini. Tumewahi pia kusikia kwenye vyombo vya habari baadhi ya wagunduzi wa vitu mbalimbali, mfano, lami ya barabara itokanayo na mmea wa manipa – Elias M.Msengi. Rasello.com *(search engine)* - Natalia Mwenda, gari litumialo injini ya pikipiki - Castor Felix na wengine wengi. Tunashindwa nini kuwathamini hawa watu ili wapate moyo wa kugundua zaidi ili hatime tupate ajira na kuibuka kwa wataalam wengi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Teknolojia na Maendeleo ya Sayansi ina athari mbaya ukiondoa yale mazuri. Naomba niendelee kuisisitiza Wizara na Serikali kwa ujumla ifanye kila liwezalo kuzuia athari hizi mbaya za Sayansi na Teknolojia. Baadhi ya athari hizi mbaya ni matumizi mabaya ya mitandao hasa kudhalilishana *(internet, facebook* na kadhalika*),* athari ya minara ya simu kwenye mazingira na kadhalika. Siyo vizuri kupuuza hata kidogo athari hizi hata kama ni ndogo kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mitandao ya simu (Kampuni za Simu) limeleta neema kubwa kwa Watanzania, mfano huduma za pesa, ajira na kadhalika. Napenda kuzipongeza kampuni hizi, lakini pia nitoe rai kwa kampuni hizi ziepuke kupandisha gharama za simu ili kuwafanya watumiaji wengi hasa wenye uwezo wa kati na mdogo kumudu zaidi. Ni vyema kampuni hizi zifahamu kuwa gharama za simu zikiwa juu, hata wateja watapungua na faida itakuwa kubwa zaidi. Baadhi ya gharama zinazopaswa kupunguzwa ni kama vile upigaji wa simu huduma za *M-PESA, EZT-PESA,AIRTEL MONEY* na *TIGO PESA* na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha Vijijini nalo linahitaji kukumbukwa katika ramani ya sayansi na teknolojia kama nilivyochangia mwaka 2011, bado maeneo kadhaa katika Jimbo langu halipati huduma za simu na redio ya Taifa (*TBC* Taifa). Maeneo haya ni Kata za Ruvu, Kijiji cha Kitomondo, Janga, Kijiji cha Makazi Mapya hazipati huduma za simu. Kuna umuhimu wa kuweka minara ya simu ili maeneo haya nayo yapate kuunganishwa na dunia. Kata ya Soga, Vijiji vya Dutuni na Magindu vinakosa huduma ya *Radio* ya *TBC* Taifa. Hii ni aibu kwa Jimbo ambalo liko karibu kabisa na Jiji kubwa la Dar es Salaam kukosa huduma hizi.

**MHE. ANNA MARYSTELA J. MALLACK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye asili ya mema yote. Pia nichukue nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwa maandishi.Nianze kwa

kuongelea utayari wa Watanzania kuelewa na kupokea teknolojia ya *digital* na kuachana na mfumo wa *analogue* hasa kwa upande wa *Television*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)* kutoa elimu kwa Watanzania, kwani kuna baadhi ya Watanzania waishio Vijijini wameacha kabisa kununua *television* (luninga) wakiamini kuwa zimeacha kutumika na kwamba zinakuja za aina ya *digital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atueleze ni lini sasa elimu hii itatolewa ili Watanzania waepukane na dhana hii potofu? Muhimu katika maisha yetu ni mawasiliano, lakini mawasiliano yamekuwa ni tatizo katika Tanzania yetu hasa pale mitandao inaposambaa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ni *coverage* ya *networks,* kwani kuna maeneo mengi hasa Vijijini wananchi wanaishi bila mawasiliano. Naiomba Wizara kuwasiliana na Makampuni ya Simu nchini ili kuhakikisha wanapeleka mawasiliano Vijijni ili kuwawezesha na wakulima nchini na wafanyabiashara wapate mawasiliano. Naomba Mheshimiwa Waziri aniridhishe atakapokuwa akifanya majumuisho. Je, kwa kuwa zipo sehemu nyingi hasa Vijijini hakuna mawasiliano kabisa na wananchi wanashindwa kupata au kufikiwa na habari nyingi hasa kwa wananchi wasio na redio, watapataje habari kuhusu ya mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka *analogue* kwenda *digital*? Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu Waziri, na Mwanangu wa kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote waliyoshiriki kuandaa bajeti hii mahiri yenye lengo la kuboresha sekta zake zote kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtia moyo na kumtoa wasiwasi, kwani amepata Naibu Waziri mahiri, makini na mwenye uwezo wa juu. Hivyo amtumie atamsaidia sana. Mimi nimejifunza mengi sana kwa kipindi ambacho alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, nami nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Ninawaombea Mungu wote awape afya, nguvu, mahusiano mazuri ili muweze kutekeleza malengo yenu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuweka mpango mzuri na wenye Makampuni ya Simu kwani yanashirikiana na wafanyabiashara kutoa matangazo mbalimbali ya biashara kisha wenye simu kukatwa fedha nyingi bila makubaliano. Hii ni kuwaibia wananchi wenye simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwa niaba ya wapiga kura wangu ambao wengi wao wanazo simu za mikononi kuwa gharama za matumizi ya simu ni kubwa sana kulingana na uwezo au vipato vya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa kilio cha watumishi wa Shirika la Posta kuwa mishahara wanayopata ni duni sana hata stahili nyingine nyingi mfano posho za safari na kadhalika, hawapati kwa wakati. Ili kuwapa moyo watumishi hawa, ni vyema maslahi yao yakaangaliwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kuyahimiza Makampuni ya Simu kufikisha mawasiliano vijijini Mkoani Singida. Napenda kuiomba Serikali ikumbuke kupeleka mtandao maeneo ambayo bado hayana mawasiliano. Kwa mfano, Manyoni Tarafa ya Nkonko, Wilaya ya Iramba, maeneo ya Vijiji vya Iramba Mashariki yaani Tarafa ya Nduguti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumaliza kwa kuunga mkono hoja na kuwatakia utekelezaji wenye tija.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kuleta masikitiko yangu kwamba bajeti ni ndogo sana katika Wizara hii muhimu kuweza kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kuwa mtandao unakua kwa kuwa umeshapatikana mkongo. Lakini mimi niseme, bado kuna matatizo makubwa, kwani leo siku ya nne wananchi huko Dar es Salaam, wanakwenda Ofisi ya *TRA* ili kulipia mizigo yao, wanaambiwa *system* iko *down* na huwa wanapewa tarehe nyingine. Lakini wakienda ndiyo hivyo hivyo. Hii

inawapa usumbufu sana wananchi na wengine kuthubutu kusema afadhali zamani ilikuwa hatupati usumbufu kuliko mfumo huu wa kuwa na *system.* Naishauri Serikali ilione hili na ilipatie ufumbuzi, kwani huu ni usumbufu, na wananchi wataamua kutumia Bandari ya Mombasa na hii itaweza kutukosesha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwa na dhamira nzuri ya wanafunzi kutumia mtandao ili waweze kuendana na wakati, lakini badala ya kutumia hizi *Computer* kwa ajili ya masomo yao, wameanza kufanya maajabu yanayokiuka maadili ya Tanzania, kwa kuwa mtu anapotaka kujiunga kwenye *internate* anatakiwa aandike miaka yake, basi naomba kuwe na utaratibu, hizo sehemu ambazo ni za matusi watoto wasofikia umri wa miaka 21 wasiweze kufungua hizo sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko yangu kwa Shirika la Posta na Simu Tanzania, Shirika hili ndiyo lilianza mwanzo kufanya kazi humu Tanzania. Lakini Shirika la Posta hivi sasa ndiyo limekuwa la mwisho katika huduma za simu. Naiomba Serikali ipange mipango mizuri ili Shirika hili liweze kurudi katika hadhi yake ya zamani.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii kama inavyojionyesha ya Wizara kutokupelekewa fedha za kutosheleza kama zilivyoidhinishwa na Bunge, inatoa maswali mengi kuliko majibu. Je, mfumo umewashinda? Je, makusanyo hayafanyiki? Je, ni urasimu wa Hazina? Je, kuna ufujaji

na ubadhirifu wa fedha Hazina? Au kuna matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge yaliyopewa umuhimu mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo ziliidhinishwa tarkribani Shilingi bilioni 40,218, na hadi Mei zimepokelewa jumla Shilingi bilion 13,712. Inasikitisha, lakini kwa takwimu hizi tunajifunza nini? Kama nchi, tujitahidi kujitegemea badala ya kupanga mipango yetu kutegemea hisani na ufadhili wa wajomba zetu wa Marekani na Ulaya. Mwaka 2011/2012 fedha za maendeleo toka nje ni zaidi ya Shilingi bilioni mbili, tumeruzukiwa na wahisani wetu Shilingi milioni 668 tu hadi Mei 2012. Ni aibu kwa Taifa tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuendelee na kasi ya mabadiliko duniani, utafiti ni eneo muhimu sana, lakini hatuwezi kukamilisha tafiti zetu kama fedha hazitatolewa kama inavyoidhinishwa na Bunge. Mwaka 2011/2012 jumla ya zaidi ya Shilingi bilioni 25 hadi Mei, Serikali imepeleka Shilingi takribani bilioni 10 na kazi zilizopangwa kwa mwaka zilihitaji Shilingi bilioni 19. Hivyo fedha zilizobaki zinazosubiri kulipwa ni Shilingi bilioni nane. Hivi sasa nitapenda kujua fedha hii inayodaiwa, Serikali itatoa lini au kama deni hili limezingatiwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Taasisi ya Utafiti ni lazima iwezeshwe kikamilifu ili kupiga hatua katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia. Hivyo basi, naiomba Serikali kuiwezesha Wizara hii na Taasisi zake kupewa fedha na

vitendea kazi kwa wakati na tuondokane na bajeti tarakimu, tuwe na bajeti zinazotekelezeka.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknologia kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namkumbusha Mheshimiwa Waziri, ahadi yake ya kuweka minara ya simu katika tarafa ya Kilimarondo, hususan Vijiji vya Mbundo, Kilimarondo, Matekwe na Kiegei. Suala la mtandao katika Tarafa hizi ni la kisiasa na sasa hivi Chama cha Mapinduzi na Serikali yake zina tatizo kubwa katika Tarafa hizi pamoja na mambo yote mazuri yanayofanywa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naishauri Wizara ianze kufikiria na kutoa majawabu kuhusu *safe disposal* ya *computer* na simu mbovu na vifaa vyake. Kwa sasa vitu hivi havina mahali maalum ambapo vinapelekwa vinatupwa katika madampo ya kawaida ya Mijini na Vijijini. Vifaa hivi vina athari zake. Ni vyema sasa Wizara ikaleta utaratibu wa kuviharibu vifaa hivi kwa usalama wa Raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia kuunga mkono hoja na kuitakia Wizara utekelezaji mzuri wa mipango yake ukiwemo ule wa ku-*monitor* simu na *sms* na *data transfer* kupitia Makampuni ya Simu. Najua mchakato umeanza, lakini sasa ukamilishwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuipongeza Serikali kwa jitihada yake ya kupeleka huduma za mawasiliano hadi vijiini hasa mfuko wa mawasiliano *(UCAF),* ni mategemeo ya wananchi wa Jimbo la Mbulu ambao katika sehemu za Mama Isara, Maretadu, Tumati wakitaka kupiga simu mpaka kupanda miti, sasa watapata mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mabadiliko ya mfumo wa utangazaji kutoka *analogue* kwenda *digital* unatekelezwa sawa na upatikanaji wa *TV sets* zinazohusika. Aidha, iwapo *video conference* itaanza, itaokoa fedha nyingi ya Maafisa kusafiri, kwani watabaki kwenye vituo vyao wakiwa wakishiriki Mikutano ya mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenye leseni za *M-Pesa* wadhibitiwe ama wanatoza watu wanaotuma fedha tozo za uongo au wanachelewesha kutuma fedha kwa sababu wanatumia fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iongeze bidii ya kutunza haki ya watumiaji wa simu za mkononi wanaotumiwa *sms* za upuuzi, *airtime* inakwisha bila kutumiwa. Watu wabaya wanaotumia simu wachukuliwe hatua za kufungiwa simu na kushitakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ujenzi wa Mkongo wa Taifa *(National ICT Broadbank Backbone Infrastructure)* ukamilishwe.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu leo. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbarawa pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Makamba kwa kufanya kazi zao kwa umakini zaidi, lakini tunawaomba waongeze bidii katika mawasiliano ambayo ni muhimu kwa Watanzania na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa dhati na kwa undani wa moyo wangu kwa kuona vijana wanasayansi na wavumbuzi wa nchi hii wasiothaminiwa. Mheshimiwa Waziri, kama kichwa cha wanasanyansi hawa pamoja na uvumbuzi wao, ni namna gani unapokaa kwenye Baraza la Mawaziri unawaongelea ili kuweza kuwaboresha na kuwatumia hapa nchini bila kuleta wataalamu kama hawa kutoka nje ya nchi? Mfano, *Dar es salaam TEKNOHAMA Business (ICT) incubator*.

Ni vizuri sasa kuwaambia Mawaziri wengine kama Waziri wa TAMISEMI ili Halmashauri zote nchini ziweze kutumia vijana hawa kwa kufungia mfumo uitwao *MRECOM* ili Halmashauri ziweze kukusanya kodi na kuongeza kipato. *DTBI* wamefunga mitambo yao katika Halmashauri ya Temeke na Halmashauri hiyo kuongeza mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DTBI* mpaka sasa imeweza kuwasaidia Uhamiaji, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mahakama Kuu na Koti ya Rufaa, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora sasa tukawa makini na ubunifu wetu na kuwatumia vijana wetu ili kuongeza ajira kwao. Pia kuna mambo mengi ambayo kama Wizara ni bora kutumia nguvu zenu zote kujitangaza. Mfano, *DIT* kuna ubunifu ambao gari yaweza kutumia gesi kwa kuendeshea. Huu ni ubunifu mzuri, lakini hawajajitangaza vya kutosha. Mfumo wa uhesabuji kura bila kuchakachua kura hizo kiutaalamu, haya yote ni matunda ya teknolojia. Hivyo ni bora sasa vijana hawa wakapata uwezesho na kutangazwa na mwisho watumike hapa nchini bila kujali mtaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekua kero kubwa kwa Makampuni ya Simu kwa kila mara kutuma ujumbe bila ukomo wa matangazo ya biashara kwa njia ya *message.* Ni vizuri mkawafahamisha matangazo ya biashara wapeleke kwenye vyombo vya habari na siyo simu za watu za viganjani. Huu ni usumbufu mkubwa na umalizaji wa chaji za watu kwenye simu ambapo wengi wao huchaji simu hizo kwenye vibanda vya kulipia huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba matangazo watangaze kwenye vyombo vya habari na siyo usumbufu uliopo sasa. Hii ni muhimu.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Kwanza kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri sana. Natoa masikitiko yangu makubwa kuhusu kukosekana kwa mitandao katika

eneo langu la Mkoa wa Geita katika Wilaya Mpya ya Nyang'wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Nyang'wale katika Kijiji cha Kakora, Nyarubele, Kabiga Nyijundu, hali ni mbaya sana wananchi hawa wakitaka kupiga simu inawabidi wapande kwenye miti ya miembe au wapande mlimani ndipo wapate mawasiliano. Hii ni hatari kubwa. Kuna baadhi ya wananchi wameng'atwa na nyoka huko porini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri asikie kilio changu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara kwa hotuba yao nzuri iliyowasilishwa kwa umahiri mkubwa. Mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo kadha wa kadha ambayo bado ni changamoto katika Wizara hii. Jambo la kwanza linahusu upungufu wa fedha ambayo Serikali huitenga kwa ajili ya Wizara kwa kuzingatia umuhimu wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya nchi. Fedha inayotengwa hailingani na mahitaji. La kusikitisha zaidi ni kuwa, hata fedha iliyotengwa haitolewi yote kwa Wizara. Je, kwa mtaji huu, tutafika lini huko tunakotaka kwenda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo ni muhimu sana ambayo haishughulikiwi kwa

kasi inayotakiwa ni utekelezaji wa mradi wa anuani za makazi na *symbol* za Posta. Ingawa *TCRA* (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasilinao Tanzania) imesema utaratibu wa awali wa anwani za makazi na *symbol* za Posta uko tayari, lakini tatizo ni kwamba Serikali hadi sasa haina mpango/mkakati wowote wa kutekeleza mradi huu muhimu sana kwa Taifa. Tunapenda Mheshimiwa Waziri atuambie, kuna mpango wowote wa uhakika unaoandaliwa ili kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye changamoto kubwa kabisa ya uhawilishaji wa sayansi na teknolojia kutoka kwenye Vituo na Vyuo kwenda kwenye jamii pana ili teknolojia hiyo itumike kukuza uchumi. Ili nchi iendelee, lazima teknolojia hiyo ihawilishwe na isambae kimatumizi. Pamoja na juhudi zilizopo za kuhawilisha teknolojia zinazofanywa na Taasisi na Vyuo Vikuu vilivyopo, bado kasi ni ndogo sana. Kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili katika nchi nyingi, Serikali kushirikiana moja kwa moja katika shughuli ya uhawilishaji badala ya kutegemea viwanda vya watu binafsi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isiandae mazingira ili Taasisi na Vyuo Vikuu vinavyohusika na teknolojia vianzishe Kampuni ya Teknolojia ya pamoja, itakayoendeshwa kwa ubia na sekta binafsi? Kampuni hii kazi yake iwe kuratibu magunduzi yote na teknolojia nyingine ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa na kuyazalisha pamoja na kuyasambaza katika maeneo ambayo yanahitaji teknolojia husika. Wazo la kutumia mbinu ya Kongano (*Chester)* kama njia ya kuhawilisha teknolojia ni zuri na linafaa kuendelezwa.

Mbinu hii itengewe fedha ya kutosha kila mwaka ili kongano zienezwe sehemu nyingi nchini ili kuwasaidia wananchi kupunguza umasikini. Wananchi wa Jimbo la Bukombe wangependa Wizara iwapelekee kongano ya asali itakayowasaidia kuongeza maarifa na kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni *sms spoofing.* Kwa mujibu wa taarifa za hivi karibuni, kuna mtambo ambao unaweza kutumika kutuma ujumbe kutoka simu ya mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine. Habari zinasema kuwa mtambo huu tayari uko hapa na unamilikiwa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Je, taarifa hizi ni sahihi? Kama ni sahihi mtambo umenunuliwa kwa lengo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nitakaloongelea ni Bunge mtandao *(e-parliament).* Hivi sasa Serikali iko mbioni kuanzisha Serikali, mtandao tiba, mtandao na kadhalika. Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha Wabunge waachane na utumizi wa makaratasi na badala yake waanze kutumia mtandao kupata taarifa zote zinazohitajika kwa shughuli za Bunge? Serikali inapaswa kulitafakari jambo hili na kulipangia utaratibu wa utekelezaji.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rejea barua ya wapiga kura toka Kata ya Muhukuru waliojichangisha Sh. 400,000/= na kusafiri mpaka Dar es Salaam kuomba mnara wa simu eneo la Muhukuru mpakani mwa

Tanzania na Msumbiji ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kulinda mipaka kwa muda mrefu sana. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini? Ni kero kubwa sana, na inapelekea wananchi kukosa imani na Serikali yao kupitia ahadi ya Mheshimiwa Rais. Vile vile Vijiji vya Ifinga, Ndongosi, vyote mpakani, lini vitapata mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam kwa kuandaa hotuba nzuri na mpango wa bajeti wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ijipange ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili ibuni mbinu za kutumia teknolojia kupunguza uhaba wa waalimu, vitabu na vifaa vya kufundishia. Mtandao uandaliwe ili mwalimu mmoja afundishe maeneo mengi na *materials* za kufundishia ziwe zinapatikana ki-*electronic.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maeneo yasiyo na minara ya simu za mkononi yapatiwe mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Makami, Kiteto lipatiwe mnara. Hii ni Tarafa nzima isiyo na mawasiliano na viongozi wa Kitaifa. Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Msekwa - Makamu Mwenyekiti wa

Chama cha Mapinduzi Taifa na Katibu Mkuu Chama cha Mapinduzi wametoa ahadi ya Makami kuwekwa mnara tangu mwaka 2008. Tafadhali ahadi hizi sasa zitimizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iandae mkakati wa Serikali kupata mapato yake halali kutoka kwenye Kampuni za Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria na Kanuni zilizopo zisimamiwe vizuri ili kumlinda mlaji. Hivi sasa Kampuni za Simu zinawashurutisha walaji kulipia bidhaa wasizohitaji kama vile muziki na *sms* ambazo ni usumbufu kwa mlaji.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kuchukua nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa January Makamba kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii muhimu. Binafsi ninaomba kuwashukuru watendaji wa Wizara hii kwa kuwa wanajitahidi sana kusambaza mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu, ninapenda kuishauri Wizara kuangalia kwa makini na upendeleo wa pekee Mikoa iliyoko pembezoni na hasa vijiji vilivyoko mipakani kama vile Kigoma.

Ninaomba niorodheshe tena vijiji ambavyo havina minara ya simu katika Jimbo langu la Kasulu vijijini, kama ifuatavyo:-

(i) Kijiji cha Kitanga ambacho kiko mpakani mwa Tanzania na Burundi;

(ii) Heruushingo;

(iii) Kagerankanda;

(iv) Kurugongo;

(v) Titye na Latambe; na

(vi) Kabhulanzwiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nieleze kwamba tunakosa nafasi ya kupata wahudumu wa sekta mbalimbali kama vile elimu na afya kwa sababu ya kukosa mawasiliano ya simu huko vijijini.

**MHE. HAROUB MUHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa neema na rehema zake nyingi anazonineemesha, sina budi kusema *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano, sayansi na teknolojia ni sekta muhimu sana kwa ustawi wa jamii yoyote hapa ulimwenguni. Sekta hii ndiyo inafanya maisha ya wanadamu yawe mepesi na laini. Kwa mantiki hiyo basi, Wizara hii ina jukumu kubwa, zito na muhimu sana la kuhakikisha maisha ya watu wetu yanaboreka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Kikwete kwa upeo wake wa kuunda Wizara hii. Pia nampongeza kwa namna ya pekee

Profesa Makame Mbarawa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii, kwa hakika uteuzi wa Rais umejibu "Jembe limepewa mkulima".

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ambayo pamoja na majukumu yetu mengi tunasimamia pia Wizara hii, hivyo nimejionea kwa macho juhudi, weledi na ufanisi wa Wizara hii. Napenda niwape hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za sayansi za *DIT* na *MIST* zinafanya uvumbuzi na ubunifu ili kupiga hatua kwa nchi. Serikali kwa upande wake ina wajibu sasa wa kuziunga mkono juhudi za taasisi hizi na kuzitangaza ili ziweze kuuzika na kuongeza mapato ili kukuza uchumi kama dhana ya sayansi ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa makusudi pia itangaze kazi za maabara ya udongo iliyopo *DIT* ili watu waweze kuitumia kwa shughuli zao za ujenzi hata wa nyumba ili nyumba hizo ziwe na ubora na muda mrefu wa kuishi jambo ambalo ni moja ya hatua za kukuza uchumi. Sambamba na hilo, maabara hiyo ni ya zamani sana na imechakaa, Serikali sasa iboreshe maabara hiyo iendane na jina la chuo na karne hii ya 21. Kufanya hivyo kutapelekea hata makampuni makubwa ya kigeni ya ujenzi yaliyopo nchini kuiamini na kuitumia, hivyo kuongeza mapato lakini pia nchi itakuwa na uhakika zaidi wa kazi za ukandarasi zinazofanywa na makampuni ya kigeni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya simu, pamoja na juhudi zinazofanywa na makampuni haya

katika sekta ya mawasiliano bado kuna kero nyingi zinazohitaji kuondolewa haraka. *Messege* nyingi za "*advertisement"* ambazo wadau wanalalamika kutozwa pesa kwa *message* hizo wanazotumiwa. Pia kupigiwa simu "phone calls" kutoka mitandoa ya simu hata usiku wa manane! Jambo linalokera sana hasa Zantel. Vilevile simu kukatikakatika mara kwa mara wakati wa maongezi hasa Tigo. Jambo linalokera sana, kupoteza muda wa mtumiaji na pia kuongeza gharama kwa mtumiaji. Namtaka Mheshimiwa Waziri anipe majibu yaliyo bora kwa mambo haya wakati akifanya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo, Serikali sasa iongeze bajeti hasa ya maendeleo kwa Wizara hii ili kukidhi haja ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,fedha za ndani za maendeleo zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu 2012/2013 ya Sh.1,125,878,000/= ni kidogo sana, fedha yote (nyingi) Sh.38,706,547,000/= tunategemea kutoka kwa wafadhili, hii ni hatari sana kwa ustawi wa Taifa letu. Kutegemea wafadhili kwa maendeleo yetu ya sayansi tutakuwa tunaota ndoto za mchana, watu hawa wanatamani sisi tuendelee kuwa na teknolojia duni milele ili waendelee kutunyonya, iweje watuwezeshe kisayansi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izinduke bado ni mapema kabla muda haujatuacha. Siku zote maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe, kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kutaka nchini iwe ni *medium economy country* ifikapo mwaka 2025,

iongeze bajeti ya ndani ya maendeleo kwa Wizara hii, kinyume na hivyo tutaendelea kuimba tu kuifikisha nchi katika uchumi wa kati. Lengo hilo halitafikiwa hata mwaka 2050 licha ya 2025.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Nchi yetu kwa sasa inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mabadiliko ya tabianchi. Tanzania kwa sasa inayo changamoto kubwa ya uhaba wa nishati ya umeme ambapo kuna uharibifu wa mazingira kwa kukata miti kwa lengo la kuchoma mkaa na kuni. Ili kukabiliana na changamoto hii ya aina yake ipo sababu ya msingi ya kuwekeza katika nguvu za kiatomiki kwa kuanza mchakato wa kuwekeza umeme (*nuclear reactors*) kwa ajili hiyo Mungu ameijalia nchi yetu kuwa na madini ya urani huko Wilayani Namtumbo Mkoani Ruvuma na zipo taarifa za kuwepo kwa madini ya aina hii katika Wilaya za Bahi na Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa yote yaliyotaabika na kufikia upeo katika ustaarabu na maendeleo, yanajivunia chanzo cha nguvu za umeme kwa kupitia vyanzo vya nguvu za kiatomiki mifano michache ya mataifa hayo ni pamoja na USA, Russia, China, Japani, Ufaransa, Ujerumani, India, Korea zote mbili za Kaskazini na Kusini, Israel na kadhalika. Kwa vile Mungu Mwingi wa Rehema ametujalia kuwa na malighafi ya madini ya urani iko sababu ya msingi kuwekeza katika sekta ya umeme kwa kujenga vinu

vya kuzalishia umeme ili umeme upatikane kwa wingi na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji katika sekta ya viwanda. Upatikanaji wa umeme rahisi katika maeneo ya mijini na vijijini itaepusha kansa inayolitafuta Taifa letu la ukataji miti na kuharibu mazingira na kusababisha mabadiliko ya tabianchi na kuathiri upatikanaji wa mvua katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano ni jambo la msingi, naipongeza Wizara kwa kuendelea na jitihada za kusambaza minara ya mawasiliano sehemu mbalimbali nchini mwetu. Hata hivyo, naomba Wizara itupatie mitandao katika Kata za Ilolangulu, Ushirika, Ngemo, Isebya, Ikobe, Nhomolwa, Bukandwe, Iponya na Nyasato ili kuwe na mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka Serikali kupitia Waziri wa Wizara hii aliambie Bunge lako Tukufu kuwa ni lini hasa Mbeya *Institute of Scence & Technology* (*MIST*) itakuwa Chuo Kikuu kamili? Maana sasa ni muda mrefu Bunge lako na pia wananchi wa Mbeya wamekuwa wakisikia maelezo bila kuona utekelezaji. Kwa hiyo, ili kuondoa hali ya sitofahamu kuhusiana na suala hili, namtaka Waziri aseme ni lini hasa *MIST* itakoma kuwa taasisi na iwe Chuo Kikuu kamili, nikirudia kwa msisitizo. Nasuburi majibu.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa bajeti ya Wizara. Kwa vile

dunia inakwenda mbele katika sayansi na teknolojia na Tanzania bado inaonekana ipo nyuma kisayansi, nashauri Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia ianzishe *programme* ya sayansi kuanzia *primary school na secondary school* ili wanafunzi wapate uelewa wa masomo ya sayansi na waweze kuyapenda masomo haya. Pia ni lazima tuibue vipaji vya watoto mapema na Serikali itaweza kuwaendeleza na kupata Walimu na wafanyakazi bora wa sekta ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya utafiti kama ipo iboreshwe na kama haipo ianzishwe, tena kwa haraka ili iweze kulinda tafiti na watafiti wetu kuliko kila Wizara ikiwa na utafiti wake ambao unatekelezwa kutokana na sera ya Wizara yake. Serikali igharamie tafiti zetu kwa kuongeza bajeti yake ili wananchi wengi wanufaike hasa wa vijijini zipelekwe kama zile tafiti za kilimo zifanywe kila Wilaya ijulikane ni zao gani linakubali ili wakulima washauriwe kikamilifu kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iratibu uingizaji wa ving'amuzi nchini kwa kujua ubora wake katika kipindi hichi cha mabadiliko ya kutoka analojia *to* digitali kwani wananchi wasije kuuziwa ving'amuzi visivyo na ubora na kuwatia hasara wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia itajenga ofisi kwa upande wa Zanzibar ili kuweza kuratibu kazi zake kwa urahisi zaidi na kuondokana na tatizo la kuazimwa ofisi katika majengo ya ofisi nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali idhibiti uingizaji wa simu za viganjani ili simu zinazoagizwa ziwe na ubora zaidi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kwa kifupi sana kwani mengi nilichangia bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusikitishwa na kasi ndogo ya ufikaji wa mawimbi ya televisheni kwa mujibu wa takwimu zilizoonyeshwa kwenye kitabu cha Wizara 2012/2013. Ukurasa wa 93 unaonyesha kuwa idadi kubwa ya Watanzania zaidi ya asilimia sabini hawajafikiwa na mawimbi ya televisheni. Ingawa takwimu zimekosewa na chanzo chake ni *TCRA,* Juni, 2012 kwenye *piechart* ni zaidi ya asilimia 120 lakini pamoja na hayo tunashuhudia ujenzi mdogo sana wa mawimbi ya analojia na yale ya dijitali. Hii inaonyesha ni kiasi gani bado Watanzania hawapo tayari kutumia teknolojia ya dijitali na Serikali haijawekeza zaidi katika kukamilisha uwepo wa mawimbi ya television kwa Watanzania walio wengi kwani ni njia mojawapo muhimu ya kutoa habari kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni dhahiri kabisa kwa kuingia kwenye digitali ni muhimu lakini inawalenga watu wachache sana. Pia wananchi wengi wanalalamika hasa kwa gharama za uendelezaji wa digitali ambapo watawajibika kulipia shilingi 9,000/= kila mwezi kwenye kampuni ya *Star times.* Hii ni mbali ya *initial costs* ambazo ni zaidi ya laki 100,000/= wakati wananchi wakiangalia gharama za analojia ambazo ni ndogo na za manunuzi ya mwanzo

ya ununuzi wa kifaa, lakini inakuwa haina *monthly fee,* hii ni changamoto ambayo Serikali inawajibika kutoka utatuzi wa urahisi wa kutumia teknolojia ya dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia vijana wengi wa Kitanzania wakivumbua teknolojia mbalimbali kama kutengeneza redio, kutengeneza pikipiki, magari, kutengeneza *chilled detector* na kadhalika lakini hawaendelezwi na badala yake teknolojia zao au uvumbuzi wao huchukuliwa na watu wengine bila hata wao kupewa fidia wala hati miliki. Hii siyo haki napenda Serikali ituambie kwa nini hawa Watazania hawaendelezwi na kwa nini hawalipwi fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni juu ya kero ya makampuni ya simu kukata fedha za dakika moja wakati mtumiaji kaongea kwa sekunde kadhaa. Kumpigia simu mteja hata nyakati za usiku na akipokea mapema ni matangazo yao, hii siyo haki kwa mlaji sababu inatoa usumbufu. Vilevile wanatuma *message* muda wowote bila kuja *private* ya mtumiaji. Serikali iniambie kwa nini haichukui hatua juu ya kero hii.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia bajeti hii na kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa minara ya simu Wilaya ya Kibondo. Katika Kata 13 za Wilaya Kibondo ni Kata tisa (9) zenye upungufu wa kukosa mawasiliano ya simu za mkononi mfano wa Kata hizo ni Murungu, Kumsenga, Rugongwe, Mabambo, Kigogo,

Busagara, Busunzu na kadhalika. Naomba Serikali ipeleke huduma hii haraka kwani Wilaya ya Kibondo ni moja ya Wilaya chache zenye shida kubwa ya mawasiliano ya simu lakini pia hata Kibondo Mjini "*network*" ya simu inasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi kwenye makampuni ya simu, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kupitia upya utaratibu wa kodi kwenye makampuni ya simu mfano *Vodacom* peke yake imepitisha shilingi trion 6.6 kwenye M-pesa achilia mbali makampuni ya Zain (Airtel), Tigo, Zantel na kadhalika. Napenda kuishauri Serikali itoze kodi huduma zote zinazofanywa na mitandao ya simu siyo *corporate tax* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia (gesi, mafuta, madini). Napenda kutoa ushauri kwa Serikali kuwekeza kwenye taaluma hizo kwani kutokana na mafuta, gesi iliyogunduliwa tunapaswa kuwekeza kwenye tafiti na kusomesha wataalam kwenye sekta hii nyeti ili baadaye tuweze kuwa na wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ili nchi yoyote iweze kuendelea ni muhimu kuwa na *focus* inayoeleweka juu ya falsafa za sayansi na teknolojia. Kwa sasa nchi yetu tunazalisha wasomi wengi kwenye *Arts* kuliko sayansi, napenda kuishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafundi kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kibondo kuna ofisi ya posta ndogo ya kizamani na haikidhi

mahitaji na haina uwezo wa kutoa huduma ipasavyo. Napenda kuomba kwamba Serikali ijenge ofisi hii ya Kibondo.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Wizara hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda digitali. Ni muhimu Taifa kufanya mabadiliko haya, hii ni kutokana na maendeleo ya kiteknolojia yasiyokwepeka kwa hatua ya sasa kote ulimwenguni, tena mimi naona kama nchi yetu imechelewa lakini kwa kuwa tumeshaanza, ni vizuri Serikali ikaweka udharura katika suala hili ili kuliwezesha Taifa letu kupata mafanikio mengi zaidi na miongoni mwa mafanikio hayo ni haya yafuatayo:-

(i) Huduma zinazotumia teknolojia ya digitali zinakuwa na ubora wa hali ya juu ukilinganisha na ya analojia.

(ii) Kupatikana kwa fursa ya masaa ya ziada katika teknolojia ya digitali ukilinganisha na analogia. Hivyo kwa malengo yaliyowekwa na Taifa letu Kimataifa, itawezesha wawekezaji wengi sana kuhudumiwa kwa masafa yaliyopo na hiyo itawezesha kuongeza faida zaidi kiuchumi kwa wawekezaji na zaidi pia itaongeza ajira na hasa kwa vijana wanaomaliza vyuo katika *course za IT, Computer Science.*

(iii) Kurahisishwa zaidi kwa huduma ya mawasiliano katika suala zima la mfumo na hivyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata taarifa mbalimbali mahali popote walipo na kwa kutumia vyanzo vingi vya habari na mawasiliano kama vile simu za mkononi, kompyuta na kadhalika.

(iv) Mwisho ufanisi mkubwa katika kutayarisha vipindi vya televisheni na shughuli za urushaji wa matangazo hivyo kuongeza wataalam zaidi na hata muda wa kuandaa vipindi hivi utapungua na hivyo muda mwingine uliokuwa ukipotea wakati wa utumiaji wa teknolojia ya analojia utatumika kufanya mambo mengine na hivyo kuongeza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anuani za makazi. Zoezi hili ni zuri sana kama litafanikiwa kama Serikali au Wizara ilivyolipitisha lakini napenda kuzungumzia zaidi maeneo ya vijijini kwa kuwa wananchi wanaoishi Wilaya za pembezoni wamekuwa wakisahaulika mara nyingi mara itokeapo suala la maendeleo. Je, Serikali imeshaanza kuwaandaa au kuwapa semina wananchi wanaoishi vijijini ili na wao waweze kuelewa umuhimu wa anuani hizi za makazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa ikifanya au kuanzisha teknolojia mbalimbali bila kuanza kutoa elimu kwa wananchi na hatimaye kunakuwa hakuna maana tena ya umuhimu wa teknolojia hizo na hata kusababisha hasara kwa Serikali na ucheleweshaji wa maendeleo katika Taifa letu.mimi naiomba Serikali na Wizara husika itoe elimu kwanza kwa wananchi juu ya umuhimu wa teknolojia mpya yoyote

itakayoanzishwa ili kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Pia nimpongeze Waziri Profesa Mbarawa kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa 2012/2013. Nimpongeze kwa kazi nzuri anayofanya ya kusimamia, kuimarisha na kuendeleza teknolojia ya habari, mawasiliano, sayansi na teknolojia. Napenda kupata ufafanuzi katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni lini *Telecommunications Traffic Monitoring System* itaanza kazi? Sekta ya mawasiliano hapa nchini inakuwa kwa kasi kubwa sana, tumeshuhudia uwepo na kampuni mbalimbali ya simu na ongezeko kubwa sana la watumiaji wa simu hapa nchini mijini na vijijini. Ninasikitika kuona kuwa ongezeko kubwa la matumizi ya simu halijaleta ongezeko zuri katika mapato ya kodi kwa Serikali. Hivyo napenda kupata ufafanuzi toka kwa Waziri mipango ya Wizara ni ipi katika kuweka mfumo wa ku-*monitor* simu zote zinazopigwa na kupokelewa hapa nchini. Pia Waziri atueleze ni lini *Telecommunication Traffic Monitoring System* itaanza kutumika nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu siyo tu kwamba utawezesha upatikanaji wa mapato ya kodi sahihi na ya haki kwa nchi, lakini pia utawezesha kuboresha sekta ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu kwa

sababu ninaamini kuwa mfumo huu pia una uwezo wa ku-*track, detect na ku-block* udanganyifu katika mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, je, Wizara ina Sera na Sheria zozote za kuthibiti *ICT Asset Disposal* na kama zipo zinatumika ipasavyo? *ICT* ina nafasi kubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu hasa katika masuala ya afya, elimu na maendeleo ya sayansi. Hata hivyo, vifaa vya *ICT* (*computers, TV, mobile phones)* ni gharama kuvipata na kuvitunza hali hii imepelekea kuwepo kwa mahitaji makubwa sana ya bidhaa za *ICT* ambazo tayari zimetumika (*secondhand*) au hazikidhi mahitaji ya watumiaji katika nchi. Kinachosikitisha zaidi ni kuwa baadhi ya vifaa hivi vinavyoingizwa nchini vipo katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi Tanzania imekuwa ni kama jalala la vifaa chakavu vya *ICT* toka nje hasa China, Japan, Malaysia na UK. Nimeshuhudia hatua kadhaa zikichukuliwa kwa vifaa feki na siyo chakavu. Kuingiza vifaa chakavu sana kunaweza leta madhara kwa nchi hasa katika afya na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo ya ufafanuzi kama kuna *any legal na regulatory framework for ICT assets disposal* hapa nchini na kama hakuna, Wizara imejipangaje kukabiliana na suala la uingizaji *ICT products* ambazo ni *secondhand?* Je, ni vipi Wizara wanaweza kujiridhisha kuwa vifaa hivi havina au havitakuwa na *negative impact* kwa nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipatiwe majibu ni vipi Wizara inaratibu na kusimamia *e-waste.*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami kuchangia katika hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba makampuni yatakayopewa kazi ya kurusha matangazo ya *digital* lazima yahakikishe kuwa *local television* zinapatikana *free* kwa Watanzania kama ilivyo katika nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina mashaka kuhusu mpango huu wa kuhama kutoka analojia kwenda digitali*,* ukitilia maanani kwamba licha tu ya kuwa ni gharama kubwa lakini pia katika nyumba zetu nchini hakuna *network system* (*cables*) kama ilivyo katika nchi nyingine duniani, kitu ambacho itatuchukua muda mrefu kufika huko. Naiomba Serikali kuongeza muda wa ku-*migrate* kutoka analojia kwenda digitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha televisheni zilizopo hapa nchini, nyingi hazitakuwa na uwezo wa kufanya kazi endapo tu tuta-*migrate* Desemba hivyo nashauri kuhakikisha kuwa *TV* zote zinazoingizwa nchini kuanzia sasa ziwe na uwezo wa kufanyakazi katika mfumo wa *digital* ili kuwapunguzia gharama wananchi na ikiwezekana Serikali ipige marufuku uingizaji wa *TV* ambazo hazina mfumo wa kisasa wa *digital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Kata za Bukundi, Imalaseko, Mwanjolo na Mwamalole zitapelekewa mawasiliano ya simu ya kudumu ikiwa ni pamoja na kujenga minara ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi wa hotuba ya Waziri, Ibara ya 84(vi) ya hotuba iliyopo ukurasa wa 70 kuhusu kuanzishwa kwa mradi wa matibabu mtandao (*Telemedicine).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri na kama tutaza kamba basi inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 18 inayoelezea, nanukuu:-

*"Mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na elimu iliyotolewa lakini bado wananchi wanahitaji elimu zaidi kwani kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine lazima kunatakiwa kuvuka vikwazo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU), pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), haya ni mataifa makubwa na ni lazima kusisitiza kwa kuanza kwa mtandao huo. Kwa Tanzania bado mapema, tuendelee na elimu kwanza, tusubiri, tusisitishe ifikapo Desemba 2012, kuna baadhi ya Watanzania wenzetu tutawaacha nyuma. Elimu izidi kutolewa mashuleni kwa matumizi ya kutoka katika analojia kwenda dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwa upanuzi wa baadhi ya posta za Tanzania Bara na ile iliyopo Zanzibar Mahonda. Lakini pia iboreshe na huduma za utendaji wa kazi katika Posta zetu kwani tokea kuwe na utendaji kazi wa *internet,* mitandao ya posta imepoteza mwelekezo wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu anuani za makazi, huu utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi na simbo za posta kwa kweli suala hili ni ndoto kwani mitaa na makazi yetu ya Zanzibar yameparaganyika, hayana anuani kamili na wananchi wanaishi bila ya kuwa na anuani kamili, vipi wataweza kuwafikia wananchi kwa kutumia mfumo huo? Ninaomba ufafanuzi kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa (*Fibre Optic*). Kwa kuwa taarifa ya kuwepo Mkongo wa Taifa ni kupunguza

gharama za simu, ni kwa nini gharama za simu bado ziko juu sana? *TCRA* ichukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo mtandao wa kutosha hususan vijijini. Maeneo mengi na yenye umuhimu wa kuinua uchumi nchini kama vile Wilaya ya Serengeti, sehemu kubwa haina mawasiliano ya simu na hii inasababisha utalii na huduma nyingine kuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofautiana kwa gharama za simu katika makampuni, ni vyema *TCRA* ichukue hatua ya kurekebisha viwango hivi katika simu ili kusiwe na tofauti kubwa ili kupunguza gharama za utumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufundisha elimu ya kompyuta mashuleni, kwa nini hakuna utaratibu wa makusudi ili kufundisha elimu ya kompyuta na kuwezesha sayansi iweze kusambaa haraka nchini kwa sababu elimu ya kompyuta itarahisisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga zawadi kubwa kwa wagunduzi, kiwango kinachotolewa kama zawadi kwa wagunduzi ni kidogo mno. Ni vyema kutenga zawadi kubwa na maalum na ijulikane ili watu binafsi ama taasisi waweze kushindana kwa manufaa ya kuongeza tija (*COSTECH).*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera na sheria ya kuanzishwa kwa makampuni ya kibiashara miongoni mwa taasisi za Serikali kama "DIT". Imekuwa ni rai yangu kwa Wizara na Serikali kwa

ujumla kushauriwa nami juu ya kuletwa kwa sera na sheria Bungeni itakayotoa fursa kwa taasisi za kiufundi zinazotoa elimu nchini kuruhusiwa kuanzisha makampuni ya kibiashara hapa nchini ambayo yatakuwa na jukumu la kuchukua tenda zote ambazo zipo ndani ya uwezo wao. Hii ina maana kwamba Serikali itoe kazi zote kwa makampuni hayo ili kuwezesha vyuo kama *DIT* kuweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya Serikali kila mwaka katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuanzishwa kwa makampuni katika taasisi kama "*DIT*", kimsingi vyuo vyenye teknolojia mbalimbali kama *DIT* na vikipewa fursa ya kuanzisha makampuni na ku-*marketise*" huduma za ujuzi na bidhaa zake, taasisi hizo zitaweza kujitegemea kifedha na hivyo kutotegemea ruzuku ya Serikali. Lakini pia Taifa litaepuka kupoteza mapato (fedha) yanayochukuliwa na makampuni ya kigeni yanayofanya kazi hapa nchini kwa mfano makampuni ya barabara kutoka China yanachukua fedha nyingi (faida) na kuipeleka kwao, Taifa linabaki maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DIT* na taasisi mbalimbali kama *UDSM, Nelson Mandela* na *VETA,* wana ujuzi na teknolojia mbalimbali, kwa nini tusilete sera na sheria haraka (Muswada) utakaoruhusu taasisi kuanzisha makampuni ili fedha zote zibaki nchini na faida itakayopatikana itumike kwa maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa ni *"concern"* yangu ya muda mrefu na mara ya mwisho mnamo mwezi Juni, 2012 tukiwa *DIT* niliuliza na kushauri Sera na

Muswada, vilevile Bungeni, Naibu Katibu Mkuu aliahidi kuwa wataleta, je, Sera na Muswada wa Sheria vipo wapi? Mtaleta lini au mmeahirisha? Naomba majibu na sababu za kuchelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii muhimu kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni mawasiliano ya simu. Napongeza ongezeko kubwa la simu za mkononi nchini ambazo zimerahisisha mawasiliano, ununuzi wa vocha, huduma za kibenki, umeme na kadhalika. Hata hivyo, bado gharama za matumizi ya simu ni kubwa hasa kwa kuwa uwezo wa Mtanzania kifedha ni mdogo. Lakini pia katika matumizi ya simu kunajitokeza kero nyingi, kwa mfano meseji nyingi kutoka makampuni ya simu. Je, ni lazima makampuni watume na kujaza meseji kwenye simu japo wateja hawapendi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Chambeni hasa Ukanda wa Mashariki una matatizo makubwa ya simu. Naomba Wizara hii itembelee kuona ukubwa wa tatizo ili hatimaye makampuni yajenge minara hasa Zantel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mkongo wa Taifa, pamoja na Serikali kutandika mkongo wa mawasiliano bado hatujaona unafuu wa bei katika matumizi ya Intaneti. Naomba Serikali ihakikishe dhana ya kuleta mkongo wa mawasiliano inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uanzishaji wa *e-Government na e-Parliament*. Matumizi ya teknolojia hii katika Bunge na Serikali kwa ujumla ni jambo muhimu katika ulimwengu wa leo. Lakini matayarisho yake yanahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka hasa katika ngazi za Mikoa na Wilaya ambako sehemu nyingine hakuna nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi na teknolojia kwa sasa ni muhimu kwa kila kitu lakini inahitajika utafiti mkubwa kulingana na mazingira yetu. Hivyo Serikali inapaswa kuongeza bajeti ya Wizara hii ambayo kwa sasa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya teknolojia kutoka analojia kwenda dijitali tunaikaribisha kwa sababu itaboresha matangazo ya *TV* zetu. Hata hivyo, tunaomba gharama za teknolojia hii iwe chini sana ili Watanzania wengi waweze kufaidika.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Wizara nzima kuanzia Waziri na Watendaji wote kwa hotuba nzuri inayokidhi, tunashukuru kwa jitihada zao

katika kuhakikisha mawasiliano yanaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri ufuatao:-

(i) Tunaomba ving'amuzi vyote vioneshe (*local channels)* zote bila malipo ya ziada.

(ii) Tunaomba matumizi ya *analogy* yaendelee mpaka 2015.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*). Mimi naipongeza sana Serikali kwa kufikiria kuanzisha mpango huu kwa nia ya kupeleka mawasiliano katika maeneo ambayo hayana mawasiliano hapa nchini. Leo nasimama mara ya pili kuongelea mpango huu wa mawasiliano kwa wote. Mpango huu ndio mkombozi peke wa Watanzania walio wengi huko vijijini lakini mpango huu sasa umechukua muda mrefu mno kuanza. Serikali ifikie mahala sasa *logistics* hizi ziishe na mradi huo uanze kutoa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wakati anajibu swali langu lililohusu tatizo la mawasiliano Wilaya ya Liwale tarehe 19/6/2012, alisema kwamba Serikali inatarajia kupeleka mawasiliano katika vijiji vipatavyo 2,175 nchini kote. Waziri aliendelea kusema kwamba

Serikali ilipata shilingi bilioni 45 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya mpango huu na mwaka jana Serikali ilitangaza zabuni na haikuweza kupata mzabuni wa kujenga minara hiyo kutokana na gharama kubwa kuliko pesa zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kushauri Serikali kwamba vijiji 2,175 ni vingi sana, kwa vyovyote vile ujenzi wa minara hiyo ni lazima ufanywe kwa awamu na mradi huu unapaswa kuwa endelevu mpaka pale kusudio la Serikali la kupeleka mawasiliano kwa wote huko vijijini litakapokamilika. Serikali sasa ianze kutekeleza mradi huu kwa kuangalia maeneo ambayo kweli yana matatizo ya mawasiliano kama vile Wilaya ya Liwale na nyinginezo na iende hivyohivyo hadi vijiji hivyo vilivyokusudiwa vikamilike. Bajeti ya mwaka ujao, *seriously*, tunataka kusikia kwamba *project* hii imekwishaanza na tutajiwe maeneo ambayo tayari minara kadhaa itakuwa imejegwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu kampuni za simu za mikononi za *Airtel, Zantel, Tigo* na *Vodacom*. Kampuni hizi zimetusaidia sana kutuleta mawasiliano katika baadhi ya maeneo huko vijijini kwetu. Mimi naendelea kuwaomba sana Wilaya ya Liwale ina tatizo kubwa sana la mawasiliano, ninaomba mje mfanye *feasibility study* tena Wilaya ile mnayofahamu miaka ya nyuma, sio hiyo miaka ya nyuma kidogo Wilaya ilikuwa na wakazi wapatao 40,000 sasa hivi Wilaya ina wakazi zaidi ya 100,000 na nafikiri baada ya sensa Wilaya ya Liwale inaweza kuwa na wakazi takribani 150,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ina fursa nyingi sasa za biashara kwenye kilimo cha korosho, ufuta, utalii ndani ya hifadhi ya *Selous*, wachimbaji wa madini wadogowadogo na wakubwa, hali ya uchumi wa Wilaya ile umepanda, watu wanahitaji mawasiliano kwa kila hali, watu wanahitaji matumizi ya simu sio kupiga tu, kutumia pesa, kutunza pesa zao katika simu zao, kuangalia intaneti na matumizi mengine. Kwa hiyo *seriously* kuna uhitaji mkubwa wa mawasiliano. Tafadhali mje muwekeze katika Wilaya ile mtafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wa *Airtel* waliniahidi kunijengea minara kadhaa kule Liwale tangu mwaka jana, nimeshafuatilia sana mpaka sasa *Airtel* bado wako kwenye *logistics.* Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, naomba unisaidie ndugu zangu hawa wa *Airtel* ile minara minne walioniahidi katika vijiji vya Lilombe, Likombora, Makata na Barikiwa, ninaomba sana mnisaidie, wananchi wanasubiri kwa hamu kupata mawasiliano. Tafadhali njooni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa minara huko vijijini. Mimi nataka kushauri Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia na makampuni ya watu binafsi ya *Airtel*, *Vodacom, Tigo* na *Zantel*, wanapofikiria kujenga mnara katika kijiji fulani ni vema mnara huo ujengwe katika eneo la Serikali ya kijiji ili mapato yatakayopatikana kutokana na minara hiyo yaingie katika mfuko wa Serikali ya kijiji na mapato hayo baadaye yataweza kuwasaidia wanakijiji hao katika shughuli zao za maendeleo ya kijiji, badala ya utaratibu

wa sasa wa kujenga minara hiyo kwenye maeneo ya watu binafsi na hivyo mapato hayo kwenda kwa watu binafsi. Kwa upande wa mjini sawa lakini kwa vijijini tuna maeneo mengi sana ya Serikali ya vijiji ni vema kuwa na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya sayansi na teknolojia, kumekuwa na tafiti mbalimbali zinazoendelea hapa nchini na tafiti hizo zinafanywa na Vyuo vyetu Vikuu, *Institutions* mbalimbali kama vile *TIRDO, TBS, TFNC,* Mkemia Mkuu, watu binafsi na *Institutions* nyinginezo nyingi. Wasiwasi wangu ni kwamba, je, kuna chombo chochote ambacho kina *records* za tafiti hizi zote zinazofanywa hapa nchini? Kama utaratibu wa namna hii haupo ni vema uanzishwe, kuwepo kwa utaratibu huu na kuwa na *records* za *researchers* wote kutasaidia sana kutorudiwarudia kwa *research* moja mara kadhaa na hivyo kupoteza *resources,* muda na *funds* bila sababu. Naishauri Wizara ya Sayansi na Teknolojia kutengeneza utaratibu huu hapa nchini badala ya utaratibu wa sasa wa kukuta taarifa hizo kwenye *institutions* ambazo watafiti hao walikuwepo, tafiti zilizokwishamalizika na kutoa matokeo mazuri, zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa kazi nzuri ya kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa siku za karibuni kumekuwa na tatizo la wizi wa fedha katika akaunti za watu na taasisi kwa kutumia mbinu za *computer* au kwenye *ATM,* ni vipi Serikali inadhibiti hali hiyo ili kutoa hofu kwa wateja wa mabenki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wimbi la wizi wa simu na komputa ndogo (*laptop)* limekuwa kubwa sana. Nashukuru kuwa teknolojia ya kudhibiti wizi na kuwafuatilia wezi imeanza nchini kama inavyotangazwa kwenye vyomba vya habari. Sijui ni lini teknolojia hii itasambaa hadi maeneo ya vijijini ili kulinda wamiliki wengi wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao ya simu imekuwa njia ya kutuma ujumbe wa vitisho na uchochezi katika jamii kwa siku hizi. Ni namna gani Serikali itabuni mbinu ya kukamata au kuwafuatilia wenye simu zinazotumika vibaya hivi, kwani inaweza kuhatarisha amani ya nchi yetu. Hivyohivyo mitandao ya kijamii imetumika vibaya licha ya malengo mazuri yaliyokusudiwa. Vivyohivyo mitandao inatumika kwa picha za aibu (ngono) na hivyo kuharibu maadili hasa kwa vijana. Serikali lazima ione namna ya kudhibiti hali hiyo.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa uchungu sana hoja hii ya mawasiliano. Nasema kuwa nimekuwa nikiahidiwa mara kwa mara na Waziri aliyepita kuwa ufungaji wa minara ya simu katika maeneo ya Kata zilizomo Jimboni kwangu kama Kata ya Shabaka, Bukwimba, Busolwa, Nyungwa, Nyijundu, Mwingiru, Nyaburanda,

Kafita, Nyang'hwale, Kakora, zingekuwa zimefungiwa kufikia Desemba 2011, lakini hadi leo hata mnara moja bado haujafungwa. Wananchi wanahoji ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hiyo na kupatikana huduma hii muhimu kwa dunia ya leo na kuchochea maendeleo ya Wilaya mpya ya Nyang'hwale?

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa pongezi kwa Wizara na kuunga mkono hoja ya Waziri wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simu za mkononi kupitia minara ya mawasiliano zimesaidia sana shughuli mbalimbali za wananchi na wafanyabiashara hapa nchini. Katika eneo langu la uwakilishi Bungeni (Jimbo la Ngorongoro) eneo la *Lake Natron* na Mlima Sengai, vijiji vya Engaresero, Monic, Pinyinyi na Separkashi yana shida kubwa ya mawasilino ya simu za mkononi. Umuhimu wa eneo hili ni kutokana na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni eneo la utalii, kuna Flamingo *Lake Natron;* wataliii hupanda Mlima Lengai yenye Volcano; kuna 'c*ampsites'* nyingi katika eneo hilo; kuna '*waterfall'* katika Mto Engaresero; kuna '*culture'* na boma kwa wageni kuona utamaduni wa Wamasai na Wasonjo (Wabatemi); kuna '*hot water springs';* kuna shimo la Mungu; kuna nyayo za watu wa kale; barabara ya lami ya mto wa Mbuu na Loliondo inayotarajiwa kupita huko itaanza kujengwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni mkubwa sana katika eneo hili kutokana na vivutio vilivyopo na kwa maana hiyo mzunguko wa fedha ni mkubwa na kwamba kampuni za simu zikiwekeza katika eneo hili kwa kujenga minara ya mawasiliano yatapata faida kubwa na wananchi waishio katika maeneo hayo watapata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi namwomba Naibu Waziri wa Mawasiliano, Mheshimiwa January Makamba, atumie uzoefu na umahiri wake katika sekta hii kunisaidia katika upatikanaji wa mawasiliano katika eneo la *Lake Natron* na Mlima Lengai ambapo pia kiwanda cha *Soda Ash* kinatarajiwa kujengwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Waziri kwa kuwasilisha hotuba nzuri kwa ufasaha na umakini. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wa Wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba ya bajeti yenye mwelekeo na matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa kusimamia utekelezaji wa sera kwa umakini. Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano ni mafanikio makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Gharama za mawasiliano hasa ya simu zimeteremka sana. Wizara ilinde mafanikio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isiruhusu ujenzi wa mikongo mingine kama ilivyotokea kwa ujenzi wa Mkongo wa Voda Dar es salaam na Dodoma. Makampuni hayo yote yalikataa kujenga mkongo huu unaounganisha nchi nzima! Lakini walikubali kuwa ukijengwa watautumia. *TTCL* iimarishwe ili imudu kuwa mwendeshaji mahiri wa mkongo huo. Mashirika ya umma yenye mikongo (mfano *TRL* na *TANESCO*) wakubali kuachia mikongo yao iwe sehemu ya mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio mazuri ya Wizara katika Jimbo la Bagamoyo, bado tuna changamoto kadhaa za mawasiliano ya simu. Vijiji vingine havipati mawasiliano mazuri ya simu. Mfano vijiji katika Kata ya Yombo, (Yombo, Chasimba, na Matimbwa), Kata ya Magomeni (Makurunge na Kitame). Kata ya Vigwaza (Visezi na Buyuni), Kata ya Zinga na Kata ya Kerege. Naiomba Wizara ihamasishe makampuni ya simu yaongeze mitandao yao ya simu ili mawasiliano kwa wananchi wa Bagamoyo na Taifa kwa ujumla yawe bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya, nawatakia utekelezaji wenye mafanikio ya bajeti yao ya 2012/2013. Aidha, nawapongeza sana Watendaji wa Wizara hii kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa rai zifuatazo kwa nia ya kuboresha. Naomba sana tena sana Wizara itusaidie sisi wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kupata mtandao wa uhakika wa simu za mkononi. Katika Kata zifuatazo hakuna mawasiliano ya aina yoyote labda mtumiaji wa simu apande juu ya mti au asafiri kwenda maeneo ya mtandao. Kata hizo ni Tegehero maeneo ya Kiwole, Tonunguo, Mkulazi, Matuli na vijiji vya Seregete A, B na Hubumo katika Kata ya Kidungalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadili *deadline* ya kutumia teknolojia ya analojia kwenda dijitali, kwani wananchi walio wengi bado hawajaelewa mantiki ya mchakato huu. Nashauri elimu iendelee kutolewa kwa wananchi kupitia wawakilishi wao, Walimu wa shule za sekondari, vyuo na shule za msingi ili zoezi hili lifanikiwe. Ni vyema Serikali ikaongeza muda wa kipindi hiki cha mpito ili kupunguza usumbufu unaojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie upya *rate* zinazotozwa na makampuni ya simu, kwani zinabadilika katika kampeni za *promotion* mara kwa mara na kuyumbisha watumiaji. Aidha, naomba haya makampuni yatengeneze mpango unaoeleweka wa kutoa misaada ya kijamii kwani wanaegemea maeneo ya mijini tu au katika maeneo ya viongozi wanaowafahamu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anihakikishie kwamba Morogoro Vijijini watapata huduma za simu za kiganjani kwani walio wengi

wanazo simu ambazo hawawezi kuzitumia wakiwa katika maeneo yao. Nitaunga mkono hoja nikiamini kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2005 na 2010 itatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara mwaka 2012/2013.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya *internet* na kompyuta ni mazuri na yana faida nyingi kama ifuatavyo: hurahisisha mawasiliano kwa njia ya *e-mail*, hutunza kumbukumbu kwa kutumia *flash* badala ya kulundika mafaili mengi ofisini, huwezesha watu kusoma kwenye mtandao badala ya kwenda chuoni, huwezesha kufundisha kwa njia ya mtandao, hurahisisha utafiti kwa kupata taarifa husika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida hizo, kuna watu wanaotumia vibaya mitandao ama kwa makusudi ama kwa kutokujua kuwa kosa litokanalo na matumlzi mabaya ya komputa linaweza kuchunguzwa na hatimaye mhalifu kubainika. Tatizo tulilonalo nchini ni ukosefu wa sheria ya makosa yatokanayo na matumizi mabaya ya kompyuta (*cyber laws).* Naiomba Serikali ilete sasa Muswada wa Sheria ya *Cyber Crimes* ambayo itasaidia kudhibiti uhalifu ufanyikao kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara husika ilete haraka '*comprehensive legislation*' ili turudishe

heshima ya nchi yetu, viongozi wetu na Watanzania kwa ujumla. Sasa hivi kuna baadhi ya watu wanachafua viongozi kupitia mitandao kwa sababu hatuna sheria ya kuwadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini, Waziri mwenye dhamana ameshatembelea katika Kata ya Kizama na kuona matatizo yanayokabili na kuahidi kwamba mawasiliano yatakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu lina maeneo mengi ambayo hayana mawasiliano ya simu mfano Kata ya Mkazamo, Kata ya Mpale na Kata ya Magoma kwenye kijiji cha Kijango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina watu makini sana, Waziri na Naibu Waziri kwa maana hiyo ukizingatia kuwa Naibu Waziri mwenye dhamana aliisha kwenda kukagua sehemu husika, naamini kuwa suala la mawasiliano ya simu katika eneo husika litaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Waziri wa Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa weledi wake wa kuiongoza Wizara hii kwa ufanisi zaidi. Nampongeza pia Naibu Waziri wake kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi hii. Hali kadhalika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza watendaji wengine wa Wizara hii kwa kuiongoza Wizara hii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia cha karne ya ishirini na moja, ni la lazima ili kufanikisha suala la uharakishaji wa maendeleo. Kwa bahati nzuri katika nchi yetu tumebahatika kupata mitandao ya kila aina kwa lengo la kuharakisha mawasiliano hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali na hoja, hadi sasa ni kampuni ngapi za simu za mkononi zimepata vibali vya kufanya huduma hiyo ya mawasiliano hapa nchini? Kampuni hizo ni zipi? Je, Serikali imenufaika na uwingi wa makampuni haya ya simu za mkononi? Je, wamelipa kodi shilingi ngapi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungno wa Tanzania? Je, Serikali imehakikishaje kuwa makampuni haya ya simu yanalipa kodi na wala hayakwepi kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inadaiwa kuwa makampuni mengi ya simu yamekuwa yakiwaibia wananchi wa Tanzania kwa kukata muda wao wa maongezi bila taarifa yoyote. Je, Serikali inalifahamu hilo? Kama inalifahamu, je, Wizara imechukua hatua

gani? Kwa kuwa suala la mawasiliano ni haki kwa kila Mtanzania, je, ni lini Wilaya ya Tarime itapata huduma za simu za mikononi katika Kata za Nyanungu, Itiryo, Muriba, Nyamwaga, Sirari, Susuni, Bumera, Nyarukoba, Gorong'a, Nyandoto, Kemambo, Nyarero, Magoto, Mogabiri, Manga, Komaswa, Ganyange, Nyansincha, Kitare, Kiore, Kibasuka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha kuwa Shirika letu la *TTCL* linafanya kazi kwa ufanisi zaidi? Je, Shirika la *TTCL* litafanikisha lini mitandao ya simu ya mikononi nchi nzima ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, *promoshen*i za simu za mikononi zimeliletea faida au hasara Taifa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuisemea sayansi na teknolojia, ni pande mbili za shilingi ambazo si rahisi kuzitenganisha. Hoja kwa nini hakuna mkakati maalum wa kuendeleza fani hii hapa nchini kwetu? Kwa nini zisianzishwe shule maalum za masomo ya sayansi tu hapa nchini na shule hizo ziwe mfano kwa kila kitu ili kuibua vipaji katika nchi yetu? Sayansi ni muhimu sana kwa maendeleo ya binadamu. Je, Tume ya Sayansi katika nchi yetu imeleta maendeleo gani hapa nchini tangu ianzishwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya vijana katika nchi yetu ni wagunduzi. Je, Serikali kupitia Wizara hii ya Sayansi na Teknolojia imechukua hatua gani za

makusudi ili kuwatambua wagunduzi hao? Je, kwa nini Wizara hii isianzishe tuzo maalum kwa wagunduzi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Transfer Technology* (Teknolojia Hamishi), ni kero kwa nchi za ulimwengu wa tatu hasa Tanzania na nchi nyingine za Afrika. Je, Wizara hii inakabilianaje na tatizo hili? Je, Wizara hii inatambua kuwa *transfer technology* inaua vipaji na hivyo ni kikwazo kwa maendelo ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mkakati gani wa kuwakutanisha wanasayansi wote hapa nchini kwa lengo la kufahamiana na hata kufanya kongamano ili kufahamu changamoto zinazowakabili ndani na nje ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu inafanya nini ili kuibuia vipaji kwa wasichana ambao kwa makusudi wameamua kusomea masomo ya sayansi hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tumekosea wapi kwa nini hadi sasa hatuwezi kutengeneza hata *test tube?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, matumizi ya simu, *internet* na mitandao na haki ya usiri ya mteja.

*Technology* ya kutumia simu, *internet* na mitandao mingine imerahisisha sana mawasiliano kati ya mtu na jamii na Taifa kwa ujumla. Pamoja na kuwa na faida kubwa, matumizi haya yamekuwa yakifanywa kinyume na taratibu kwa sababu zifuatazo:-

(a) Mara kadhaa kumekuwa na mwingiliano wa mazungumzo au ujumbe mfupi na maneno kati ya wateja na kampuni husika. Hii inaondoa hali ya faragha ya mtumiaji wa *technology* hii na mara nyingi mwingiliano huu hutumika kuchafua baadhi ya watu. Ni kwa nini hakuna sheria inayozuia kuingilia haki ya faragha ya mtu? Sheria zinazotumika ni zile nyingine lakini hakuna '*comprehensive law'* ya kuwabana watu wanaongilia faragha za wenzao.

(b) Hivi karibuni kumejitokeza maneno kwamba kuna mtambo ambao umeingizwa toka Marekani ambao una uwezo wa kutumia namba ya simu ya mtu mwingine na kutuma *message* aidha ya matusi au ya vitisho! Je, sheria inasema nini kuhusu jambo hili la kuingilia uhuru wa mtu wa mawasiliano? Serikali inatoa tamko gani kuhusu mtambo huu ambao ni tishio kwa mstakabali wa mawasiliano nchini? Tafadhali naomba majibu na tamko la Serikali kuhusu janga hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, elimu na mafunzo kwa watumishi wa umma na sekta binafsi. Matumizi ya *technology* ya kisasa ya mawasiliano ni mazuri kwani yanarahisisha utendaji kazi katika sekta ya umma na binafsi, uzoefu umeonyesha kwamba hakuna mafunzo ya kutosha kwa watumishi ili kuweza kutumia teknolojia hii ya kisasa. Serikali bado haijaonyesha nia ya dhati ya

kuwafanya watumishi wote nchini waweze kutumia vifaa vya kisayansi mfano *computer* katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa vitendea kazi vyenyewe pia ni tatizo kwa watumishi nchini. Wizara ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha kwamba elimu pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi vinatolewa kwa watumishi wote nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kodi inayotozwa kwa makampuni ya simu. Kumekuwa na udanganyifu wa hali ya juu katika kuonesha mapato yanayopatikana kwa makampuni ya simu na hivyo kushindwa kutoa kodi stahiki kwa Serikali kwa mapato wanayopata. Makampuni ya simu yamekuwa yakichezesha bahati nasibu za aina nyingi na hivyo kuvuna mamilioni ya pesa. Je, Wizara kwa kushirikiana na *TCRA* na *TRA* inatumia mbinu gani kuweza kubaini ni mapato ya kiasi gani makampuni haya huvuna na hivyo kubaini kiasi cha kodi inayotakiwa kulipwa? Naomba majibu kwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *TTCL* na Mkongo wa Taifa, Serikali imeonesha nia thabiti ya kufanya shughuli zote za mawasiliano zinakuwa za kisasa zaidi kwa kuanzisha Mkongo wa Taifa. Lakini cha kusikitisha haijaonesha nia njema ya kuiendeleza kampuni ya *TTCL* ambayo ni ya Serikali na kuwaacha ikiendelea kushindana na makampuni ya kigeni ambayo yamekuwa yakijitangaza sana. Kwa kuwa *TTCL* inapewa ruzuku na Serikali, ni vema sasa isilazimishwe kuchangia 70% kwenye Mkongo wa Taifa kama

makampuni mengine ya kigeni na yenyewe ipewe fursa zaidi ya kuchangia angalau 25% ili iweze kujiendesha kibiashara zaidi. Si busara kumtelekeza mtoto wa kumzaa na kumkumbatia wa jirani. Serikali itumie busara katika kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yetu Jimbo la Handeni ni kuwezesha kuunganishwa na Mkongo wa Mawasiliano hasa ikizingatiwa kuwa baada ya muda si mrefu shughuli za sekta za madini zitashamiri sana. Ipo karibu migodi mitatu ambayo itaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba minara ya simu katika maeneo ya Kata ya Komkonga na Kata ya Ndolwa pamoja na maeneo ya vijijini huhitaji sana huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupate utaratibu wa kuanzisha Radio- Handeni (*local radio*) utaratibu unakuwaje? Nitashukuru kupata majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na

pongezi hizi, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni minara ya simu katika Jimbo la Karagwe. Katika karne ya sasa bado kuna maeneo mbalimbali katika Wilaya (Jimbo) la Karagwe hakuna mawasiliano ya simu za mkononi. Tayari nilishawasilisha maombi tangu mwaka jana kama tulivyoshauriwa na aliyekuwa Naibu Waziri na Wizara hii, Mheshimiwa Kitwanga na pia nimeainisha maeneo haya kwa mara ya pili kama tulivyoelekezwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo husika ni pamoja na Kata ya Nyakakika, Kata ya Nyakabanga, Kata ya Bweranyange yaani vijiji vya Chamuchuzi na Kijumbura. Vilevile kijiji cha Ruhita, Kata ya Rugu, kijiji cha Ihembe Na.2 na Kibogoizi Kata ya Ihembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu uanzishwe mfuko wa mawasiliano nchini, nimekuwa nikiomba *Tele-centres* katika vijiji mbalimbali katika Jimbo la Karagwe, kisingizio imekuwa vijiji hivi havina umeme. Sasa umeme umeshafika, je, ni lini *Tele-centres* hizi zitapelekwa katika vijiji vya Ihembe Na.2, Ihembe Na.1, Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishazi, Kasheshe, Rugu, Bujala, Kahanga, Nyakasimbi, Mishi, Rubale, Ruhita, Kibogoizi, Omurusimbi. Orodha ni ndefu sana na kwa kuwa Serikali imeahidi kupeleka umeme mwaka huu wa fedha Tarafa nzima ya Nyabigyo yenye vijiji vya Kaiho, Kanogo, Chabuhora, Kanywamagana, Kayungu, Nyabweziga, Kakulaijo, Kibondo, Nyakaiga,

Nyabiyonza, Bukangara, Ahakishaka, Chamuchuzi, Kijumbura, Kafunjo, Kamagambo, Nyakagoyagoye, Kiruruma, Biyungu, Rwenkorongo, Ihanda, Rukole, Chonyonyo, Rularo na Nyakahanga, Wizara ipeleke *Tele-Centres* katika vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, gharama za simu za mikononi, pamoja na gharama za simu za mkononi kushuka kidogo, lakini bado gharama za simu ziko juu katika nchi yetu. Nashauri gharama hizi zipungue sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TCRA,* napongeza *TCRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini bado wananchi wengi hawajajua haki zao hasa pale wanapovunjiwa heshima zao na kudhalilishwa. *TCRA* iendelee kutoa habari kwa wananchi kuhusu haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za sekta mbalimbali zinazoongozwa na Wizara hii muhimu. Nampongeza pia Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuungana na Mheshimiwa Profesa Mbarawa kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Dkt. Florence Turuka, Katibu Mkuu na Dkt. Patrick Makungu,

Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Wakurungenzi wa Idara za Wizara na Wenyeviti na Wakurugenzi Wakuu na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Naomba nitamke kuwa naunga mkono hoja hii kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango kwa hotuba ya Waziri, kwanza ni Sera ya Utafiti. Wizara hii kupitia *COSTECH* imepewa dhamana ya kuratibu utafiti kwenye sekta zote nchini. Naomba kujua taratibu au vigezo vinavyotumiwa kugawa fedha za utafiti kwa taasisi na watu mbalimbali wanaojishughulisha na utafiti kwenye fani mbalimbali nchini. Chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuna wakala wa utafiti wa nyumba na vifaa vya ujenzi. Kazi za wakala huyu zinakwamishwa na upungufu wa fedha wanazotengewa kwenye bajeti ya Serikali. Je, wakala huyu anatakiwa kufanya nini ili wapate fedha toka mfuko wa utafiti unaosimamiwa na *COSTECH*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Sera ya Atomiki. Tanzania imejaliwa kuwa na madini mengi ikiwemo ya *uranium* ambayo ni rasilimali muhimu katika utengenezaji wa nguvu za '*nuclear'.* Kwa kuzingatia kuwa Wizara hii kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki ndiyo yenye jukumu la kusimamia utafiti na hatimaye kushauri juu ya uendelezaji wa vyanzo vya atomiki vilivyopo, je, kuna mpango gani wa kujenga ushirikiano baina ya Tume ya Nguvu za Atomi na Wizara ya Nishati na Madini ili kutumia fursa na rasilimali zilizopo nchini kujenga mitambo ya *nuclear* kwa ajili ya kuzalisha umeme ili Taifa liondokane na kero ya upungufu wa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti, sina uhakika kama Tume imewahi kufanya uchunguzi wa usalama w mitambo ya *X-Ra*y inayotumiwa kukagua Waheshimiwa Wabunge kila siku waingiapo kwenye eneo la Bunge. Kama haijafanya hivyo, nashauri kuwa waanze mara moja kwani kupigwa mionzi kila siku kwa miaka mitano ikiwa mitambo hiyo sio salama athari zake zinaweza kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mradi wa anuani na simbo ya Posta. Kwanza, naomba kuipongeza Serikali pamoja na *TCRA* kwa kuanzisha mradi huu muhimu kwa ustawi wa maendeleo ya nchi yetu. Mradi huu ulianza kutekelezwa kwa majaribio mjini Arusha. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huo katika mji wa Arusha unaonekana kusimama kwani inavyoelekea pamoja na ushirikishwaji uliofanywa na *TCRA* kwa uongozi na watendaji wa Manispaa mradi haujawa kipaumbele kwa Halmashauri. Kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huu katika uandaaji wa vitambulisho vya Kitaifa ambavyo ni muhimu sana kwa usalama, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, je, Wizara itasaidiaje kuamsha ari na kuendeleza utekelezaji wa mradi huu kwa wakazi wote wa Arusha wakiwemo wale wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwa kuwa Wilaya hizo mbili hutegemeana kwa shughuli zote za maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, mchakato wa kubadili mfumo wa utangazaji toka analojia kwenda dijitali. Tunatambua jitihada zilizokwishafanywa na Wizara kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo *TCRA* na watoa huduma wote kwa

kupokea na kutekeleza maamuzi ya *ITU* kubadili mfumo wa utangazaji toka analojia kwenda dijitali. Ufuatiliaji niliofanya hususan kwenye Jimbo, umeonesha kuwa wananchi wengi hawana taarifa juu ya mabadiliko yanayoendelea, hawajapata vifaa vya kupokelea matangazo ya *digital* na hivyo tarehe ya mwisho itakapofika wataachwa gizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa ili kuhakikisha kuwa mabadiliko haya yatakuwa ya manufaa kwa Watanzania wote, hatua zifuatazo zichukuliwe. Kwa miezi iliyobaki elimu kwa umma itolewe kupitia redio na *television* zilizo kwenye miji yote nchini. Mashauriano yafanywe na *SADC* na *EAC* ili kuona uwezekano wa kusogeza mbele tarehe ya mwisho ya matumizi ya analojia kwa mwaka mmoja. Waheshimiwa Wabunge, wapewe mafunzo juu ya mabadiliko haya na wawezeshwe waende kuelimisha wapiga kura wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, taasisi ya Nelson Mandela. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ilitoa ardhi kwenye Kata ya Bwawani kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya Nelson Mandela. Je, ni lini ujenzi wa majengo na miundombinu ya Taasisi hiyo itaanza? Kuna eneo la shamba la Tanzania *Plantations* lililoombwa na Taasisi hiyo kwa ajili ya utafiti. Uthamini umekwishafanywa lakini hadi sasa hakuna malipo yaliyofanywa wala kuwepo dalili kuwa yatafanywa. Je, Wizara ina mpango gani kulipa fidia kwa mwenye shamba hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na narudia kusema naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia kuhusu mawasiliano ya simu. Naomba Wizara iweke msukumo wa kutosha eneo hili kwa kuwa ni kichocheo muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi, jamii na siasa pamoja na utawala. Hii ni dunia ya taarifa. Napenda kusisitiza tena, Wilaya mpya ya Uvinza inayo maeneo mengi yenye soko la kutosha lakini hakuna mawasiliano ya simu kwa mfano vijiji vya Kalya, Kashagulu, Mtego, Buhingu, Sigunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mapato ya kampuni za simu. Natambua kuna lengo na hatua katika kutekeleza jambo hili, naomba kutoa msisitizo kuwa kasi ya utekelezaji iongezwe kwa kuwa kuna gharama ya kuchelewa. Mtambo uwezeshe *TCRA* na *TRA* kujua mapato yote yanayofanywa na kampuni za simu katika biashara zote zinazofanywa na kampuni za simu. Lakini zaidi imsaidie mteja kutodhulumiwa muda wa maongezi. Kuna hisia kuwa wateja wa simu wanadhulumiwa muda wa maongezi na hakuna utaratibu wa kudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tafiti za uchumi. Maamuzi na mipango mingi nchini inafanywa bila tafiti, hata Serikali haifahamu mambo mengi kutokana na kutofanya tafiti. Jana Waziri kajibu Serikali haijui kiasi cha vijana wenye ajira na wasio na ajira nchini, isaidieni Serikali kufanya tafiti, bila tafiti hakuna mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nafasi ya sayansi katika uchumi. Nchi yetu ina fursa nyingi lakini hatujielekezi kwenye mahitaji. Wimbi la sasa la Tanzania kuelekea kuwa nchi ya gesi, huku ikiwa nchi ya madini na nafasi kubwa ya kilimo duniani, inapaswa kuwa changamoto kwa Serikali kuwa na mipango maalum kuandaa wataalam wa kutosha katika tafiti, watalaam wenye ujuzi wa sayansi za gesi, watalaam wa kutosha katika sayansi ya madini na watalaam wa kutosha katika sayansi ya kilimo. Vyuo vingi bado vinatoa elimu kwa mazoea. Nashauri taaluma za sayansi, sheria na uchumi katika maeneo ya gesi iwe agenda ya nchi kwa sasa tuepuke kurudia makosa tuliyoyapata kwenye madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, mapato ya kampuni zinazoingiza teknolojia kwa mfano *VISA CARDS.* Makampuni mbalimbali yamekuwa yakiingiza teknolojia mbalimbali katika huduma lakini haijulikani Serikali inapata kodi kiasi gani. Ningependa kujua teknolojia kama za *VISA CARD* ambayo imeletwa na kampuni za nje, je, Serikali ina uwezo wa kiteknolojia kujua mapato ambayo kampuni hizi zinapata ili kuingizwa katika mfumo wa kodi? Ninaamini Wizara hii ikifanya kazi kwa ufanisi, tutaokoa fedha nyingi zitokanazo na teknolojia mpya za makampuni mbalimbali yanayoingia nchini.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ya kusimamia na kuendeleza sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tanzania ni mojawapo ya nchi chache za Afrika ambapo mawasiliano ya simu yamekuwa kwa haraka sana. Nipongeze makampuni mbalimbali ya simu kwa kazi ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na tovuti na mitandao ya *internet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumiaji wa simu na mitambo mbalimbali ya mawasiliano kwa muda mrefu wametaka kujua madhara yatokanayo na matumizi ya vifaaa vya mawasiliano zikiwemo simu, luninga na *computer* kama vifaa vingi vitumiwavyo vilivyo na vinavyowekewa maelezo ya tahadhari, ni kwa nini sasa vifaa hivi muhimu vinarusha mawasiliano mbali hadi haviwekewi maelezo ya tahadhari? Kwa nini wananchi hawaelimishwi madhara ya jumla yatokanayo na utumiaji wa vifaa hivi vya mawasiliano? Wananchi wamebakia tu kusoma magazetini kuelezana wenyewe kwa wenyewe kama vile hamna Wizara na Mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sayansi na teknolojia ni pamoja na vipaji maalum mbali na kisomo cha shahada za juu. Hadi sasa bado mkakati maalum wa kuwatambua wataalam na wanasanyansi hawa wanaogundua vifaa na mitambo mbalimbali na kuwasaidia ili waweze kuendeleza teknolojia waliyoigundua pamoja na hayo kuwasaidia kutunza na kulinda uvumbuzi huo kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati sasa wa kuoanisha uvumbuzi na mahitaji maalum ya mazingira

ya nchi yetu ya maendeleo ya kisayansi na teknolojia. Tukifanya hivi tutapunguza utegemezi wa sayansi na teknolojia kutoka nchi za nje ambazo ni gharama kubwa kuzipata na tunaishia katika kuzitumia (*only in application).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti nyingi za kisayansi zimefanywa na zinaendelea kufanywa, ni muda sasa umefika wa kuchukua tafiti ambazo zitagusa hasa maeneo yetu muhimu ya kiuchumi kama kilimo na hatimaye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taasisi kama ile ya Kijeshi ya Nyumbu pale Kibaha. Uwezo wa Taasisi hii umeendelea kudidimiza na kupitwa na wakati maana hakujawa na mikakati ya kutambua na kuendeleza Taasisi hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itueleze ni kwa kiasi gani Serikali ina mpango wa kuendeleza Taasisi hii ili iweze kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nyingi kwa Waziri na Naibu wake (mdogo wangu January) naomba kusema kuwa naunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono huku naomba Wizara isimamie utatuzi wa kero zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mawasiliano Vijiji vya Segese, Ngongwa na Mwanase katika Jimbo la Msalala. Tatizo la mnara maeneo hayo hasa Kijiji cha Segese chenye wakazi zaidi ya 46,000 ni la muda mrefu na kampuni ya *Airtel* walishaahidi kuweka mnara toka 2008, lakini hakuna utekelezaji. Naomba sasa kwa imani kubwa niliyonayo kwenye timu hii ya Wizara, mnara ujengwe Segese mwaka huu 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya ardhi (ushuru) kwenye Vijiji ilipo minara ya mawasiliano, wananchi wa Bugarama, Kakola, Masabi, Busangi, Ngaya, Chela, Bulige, Kagongwa na Isaka ambapo kampuni za *Airtel* na *Vodacom* zimeweka minara, lakini hayalipi chochote kwa wananchi pamoja na kuahidiwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wananchi wa Vijiji hivyo walipwe haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii ambao kwa namna moja ama nyingine wamewezesha kufanikisha uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kutoa mchango wangu kwa Makampuni ya Simu, pale mteja anapopiga simu au anapopigiwa simu. Mara tu baada ya mteja kuongea na mteja mwingine, basi akipiga tena hapo hapo atajibiwa na mitambo kuwa mteja unayempigia hapatikani kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii huwa inatupa usumbufu mkubwa wateja wa simu kwani muda huo unapojibiwa hivyo wakati mwingine ndipo mteja unakuwa na shida muhimu sana kama kufiwa, kuuguliwa, ajali, na kadhalika na hapo mteja anataka kutoa taarifa kwa ndugu au vyombo muhimu lakini anajibiwa, mteja unayempigia hapatikani kwa sasa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atueleze ni tatizo gani linalosababisha kuwa hivyo na wataliondoaje ili wateja tuondokane na usumbufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni tatizo la makampuni kutoza fedha nyingi pale mteja anapotumia mawasiliano kwa mitandao tofauti; mfano kupiga simu kutoka *Tigo* kwenda *Zantel* na kadhalika. Namwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze ni kwa nini asiyashauri makampuni kukubaliana kwa kuweka kiwango kinachofanana, ili kuwapunguzia gharama kubwa wateja wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano na sayansi na teknolojia ni miongoni mwa maendeleo ya nchi. Ili Tanzania nayo

iendelee na tuwe katika kundi la watu wa ulimwengu, basi na sisi inabidi tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2011/2012, ilikuwa ni Sh. 64,017,516,000/= na ukilinganisha na ya mwaka huu ambayo ni Sh. 70,107,712,000/=. Fedha hii ni ndogo sana ukilinganisha na kazi ambazo zinataka kutekelezwa kwa vitendo japokuwa zimeongezeka kidogo, lakini kutokana na hali halisi ya uchumi hizo Sh. 70,107,712,000/= hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha au Hazina, nao huwa hawatoi fedha yote kwa Wizara; nayo pia ni changamoto ya kusababisha miradi izorote. Wafadhili ni tatizo, wengi huwa hawawajibiki kutoa fedha kwa wakati. Hii husababisha maendeleo ya nchi kuwa nyuma, ni bora fedha inayotoka kwa wafadhili iwe inatoka Serikalini, ili miradi iliyopo ipate kuendelea kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa teknolojia unawapa ajira vijana. Asilimia kubwa ya vijana wamejiajiri wenyewe katika kuuza kadi za simu na laini zake, ili kupunguza wimbi kubwa la vijana kukosa kazi na angalau kusaidia familia na wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna makampuni mengi ya simu Tanzania, lakini pato lao huwa halijulikani na kusababisha kulipa kodi ya chini, ukilinganisha na kampuni nyingine za nje ambazo nchi hizo ni ndogo lakini mapato yao ya kodi ni makubwa. Hii inatokana na ukakamavu wa Serikali na ujazaji wa mikataba kwa kuwabana wenye mashirika na Kampuni. Wawekezaji

ni lazima watoe fedha za kodi za uhakika na pia kuziba mianya ya rushwa kwa asilimia kumi. Serikali ijitahidi kuwabana na hapa ndipo Serikali, itapata kipato cha kuendeleza nchi na pia uchumi wa nchi utapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa uwazi wa makampuni. Kuna makampuni ambayo ni ya kitapeli, hukaa kwa muda wakifanya kazi zao wanapokuwa karibu ya miaka yao kwisha, huhama na kuipisha Kampuni nyingine na kampuni hiyo kulipa kodi ambayo ilistahili. Serikali, kuweni macho na mtindo huu ambao upo kwa baadhi ya Makampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya simu si makubwa ukilinganisha na nchi nyingine mfano Kenya, China na kadhalika. Ukipiga simu kama upo Kenya au China, kama utapiga Tanzania unalipa mara mbili pamoja na yule anayekupigia au kumpigia bado anakatwa. Mfano China, kama unakwenda Mji mwingine, unakatwa mara mbili; hivyo ukilinganisha na huku kwetu bado malipo ni rahisi. Lakini ukilinganisha na maisha yalivyo hapa nchini, wanaomiliki simu ni wengi mpaka vijijini, hivyo wanahisi malipo ni makubwa na watumiaji wengi ni wenye kipato cha chini. Ni vyema Serikali, ikatoa elimu hii kwa kuilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu bado wanawapigia simu wenzao na kuwatukana au kutuma *sms* na unapowapigia wao, utaambiwa simu hii mwenyewe hapatikani; bado wahusika wanashindwa kuzi-*monitor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania, itoe elimu ya kutosha kwa wananchi wake kuhusu kutoka analojia kwenda digitali, ili waweze kujua na kutambua na kujua faida na hasara yake. Gharama ya King'amuzi ni ghali, si rahisi watu wa chini kununua na kumiliki ving'amuzi hivi, hasa inapokuwa kila mwezi ulipie; kama hulipi unakosa kuangalia *TV* na kupata habari. Maisha ya sasa ni kujua taarifa za ndani na nje ya nchi yako, pamoja na ulimwengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hata malipo ya kila mwezi yapungue, ili kila mmoja aweze kumiliki na kupata kuangalia *TV* hasa ukizingatia kuwa watu wanataka ku-*relax na* ku-*refresh mind*.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watumishi wote walioandaa bajeti hii ya Wizara yao. Japo mgawo wao wamepata usioridhisha kutokana na majukumu makubwa waliyo nayo ya kubadilisha nchi iendane na kasi kubwa ya dunia ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya dunia ya sasa inayobadilika kwa kasi kisayansi na teknolojia katika maisha ya watu, Wizara hii ni muhimu kusimamia kasi ya mabadiliko hayo na kuona jinsi ya kuongeza wataalam vijana, wanaoweza kupata elimu ya kutosha kuendesha tafiti za kisayansi na wanaoweza kusimamia maeneo yenye uwekezaji wa kisasa na unaotumia teknolojia ya sasa, kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kufanya mambo yetu kwa vitendo, kusimamia, kuhakikisha kupata vijana wanaopata elimu inayohitajika katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia ni gharama. Hivyo ni lazima tukubali kugharamia changamoto zote zilizotolewa na Wizara hii kwa vitendo. Kupata fedha ndogo za bajeti na kupatikana kwa fedha hizo nje ya wakati, kunadhoofisha juhudi tunazozitarajia zenye matunda za Wizara hii, kupatikana pia kwa wakati au kutokupatikana kabisa kabisa na dunia ikatuacha sisi tukiiangalia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tusomeshe vijana kwa wingi wapate taaluma ya sayansi. Lazima tuwe na miundombinu ya (TEHAMA) itakayosaidia kurahisisha kazi za kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa na tafiti nyingi za madini na imeonekana kuwa na matokeo mazuri ya kuwa na *Urani-Gas* kwa wingi na eneo hili litahitaji Wataalam wa kutosha, vijana watakaoweza kushika nafasi za kukabiliana na teknolojia za sasa zinazotumika katika *operation* za maeneo hayo kiuchimbaji, utunzaji, usafirishaji na matumizi yake.

Hivyo, Serikali ni lazima iwekeze katika kuwasomesha vijana wetu nje wakati tunaendelea kujiimarisha katika kujenga au kukamilisha vizuri vyuo vyetu, kuwa na uwezo na vifaa vya kisasa vya utafiti na kuelimisha vijana wetu ili kupata elimu inayoendana na ushindani uliopo sasa wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imegudulika kuwa na madini mengi ya *Urani*. Nchi yetu tuna tatizo kubwa la kukidhi bajeti zetu na ili kuweza kufikia uwezo mbalimbali ni lazima tutumie rasilimali zetu kutuongezea pato ili tuweze kukidhi haja ya kuiendeleza nchi yetu wenyewe. Hivyo, *Urani* ni moja ya rasilimali hiyo, tunachohitaji tuichimbe kwa uangalifu wa kitaalam chini ya ushirikiano wa Wataalam wa Wizara hii. Tushirikiane kwa karibu kuangalia kazi za uchimbaji na usafirishaji nje zinafanyika kwa mujibu wa viwango vinavyotakiwa na kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiache kuchimba. Wenzetu, wanachimba na wanapata faida inayoendesha nchi zao. Kwa nchi zinazochimba, kama kungekuwa na madhara makubwa tungekuwa tumepata habari. Kwa hali tuliyonayo sasa ya TEHAMA na ilivyo duniani, tumekuwa tukisikia kwa wale wanaotumia na hasa ikiwa kumetokea ajali isiyoepukika kama lilivyotokea tetemeko la Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tusimamie uchimbaji wa *Urani* kwa karibu, tuweze kupata mafanikio ya maendeleo ya wananchi wetu na nchi yetu kwa ujumla.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia siku ya leo. Kwanza nitangulize shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu na pili kwa wananchi wa Babati vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii muhimu inahitaji kupata bajeti ya kutosha na si kupunguza bajeti kila mwaka. Mbaya zaidi, fedha zinazopangwa za maendeleo hazipelekwi zote na zinazopelekwa zinachelewa kupelekwa. Ili tuwe na Wataalam wazuri Serikali, haina budi kutoa bajeti inayokidhi mahitaji. Pia Serikali, iangalie namna ya kuboresha masomo ya sayansi kuanzia shule za msingi na kuhakikisha shule zetu za Sekondari zina Walimu na vifaa vya kutosha kufundishia sayansi. Tunaweza kutumia teknolojia ya mawasiliano kufundisha sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali na kuipongeza kwa kuanzisha Chuo cha Nelson Mandela, ambacho kitakuwa cha mfano Afrika katika Elimu ya Sayansi na Teknolojia. Tunaomba Serikali, iangalie namna ya kutoa fidia ya ardhi kwa mmiliki aliyetoa manufaa ya umma na pia kuangalia namna ya kuomba ardhi ya ziada kwa ajili ya upanuzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, iangalie kwa haraka namna ya kuweka mtambo au chombo cha kudhibiti matumizi ya mawasiliano, ili yasitumike vibaya. Leo hii mitandao ya jamii na mawasiliano ya simu yanatumika kwa anasa na kumomonyoa maadili ya Taifa letu na utamaduni wetu. Watoto wadogo wanaweza kutumia mitandao bila udhibiti wowote na kuleta athari mbaya kimaadili. Hakuna namna ya kudhibiti picha za ngono, muziki na mitindo isiyoendana na mila na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali, iangalie namna ya kupunguza bei ya mawasiliano hasa ya mtandao (*DATA*), ili wanafunzi wetu ngazi zote waweze kutumia mawasiliano ya *DATA* kupata elimu. Pia, sehemu zenye upungufu wa Walimu, kwa kupitia teknolojia ya mawasiliano, wanafunzi walioko katika madarasa mengi na hata shule za mbali wanaweza kupata elimu kwa *video conferencing,* ambako wanaweza kuangalia kwa picha za *video* na pia kuuliza maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali, kuanzisha anwani za makazi kwa kupitia Posta Tanzania. Nashauri sekta hii ifanyiwe kazi mapema, ilete manufaa mengi na kuongeza kasi ya maendeleo. Pia, naiomba Serikali, iangalie katika Wilaya ya Babati, tuwe na minara ya mawasiliano katika sehemu zilizobaki, ili sisi kama Halmashauri pamoja na wadau wa elimu na maendeleo, tunataka kuweka *computers* angalau kila Kata, ili taarifa na maagizo yote ngazi za Kata na Wilaya zitumwe kwa (TEHAMA) kupitia *internet*. Hakuna haja ya viongozi na Watumishi kusafiri kuja Wilayani kila leo, bali wabaki Vijijini na kuendelea kutoa huduma, itapunguza gharama na kuongeza muda wa kazi vijijini na wanaweza kujiendeleza kielimu bila kuhama. Pia, itawezesha wanafunzi wengi kupata elimu kwa njia ya mtandao (*on-line-education).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali, itambue na kuwapa heshima watafiti wetu wanaogundua masuala mbalimbali na pia kuangalia namna ya kuwasaidia kuendeleza utafiti wao. Nashauri bajeti ya *Costech* iongezwe na pia naomba fedha za

maendeleo ziwafikie mapema, ili waweze kutimiza mipango yao mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naishauri Serikali, iangalie namna ya kufikisha mkongo wa Taifa katika vyuo vyetu vikuu, hasa Chuo cha Kilimo cha Sokoine, ambacho hakiwezi kumudu gharama ya kufikisha chuoni kutoka Makao Makuu ya Mkoa. Serikali, iangalie gharama ya mawasiliano, ifanye utafiti nchi nyingine, gharama zetu ni kubwa mno. Pia, Serikali, iangalie namna ya kuboresha *TTCL*, ni Shirika letu na tunategemea huduma kubwa itolewe na *TTCL*, uzalendo wa mali za Watanzania. Pia, Wizara hii iangalie sehemu mbalimbali ambako Wataalam na Watafiti, wanafanya utafiti wa kuboresha teknolojia kuturahisishia kazi zetu kwa kutumia malighafi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, kuwateua Waziri na Naibu Waziri, wenye maono ya mbele, wachapa kazi na wenye uzalendo. Ahsante.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, nchi yetu imefikia hatua nzuri ya msambao wa mawasiliano ya mitandao ya simu, nasikitika kukujulisha kuwa bado Mikoa ya Kusini imeendelea kuachwa nyuma bila ya mitandao hiyo. Ni vyema sasa Wizara, ikayasukuma Makampuni ya Simu kwenda kutoa

huduma hiyo katika Wilaya ya Ruangwa, ambako wananchi wake wana uwezo mzuri wa kiuchumi na wanao uwezo wa kutumia simu kwa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi hayana mtandao. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, kuipa kipaumbele Wilaya hii ili wananchi wanufaike.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia Hotuba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo:-

Watanzania wengi wanaoishi pembezoni hawana elimu ya Digitali pamoja na kuwa tunaingia katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia, hasa katika masuala ya TEKNOHAMA. Ingekuwa bora watu wapate elimu sambamba na uingiaji wa teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanaoishi pembezoni hawana elimu ya kutosha kuhusu mambo ya sayansi na teknolojia. Tukumbuke kuwa, wananchi waliosoma miaka ya nyuma hawana elimu ya sayansi na teknolojia, hawajui kutumia *computer*. Serikali, kupitia Wizara hii, ihakikishe inapeleka elimu ya kutosha vijijini sambamba na uingiaji teknolojia ya digitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama za simu za mkononi. Kumekuwa na gharama kubwa sana za matumizi ya simu za mkononi; gharama hizi zote anabebeshwa mtumiaji wa mwisho hasa ukizingatia

makampuni mengi ya simu za mkononi yamekuwa yakipata nafuu za ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa nini makampuni mengi yanapata unafuu wa kodi, lakini wao wanatoza gharama kubwa kwa watumiaji wa simu za mkononi? Je, Kwa nini, bado kuna gharama kubwa kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine? Je, Serikali, ina mkakati gani maalum wa kuyabana Makampuni haya ya Simu kulipa kodi kwa kadiri wanavyopata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Serikali, imekuwa inaahidi tu gharama za mawasiliano zitashuka, lakini kumekuwa hakuna tofauti yoyote baada na kabla ya Mkongo wa Taifa wa mawasiliano. Je, ni lini gharama za mawasiiano zitashuka kama Serikali, ilivyowaahidi wananchi? Je, Serikali, haioni umuhimu wa kuwatangazia wananchi upunguzaji wa gharama za mkongo wa mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kero za wananchi ambao wanatoa maeneo yao, kwa ajili ya kujengea minara ya simu. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi waliotoa maeneo kujengwa kwa minara ya simu. Malalamiko yao ni kutolipwa kodi ya pango, kama walivyokuwa wamekubaliana toka awali na kusababisha kufanya safari zisizokuwa na lazima za umbali mrefu kwa ajili ya kupeleka madai kinyume na mikataba yao ya awali. Pamoja na hayo vile vile kuna tatizo la walinzi wanaolinda minara hiyo, ambayo ipo pembezoni mwa miji, ambapo hakuna huduma muhimu za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara inawasaidiaje wananchi hawa waliotoa maeneo yao wawe wanapata malipo yao kwa wakati muafaka? Je, Wizara itawasaidiaje walinzi wa minara ambao wapo pembezoni wapate haki zao stahiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya sayansi kwa watoto wa kike. Naipongeza Serikali, kwa kutoa kipaumbele kwa masomo ya sayansi kwa wasichana, lakini bado wanaoitikia wito huo ni idadi ndogo sana na hivyo Serikali, bado haijaweza kuwadhamini wote vyuo vikuu. Je, Serikali, ina mkakati gani wa kuhamasisha zaidi watoto wa kike katika masomo ya sayansi? Je, Serikali, ina utaratibu gani wa kuwadhamini wanafunzi wa kike ambao wamefaulu sayansi, kujiunga na Vyuo Vikuu? Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha shule zote za Sekondari na Vyuo Vikuu wanapatiwa vifaa vya kufundishia vya maabara?

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie bajeti hii kwa njia ya maandishi. Napongeza jitihada za Wizara, kuanzisha Mfuko wa kuhakikisha mitandao inaenea nchi nzima. Pamoja na pongezi hizo, naomba kushauri, maeneo ya visiwani kama Goziba, Bumbiile na Mazinda, Ziwani Victoria yapewe kipaumbele. Hawa watu wametengwa kutokana na hali ngumu ya usafiri wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la ubinafsishaji wa *TTCL* na umiliki wake. Uamuzi wa

Serikali na utekelezaji wake kimsingi haukuleta tija. Kampuni hii imekuwa shamba la kuchuma na kuondoka au ngazi ya kupandia. Ushauri wangu ni kwamba, Kampuni ya *TTCL* iachiwe huru, irudi mikononi mwa umma na iachwe ishindane katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri juu ya haja ya Wizara hii kuwa mstari wa mbele kusimamia matumizi ya TEKNOHAMA mashuleni. Ni kwa Wizara hii kusimamia suala hili la shule, vyuo na hata vijiji vitaweza kupata huduma hii. Si busara kuachia soko kusimamia kuenea kwa TEKNOHAMA. Hivyo, nashauri Serikali, kupitia Wizara hii isimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maoni yangu kama ifuatavyo:-

Wizara hii kwa miaka ya nyuma ilikuwa kwenye Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, lakini ilisambaratishwa. Sasa ushauri wangu, naomba irudishwe ilikokuwa ili kazi zake ziendane na elimu ya juu, maana watafiti wengi wako vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisheria nani mwenye dhamana ya kusema mnara wa simu, redio na *TV* ikae wapi, kati ya *TCRA* na Halmashauri za Wilaya, maana naona kuna mkanganyiko kidogo; je, mnara unatakiwa kuwa umbali gani na makazi ya watu na idadi gani ya watu kwenye miji mikubwa au hata Kijiji? Je, zoezi la kuhamisha minara husika ni kwa watu wa simu na redio na *TV* tu? Maana redio zote

zinalazimishwa kuhamisha minara kutoka katika makazi ya watu bila kupewa muda maalum wa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna leseni ya Mkoa na haifiki sehemu zote na mtu anaruhusiwa kuongeza *site transmission.* Sasa, kwa nini kunakuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kupata leseni kwa vituo vya redio ambavyo vimekuwa vikifanya kazi nzuri na kuhamasisha maendeleo vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makampuni ambayo yameingia Mkataba na baadhi ya Wasanii, kwa ajili ya kutumia milio ya simu ya nyimbo zao, lakini si mikataba mizuri. Je, mikataba hiyo imepitia *TRCA*? Au ni nani wa kudhibiti hilo? Lakini pia, pamoja na mikataba ya Makampuni ya milio ya simu, bado hawawalipi wahusika fedha zao kwa wakati. Naomba sana lifuatiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kukatwa fedha kwenye simu Sh. 400/= mara kwa mara, hasa kwenye mtandao wa *Vodacom*, bila idhini ya mwenye simu. Je, huu si wizi? Kwani wao hudai eti umelipia wimbo uliochaguo wakati hujafanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *message* zinazotangaza biashara kwenye simu baada ya kupiga simu. Kabla hujapokelewa ama kumkosa unayemtafuta, yanaanza matangazo hasa *Airtel* na *Tigo.* Tunaomba waache mara moja, waende

wakatumie *Media*, kutangaza biashara zao ili walipie hayo matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, ijitahidi kupeleka mitandao Singida, kwani kuna maeneo mengi bado ni giza la mawasiliano na watu wana fedha za kutumia mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza *TCRA* kwa kazi nzuri wanayofanya na tuendelee kuwatia moyo wafanye kazi nzuri zaidi, hasa suala la anwani za makazi. Ningeshauri liende pamoja na la vitambulisho, sensa, ili kupata kitu kilichokamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, katika kusimamia maendeleo ya TEHAMA hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi ninayo maoni au maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la mtandao Kijijini Manyoni. Napenda kukumbusha ombi nililowasilisha Wizarani, siku zilizopita kuhusu Kata za Sanza, Iseke na Makonda la kupatiwa minara ya simu, ili waweze kupata mawasiliano ya simu. Makampuni ya *Vodacom, Airtel* na *Tigo* yamefika katika maeneo hayo kufanya utafiti wa soko, hivyo wahimizwe watekeleze.

Aidha, Mfuko wa *UCAF* utazame pia maeneo haya ya Vijijini (Manyoni).

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya TEHAMA kwa umma. Jitahada za kusambaza mtandao kupitia Mfuko wa *UCAF* zinastahili pongezi. Hata hivyo, zianzishwe jitihada kama hizo katika utoaji elimu ya TEHAMA kwa umma kuhusu vijana mashuleni. Mpango huo uwe na lengo la elimu ya TEHAMA, ianze kufundishwa mashuleni kuanzia angalau sekondari, kwa kutumia umeme wa jua. Nchi ya Rwanda, wamepiga hatua katika suala hili. Hivyo, kama Rwanda wamethubutu kwa nini na sisi tusithubutu.?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Makampuni ya Simu katika pato la Taifa. Tunajua kwamba, sekta ya mawasiliano ya simu inachangia asilimia 2.2 katika uchumi wa Taifa, zinasikitisha. Ombi ni kwamba, kwa kuwa, wananchi takribani milioni 23 ni wateja wa mitandao, basi matumizi yao ambayo ndiyo mapato ya Makampuni ni makubwa. Serikali, ijipange kuyafuatilia Makampuni hayo yalipe kodi stahiki. Aidha, bei ya kufunga simu pia zitazamwe kwa lengo la kuzishusha. Tunahitaji wateja wanufaike na wawekezaji nao wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, katika Mji Mdogo wa Kitangari, Wilaya ya Newala. Shirika la Posta, miaka minne iliyopita lilikubali na lilianzisha Ofisi ya Posta. Huduma ya Posta Kitangari,

ni muhimu sana kwa sababu mbili; inahudumia Chuo cha Ualimu, Kitangari; Sekondari mbili; Kituo cha Afya, Kitangari; *Trading Centre;* Kituo cha Polisi; Kituo cha Maji. Mitema; Ofisi ya Tarafa; Mahakama ya Mwanzo na Vijiji 27 vinavyozunguka Mji Mdogo wa Kitangari. Naomba sasa Posta ya Kitangari ipandishwe hadhi ili itoe huduma kama zinazotolewa na Posta kubwa ya Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuwa eneo kubwa la Wilaya ya Newala, linapata mawasiliano ya simu za mkono. Hata hivyo, mawasiliano katika Tarafa ya Mkunya ni hafifu sana. Niliwaomba *Airtel* wajenge mnara katika Tarafa hiyo wakakubali, wakafika Newala na kuchagua eneo la shule ya Sekondari KIUTA, kuwa mahali pa kujenga mnara. Tumesubiri kwa miaka mitano sasa, lakini hawajajenga. Eneo hili liko bonde la Mto Ruvuma, hivyo mawasiliano ni shida. Naomba *Airtel* watekeleze ahadi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Mkoma II, Nambali, Mchole I, Mchole II, Chilangala, Mayombe na Chihangu mawasiliano yake siyo mazuri sana. Wizara izishawishi Kampuni za Simu kupeleka huduma katika Kata hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa na Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa January Makamba kwa kukabiliana na changamoto nyingi zinazoikabili

Wizara. Aidha, napenda kuunga mkono hoja ingawa nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TCRA* ni lazima iwasimamie vizuri *operators* wa simu za viganjani kama *Tigo*, *Zantel*, *Airtel* na *Vodacom*, katika maeneo mawili ambayo, kwanza ni namna wanayochangia kwenye pato la Taifa. Makampuni haya daima wanatoa hesabu zisizo sahihi na hivyo kutoa mchango mdogo kwa pato la Taifa. Ni vyema mpango wa uwekaji mtambo wa kuhakiki mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano ukaharakishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuachane na kauli za "mchakato wa kupatikana kwa mtambo unaendelea", tunataka kasi na viwango katika kuweka mtambo huo, ili Taifa liongeze mapato yake. Tumechoka na *understatements* za hesabu za Makampuni haya ya Simu. Aidha, *TCRA* haioneshi nia ya dhati ya kuwabana *operators* hawa, pale wanapotuma *sms* kwa wateja zisizo muhimu kwao. *Sms* hizo ni kero kubwa na huenda zinagharimiwa na wateja pasipo ridhaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za karibuni, Watanzania wengi wamekuwa wanalalamika kuibiwa taarifa zao mbalimbali, ikiwemo fedha benki. Kutumika kwa taarifa na kuzibadilisha bila ridhaa ya mwenyewe na hivyo kusababisha kuchafuliwa hadhi na majina ya watu. Hali hii inashika sana kasi nchini na njia kubwa ni matumizi ya mitandao ya Kompyuta inayoitwa mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara hii haileti Bungeni Sheria ya kudhibiti vitendo hivi, huku wananchi wakiendelea kuumia? Wakati umefika kwa Serikali, kuleta *Computer Misuse Altitude* Au *Cyber Criminals Act,* ili kudhibiti vitendo vinavyoshika kasi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kupeleka huduma za mawasiliano vijijini hauendi kwa kasi tuliyokuwa tunaitarajia. Utaratibu na mkakati uwekwe, ili Tanzania iboreshe mawasiliano vijijini. Ikumbukwe kuwa, vijijini ndiko kuna idadi kubwa ya Watanzania, lakini wana matatizo mengi kama vile usafiri, matibabu, na kadhalika. Ukiboresha mawasiliano utawakomboa kwani itawasaidia kupata huduma kwa wepesi kwa kupitia simu hizo na hivyo, kupunguza vifo na ugumu wa maisha walio nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali, kuanzisha kwa haraka kwa bajeti ijayo mradi wa *video conference* kwenye ngazi za Wilaya zote nchini. Wilayani ndiko chanzo cha taarifa nyingi za nchi na hata Mkoa utegemee *data* kutoka Mawilayani. Sambamba na hilo, ningependa kuona teknolojia ya kompyuta inafikishwa haraka kwenye shule za vijijini, ili kujenga ubora wa elimu inayoendana na karne ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hoja hii kwa kuunga mkono kwa kuwa imezingatia mahitaji hata ya nchi yetu. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, bado Wizara ina changamoto nyingi ambazo inabidi izifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa mawasiliano katika baadhi ya maeneo yote ya *Delta*, yenye wakazi zaidi ya 35,000 hawana mawasiliano kabisa na endapo wanataka kutumia simu inabidi watembee kwa dakika kadhaa ili wafike mahali penye mtandao, hali hii si nzuri. Ni vizuri kwa Serikali, kwa kutumia Kampuni za Simu hasa *Tigo*, *Airtel* pamoja na *Vodacom*, wanafanya utafiti hasa katika Kijiji cha Ruma huko Delta na kuona uwezekano wa kuweka mnara wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine kwenye Jimbo la kibiti ni Kata yote ya Dimani, Kata ya Mchukwi na maeneo ya Kata ya Mwambao. Kwa kuwapatia mtandao wananchi wa maeneo hayo itasaidia sana kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, Wizara kwa kupitia Taasisi ya Teknolojia, Dar es salaam, walikuwa na mkakati wa kuanza kutumia gesi badala ya petroli kwenye magari. Tangu mkakati huo uwekwe, hadi sasa hakuna taarifa zozote za maendeleo kuhusiana na teknolojia hiyo. Jambo hili tayari lililetwa hapa Bungeni na Wabunge wengi waliorodhesha magari yao yarekebishwe na kutumia gesi. Lakini, hadi sasa hakuna maendeleo yoyote kuhusiana na teknolojia hiyo na hata kwenye hotuba ya Waziri, hakuna hata aya moja inayoelezea kuhusu mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, ieleze wazi kwamba, teknolojia hiyo kwa sasa imefikia wapi? Au ndio kusema ilikuwa kiini macho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MUHAMED OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza naunga mkono hoja. Naishukuru Serikali, kwa hatua nzuri iliyofikia katika sekta hii; ni jambo la kupigiwa mfano, lakini pia naiomba Serikali, ipunguze gharama za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua Watanzania walio wengi ni maskini hususani wa vijijini na Watanzania hao wengi wanatumia mawasiliano hususani simu za mkononi. Wengi wao hawatimizi milo miwili kwa siku, lakini ni lazima huduma hii waipate. Lazima Serikali, iwaangalie Watanzania hawa kwa jicho la huruma katika mitandao yote ya hapa nchini, ili wananchi wote wapewe au wazidi kuwa na imani zaidi ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Makampuni ya Simu za mikononi wanatukera kwa kutupigia simu, tunapopokea wanatuwekea miziki, hususani sisi Waislam katika kipindi kama hiki cha Ramadhani na pia miezi yote wanatukera, hatutaki. Lakini pia waache mara moja kututumia *sms* za ajabu ajabu usiku mkubwa au alfajiri; huu si ustaarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kero kubwa sana hususan watu wa *Zantel*, hivi vitu vinatuchukiza wengi.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie suala hili; namtakia kila la kheri.

**MHE. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kuhusu Wizara hii, katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya Teknolojia ya Utangazaji kutoka Analojia kwenda Digitali. Katika hili napenda Serikali, kabla ya ku-*implement* mabadiliko hayo, kwamba Tanzania, tusiwe dampo kwa bidhaa zisizo na maana tena, elimu ya kutosha itolewe. Nashauri, pamoja na umuhimu wa Digitali katika kuharakisha mambo haraka tu bila kujipanga, ili watu wawe na faida na si hasara. Uwezekano wa ving'amuzi kupatikana kwa bei nafuu kwa wananchi wetu Serikali, iandae mazingira hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu anuani za makazi na simbo za Posta; huu ni mpango muhimu, hasa kwa kurahisisha mawasiliano. Serikali, iwe na mpango mkakati na wa uhakika katika kufanikisha zoezi hili Mijini na Vijijini. Serikali, itenge fedha za kutosha, ili kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe makini katika kuhakikisha Makampuni yote ya simu za mkononi yanalipa kodi stahiki, ili kukuza uchumi wa nchi. *TCRA* iwe makini zaidi, ili kupunguza matumizi mabaya ya simu za mkononi, kubaini na hata kuchukua hatua za kinidhamu kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania lipate kuimarishwa. Maana hili ndilo shirika letu, tofauti na mashirika binafsi. Shirika la Posta huduma yake imedorora; Serikali, iimarishe Ofisi za Posta za Wilaya, huduma ya Posta Karatu ni dhaifu, Serikali itazame kwa jicho la pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwekeze zaidi kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ili kuhakikisha mawasiliano yanamfikia kila Mtanzania kila kona ya nchi hii. Serikali, itumie mashirika ya simu, ili kuchangia Mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa njia ya maandishi. Awali nimshukuru Mungu, kwa kunifikisha leo na kuweza kuchangia hoja hii. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba hii ya Waziri, kuhusu Kampuni za Simu kutuma meseji; hivi sasa Kampuni za Simu zina mtindo wa kutuma meseji mara kwa mara, jambo ambalo linatupotezea wakati sisi wateja wao. Mtindo huu wa meseji za kila wakati unachosha na baadhi ya wakati huwa tunapuuza meseji kwa kufikiria kuwa ni meseji za Kampuni za Simu, kumbe ni meseji ya muhimu sana ambayo inatoka sehemu muhimu kwako. Naomba meseji hizo ziondoshwe, hazina faida kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni za Simu zinashindwa kutofautisha nyimbo, Kaswida na *Quran*, wao wanachanganya tu. Mfano, kama kutakuwa na *Quran* kwenye wito wa simu, basi utasikia msemo unasema kuwa, kama unapenda wimbo huu, bonyeza nyota. *Quran* sio wimbo. Kwa hiyo, kukiwa na tukio la *Quran*, basi kompyuta zao zieleze, kama unapenda sura ya *Quran* hii, bonyeza nyota. Kwenye kaswida za Kiislam, waseme kama unapenda kaswida hii, bonyeza nyota. Kama hilo hawawezi, basi ni bora waache kuweka *Quran* na Kaswida, inakuwa wanaidhalilisha *Quran* kwa kuita nyimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu meseji za vitisho na matusi. Bado meseji za matusi au vitisho zinaendelea kutumwa kwa watu wengi tu, lakini bado hawajaweza kudhibitiwa wale wanaotuma meseji hizo. Huenda ikawa, laini wanazozitumia bado hazijasajiliwa. Kwa hiyo, naomba Wizara walitafutie ufumbuzi na kulidhibiti tatizo hili, ili lisitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mbozi Magharibi baadhi ya maeneo kama vile Tarafa nzima ya Msangano, ambako ndio Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Momba, hakuna kabisa mawasiliano ya simu kupitia mtandao wowote nchini. Hivyo basi, tumekuwa tukiomba sana kuletewa mtandao wowote wa simu ama *Vodacom, Airtel, TTCL,*

*Tigo* au *Zantel*, ili uweze kuwasaidia wananchi wa Wilaya mpya ya Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tunaomba Wizara itueleze ni lini tutapatiwa mnara wa simu ambao utasaidia mawasiliano kwa Watanzania wanaoishi katika Jimbo la Mbozi Magharibi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara kwa Shirika la *TTCL* ambazo zimekuwa zikitajwa kwenye vyombo vya habari kufikia shilingi bilioni mbili. Wizara, itupatie maelezo, hatua zilizochukuliwa na sababu zilizosababisha Shirika hilo la Umma lipate hiyo hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimwa Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri ambayo hata mchango wa bajeti yake unafaa kuigwa na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inafaa kupongezwa, kwani imedhamiria kuleta mapinduzi halisi ya teknolojia hapa nchini. Serikali, imeonesha dhamira yake kwa kutenga fedha nyingi za ndani ili kugharamia shughuli za maendeleo katika Wizara hii na hivyo kupunguza utegemezi wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mpangilio mzuri wa hotuba ya Wizara hii, kwa takribani miaka miwili mfululizo bado Wizara hii imeshindwa kuyasimamia vizuri Makampuni yanayotoa huduma za

Mawasiliano hapa nchini. Hadi sasa mchango wa Makampuni ya Simu mfano, *Airtel (TZ), Vodacom (TZ), Zantel (TZ)* na *Tigo* hauridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara yenyewe katika hotuba yake, ukurasa wa 9-11, imeonesha wazi kwamba, mchango wa Makampuni ya Simu kwenye *GDP* ni mdogo; Je, Serikali, inasubiri nini, mtambo wa *Traffic monitoring system (TMS),* ambao utasaidia kubaini udanganyifu unaofanywa na Makampuni ya Simu kukwepa kutoa taarifa sahihi juu ya mapato wanayokusanya kwa siku, mwezi na hata kwa mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Makampuni haya yameifanya nchi yetu kuwa shamba la bibi kwa kujikusanyia utajiri mkubwa na kuilipa Serikali mapato finyu, namwomba Mheshimiwa Waziri, aliambie Bunge lako Tukufu, mara baada ya kupatikana kwa mtambo wa *TMS* na ukibaini kuwa Makampuni yalikuwa yanaiibia nchi yetu mapato ya Serikali, itayachukulia hatua gani Makampuni haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuleta maendeleo ya sayansi na teknolojia Serikali, haina budi kuunganisha vituo ambavyo kwa tafsiri isiyo rasmi vinaitwa *scientific incubator centres,* yaani vituo ambavyo, watoto wetu wataanza kufunzwa maarifa mbalimbali yahusuyo sayansi, ili baadaye Maarifa hayo wayaendeleze na hatimaye waweze kuvumbua vitu mbalimbali ambavyo vitasaidia Taifa katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mapinduzi ya sayansi katika kilimo, utafiti na vifaa au madawa katika

Hospitali zetu, sekta ya viwanda na hata kuhusu ulinzi wa Taifa letu. Napenda pia niishauri Serikali yetu kwamba, iongeze bajeti yake, ili iwadhamini wanafunzi wa Kitanzania wanaosomea masomo ya sayansi, ili Taifa letu liweze kuwa na wataalam wake wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Wizara, kwa kazi nzuri ikiwa ni pamoja na kuboresha sekta ya mawasiliano na kuwatambua wabunifu au wagunduzi wetu kwa kuwapa tuzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, maendeleo ya sayansi na teknolojia yanatokana na uwepo wa Wanasayansi, Serikali, iendelee kuwahimiza vijana wetu wasome masomo ya sayansi kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia pia kuwapa vivutio. Mwelekeo wa watoto kiubunifu ufuatiliwe tangu wanapokuwa shule za awali na taarifa ziandikwe katika fomu zao za maendeleo, ili vipaji vyao vijulikane mapema na viendelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wagunduzi waliopewa tuzo inaonekana ni wanaume tu; Serikali, iwahimize wanawake kushiriki katika ugunduzi. Iwape maelekezo kuhusu masuala yanayozingatiwa ili mtu atambuliwe kuwa mgunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utandawazi una faida na hasara zake katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kielimu na kiutamaduni. Ni jukumu la Serikali kudhibiti

hasara za utandawazi kwa kuwaelimisha wananchi, hasa vijana pia, kutunga na kurekebisha sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba za simu zipo zinazotofautiana kwa tarakimu moja tu. Suala hili husababisha baadhi ya wananchi kupoteza pesa zao kwa kukosea tarakimu moja tu, pale wanapotuma pesa kwa kutumia *Tigo Pesa, M-Pesa* na *Airtel Money*. Je, wateja wanaotumia huduma hizi wanalindwa vipi? Kwani, hili nililolitaja limetokea mara nyingi na wengi wamekwishapata hasara. Serikali, iweke utaratibu wa kuwalinda wateja wa huduma za kifedha kupitia simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi la kusajili namba za simu, wananchi waliambiwa kwamba, faida mojawapo ni kwamba, simu ikiibiwa ni rahisi kupatikana kwa kupitia *Serial Number* na kwamba, wizi wa simu utapungua au kwisha kabisa. Naomba Serikali, itupe takwimu kama wizi wa simu umepungua au kati ya simu zilizowahi kuibiwa ni asilimia ngapi zimepatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanapohitajika kufanya udahili wa vyuo kupitia mtandao wanapata taabu sana, kwani wapo wengi wanaotokea maeneo ya vijijini ambako hakuna *Internet.* Hii husababisha wengi kupitwa na wakati ilhali wamefaulu; Serikali, imeandaa mazingira gani kuweka usawa? Vile vile majibu huchelewa kutoka kwenye mtandao na pengine majibu hasi kwa aliyefaulu kwa kiwango cha juu na majibu chanya kwa aliyefaulu kwa kiwango cha chini kwa masomo yale yale. Je, ni kweli kwamba mfumo wa uchambuzi ulikosewa? Naomba

Wizara iwape ufafanuzi vijana wetu kupitia Bunge, kwani wanalia kwa kupoteza fedha nyingi bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mufindi Kusini, Vijiji vya Idete, Kwatwanga na Vijiji vingine, vina tatizo kubwa la mtandao. Hakuna kabisa mnara wa Kampuni yoyote, naomba minara ijengwe katika vijiji hivyo nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Gharama za mawasiliano ni kubwa sana, naomba zipunguzwe. Muda wa mawasiliano ni gharama, sababu utaona kwa mfano unajaza vocha ya Sh. 5,000/= utakuta inakwisha hata kabla ya dakika tatu hazijakwisha. Naomba mtu anapojaza vocha lazima ajue muda gani atatumia kulingana na thamani ya fedha ya vocha aliyoweka. Kodi isitozwe kwa vocha.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza Wizara na Mawaziri wa Wizara ya Mawasiliano kwa hotuba nzuri iliyo na matumaini ya maendeleo ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Hivyo, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Manyovu linayo matatizo makubwa sana ya mawasiliano kwa kukosa minara katika Tarafa ya Muyama, yenye Vijiji vilivyo karibu sana vipatavyo 13. Tumeona vimeorodheshwa

kwenye taarifa yenu ya Wizara, lakini ombi langu ni lini mnara utawekwa katika vijiji hivyo kuondoa kero kubwa sana, hasa ukizingatia ni mpakani? Mimi Mbunge nimeambiwa nisifike huko mpaka litatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kuimarishwa kwa mtandao, kwani utakuta mitandao ya simu inakosa mawasiliano *(network),* inajaa na kufanya huduma za kupiga simu na kutuma fedha kwenye baadhi ya simu kutofanyika. Hii imeleta kero kubwa sana kwa huduma hiyo, naomba kero hiyo iondolewe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa utendaji wao. Wizara hii ni nyeti sana kwa uchumi wa Taifa letu. Ni vyema Serikali, ikatenga fedha za kutosha katika eneo hili, ili jambo litendeke kwani, limepita katika hatua muhimu na muhimu zaidi ni uvumbuzi. Uvumbuzi hauwezi kuwepo kwa Wizara ya Sayansi na Teknolojia kuachwa nyuma. Naishauri Serikali, iwekeze zaidi katika eneo hili kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la kuangalia ni eneo la mawasiliano. Mawasiliano ni muhimu sana kwa wananchi nchi nzima, bila kuangalia wapi bora na wapi sio bora. Ni vyema Serikali, ikawa mhimili mkubwa wa mawasiliano kuliko kuachia Mashirika na

Makampuni ya mawasiliano kutawala katika eneo hili. Ni muhimu sana hata kwa eneo la usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana kwa mara nyingine Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kuniletea mawasiliano katika maeneo yafuatayo ambayo yana wakazi wengi wanaotumia simu, lakini hakuna Mnara; mfano, Mpanda *TAZARA,* Kipanga, Kilosa, Mufindi, Chogo, Ilimbo, Wami, Ikweha na Isipii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa bajeti nzuri ya mwaka 2012/2013. Pamoja na mazuri zipo changamoto nyingi katika Wizara ambazo zinatokana na Makampuni ya Simu miongoni mwa changamoto hizo ni wateja kupoteza fedha kwa bahati mbaya na kampuni kukosa suluhisho, huduma za kutuma na kupokea fedha kufanywa katika mazingira ya ovyo kiasi cha kuivunjia heshima fedha ya Tanzania, kutuma meseji zisizo na umuhimu kwa wateja na kuwakata fedha bila sababu hasa Tigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wateja wanapoingiza salio na kwa bahati mbaya akakosa tarakimu moja tu fedha hiyo hairudi na *Tigo* wanasema hawana njia ya kukusaidia japo wanaona akaunti uliyoingiza imefungiwa na haitumiki. Huu ni wizi wa macho macho

mbona fedha zikienda kwa mteja mwingine kama hazijatumika zinarudishwa kwa mhusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kutuma na kupokea fedha zinafanywa kwenye meza na mwavuli na mtu anayetambuliwa na *Tigo* na *Vodacom* tu, lakini hana makazi maalum yaani ofisi. Ushauri wangu ni kuwa, punguzeni wateja wekeni wenye uwezo wa kuhudumia vizuri na ofisi zenye hadhi na heshima ya fedha ya Tanzania. Pia wapewe faida nzuri, vijana wengi wanafanya kazi hizi lakini mzunguko ndiyo unaotoa faida na faida ni ndogo sana na hawana hata bima ya kuhifadhi na kulinda fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia ya Makampuni ya Simu ya kutumia meseji mteja au kuweka nyimbo ambazo mteja hajaziomba na kumkata fedha, hii ni dhambi na kinyume na makusudio ya mteja. Ushauri wangu ni kuwa, tubadili mwenendo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba ushauri wangu uzingatiwe. Ahsante sana.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano na teknolojia ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi, naipongeza Serikali kwa kuridhia kuwa na mitandao ya simu za mkononi. Mitandao hii michache Serikali itafutie wawekezaji zaidi katika *sector* hii ili ushindani uwe mkubwa na hatimaye bei za *airtime* zitapungua (mfano, UK - makampuni yanashindana na bei ya mawasiliano *prepaid /post paid* zinakuwa nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifuatilie namna ya operesheni ya Kampuni za *Vodacom, Airter, Tigo.* Wakati mwingine wanapeleka ujumbe kwa mteja ya kuwa una sekunde 50 za kupiga simu mtandao wowote mpaka tarehe fulani. Ujumbe huu mara nyingi ni wa upotoshaji kwa sababu muda uliotolewa siyo wa kweli ya kuwa simu ukipiga hakutakuwa na *charge,* wanadanganya wananchi, nashauri Serikali ifuatilie kulinda haki ya wananchi. Mitandao isidanganye waseme ofa za kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingine *Vodacom* wanatoa kama *notice* kuwa mlio wako wa *swaga* ume-*expire* hivyo unataka kuwa *renewed.* Ingawa mwananchi anakuwa haja-*sign* au kukubaliana na huo mlio, lakini fedha inakatwa kutoka katika akaunti ya mwananchi huyu. Ofa nyingi zinatolewa usiku sana wakati wananchi wanakuwa wamelala kuanzia saa nne usiku mpaka saa 12 asubuhi, kwa nini ofa hizo zisitolewe mchana, ambapo wananchi wanahitaji kuwasiliana au huu ni udanganyifu kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kupiga simu toka *Vodacom* kwenda *Tigo* au *Airtel* ni kubwa sana, nashauri Serikali *irregulate* bei za mitandao hii ili mawasiliano yawe nafuu kwa mwananchi wa kawaida. Ipo minara imewekwa katika maeneo ya vijiji, wananchi wenye viwanja vyao taasisi na kadhalika, pango linalilipwa la dola 400 – 600 kila mwezi na dola 600 – 700 kwa maeneo ya mjini ni kidogo ikilinganishwa na umuhimu wa minara hiyo. Wenye minara (*Vodacom*) wanawapunja wenye maeneo kwa

kulazimisha kulipa pango kwa kutumia shilingi ya Tanzania na bila kujali *exchange rate* ya dola (*USD*) ya siku hiyo na hivyo kusababisha manung'uniko kwa wananchi, vijiji au taasisi wanakoweka minara. Nashauri Serikali itoe agizo kwa *Vodacom* kulipa haki za Watanzania wanazopunjwa na wapewe agizo walipe pango hata kama ni kwa shilingi ya Tanzania, lakini kwa *current excharge rate* iliyopo siku ya malipo.

Katika mradi wa utambulisho, anuani za makazi ni muhimu *TCRA* imesema imeweka *postal codes na address* za makazi, lakini hazionekani, zimewekwa maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkongo wa Taifa ulipowekwa wananchi walielezwa utarahisisha na kupunguza gharama za mawasiliano eneo moja tulilotarajia ni minara ipungue. Nchi nyingi Afrika na Ulaya minara haijaezekwa kiasi kikubwa, sasa hivi nchi imekuwa nchi ya minara. Serikali ina mkakati gani kuona kuwa mitandao haitumii minara na badala yake wanatumia teknolojia mbadala isiyoeneza minara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuweka Chuo cha Teknolojia Arusha – Nelson Mandela, hakika chuo hiki kitakuwa ngazi na daraja la kuunganisha taasisi zetu Tanzania kwa kuwatumia wataalam watakao-*graduate* kutoka chuo hicho, badala ya kutumia wataalam wa nje, chuo hiki vema pia kichukue wanafunzi kutoka nchi za Afrika Mashariki na kwingineko. Chuo kijitangaze kupata wanafunzi kutoka nchi nyingine pia.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja, sababu Wizara imejaa ahadi zisizotekelezeka kwa kuahidi Wabunge kuwa muda siyo mrefu watapata mawasiliano katika maeneo yasiyokuwa na mawasiliano na Wabunge wanawaahidi wananchi kadiri wanavyoelezwa na kudanganywa na Wizara jambo ambalo limeanza kuleta hali ya sintofahamu baina ya Wabunge na wananchi.

Wizara imeshindwa kupeleka mawasiliano ya simu za mkononi ukanda wote wa mwambao mwa Ziwa Tanganyika hasa Kusini mwa Jimbo la Nkasi Kusini, wananchi wananyang'anywa kila siku mali zao zikiwemo vifaa vya uvuvi na fedha. Wizara haijabaini na kuona ukweli kuwa mawasiliano ya simu katika maeneo yasiyofikika yangeweza kuwapa faraja na kuokoa maisha ya akina Mama na Watoto ambao kwa kutumia mawasiliano ya simu wangeweza kutoa taarifa za dharura ili kujaribu kuokoa wananchi hawa Kata za Wampembe na Ninde, Jimbo la Nkasi Kusini kwao simu za mkononi ni msamiati mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa kila siku ikiwaeleza Wabunge waorodheshe maeneo yasiyofikika kimawasiliano ili wapitishe bajeti zao nisipopata uhakika wa kupata mawasiliano ya simu katika Jimbo langu. Nitatoa shilingi Mfuko wa *UCAF* usitumike kwa upendeleo kwa kuanza kuorodhesha vijiji kwa viongozi. Hiyo siyo sawa, jambo ambalo lilishuhudiwa katika orodha iliyokuwa imeandaliwa, mfano vijiji vya Mpanda na vingi vikiwakilisha Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona kazi iliyofanyika ya kunishawishi kuunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni lini minara ya simu na mawasiliano ya simu za mkononi yatapatikana katika vijiji vifuatavyo:-

Tarafa ya Ismani; saka, Nyakarangala, Makadupa, Mkulula, Usolanga, Iguluba, Igula, Ngomo, Mangawe, Mawindi, Mikongwi, Izazi, Mnadani, Ismani Tarafani, Ismani Sekondari, Isimani Mission na Makuka.

Tarafa ya Idodi, Vijiji vya Idodi, Maluninga, Kitisi, Tarafa ya Pawaga, Vijiji vya Kisanga, Isele, Kinyike, Luganga na Mkombilenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa masikitiko yangu makubwa kwa Waziri kwani nilimwandikia barua juu ya tatizo la kukosekana kwa mawasiliano ya simu za mkononi katika Kata na Vijiji vifuatavyo:-

Kata ya Milepa, Vijiji vya Milepa, Kisa na Msia, Kata ya Kaoze; Vijiji vya Kiandi, Igoda, Tululu na Chombe. Kata ya Mfinga; Vijiji vya Kisekela, Mfinga, Mtapenda, Nkwilo na Msila. Majibu yake ilikuwa mwaka jana awe ameshatekeleza tatizo hilo, cha ajabu hadi leo hii hakuna kinachoendelea. Naomba majibu.

Waziri naomba ajue kuwa maeneo haya mara kwa mara huwa kunakuwa na uvamizi wa majambazi, wananchi wanakosa mawasiliano ili kutoa taarifa za haraka katika vyombo vya dola. Hivi Waziri anataka niseme nini ndiyo anielewe, kila siku ni kuorodhesha vijiji, vitendo hatuvioni, naomba Waziri atoe maelezo ili wananchi wa Jimbo la Kwela wakusikie wewe mwenyewe, kwa kauli yako kuliko mimi kuendelea kupata lawama na wananchi kushindwa kunielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuridhika na maelezo yako, nitaunga mkono hoja.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Pia naomba nitoe pongezi kwa Waziri, Naibu wake na watendaji kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa msisitizo kwenye maeneo yafuatayo:-

Mawasiliano ya simu ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya Mtanzania wa leo. Hata hivyo, bado mtandao wa mawasiliano haujafika katika sehemu kubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni gharama kubwa za mawasiliano ya simu. Hatua za haraka na za lazima zichukuliwe ili gharama za mawasiliano ziweze kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linaathiri matumizi ya simu ni matumizi mabaya ya simu

kwa utumiaji wa lugha za matusi au kutishiana maisha. Ipo haja ya kuongeza udhibiti wa matumizi mabaya ya simu ili iwe rahisi kuwapata *offenders* kirahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *cyber crime*, matumizi ya TEHAMA yameleta maendeleo, lakini pia imetoa nafasi ya uhalifu kufanyika kwa haraka na kwa wingi. Nashauri kwamba *Cyber Crime Law* na *Regulations* ziandaliwe kupunguza tatizo hili. Aidha, *gudgets'* zinatumika hasa kwenye *ATM* na mashine nyingine ziwekewe *security features* ili kuongeza usalama.

Elimu ya sayansi ili Taifa linufaike na maendeleo ya teknolojia, ni lazima liwaandae watoto wa Tanzania kushiriki kikamilifu hili litatimia tu iwapo elimu inayotolewa kwenye shule kuanzia za msingi zifikie kwenye weledi wa sayansi. Hivi sasa vijana wetu wanashindwa vibaya kwenye masomo ya sayansi, Serikali lazima iandae mkakati wa kuinua matumizi ya elimu ya sayansi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *E-Government,* kuna haja ya kufanya maandalizi ya haraka ili tuiendeshe Serikali kwa mtandao. Jambo hili litaongeza ufanisi katika nyanja tofauti na kuongeza uzalishaji na utoaji wa huduma.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye mwelekeo wa maendeleo. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la uhalifu kupitia mtandao ikiwa ni pamoja na wizi wa fedha kutoka mabenki hapa nchini na wizi huu

umehusisha wageni kutoka nchi za nje. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na changamoto hii

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni ya Simu nchini hayalipi kodi stahiki kutokana na ukweli kwamba makampuni hayo hayatoi taarifa sahihi ya faida wanayopata. Naipongeza Wizara kwa mpango wa kuanzisha mtambo wa *traffic monitoring system* kwa madhumuni hayo pamoja na mambo mengine, hata hivyo kwanini Serikali iingie gharama zote hizo badala ya Makampuni hayo ya Simu kuhitajika kujiandikisha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)*, hatua ambayo itaiwezesha Serikali kufahamu faida halisi ya Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha makampuni haya yanafanya biashara ya kutuma fedha (M-pesa, *Tigo* pesa na kadhalika), lakini Serikali haifahamu faida kubwa ipatikanayo kwenye makampuni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ilifanyie kazi suala hili.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa mawasiliano, sayansi na teknolojia. Naomba nianze kwa kuchangia suala la mawasiliano. Kumekuwa na makampuni mengi ya simu ambayo kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakijenga minara kwenye maeneo tofauti ya Serikali na ya watu binafsi. Kinachonishangaza malipo wanayoyafanya kwa wenye maeneo haya yanakuwa yanatofautiana kwa kiasi kikubwa na kwa hakika hawawatendei haki wenye maeneo haya kutokana na kiwango kidogo

cha fedha wanachowalipa. Naishauri Wizara iliangalie hili kwa umakini na kiwango cha ulipaji kiwe kinafanana kwa Mijini, Vijiji na Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo linanipa shida ni suala la ushuru wa makampuni haya, ni kwa nini Makampuni ya Simu hayalipi ushuru kwenye Halmashauri zetu? Wizara haizitendei haki Halmashauri kwa kuwa watazamaji tu wa minara hiyo bila wao kufaidika hata shilingi moja tu. Naishauri Wizara iangalie upya utaratibu huu mbovu ambao kwa hakika Halmashauri zinakosa mapato yake, ni vyema Halmashauri zipewe angalau asilimia kidogo ya mapato yanayotokana na minara ya simu, ukizingatia hata huduma za kijamii wanatoa zaidi maeneo ya mijini, hebu waangalie na maeneo ya vijijini ili waweze kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja lakini pia suala la *line* za simu kuuzwa kama karanga usitishwe kwani linasababisha mtu kununua *line* kwa ajili ya kumtukana mtu na anapomaliza nia yake anaitupa *line* hiyo. Naomba tuige nchi nyingine kupata *line* ya simu ni shughuli kubwa.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza mchango wangu katika sekta ya mawasiliano ya simu nchini, sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, nayapongeza Makampuni ya Simu ambayo yamekuwa yakitoa huduma hizi na kuongeza wigo wa mawasiliano mpaka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi napenda kutoa rai kwa makampuni haya ambayo yamesambaza minara kila kona, kila kijiji ili wananchi wapate mawasiliano. Tatizo si kuweka minara, tatizo ni kwamba maeneo ambayo yanawekwa minara hiyo wanalipia inavyopaswa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi baadhi ya maeneo ambayo makampuni haya yameweka minara hayalipiwi yaani hayawalipi wenye maeneo. Maeneo haya mengi ni ya vijijini, makampuni haya yamekuwa yakiingia mkataba na wananchi na kutowalipa kodi. Eneo la Kata ya Maganzo, Wilaya ya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga kuna mzee mmoja ambaye alitoa eneo lake kukawekwa mnara wa kampuni ya *ZANTEL,* tokea mnara huo uwekwe mpaka leo mzee huyo hajapewa hata shilingi moja, watendaji wa kampuni wamekuwa wakimsumbua malipo yake na mkataba alishasaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haya Makampuni yamekuja kudhulumu wananchi? Naomba suala hili lichunguzwe kwani lazima siyo eneo hilo tu inawezekana tatizo hili likawa maeneo mengi. Wananchi wamekuwa wakinyimwa haki zao bila Serikali yao kujua, miongoni mwa wachangiaji wa dhuluma hizi ni viongozi wa maeneo husika, mawasiliano ni kitu muhimu kama nilivyozungumzia mwanzoni mwa mchango, lakini kumekuwa na wimbi la minara katika maeneo ya nchi yetu kila Kijiji, Kata, Wilaya, Mikoa ni minara kwa minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haya makampuni hayawezi kutumia mnara mmoja kwa kila eneo? Utitiri

huu wa minara ungepunguza hata gharama za uendeshaji kwani wangeweza kutumia mnara mmoja wakaweka hizi *buster* zao kwenye mnara mmoja wote, hata gharama za mafuta wangeweza kuchangia katika mnara mmoja, Serikali inasema nini kuhusu jambo hili? Yakitokea makampuni mengine kama kumi mapya nchi hii itajaa minara kila eneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka huu Serikali imeipunguzia fedha Wizara hii kwa ajili ya maendeleo tofauti na fedha iliyotengwa mwaka jana yaani 2011/2012. Kimsingi Serikali imeonesha ni jinsi gani haioni umuhimu wa kuwekeza kuendeleza na kukuza teknolojia katika nchi yetu. Ningependa kupata majibu kwa nini Serikali imepunguza kiasi hicho cha fedha ambazo ni takribani sh. 385,832,000/=?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea kwenye digitali kutoka analojia, je, ni kwa kiasi gani wananchi wanaelimishwa kuhusu ujio wa mfumo huu mpya? Kwani bado wananchi wana maswali mengi juu ya hili, wengine wakidai luninga zao zitakuwa hazifai tena. Naomba Wizara iandae utaratibu ambao kila mwananchi ajue umuhimu wa mfumo huo wa dijitali na umuhimu wake na nini wanatakiwa wafanye kama wananchi wa kawaida na hasa walioko pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongezeka kwa watumiaji wa luninga Serikali iangalie ni jinsi gani itawasaidia wananchi wake kutoka katika mfumo wa analojia kwenda mfumo wa dijitali. Kuna watumiaji takribani 23 milioni ambao ni karibu ya nusu ya Watanzania wanamiliki simu lakini pato la Taifa kutoka

katika makampuni haya ambayo ni takribani yanachangia kiasi cha asilimia 2.2 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato hili ni dogo sana ukilinganisha na mapato ya nchi tofauti ambazo nazo watumiaji wake wa simu ni karibu nusu ya *population* yao, naiomba Serikali iangalie upya viwango vya kodi katika makampuni haya kwani inawezekana kabisa kuna mianya ya ukwepaji kodi, hivyo, kulikosesha Taifa mapato sitahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishia hapa huku nikisubiri majibu ya Serikali.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *commitment* ya Waziri kuwa ni lini italetwa Sheria ya kuthibiti gharama za mawasiliano kupitia mitandao ya simu kwa kuwa fedha wanazokata kwa ajili ya mawasiliano ni kubwa mno ukilinganisha na hali ya kiuchumi ya Watanzania. Utabiri wa hali ya hewa ni vyema sasa kama nchi tuweze kufuatilia mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaweza kusababisha madhara makubwa kama yale yanayotokea baharini na nchi kavu, hivyo kuzuia vyombo vya majini visiruhusiwe kuondoka kwa kuwa vitasababisha ajali na hivyo kuleta maafa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya ving'amuzi, kwa kuwa Serikali imeondoa kodi ya ving'amuzi kwa wafanyabiashara sasa ni kwa nini bei ya ununuzi kwa wananchi wa kawaida isishuke.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa mfumo wa makazi na simbo za posta ambao unatoa fursa kwa kila mkazi wa Tanzania kuwa na anuani kamili ambayo itaweza kumtambulisha vema zaidi kuliko ilivyo sasa ambapo wengi wetu tunatumia masanduku ya posta ambayo kimsingi ni machache sana hapa nchini. Ningependa kujua utekelezaji huo utamalizika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa video *conferencing* ni wa muhimu sana hasa kwa wakati kama huu ambapo kuna msongamano mkubwa wa magari jambo ambalo linachangia kuzorotesha utendaji kazi wa idara mbalimbali za Serikali. Wizara na Serikali iharakishe kwa kutenga fedha ya kutosha kukamilisha mradi huo ambao utasaidia sana katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu Serikalini kwa kupunguza gharama na muda unaotumika katika mawasiliano na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Wizara hii imeelezea kuhusu ving'amuzi kuondolewa kodi, unafuu huu kwa kiwango kikubwa ni kwa wafanyabiashara wa ving'amuzi tu. Bado wananchi walio wengi wana kipato kidogo na bei ya ving'amuzi bado ni kubwa, utaratibu wa ving'amuzi vitatu ni kujaza maboksi katika nyumba na ni gharama, kwa nini

isiwe king'amuzi kimoja ili kupunguza gharama lakini kipate chaneli zote?

Wakati Tanzania tunapata Uhuru mwaka 1961, nchi kama Malaysia na Singapore hazikuwa na tofauti sana kiuchumi na nchi yetu. Lakini sasa wametuacha mbali sana, tujiulize wao wamefanikiwaje? Tujifunze kutoka kwa wenzetu ili na sisi tuweze kupiga hatua katika maendeleo ya sayansi na teknolojia. Tuangalie pia bajeti inayotengwa kwa Wizara hii muhimu, mwaka uliopita bajeti iliyotengwa ilikuwa bilioni 64 na hadi sasa ni 23% ndiyo fedha iliyotolewa kwa Wizara hii kwa ajili ya maendeleo, pengine ndiyo maana Wizara hii inashindwa kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Serikali wa kuwa na Wizara nyingi inaweza kuwa ni sababu kubwa na kushindwa kwa Serikali kuzitengea Wizara fedha za kutosha, kiwango kinachotengwa kwa Wizara hii hakitoshi kabisa. Ni lazima tujiulize tunawezaje kupiga hatua katika teknolojia kama Malaysia au Singapore? Bajeti itengwe ya kutosha, kujenga uwezo wa vijana katika teknolojia. Kwani Wizara hii inaweza kabisa kuendeleza uchumi wetu, jambo ambalo kwa sasa hivi halifanyiki.

Sekta ya simu haitoi mchango wa kutosha katika maendeleo kwa kutoa mchango wake wa mapato kwa nchi yetu. Wananchi wanalalamika kwamba gharama bado zinawaumiza kutokana na vipato vyao kuwa chini. Mwananchi wa kawaida hawezi kumudu, hakuna uwiano wa Kampuni za Simu kati ya kodi wanayolipa na faida wanayoipata. Sekta hii haijatoa

mchango wa kutosha katika kutoa ajira kwa vijana na pia katika kuchangia ukuaji wa uchumi wetu; kukosekana kwa uwazi, hatujui makampuni yanaingiza faida gani na uhalisia wa kodi haujulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* siku za nyuma ilikuja na utaratibu wa kusajili simu zote nchini kwa maelezo kwamba ingesaidia kubaini uovu na matumizi mabaya ya simu, ningependa kuuliza wamefanikiwa kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wafanyabiashara kusikia kwamba Tanzania itaondoka kutoka mfumo wa analojia na kwenda digitali ifikapo Desemba 31, 2012 kumekuwepo na wimbi kubwa hivi sasa la uingizaji wa vifaa vya analojia jambo ambalo matokeo yake ni nchi yetu kuwa dampo na hivyo baadaye kuwa na uchafuzi wa mazingira. Je, Serikali inakabilianaje na tatizo hili la nchi yetu kuwa dampo la vifaa vya analojia?

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii ya kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ili niweze kutoa mchango katika Wizara hii. Sambamba na shukurani hizo naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Yusufu Makamba, Naibu Waziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kazi yao nzuri ya kukuza matumizi ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano katika maeneo kadhaa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunakuwako na uhalifu mkubwa kupitia mitandao, watu wengi wanaibiwa fedha zao, wananchi wanapata adha kubwa. Je, Serikali inajipanga vipi kukomesha uhalifu huo? Pamoja na kwamba mtandao ni mzuri kwa maendeleo ya Taifa, lakini kuna watu wengine wanatumia mtandao kuwachafua wengine (*facebook*), je, ni vipi uhalifu utakomeshwa na ikiwezekana kuwagundua? Mitambo ya simu imejengwa mingi sana katika nchi hii, mingine imejengwa mbali na makazi ya watu, lakini mingine imejengwa karibu na makazi ya watu. Je, hayana madhara yoyote kwa binadamu kwa maana ya mionzi na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa na dunia kwa ujumla tupo katika teknolojia hii mpya. Je, Serikali imejipanga vipi katika kufanya utafiti ili kama kuna madhara yoyote kwa mtumiaji na kuweka usalama katika matumizi ya ujumla ya teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI KHAMISI SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la kupatikana kwa nishati mbadala ya kupikia badala ya kuni na mkaa. Kwa kutegemea kuni na mkaa kwa kupikia nchi yetu inaendelea kuwa jangwa kwa ukataji mkubwa wa miti. Ili nchi yetu iwe salama ni lazima wapate nishati

mbadala ya kupikia. Ni Wizara hii ndiyo inayohusika kufanya utafiti kisayansi wa nishati mbadala ya kupikia.

Tume ya utafiti wa kisayansi *COSTECH* wamefikia hatua gani kiutafiti katika kupata nishati mbadala ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mkongo wa Taifa umo katika kusambazwa hapa nchini na sehemu nyingi zimeanza kuwa na mkongo huo. Inavyodaiwa mkongo huo mawasiliano ya simu yatakuwa bei afadhali, ni kwa nini hata ishara haionekani kuwa bei zitapungua kwani baadhi ya maeneo tayari mkongo wa Taifa umeshafika, au tuseme bei zitapungua iwapo mkongo huo uwe umeshaenea nchi nzima? Ni lini pia mkongo huo utaenea nchi nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa masomo ya sayansi katika shule zetu yako chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini katika masomo hayo ya sayansi wanafunzi wetu ufaulu wao umekuwa ni mbaya. Je, Wizara hii imeliona tatizo hilo na inaelewa kwa nini wanafunzi wetu matokeo ya mitihani yao kwa masomo ya sayansi yako hivyo? Je, Wizara hii imewahi kutoa ushauri kwa Wizara husika ili wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri katika masomo ya sayansi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Wizara ukurasa wa 19, kifungu cha 23, kinaelezea uwepo wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta *(EPOCA)* ya mwaka 2010. Kikawaida sheria yoyote haiwezi kufanya kazi ipasavyo kama hakuna kanuni na

ndiyo maana hivi sasa Waziri anataka kutunga kanuni za sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezekano au uzoefu uliopo wa utungaji wa kanuni huchukua muda mrefu wakati tumebakiwa na miezi karibu sita ili nchi iingie katika matumizi ya digitali kutoka analojia ikiwa hakuna kanuni za sheria inayohusiana na mawasiliano ya kidigitali, je, kweli nchi yetu ifikapo Disemba, 2012 itaweza kuingia kwenye mfumo wa digitali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri, una dakika 30 na mtoa hoja atakuwa na dakika 40.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa uliyonipa na mimi kuchangia hoja hii ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Nianze kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na baraka zake zote, nawashukuru wazazi wangu kwa malezi, makuzi, masomo na familia yangu kwa upendo na uvumilivu; watoto wangu wawili kwa kunipa sababu ya kuamka kila siku asubuhi. Namshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunipa fursa ya ziada ya kuitumikia nchi yangu na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa Bumbuli kwa kuniamini niwe sauti yao na mwakilishi wao. Nawashukuru kwa kuniinua hadi ulimwengu ukaniona. Kwa imani hiyo, sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru hasa Wabunge wote wa Vyama vyote kwa ushirikiano, urafiki na udugu ambao mmeuonyesha na kwa kweli kila Mbunge ninayekutana naye anakuwa ni sawa na ndugu yangu bila kujali Chama cha Siasa. Nawashukuru kwa upendo na ushirikiano ambao mmenionyesha tangu nikiwa Mwenyekiti wa Nishati na Madini hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa kwa ushirikiano na mwongozo anaonipa katika kutimiza majukumu yetu ya Wizara. Nawashukuru pia watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Florence Turuka, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Patrick Makungu, Wakuu wa Idara, Eng. Clarence, Dkt. Yona, Prof. Mbede, Bi. Mazoea na timu yao nzima kwa kunipokea vizuri Wizarani na kunipa ushirikiano mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namshukuru Mheshimiwa Spika, wewe pamoja na Wenyeviti wa Bunge. Nawapongeza kwa namna ambavyo mmekuwa mnaliongoza Bunge letu na ninawashukuru kwa ushirikiano ambao mmenipa. Vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa uongozi wake mahiri Bungeni na nje ya Bunge. Vilevile na mimi naomba niongeze sauti yangu na majonzi kwa ajali iliyotokea

Zanzibar ambayo tumewapoteza ndugu zetu, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kujibu hoja mbalimbali zilizochangiwa na Wabunge wakati wa kujadili hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia ni wengi, Mheshimiwa Waziri atawataja kwa majina, na kwa muda tulionao hatutaweza kutoa majibu yote. Kwa hiyo, majibu mengine tutawaletea kwa maandishi katika siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na mchango alioutoa Ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe kuhusu kampuni ya *On Mobile* na haki za wasanii. Kulikuwa na mambo mawili. La kwanza, kwamba kuna kampuni ambayo inafanya biashara hapa nchini bila leseni na la tatu ni gawio dogo wanalopata wasanii kutokana na kazi zao. Lakini la ujumla ni namna na utaratibu mzima wa kusambaza kazi za wasanii na mapendekezo kwamba tutumie Posta.

Sasa kwenye hili la kwanza, ni kweli kuna kampuni inaitwa *On Mobile* ambayo ipo nchini na inafanya kazi na imeshirikiana na Makampuni ya *Vodacom* na *Airtel.* Kampuni hii iliomba leseni *TCRA* tarehe 29 Februari, 2012. Utoaji leseni ni mchakato kwamba unapoomba leseni *TCRA* inapitia maombi ya leseni na inakuandikia na kukueleza upungufu uliopo kwenye maombi yako. Kwa hiyo, waliandikiwa barua tarehe 12 Julai, 2012

wakaambiwa upungufu uliopo kwenye maombi ya leseni.

Baadhi ya upungufu ni kwamba, hawakujiandikisha, kwani ni lazima wawe wamesajiliwa hapa nchini wawe na leseni ya biashara ambayo inatolewa na *BRELA,* lakini vilevile ni lazima walete mchanganuo wa kibiashara ili kuonyesha biashara hiyo wanayotaka kuifanya inawezekana kifedha na kibiashara. Lakini katika mazungumzo ilibainikaka kwamba tayari Kampuni hiyo inafanya kazi nchini na inatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, *TCRA* wakawaandikia kampuni hiyo, yaani wakaagizwa kwamba wasitishe kutoa huduma nchini, wafanye biashara. Kwa hiyo, majibu yetu ni kwamba hata kabla gazeti halijaandika hii habari, tayari Serikali ilishachukua hatua kwa kuisimamisha kazi hii kampuni. Lakini mchakato wa leseni utaendelea na kama mwisho wa leseni utaendelea na kama mwisho wa leseni ni kwenye Wizara na Waziri watashauriana na *TCRA* kuangalia tunafanyaje kuhusu maombi yao ya leseni. *(Makofi)*

La pili ni kuhusu gawio, kwamba ni kweli wasanii wanauza; kuna vitu viwili, kuna kitu kinaitwa *ring tone* na *ring back tone. Ring tone* ni ile ambayo ukipigiwa simu inavyoita unasikia mziki. *Ring back tone* ni ile ambayo ukimpigia mtu unaisikia wewe kama mwitikio. Hivyo ni vitu viwili tofauti. Tunachoongelea hapa ni *ring back tone,* hiyo ndiyo yenye pesa. Siyo *ring tone*. Kwa hiyo, hilo tuliweke sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Serikali, tumechukizwa na tunachukizwa pale ambapo wasanii vijana, wasanii wa *Gospel*, wasanii wa bendi na kadhalika wanapopunjwa au kunyimwa haki zao. Aidha, iwe na Makampuni ya Simu, *promoters* au *radio stations* ni jambo ambalo Serikali halilitaki. Sasa, ni kweli haki na kwa mujibu wa taarifa zilizopo, huu mgawanyo uliopo haukubaliki kabisa.

Dhuluma kwa wasanii ipo kwenye kila kona. Sasa hivi tunaongelea Makampuni ya Simu, lakini kisheria na kiutaratibu kila mziki unapopigwa kwenye *radio* au unapoonyeshwa kwenye *TV,* msanii ni lazima apate mrahaba. Lakini hilo halifanyiki. Kwa hiyo, mapambano hayo ni makubwa na sisi kwenye Serikali tutaendelea na kuhakikisha kwamba ustawi wa wasanii unakuwepo na unaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudi nyuma kwamba mapambano haya kuhusu haki za wasanii yalianza muda mrefu na nataka niseme kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Kikwete ni Rais wa kwanza kuwapa hadhi vijana wa *Bongo Flavor* kutambulika na kushiriki kwenye shughuli rasmi za kiserikali. Kabla ya hapo walikuwa wanaonekana ni wahuni tu, na mwaka 2005 kwenye Kampeni zake aliamua makusudi kabisa kwamba hawa vijana tuwashirikishe wapate mapato, lakini vilevile tuwasaidie. Sasa mwaka 2009 wakati mimi nikiwa msaidizi wake Ikulu, aliniagiza akaniambia kwamba wewe nilikupa kazi ya kuhakikisha

tunawasaidia watu, lakini naona unalegea. Sasa nataka uifanye.

Kwa hiyo, tukaanzisha vikao, tukawaita *TRA* na nikaenda kwa Kitilya akanikabidhi kwa mtu anayeitwa Fovo, nikaenda kwa *Poster Master General* mwaka 2009 ili kujadili kuhusu usambazaji wa haki za wasanii na *TRA* wakasema hawajapanga bajeti ya kutafiti suala la *sticker*. Mheshimiwa Rais akatoa shilingi milioni 16 kwenye mfuko wake kulipa mshauri mwelekezi kufanya utafiti wa jambo la *sticker* mwaka 2009 na wasanii walishiriki kwenye vikao Ikulu mimi nikiwa Mwenyekiti.

Kwa hiyo, mapendekezo ya Serikali yaliletwa kwenye bajeti, ni mchakato ulioanza Ikulu muda mrefu na ulianzishwa na Mheshimiwa Rais kwa maagizo yake ambayo alinipa mimi na mashahidi ni watu wa *TRA* na watu wa Posta na Simu. Bahati nzuri *Poster Master General* yupo. Tulijadili kwa kina kuhusu uwezekano wa Shirika la Posta, kwa sababu sehemu nyingine ya dhuluma kwa wasanii ni mfumo wa usambazaji kwamba msanii anaimba, anarekodi, *CD* anayo lakini hana namna ya kuipeleka Mikoani.

Kwa hiyo, watu wanaowapunja ni wale wanaowaambia kwamba bwana niuzie hii Shilingi milioni tatu, saini hapa, umekabidhi haki zote yeye anazi-*duplicate* au anazirudufu, wanatumia mtandao wao wa usambazaji. Sisi tukadhani kwamba tukitumia shirika letu la Posta na ukichanganya na *Sticker* ya *TRA* ambayo faida yake kubwa ni kwamba, inatoa *enforcement* ya sheria kama ambavyo Sigara au *Wine,* ukiwa huna *sticker* wanaokukamata ni *TRA* na

wanakupeleka Mahakamani. Kwa hiyo, ndiyo itakavyokuwa kwenye kazi za wasanii. Kwa hiyo, hilo nilitaka niliweke sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mitandao, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusu mitandao katika maeneo yao na asilimia kubwa ya maswali tunayoyapata Wizara ni kuhusu mawasiliano kwamba, maeneo mengi ya kwetu hayana mawasiliano na Wabunge karibu wote ambapo maeneo yao hakuna mawasiliano wamechangia kututaka tuharakishe kupeleka mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niliongelee kwa ujumla kwamba tulivyokaribisha sekta binafsi kwenye Sekta ya Mawasiliano, sekta ya binafsi wanaangalia mahali ambapo pana biashara na pana fedha na hiyo ilikuwa mwanzoni mwa mwaka 2000. Kwa hiyo, wakaja wengi wakapeleka mawasiliano kwenye maeneo yenye mvuto wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mwaka 2005 ikang'amua kwamba hapana, lazima tufanye *intervention* tukiacha sekta binafsi peke yake kwa biashara kwamba ndiyo iamue, nani ana mawasiliano na nani hana? Tutawaacha wananchi ambao wana haki ya kupata mawasiliano nyuma.

Kwa hiyo, tukaamua hapa, na ikaletwa sheria chini ya Serikali ya Mheshimiwa Rais Kikwete hapa Bungeni Novemba, 2006, Sheria ya Mawasiliano kwa wote, yaani *UCAF* ambayo msingi wake ni kutoruzuku

kwa Makampuni binafsi ili yapeleke mawasiliano kule ambapo yanadhani au yanasema kwamba kuna gharama kubwa ya kupeleka mawasiliano, kwa hiyo hayawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alisaini ile sheria mwaka 2007 na mwaka 2009 kanuni zikakamilika.

Kwa kweli sasa *operationally* ule mfuko siyo kwamba ulianza mwaka 2006, bali umeanza mwaka 2010 na katika Sheria na Kanuni za *TCRA* ni kwamba moja ya vyanzo vya mapato ya mfuko ni mapato ya Makampuni ya Simu. Asilimia 0.3 ya jumla ya mapato ghafi ya Kampuni za Simu yanakwenda kwenye Mfuko, lakini vilevile Benki ya Dunia imetusaidia, tumepata Shilingi bilioni 45.

Kwa hiyo, tunachofanya sasa ni nini? Tunachofanya sasa ni kuangalia wenzetu duniani wamefanyaje? Kwa sababu katika nchi za Kiafrika zipo nchi ambazo zina mazingira kama ya kwetu, wamekaribisha sekta binafsi, lakini sekta binafsi imekwenda kwenye mvuto.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, sasa tumeshapata namna nzuri zaidi ya kuhakikisha kule ambapo hakuna mawasiliano, yanapelekwa. Kikubwa ni gharama kwa sababu mawasiliano siyo mnara peke yake, ni barabara, uwezo wa kupeleka mafuta, umeme na ruzuku hii inatolewa katika baadhi ya  hivi vitu.  Kwa hiyo, lazima u-*design* hii *project* kwa namna ambayo fedha zitatosha na gharama hizi zitaweza ku-*cover*

maeneo mengi kwa wakati mkubwa. Kwa hiyo, sisi tunaamini kabisa kwamba mawasiliano ni haki ya watu wote. Tunasikitika, tunavyopata taarifa kwamba, wananchi wanapanda kwenye miti katika baadhi ya maeneo, wengine wanampa simu 50 mtu anakwenda Mjini *message* zinaingia na anazirudisha kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yapo mengi ambayo yanatusikitisha na kwa kweli tumeongea na Mheshimiwa Waziri mwenzetu pale kwamba, hili jambo la mawasiliano tumeliahidi sana Bungeni, Mheshimiwa Rais ameahidi na nyie Waheshimiwa Wabunge mmewaahidi wapiga kura wenu kwamba watapelekewa mawasiliano, sasa na sisi ndiyo mmetupa dhamana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwambia Meneja wa Mfuko wa *UCAF*, mimi nimechomoza shingo yangu nimeahidi mbele ya Bunge, Mheshimiwa Rais ameahidi mbele ya Bunge na Waziri ameahidi mbele ya Bunge, hili litatuangusha tusipolifanya. Kwa hiyo, amenihakikishia kwamba wame-*design* vizuri wataendelea kupata fedha za kutosha na tutahakikisha kwamba kule ambako hakuna mawasiliano, basi yanafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwape kauli na kauli ya Serikali kwamba, hili tunalo na tutalifanyia kazi. Kwa hiyo, wale wananchi, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine ni

wengi na Mheshimiwa Edward Lowassa na wote ambao wamewasilisha maeneo yao, naomba nichomoze kichwa changu kwamba hili kwa kweli lisipofanikiwa basi shingo yangu ni ya kwenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna suala la kodi na lenyewe limezungumzwa sana kwamba Makampuni ya Simu haya hayalipi kodi stahiki. Sasa kodi zipo za namna nyingi. Lakini naamini kodi tunayoizungumzia hapa ni kodi ya mapato *corporate tax,* kodi ambayo na sisi tunalipa kwenye mapato yetu. Sasa mfumo wetu wa kodi sisi ni mapato, unatoa gharama, faida ndiyo inayopigiwa kodi. Sasa uwezekano wa kupata kodi unategemea kampuni imetumia gharama kiasi gani? Lakini sasa gharama anayoijua ni yule mwenye kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sisi uwezo wa Serikali wa kutambua gharama za uwekezaji na hili siyo tu la Sekta ya Mawasiliano, Madini, Mafuta na sekta nyinginezo kwamba mfumo wetu wa kodi unamwambia bwana hebu twambie kwenye uwekezaji huu umetumia kiasi gani, anasema nimetumia bilioni tatu. Kwa hiyo, mwaka huu sikutengeneza faida. Je, zile bilioni tatu sisi tuna uwezo wa kuzipitia kimoja hadi kimoja kwa Sekta zote na Taasisi hiyo moja ya *TRA* kujua kwamba kweli hizo gharama ni halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeliongea Serikalini na tutajenga uwezo wa *TRA*, lakini uwezo wa Taasisi nyingine wa kung'amua gharama halisi za

uwekezaji ili tuseme hapana. Gharama hizi haziruhusiwi kuwasilishwa kwa *purpose* ya kodi. Kwa hiyo, hilo tunaendelea nalo na hasa kwenye Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi katika sekta ya Mawasiliano tumeamua sasa kupitia *TCRA* kuweka Chombo kinaitwa *Traffic Monitoring System* ambacho kitatwambia kwamba Makampuni ya Simu haya hasa ni kiasi gani cha dakika cha *message* ambacho kinatumika. Sasa hivi wao ndiyo wanatwambia sisi kwamba, mwaka jana zimepigwa simu kadhaa na taarifa zilizopo ni kwamba, mwaka jana kwa taarifa tu za Kampuni za Simu, jumla ya dakika zilizopigwa ni bilioni 20, dakika zilizopigwa za simu. Sasa hakuna mtu ambaye anaweza kuthibitisha au kukataa kwa sababu ni taarifa zao. Tunaamini hawana sababu ya kutudanganya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa moja ya mambo ambayo tunayafanya sasa hivi ni kujenga uwezo wetu wa kujua wenyewe ili tuweze kutoza kodi stahiki. Wenzetu wa Ghana walifunga chombo kama hiki mwaka 2010 na ndani ya mwaka moja mapato yaliyoongezeka ni dola milioni 40 kwa mwaka mmoja tu na tena wao walifunga kwa ku-*monitor* simu za nje tu siyo simu za ndani, simu za nje. Kwa hiyo, tumeamua kufanya hivyo na mwezi Oktoba, mwaka huu chombo hicho kitapatikana na mwakani tutaweza kupata mapato stahiki ya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi lingine ni hili la *Interconnection fee,* ni kweli gharama

za mawasiliano zimeshuka kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake. Lakini bado gharama ni kubwa kupiga simu kwenye mitandao tofauti kwa sababu ya gharama za mwingiliano inaitwa *Interconnection fee.* Kwa sasa hivi ni *dollar sent* 0.07 ya *dollar*. Sasa kuna utaratibu wenyewe pale *TCRA* wanaita *grey puff,* kwa kila baada ya miaka mitatu hushusha. Kwa hiyo, nia yetu ni kwamba, hizi gharama zifikie sifuri kwamba, ukimpigia simu mtu wa mtandao mwingine iwe ni sawa umepigia simu mtu wa mtandao wao. Kwa hiyo, mwezi Januari, mwakani tutakuwa na bei mpya ambayo itakuwa ni chini ya sasa na mwaka 2016 tutakuwa na bei mpya ambayo itakuwa ni ya chini zaidi na tumeamua kwamba hii njia itatufikisha mahali ambapo gharama zitakuwa *zero* kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la ubora wa huduma; kumetokea malalamiko mengi kuhusu *promotion*, kuhusu wizi kwenye mitandao, kuhusu dhuluma, kuhusu kutopata haki na sisi tumeyasikia. Sasa kwenye Kanuni ya Sheria ambazo tulizipitisha hapa Sheria ya *EPOCA* na sheria ya *TCRA* zipo kanuni kabisa zinazodhibiti ubora wa huduma inaitwa *Quality of Service of Regulations*. Sasa kama nilivyosema mwanzo bado *TCRA* na Serikali hatujajenga uwezo wa kujua kama makampuni haya yanafikia. Kwa sababu zimetengenezwa kuna vitu vinaitwa *parameters,* wigo au mipaka ya ubora wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kumpigia simu *Customer Services* inatakiwa asilimia 98 uwe umepata simu ndiyo haki yako. Lakini wote mnajua

hapa mkipiga simu *Customer Services* mnasubiri muda gani? Lakini sasa lazima tuwe na uwezo wa kujua zile *parameters* hazifikiwi.  Sasa hiki chombo ambacho nimekizungumzia pia kitatusaidia kwenye hilo. Kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu la *promotions* ambazo zinaudhi watu na watu wanakatwa hela bila kujua. Tunazungumza Wizarani kwamba, kama kuna haja ya kubadilisha Kanuni basi,  tutabadilisha Kanuni kwamba isemekane kabisa kwamba kama hutaki kupokea simu za *promotion* una uwezo wa kutuma *message* kwamba mimi sitaki *promotion* zozote. Kwa hiyo, hupokei *promotion*, nchi nyingine wanafanya, wanaita *no call register*.  Unajiandikisha kwamba mimi sitaki kupokea kitu chochote kutoka kwenu au *option* nyingine unasema kwamba mimi na-*opt out* kwamba mmenitumia, lakini natuma kwamba ahsante  sana hii iwe ya mwisho ili kuwapa watu *choice* kama unataka kupokea hizo *promotion* au hutaki.  Kwa hiyo, hilo tutalizungumza Wizarani na kama kuna haja ya kubadilisha *Regulations* tutazibadilisha ili tuweze kufikia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja nyingine ambazo Waheshimiwa Wabunge walizileta Mheshimiwa Josephine Chagulla nimekwishazungumza kuhusu mtandao.  Mheshimiwa Benedit Ole-Nangoro, nimekwishazungumza kuhusu maeneo yake. Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Daktari Mary Nagu naye amezungumzia maeneo yake, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Daktari Hadji Mponda, Mheshimiwa

Desderius Mipata, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Faith Mitambo na Mheshimiwa Kaika Telele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hao wametuandikia na wametoa mchango ambao tuna uthamini. Kwanza, kuhusu mambo ya jumla ya kurekebisha sekta yetu, lakini vile vile kuhusu maeneo yao. Naomba niwaambie wananchi wao ambao wanawasikiliza kwamba Waheshimiwa Wabunge wao licha tu ya kutoa michango hapa, lakini na mimi binafsi wamekuwa wananisumbua, wananihangaisha kuhusu mitando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kwamba tulifanya zoezi, tulisambaza orodha ambayo tuliichukua mwanzo ya maeneo ambayo hayana mitandao na ile kazi ambayo mmeifanya ya kuorodhesha imetusaidia sana. Kwa sababu ukitazama ramani tuliyonayo sisi ya maeneo yenye mitandao inaonesha eneo kubwa la nchi lina mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawa pale Nyang'hwale kwenye Kijiji fulani, ukienda kwenye ramani yetu inaonesha kuna mtandao, lakini wanakijiji pale kijijini hawana mtandao. Kwa hiyo, ambacho mmetusaidia ni kwamba, sisi tutarudi kwenye ramani yetu na tutaangalia upya na sasa tumepata picha halisi kutoka kwa wawakilishi wa watu ambao wanapokea kero za watu kuhusu mitandao.

*(Hapa kengele ililia)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Ya kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Yamezungumzwa masuala ya *TTCL*, Mheshimiwa Waziri atayagusia na atayaelezea. Lakini nirudi tena kwenye suala la kodi. Kwa kifupi ni kwamba, kuna jinamizi moja ambalo sisi kama nchi lazima tukabiliane nalo na lenyewe linaitwa *transfer pricing* kwamba asilimia 60 ya biashara ya Kimataifa si biashara kati ya nchi na nchi, si biashara kati ya Mashirika na nchi, si biashara kati ya Mashirika na Mashirika ni biashara kati ya Mashirika dada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 60 ya *value* ya biashara ya Kimataifa ni biashara kati ya Mashirika dada na hapa ndipo tunapoibiwa kwamba una Kampuni hapa inatengeneza ngozi, una kampuni dada ipo Dubai ambayo inanunua ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kampuni ya hapa inaiuzia kampuni dada ya Dubai ngozi kwa bei rahisi ili wawaoneshe mapato madogo na ile kampuni ya Dubai inaiuzia ngozi kampuni dada ya Marekani kwa bei halisi na hii kampuni ya ngozi inanunua mitambo kwa kampuni dada kwa bei ya juu ili

kuonesha gharama ni kubwa, mapato ni madogo. Kwa hiyo, ukiangalia makaratasi ya kodi yapo sawa, lakini halisi haiko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumelizungumza Serikalini kwamba na zipo kuna vitu vinaitwa *transfer pricing rules,* zipo kanuni za kujua ni kiasi gani makampuni haya yamekaribiana, zinaitwa *arms length rule*. Lakini kwa nchi kama zetu bado na sisi kwenye Serikali tunalifanyia kazi na kwa kweli ni jambo ambalo lazima tulikabili la sivyo tutakuwa tunalalamika mwaka hadi mwaka kwamba tunaibiwa na hawa jamaa, ukienda kutazama vitabu vyao vipo sawa huwezi kuwakamata hawajavunja sheria yoyote. Kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisahau kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa uongozi wake wa Kamati lakini pamoja na ushirikiano ambao anatupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Naibu Waziri kwa ufafanuzi mzuri ulioutoa kuhusu Makampuni ambayo yanafanya dhuluma. Tunategemea Serikali italiona hili na kulirekebisha na kuhakikisha linakuwa *corrected*. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kuniwezesha kusimama mbele yenu na kutoa mchango katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaouonesha katika kuliendesha Bunge letu. Nachukua fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa umakini wake wa kusimamia Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyoiwasilisha hapa Bungeni leo asubuhi kwa michango yao mizuri na yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi zimetolewa na hii ni dalili ya dhati ya mwamko mkubwa kwa upande wa kuendeleza maeneo ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na ubunifu kwa umma wa Watanzania ili tuweze kupiga hatua zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, katika michango hii imedhihirika wazi kuwa juu ya mahitaji makubwa ya mawasiliano ya simu kama ilivyokuwa huduma za usafiri wa reli, barabara na bandari kuwa ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imeonekana dhahiri kuwa masuala ya kuendeleza shughuli za utafiti yana umuhimu mkubwa katika kutekeleza programu

mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, uendelezaji wa Vyuo vya Sayansi na Teknolojia utawezesha Taifa kuongeza wataalam wa fani hizo wenye ujuzi na weledi unaohitajika katika kuleta maendeleo katika nyanja za uzalishaji na huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge mmoja aliyechangia katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupitia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii mbalimbali kuhusu Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge waliotoa maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni na wengine wamechangia kwa maandishi. Naomba sasa niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge aliyechangia wakati wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mmoja. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Wabunge 13 na waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 102.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuongea humu ndani ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa

Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Rajab Mbouk Mohammed, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni na Mheshimiwa Lucy Nkya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Daktari Titus Kamani, Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Daktari Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Daktari Lucy Nkya, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Daktari Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Abas Mtemvu na Mheshimiwa Ezekiel Maige. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallack, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa *Engineer* Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Josephine Chagulla**,** Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Ismail Aden Rage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wapo Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa

David Kafulila, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Daktari Hadji Mponda, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Daktari Mary Nagu, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Sabreena Sungura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Azza Hamad, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale**,** Mheshimiwa Felix Mkosamali**,** Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis**,** Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Waride Bakar Jabu, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Daktari Kebwe Stephen Kebwe na Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wamechangia Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Mchungaji Daktari Getrude Rwakatare, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mheshimiwa Daktari Abdullah Juma Abdulla Saadala, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Lolesia

Bukwimba, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Salim Mohamed Khamis, Mheshimiwa David Ernest Sillinde, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Margareth Sitta, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Titus Kamani, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Dustan Kitandula na Mheshimiwa David Mathayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wabunge niliowataja ilikuwa ni mizuri sana na ilisheheni busara, hekima na changamoto. Aidha, sio rahisi kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi. Naahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote. Ushauri na maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu imezingatia na maoni ya Kamati ya Upinzani vilevile yamezingatiwa. Hata hivyo, ningependa nitumie muda huu mfupi nilionao kujibu hoja kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kujibu hoja ambazo zilitolewa na Kamati ya Miundombinu. Hoja yao ya kwanza ilikuwa Kamati ilishauri Serikali ipunguze urasimu katika utekelezaji wa majukumu yake kwani kwa mwaka wa fedha 2011/2012 utekelezaji wa maagizo mengi ulikuwa bado uko kwenye mchakato au haujatekelezwa. Aidha, Kamati inapenda kuishauri Wizara kwamba maagizo yote ambayo hayajatekelezwa na taarifa yake ya utekelezaji lazima yakamilike kwenye mwaka huu. Ushauri wa Kamati umepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DIT* kupitia Idara ya Ujenzi ina maabara ya kisasa ambayo inafanya kazi kubwa ya kupima udongo kwa ujenzi wa nyumba katika maabara hiyo. Pia *DIT* ina uwezo wa kutoa ushauri wa kitaalam kupitia maabara hii ili Serikali na wananchi kwa ujumla waweze kujenga nyumba kwa kutumia maabara hii ili waweze kuendelea. *DIT* vilevile imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuboresha maabara na kuboresha mazingira ya kazi ili iweze kuendelea vizuri na kutoa ufanisi kwenye shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itaendelea kufanya juhudi kuongeza fedha za bajeti katika taasisi hii ili kuongeza utendaji wake katika utoaji elimu kwa vitendo, utafiti, utoaji ushauri wa kitaalam na miundombinu. Ushauri huu tumeupokea na tutaendelea kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili wa Kamati ya Miundombinu ilikuwa ni kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa kutekelezwa kutokana na kutotolewa kwa ukamilifu fedha za maendeleo. Wizara itaendelea kuwasiliana kwa karibu na Wizara ya Fedha ili fedha zinazotengwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya miradi hiyo ziweze kutolewa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Kamati ilikuwa Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mapema mradi wa Postikodi na Simbo za Posta kwa kuwa mradi huu ni muhimu. Aidha, Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kukamilisha mradi huu kwa kuwa itasaidia kufanikisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara, kijamii pamoja na utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna Mheshimiwa Sylvester Mabumba sikumtaja, naomba niseme amechangia kwa maandishi. Mheshimiwa George Mkuchika na yeye vile vile amechangia kwa maandishi, naomba unisamehe Mheshimiwa George Mkuchika. Mheshimiwa Maryam Msabaha amechangia kwa maandishi, naomba anisamehe, samahani kama nimefanya makosa kwenye jina. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Kamati, mradi unatekelezwa kwa ushirikiano na wadau wengine ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wizara

ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Serikali ya SMZ. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maji, Nishati, Ardhi, SMZ, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ofisi ya Takwimu na Serikali na Shirika la Posta wote wanafanya kazi kwenye mradi huu wa Simbo za Posta na anwani za makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu umeanza katika maeneo ya katikati ya Manispaa ya Arusha na Dodoma kama nilivyosema kwenye hotuba yangu leo hii asubuhi kufuatia kifungu namba 41 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kieletronikia na Posta ya Mwaka 2010. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetoa orodha ya *Symbols* za Posta au Postikodi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na imechapishwa kupitia gazeti la Serikali, *GN No.* 220 ya tarehe 22 Juni, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi bilioni 158 zinahitajika kutekeleza mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2015/2016. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa kushirikiana na wadau wengine wanaotarajiwa kuchangia gharama za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Menejimenti ya *TTCL* kuwa makini na majadiliano ya kibiashara na Kampuni mbalimbali ikiwemo *Nippon Electric Corporation* ya Japan ili kuanzisha ushirikiano wa kibiashara na kuendeleza mtandao wa *TTCL*.

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Wizara na taasisi zake ambazo zilikuwa zinadaiwa na *TTCL* na kulipa madeni haya kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ambayo yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 6.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wake ushauri wa Kamati ya Miundombinu umezingatiwa na Menejimenti ya *TTCL* wakati wote wa majadiliano ilikuwa makini kuhakikisha kuwa mkataba wao utakaosainiwa kati ya *TTCL* na *NEC* unalinda maslahi ya *TTCL* na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na hoja ya Kamati kwa kuwa Watanzania wenye vipaji vya ugunduzi kwa mara nyingine, Kamati inashauri Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuhamasisha ugunduzi huo kwa kutunga sheria maalum au sera ili kuhakikisha kwa bidhaa zinazogunduliwa zinatengenezwa kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wake Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inahamasisha utengenezaji wa bidhaa zinazogunduliwa kwa kuwezesha wagunduzi kwa kuwapatia mwega kama ifuatavyo. Tume imetoa mwega ufuatao; Sh. 829,641,000/= kwa ajili ya kubiashirashia matokeo ya utafiti na ugunduzi mbalimbali katika taasisi zifuatavyo:-

Kwanza imetoa kwenye *CAMARTEC*, jumla ya sh. 255,000,000/= zimetolewa kwa ajili ya kutengeneza na kupeleka sokoni trekta ambayo imetengenezwa *CAMARTEC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mzinga jumla ya sh. 181,000,000/= kwa ajili ya kutengeneza mashine ya kusagisha vyakula vya mifugo imepewa mwega na kupeleka kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TIRDO* jumla ya sh. 200,000,000/= kwa ajili ya kutengeneza mitambo ya kuunguza na kuharibu taka za hospitali imepatiwa mwega. Pia *TIRDO*, jumla ya sh. 14,000,000/= zimepelekwa kwa ajili ya kutengenezea *solar tannery drier* kwa ajili ya kukausha dagaa, unga wa mihogo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ina mpango wa kuunda Mfuko wa Uendelezaji na Uhaulishaji wa Teknolojia Mbalimbali yaani (*Innovation Fund)* kwa kushirikiana na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa kama vile *Grand Challenge* ya Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya Kamati iendelee kusisitiza kuwa elimu ya sayansi iimarishwe katika shule za msingi na sekondari ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa walimu kwa masomo ya sayansi na kujengwa kwa maabara ili kuwaandaa vijana kwa ajili ya masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati umezingatiwa, Serikali kwa kuona umuhimu wa wanasayansi katika kuendeleza fani hii imeweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi kwa kuwekea utaratibu wa kutoa mkopo wa asilimia 100 kwa wanafunzi wanaodahiliwa katika

masomo ya sayansi katika Vyuo Vikuu vyetu hasa kwenye fani ya Udaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wote wanaochukua masomo ya sayansi hupatiwa mikopo kwa ajili ya masomo hayo katika taasisi za Vyuo Vikuu. Vile vile Serikali imeandaa mkakati wa kupanua na kuongeza Vyuo Vikuu vya Sayansi na Teknolojia nchini katika jitihada ya kuhakikisha kuwa inapata wataalam wa kutosha wanaoshughulikia mambo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia miongoni mwa waliochangia kwa maandishi Mheshimiwa Daktari Dalaly Peter Kafumu naye amechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni nyingi kwa vile muda umekwenda, sitoweza kuzizungumza zote. Sasa naomba nizungumzie hoja ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani. Hoja ya kwanza ilikuwa bajeti kidogo ya mradi wa maendeleo. Bajeti hii imetengewa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2012/2013. Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha kwa kuzingatia vipaumbele vya kutekeleza kila mwaka kwa kuzingatia utekelezaji wa majukumu na ukuzaji wa sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilikuja na hoja nyingine ambayo inasema ufinyu wa bajeti na fedha zinazotolewa. Majibu ya hoja hiyo, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo nchini, hivyo

Serikali itafanya kila liwezekanalo na kila njia ili kupatikana fedha nzuri katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ambayo inasema kupungua kwa bajeti ya Wizara mwaka hadi mwaka. Majibu ya hoja hiyo Serikali haina nia ya kupunguza na kuwekeza katika teknolojia. Serikali inayo nia ya dhati na imedhamiria kuwekeza katika masuala ya sayansi na teknolojia. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kuwa Serikali kwa makusudi imeweza kujenga taasisi ya Nelson Mandela iliyoko Arusha kwa fedha zake za ndani kwa asilimia mia moja na kila itakapowezekana itaendelea kuisaidia taasisi hiyo ili iwe katika kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo nafikiri ni muhimu kuizungumza, ni kwamba Serikali kutotekeleza ahadi yake ya asilimia moja ya *GDP* kwa ajili ya utafiti. Jibu la hoja hiyo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha kuwa fedha inayoahidi inatolewa. Aidha, utolewaji wa fedha hizo kwa kiasi kikubwa utegemea ukusanyaji wa mapato ya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani kazi za ubunifu zihifadhiwe vizuri. Jibu la hoja hiyo ni kwamba, Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia inaendelea kutoa tunzo, mafunzo na kuwawezesha kwa kuwapa vitendea kazi wabunifu na wagunduzi ili waweze kuendeleza vipaji vyao kwa muda muafaka. Tume imeanzisha mpango wa kuwawezesha wabunifu na wagunduzi wadogo wadogo hususan wale waliopewa

tuzo ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa kuwapatia vitendea kazi ili waweze kuzalisha bidhaa zinatokana na gunduzi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa vifaa vyenye thamani ya sh. 70,673,000,000/= vimetolewa kwa wagunduzi watano. Kwanza kwa Bwana David Kyando wa Njombe aliyewahi kupatiwa tuzo na taasisi kwa kubuni na kutengeneza mtambo mdogo wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji huko Njombe mwaka 2010. Pia tuzo na zawadi imepewa kwa Bwana Joseph Kimario wa Kilimanjaro aliyewahi kupatiwa tuzo ya *TASAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimepata ki-*note* kwamba, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye amechangia kwa maandishi, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mgunduzi mwingine Bwana David Matia wa Mbuli aliyewahi kupatiwa tuzo ya TASAT mwaka 2010 kwa ubunifu wake wa kuzalisha umeme kutoka kwenye mashine ya kusagisha nafaka huko vijijini. Pia mtu aliyepatiwa tuzo mwingine ni Saidi Majulize wa Dar es Salaam amegundua utengenezaji wa rangi kutoka kwenye magome ya miti asilia naye pia amepatiwa tuzo na zawadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya, nimeshamtaja Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye hoja moja baada moja. Kwanza nianzie hoja za Kampuni ya *TTCL*. Lakini kabla ya hapo watu wanasema mtu kwao kwanza nataka kuanzia hoja ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma. Mheshimiwa Riziki alisema kwamba mpaka sasa hivi hatujatenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo la *TTCL* huko Pemba. Nafikiri Mheshimiwa Riziki hukufanya utafiti kuhusu hili, kwa sababu kiwanja kipo na tumeshaanza kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Riziki kidogo ufanye utafiti ili kuhakikisha unachosema hapa ni kitu cha uhakika. Pia Mheshimiwa Riziki alizungumza kwamba tumeitelekeza ile Posta ya Wete. Bahati mbaya nasikitika sana kwa sababu Mheshimiwa Riziki anaishi Wete nilitegemea kwamba ajue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Wete mwezi wa Nne tulipeleka vifaa vya kompyuta kwa ajili ya *internet*. Pengine hata huko Pemba akimaliza Bunge haendi, ndiyo maana akawa hajui. *Otherwise* watu wa Wete wanamsikia, naomba afike kule. Hilo nilikuwa nizungumzie tu kwa sababu ya Mheshimiwa Riziki.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye hoja ya Mheshimiwa Amina Abdallah Amour ambapo anasema pamoja na kuwa *TTCL* ni kampuni ya kwanza nchini, lakini kwa sasa imedorora kiutendaji, Serikali inaombwa ipange mipango mizuri ili kampuni hii iweze kurudisha hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo au utekelezaji. Tangu 2001 *TTCL* ibinafsishwe hakuna uwekezaji mkubwa uliofanywa katika kuboresha miundombinu yake ya kutolea huduma za simu na *data* ilikuweza kutoa huduma bora zaidi za mawasiliano na pia kushindana kikamilifu na makampuni mengine ya simu. *TTCL* imekuwa ikiwekeza kiasi kidogo cha fedha kila mwaka kutoka vyanzo vyake vya mapato ya ndani ambacho hakikidhi kuleta maendeleo tarajiwa. Hali hii imefanya utendaji wa *TTCL* kudorora mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2010 hadi sasa *TTCL* imeweza kuwashirikisha wadau wengine katika kufanikisha mipango yake ya kibiashara na maendeleo hususan *TTCL* inatumia fedha zinazolipwa na wateja kugharamia ujenzi wa miradi ya mawasiliano na *supplier's credit* ili kutekeleza mipango yake ya kibiashara na maendeleo. Ili kuinusuru kampuni ya *TTCL* Serikali inakamilisha utaratibu wa kununua hisa asilimia 35 za *BAT Airtel* ndani ya *TTCL* ili kuwa na hisa mia kwa mia ya *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu bado unashughulikiwa na Wizara ya Fedha. Iwapo *TTCL* itakopeshwa fedha na mabenki baada ya kupata dhamana itaweza kutekeleza mpango mkakati wake wa miaka mitatu yaani 2012 - 2014 ili kukuza mapato yake kupata faida na kutoa ushindani stahili katika soko la mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pia *TTCL* inaendelea na mkakati wa kuunganisha nchi zilizobakia kwenye

mkongo wa Taifa baharini kupitia Tanzania. Nchi zilizobaki ni Kenya, Uganda na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mchango wa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro *TTCL* ina mpango gani ya kupanua na kusambaza huduma za mawasiliano vijijini ikiwemo Tarafa ya Makami. *TTCL* inatumia fursa ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kutoa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini ambayo hayana mwelekeo wa biashara ikiwemo Tarafa ya Makami, Wilayani Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Wajumbe wengine wamezungumzia *TTCL*, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, amesema *TTCL* itafikisha lini huduma za mawasiliano ya simu za mkononi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mkakati wa *TTCL* wa miaka mitatu 2012 -2014, imeainisha maeneo ambayo mtandao wake utafika ikiwemo Wilaya ya Tarime kutegemea na upatikanaji wa fedha. Hivi sasa Serikali inashughulikia maombi ya *TTCL* ya kupatiwa dhamana ili iweze kupata mkopo wa Mabenki kwa ajili ya kutekeleza mpango mkakati wake. Aidha, *TTCL* itatumia fursa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo kwa vile hayo ni baadhi tu ya michango ya *TTCL*.

Mheshimiwa Spika, pia mchango mwingine unatoka kwa Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamsi. Yeye anazungumzia taasisi ya Sayansi za *TID* na *MIST* zifanye ufumbuzi na ubunifu ili kuwezesha nchi kupiga hatua kiuchumi. Majibu ya hoja hiyo; Serikali kupitia

Wizara tayari imeshazishauri taasisi hizi kuanzisha makampuni ambayo yatakuwa na jukumu la kuji...
Matokeo ya uvumbuzi na ubunifu wa taasisi hizi. Tayari *DIT* na *MIST* zimeshaanza makampuni haya. Aidha, Serikali kupitia *COSTECH* imeanzisha mpango wa kusaidia taasisi za utafiti nchini kupeleka matokeo ya utafiti kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alisema lini hasa taasisi ya Sayansi na Teknolojia, Mbeya itakuwa Chuo Kikuu kamili, maana sasa ni muda mrefu Bunge lako pia na wananchi wa Mbeya wamekuwa wakisikia maelezo bila kutokea utekelezaji. Jibu la Hoja hii ni kwamba *MIST* tayari imeshakuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia kuanzia mwaka huu wa masomo 2012/2013. Wizara inategemea kuteua viongozi wa Chuo Kikuu hicho hivi karibuni. Kundi la kwanza la wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia litadahiliwa na kuanza masomo Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja ya Mheshimiwa Betty Machangu yeye anauliza kwamba Chuo cha Nelson Mandela pia kifanye udahili, wanafunzi kutoka Afrika Mashariki na kwingineko na Chuo kijitangaze ili kipate wanafunzi kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya hoja hii ni kwamba, dhamira kubwa ya Nelson Mandela ni kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kuibua maarifa mapya na ubunifu na huduma kwa jamii katika kiwango cha Kimataifa, Uhandisi Sayansi na Teknolojia ili kuwezesha

upatikanaji wa rasilimali watu na matumizi endelevu ya mawasiliano na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia dhana hiyo taasisi inatangaza nafasi za masomo Afrika Mashariki na Afrika Kusini Jangwa la Sahara na wanafunzi wanachaguliwa kwa ushindani kutoka nchi mbalimbali za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Aidha, Nelson Mandela iko mbioni baada ya kufanikiwa kuanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Jitu Soni yeye ametoa hoja kwamba, Serikali iangalie namna ya kutoa fidia ya ardhi kwa mmiliki aliyetoa ardhi kwa manufaa ya umma na pia kuangalia namna ya kuomba ardhi zaidi kwa ajili ya Chuo cha Nelson Mandela. Jibu la hoja hiyo; kwa kutambua umuhimu wa kupanua Nelson Mandela, Serikali ilikipatia eneo lenye ukubwa wa hekta 3,285 huko Karangai na imeshafanya tathmini ya fidia ya ardhi. Ulipwaji wa fidia hiyo utaanza kufanyika mara moja.

Mheshimiwa Spika, pia kuna baadhi ya hoja kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Athumani Mfutakamba, yeye hoja yake ni kwamba, makampuni mbalimbali ya kibiashara huwa yanatumia *out sourcing* wafanyakazi kwa ajili ya kuchambua takwimu mbalimbali za kibiashara kwa kutumia kompyuta. Makampuni haya ya *IT* yapo Marekani na kwingineko, je, kwa kuwa na mkongo wa Taifa wa mawasiliano Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira inafanyaje ili

vijana waweze kupata taaluma ya *IT* ili waweze kufanya hiyo ya *out sourcing process*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu Mheshimiwa sasa hivi kuanzia mwaka huu wa fedha tutaanza kujenga kijiji mahiri ambacho kazi yake moja itakuwa ni kuanzisha hizo biashara za *Business Processing Outsourcing* na Kijiji hicho huenda kikajengwa sehemu ya Kigamboni itategemea upatikanaji wa ardhi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, tayari fursa hii inafanyiwa majaribio katika atamizi ya TEHAMA ya *COSTECH* na hata hivyo ushauri wa Mheshimiwa Mbunge utachukuliwa na kuzingatiwa ipasavyo. Pia Mheshimiwa Chikawe yeye ametoa ushauri juu ya kutowajibika kuhusu *safety deposit* au *e-west management* vifaa vya TEHAMA nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri huu na nawapongeza sana, tutaufanyia kazi; ni ushauri muhimu ambao sisi kwa kweli tumeuona na lazima tuufanyie kazi. Aidha elimu kwa umma itaendelea kutolewa ili kuandaa Watanzania kujenga jamii habari ambayo italinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia aliuliza ama alitoa hoja kwa nini hakuna utaratibu wa makusudi ili kufundisha elimu ya kompyuta na kuwezesha sayansi iweze kusambaa haraka nchini kwa sababu elimu ya kompyuta itarahisisha au italeta maendeleo. Jibu la Hoja hii; Serikali tayari imechukua hatua za makusudi za kukuza na kueneza matumizi ya TEHAMA nchini, hatua

hizo zimeanza katika sekta ya elimu kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza mitaala ya elimu imehuishwa ili TEHAMA kama somo liweze kufundiswa mashuleni na pia lifundishwe katika vyuo vya Ualimu kama nyenzo ya kufundishia. Hivi sasa shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo vya ualimu vimeunganishwa na mkongo wa Taifa chini ya mradi wa *e-school*, *TBT* pamoja na *ICIP*. Majaribio yameonesha majaribio makubwa katika shule 27 zinazotumia huduma hii ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Leticia Nyerere yeye anaiomba Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria wa *Cyber crime* ambao utasaidia kudhibiti uhalifu unaofanywa kwenye mtandao. Ushauri wako umepokelewa na tunakushukuru sana kwa ushauri mzuri. Aidha, mazingira ya kutunga Sheria kama hii yapo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaendana na kutungwa kwa Sheria yetu ya *EPOCA* ya mwaka 2010 ambayo ilianza kutumika mwaka jana. Tayari Kanuni za Sheria hii zimetengenezwa na zimeanza kutumika. Katika Kanuni na Sheria za *EPOCA* inaagiza kuanzishwa kwa kitengo cha *Computer Emergency Response Team* ambayo ni kitengo ambacho kinashughulika na usalama wa mitandao. Kitengo hiki kipo na kina wataalam 30 kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kutunga Sheria kudhibiti uhalifu wa kimtandao kwa nchi za Afrika

Mashariki umekamilika na kuridhiwa na Mawaziri wa Sekta ya TEHAMA. Aidha, mfumo kama huo wa nchi za Africa yaani *African Union Convection for Establishment of Credit Legally Framework upon a* tunaweza kuutumia hapo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda umekwisha sitaweza kujibu hoja zote. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wako kwa kujibu hoja karibu zote. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu hatua inayofuata!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 68 – WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management... ... ...* Sh. 1,558,779,000/=

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilikuwa nimemuuliza Waziri kwamba, ile mikataba ya nyimbo za wasanii na makampuni ambayo wanaingia nayo mikataba kwa ajili ya kutumia kwenye milio ya simu, mikataba ile inakuwa imeandikwa kwa Kiingereza, lakini bado

hakuna msimamizi yeyote kati ya msanii na yale makampuni na hivyo mikataba ile kwanza inakuwa imekiukwa, lakini bado wanakuwa wanavunja hata yale makubaliano yaliyopo kwenye ile mikataba. Sasa nilikuwa nimeomba Serikali wanifafanulie ni kwamba, watatumia njia zipi kuhakikisha mikataba ile inatenda haki kwa wasanii.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba lipo tatizo la uwezo wa wasanii kubaini haki na wajibu wao kwenye mikataba wanayoingia. Kwa maana hiyo Serikali tumeamua tutaunda Kamati ya pamoja kati ya wasanii, *COSOTA* ambao inasimamia haki miliki, Wizara yetu pamoja na makampuni ili hili jambo linalohusu *ring tones* na *ring back tones* tulimalize kwenye kikao kimoja na wasanii wapate haki yao wanayostahili na mikataba hii iwe mikataba inayoeleweka na wasanii wenyewe waweze kunufaika.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo hilo nilikuwa naomba Wizara ituambie kwa sababu kwa Wizara ya Fedha kuanzia tarehe 1 Januani, 2013, mfumo wa *sticker* unaanza. Tungependa mambo yote haya ya wasanii yakamilike kwa pamoja. Wizara lini mtakuwa mmekamilisha taratibu hizi za kuhakikisha wasanii wanapata mapato yao stahili kutokana na hizo *ring tones* na *ring back tones?*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mfumo wa *sticker* zinaanza tarehe 1/1/2013 kwa

sababu bado unahitaji maandalizi ikiwemo uchapishaji wa *sticker* zenyewe na utaratibu mzima wa udhibiti wa bidhaa mpya ambayo inaingia kwenye kudhibitiwa kwenye *TRA* ukiondoa hizi za kawaida za sigara na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii ambalo linahusu teknolojia hii ya *ring tones* na *ring back tones*; kwa sababu hili suala vile vile linahusu Wizara ya Habari, Utamaduni na Vijana kwa maana ya BASATA, *COSOTA* na taasisi nyingine ni lazima tufanye mashauriano. Lakini ambacho naahidi ni kwamba, kwa kadri siku zinavyokwenda msanii anadhulumiwa. Kwa hiyo, ni jambo la haraka, tutalifanya mapema na vikao vya mwanzo tutavifanya kabla Bunge hili halijakwisha.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Katika mchango wangu hapa nilizungumzia suala la ujenzi wa *TTCL* Pemba, Waziri wakati anajibu, amemjibu Mheshimiwa Riziki kwa kejeli, fedhuli na maneno ambayo hayakuwa na staha, ninachomwambia na ninachozungumza ni kwamba ujenzi wa *TTCL,* Pemba haujaanza mpaka dakika ya sasa hivi tunazungumza hapa. Ni lini ujenzi wa *TTCL* Pemba utaanza?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka kumwambia Mbunge kwamba, Pemba tunacho kiwanja tayari na utaratibu wa ujenzi upo tayari. Ukianza kujenga huanzi moja kwa moja kujenga lazima kwanza utayarishe michoro, uanze kupeleka wapimaji

pale na kila kitu. Hiyo kazi imeanza na tunaendelea vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko kwamba makampuni yetu ya simu ni miongoni mwa makampuni ambayo yanakwepa kodi, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kwamba inakabiliana na changamoto hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyoeleza wakati nafafanua hoja ya baadhi ya Wabunge ni kwamba, kwanza ni kujenga uwezo wa Serikali wa kuweza kung'amua gharama za uwekezaji ili kuweza kutoza kodi iliyo stahiki. Hilo ni la jambo la kwanza kwa ujumla na tunaendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili ni kwamba *TCRA* na Serikali kwa ujumla imeamua kununua mtambo unaoitwa *Traffic Monitoring System* ambao utatueleza kwa uhakika kiasi cha dakika zinazotumika, kiasi cha *sms* zinazotumwa na biashara nzima inaendeaje ili tusitegemee taarifa za makampuni ya simu kwenye kutoza kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba mpango huu utatusaidia kuongeza mapato na nilitoa mfano wa nchi ya Ghana kwamba katika mwaka mmoja tangu wafunge mtambo wao, mapato yameongezeka dola milioni 40. Tunaamini kwamba hilo tutalimaliza kwa mtambo huu, lakini tutalimaliza vile vile kwa kujenga uwezo wa wahasibu

wa Serikali kufuatilia matumizi ya uwekezaji wa makampuni binafsi.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anaeleza katika hotuba yake alizungumzia mkakati kutoka analojia kwenda digitali mwishoni mwa mwaka huu. Kwa kuwa mkakati huu umekuja haraka sana wananchi wengi hawajui, lakini pia unaweza ukasababisha athari kubwa ya mazingira kutokana na vifaa hivi vya elektroniki ambavyo vitakuwa havitumiki. Je, Waziri anaweza kutueleza ni mkakati gani upo katika kukabiliana na athari hii ya mazingira itakayosababishwa na mchakato huu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huo mpango upo na itakapofika tarehe 31 Disemba, tutazima mitambo ya analojia kwenda digitali, lakini kuanzia sasa kwa muda mrefu sasa tumeendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu mpango huo na wananchi wameanza kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Televisheni ambazo zinatumika sasa hivi hazitaweza kutupwa kwa hiyo hakutakuwa na tatizo la kutupa hivyo vifaa, isipokuwa wananchi wanatakiwa wanunue ving'amuzi ili waweze kupata matangazo hayo. Pia zile *channel* ambazo sasa hivi zinaweza kupatikana bure kwa wakati huo zitaendelea kupatikana bure ilimradi uwe na king'amuzi tu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Katika sera ya bioteknolojia ya Wizara ya mwaka 2010 kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 21 inaeleza kwamba tutaanzisha *association* ya bioteknolojia ya Tanzania. Nataka kujua *association* hii inaanzishwa lini kwa sababu wanamaliza Vyuo Vikuu, wanasoma bioteknolojia na taasisi zingine zinakuwa haziwatambui. Taasisi hii itaanzishwa lini.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumelisema hilo kwenye sera yetu na sasa hivi tupo katika mipango ya kufanya *implementation plan* ya sera hiyo na hivi karibuni tutaanza kutengeneza hiyo *Association* ya Bioteknolojisti.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Labda ningependa kupata maelezo kutoka kwa Waziri. Katika mitandao inayojiita mitandao ya kijamii ambayo muda mwingi imekuwa ikikashifu na kuwatukana viongozi wa Kitaifa, ni nani anayemiliki, siku moja Waziri alijibu swali humu Bungeni akisema hawajui wanaomiliki mitandao hii wakati mitandao hii ina matangazo ya biashara ya makampuni ya *Airtel* na *Vodacom* kwa nini wasianzie huko? Ningependa kupata maelezo.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao hii inamilikiwa na watu tofauti, wengine wapo hapa Tanzania na wengine wapo nje ya Tanzania. Sisi kwa kulitambua hilo, sasa tumeanzisha chombo ambacho tunakiita *(CERT) Computer Emergency Response Team*

ambayo kazi yake itakuwa kuangalia mitandao kama hii ambayo inakashifu viongozi.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu nilitaka kujua kuhusu hizi tafiti ambazo zimeshakwishafanywa ambazo mara nyingine ni za ubunifu, ambazo zipo kwenye ma-*shelves* tu zimekaa. Baadhi yake zinaweza zikaleta tija kubwa kwa nchi na kwa wananchi. Kwa mfano, zipo tafiti au uvumbuzi wa mtambo wa *electronic voting* ambao tukienda *practically* kuutengeza nchi inaweza ikauza kwa nchi nyingi na ikapata faida na tukaepuka huu upigaji kura wa makaratasi ambao una hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile zipo tafiti ambazo zimeshafanywa nyingi duniani, ni kiasi cha kuona, kwa mfano, ufugaji wa samaki baharini hasa namna tabianchi inavyobadilika, kuna uwezekano wa kufuga samaki baharini watu wote wa *coastal area* wakafaidika. Kinachohitajika ni namna gani ya vyakula watakavyolishwa wale samaki na tukaweza kufuga samaki baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya nini mpaka sasa hivi ambapo kuna mambo mengi ni faida kwa wananchi, kuweza kuwaokoa ambapo sasa hivi Wizara imelenga mifugo, tumeacha sekta ya bahari ambayo ina wananchi wengi maskini na wanaweza wakaongeza pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atufafanulie ni nini Wizara yake itafanya katika bajeti ya mwaka huu kuendeleza sekta hizo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zipo tafiti nyingi ambazo zimefanywa na sisi hilo tunalijua na baadhi ya hizi tafiti sisi tumeweza kusaidia. Kwa mfano, ukiangalia hapa leo tuna maonesho tumeleta watalaam wa *incubation,* Dar es Salaam ambao tumewasaidia ili waweze kupata soko. Kuhusu suala la Uvuvi bila shaka tutakaa tutaangalia kama upo utafiti ambao umefanywa, naamini ulikuwa unakusudia huko Zanzibar, tutaweza kulifanyia kazi.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia kwa maandishi nilimweleza Waziri kwamba, kuna watafiti wengi sana kutoka nje na hata ndani ya nchi, wanafanya utafiti katika nchi yetu bila kibali na na taarifa hizo unaweza kuzikuta nje ya nchi na hapa Tanzania hazipo. Niliomba Waziri ajaribu kutueleza atachukua hatua gani ili *COSTECH* waweze kuwa wanapata taarifa hizi na waweze kudhibiti watafiti wote wanaokuja kutafiti katika nchi yetu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSTECH* tumetayarisha *database* kwa ajili ya tafiti zote zinazofanywa hapa nchini. Tunajaribu kila mwaka kuwaita watafiti wote na kuwafuatilia ili kujua hizo tafiti zilizofanywa ili kuondoa *duplication*. Kwa sababu hatutaki watu warudie kufanya vitu ambavyo tayari vimeshafanywa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Waziri ametueleza kwamba Kanuni za kuandaa Sheria ya *cyber crime*s iko tayari na vilevile amesema kwamba, kuna watalaam takriban thelathini kama sikosei wapo wameshaanza kufanya kazi yao. Ningeomba Waziri atuelezee hawa watalaam 30 wanafanya kazi gani na kwa kutumia sheria gani ukizingatia kwamba hatujawahi kuletewa Muswada hapa Bungeni unaoshughulikia *cyber crime*s.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mbunge ni kwamba, sheria ambayo inatumika katika kutengeneza hiki chombo cha *cyber crimes, computer emergency spot team* ni kwenye Sheria ya *EPOCA* ya mwaka 2010. Lakini sheria hiyo ipo na ndiyo inayotupa uwezo wa kufanya kazi hii.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika semina ambayo ilifanywa na *TCRA* katika ukumbi wa Pius Msekwa juu ya maandalizi ya kuhama kutoka analojia kwenda digitali, ikihusisha masuala ya ving'amuzi, Wabunge tulishauri kwamba kuwe na tahadhari kubwa ili wananchi wetu hasa wa kipato cha chini wasije wakapata usumbufu kwenye ving'amuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninavyozungumza wananchi kule vijijini hususani Mwibara wanapotaka kutumia king'amuzi kupata *Star TV* wanalazimika kupata king'amuzi ambacho hakuna *ITV*, lakini ving'amuzi hivi vimesheheni mambo ya

Kiarabu na mambo mengine ya Kizungu ambayo wananchi wangu hawahitaji. Naomba Waziri anieleze, wananchi watanunua ving'amuzi vya idadi kiasi gani kujaza pale nyumbani ili anapotaka kuangalia *ITV* aende king'amuzi hiki na kama akitaka *Star TV* anafunga hiki anaanza kwenda kingine. Huu mzigo ataubeba nani? Nataka Waziri anipe maelezo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika Mkoa wa Mara sasa hivi hakuna matangazo ya giditali, televisheni ni mikoa saba Tanzania ambayo ina matangazo hayo, lakini kwa Mkoa wa Mara bado hatujafika. King'amuzi anachosema yeye si kwa ajili ya digitali inawezekana kwa ajili ya TV za *satellite*. Sisi kwa kulijua hilo hatutapenda wananchi wetu watumie ving'amuzi vitatu, *Star Media* na king'amuzi chake, Agape na king'amuzi chake na *basic transmission* na king'amuzi chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunataka king'amuzi kimoja kama ilivyo simu unaweza kubadilisha tu *sim card*, kwa hiyo itakuwa king'amuzi kimoja kwa watoa huduma zote tatu na sasa hivi tunalifanyia kazi jambo hili, kama mwananchi atanunua king'amuzi chochote ni lazima aweze kupata zile *free to dirTV's* kwa mfano *TBC, ITV, CHANNEL TEN, STAR TV* na kadhalika.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea jinsi ambavyo Makampuni ya Simu yanapenda kutoa huduma sehemu ambazo kuna

vivutio vya kibiashara na sehemu ambazo hakuna vivutio vya biashara siyo kipaumbele kwao. Je, Waziri atakuwa tayari sasa kuhakikisha kwamba mawasiliano ya simu yanapelekwa sehemu ambazo kuna uhitaji mkubwa hasa Mwambao wa Ziwa Tanganyika hasa ukizingatia suala la usalama na Jimbo la Kalambo kwa ujumla wake.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimtaje Mheshimiwa Cecilia Paresso kama mchangiaji ambaye hakutajwa naamini watu wa Karatu wamesikia kwamba umechangia. Ni kweli kama nilivyoeleza kwenye mchango wangu kwamba biashara ya makampuni ya simu ni biashara binafsi, kwa hiyo wana uhuru wa kuamua wapi wapeleke mawasiliano na wapi wasipeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, Serikali kwa kutambua kwamba tunahitaji mawasiliano kwa watu wote, kwa wakati wote na kwa wakati mmoja, tukaamua tuanzishe kutoa ruzuku kwa kupeleka mawasiliano kwa maeneo kama hayo unayoyataja. Lakini kwa kutambua kwamba mchakato huu utakuwa ni awamu, kwamba kutakuwa na awamu ya kwanza, awamu ya pili na ya tatu kabla hatuja-*cover* eneo la nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vipaumbele vitakuwa kwenye maeneo magumu ya visiwa ambapo kunahitaji mawasiliano ya haraka zaidi. Tunaamini kwamba awamu ya kwanza na ya pili zitaingiliana,

zitakwenda haraka zaidi. Kwa hiyo, tunaamini hili ni jambo ambalo tutalifanya kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda nimtaje Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kama mchangiaji kwa maandishi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu niliomba Serikali ilifahamishe Bunge ule utaratibu ulioanza mwaka 2008/2009 wa ku-*register* simu na *line* za simu ili kuondoa matumizi mabaya ya *line* ambapo tunatukanwa, watu wanatumia *chip* kwa ajili ya kutukana na kuzitupa umefikia wapi na umefanikiwa kwa kiasi gani mpaka sasa hivi? Ni kwa nini mpaka sasa hivi *chip* zinauzwa kama karanga barabarani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba moja ya sababu za kusajili simu ni pamoja na kuhakikisha usalama wa mawasiliano pamoja na *identity*, tuliamua kwamba zoezi hili tulifanye kwa hatua ili tusikate mawasiliano kwa watu wote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi asilimia kubwa ya Watanzania wameshasajili simu, lakini mfumo uliopo sasa hivi ni kwamba unapewa muda, unaweza kununua *chip* ukakaa nayo kwa mwezi na mwezi ukiisha inazimwa. Kwa hiyo, ndani ya mwezi uweze kuisajili ili kutoa ruhusa kwa dharura. Lakini kadri tunavyokwenda tutafika mahali ambapo tutakuwa hatuhitaji kipindi hicho.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (2), sasa tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu!

Kif. 1002 - *Finance and Accounts... ... ... ... ...* Sh. 283,761,500/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning... ... ... ... ... ...* Sh. 541,592,750/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit... ... ... ... ... ... ...* Sh. 97,129,750/=
Kif. 1005 - *Legal Unit... ... ... ... ... ... ... ... ... ...*Sh. 48,919,500/=
Kif. 1006 - *Government Communication Unit... ...* Sh. 96,754,850/=
Kif. 1007 - Procurement Management Unit... ... Sh.176,120,750/=
Kif. 1008 - *Management Information System... ...* Sh.99,149,750/=
Kif. 2001 - *Communication Division... ... ... ... ...*Sh. 413,614,750/=
Kif. 2002 - *Information, Comm. and Technology...* Sh.507,803,500/=
Kif. 3003 - *Science and Technology... ... ... ...* Sh. 26,451,660,584/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 68- WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Kif. 1003 - *Policy and Planning… … … … … … …*Sh. 100,000,000/=
Kif. 1008 - *Management Information System… … … … …* Sh. *0/=*
Kif. 2001 - *Communication Division… … … …* Sh.1,304,586,000/=
Kif. 2002 - *Information, Comm. and Techn. … …*Sh. 2,000,000,000/=
Kif. 3003 - *Science and Technology… … … …* Sh. 36,427,839,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2012/2013, kifungu kwa kifungu na kuyapitipisha bila mabadiliko yoyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Bunge limeyapitisha kwa mafungu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya

Matumizi na kuyapitia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2012/2013, kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yeyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa na iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, Kamati ya Miundombinu ambayo ilishughulikia taarifa hii pamoja na Kamati ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa michango ambayo kwa kweli imeweza kuboresha na Serikali imejibu yote na wametupa imani kubwa sana kwamba Mawaziri hawa wawili wanaweza kuisukuma Wizara hii na kutuletea mabadiliko makubwa sana.

Waheshimiwa Wabunge sina matangazo yoyote, nashukuru kwa ushirikiano mkubwa mlionipa katika kukaa kwenye kiti hiki kizito sana. Naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 26 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*